# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 24 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. ASMA A. MWINYI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kama mtakumbuka tarehe 20 Aprili, Mheshimiwa Jesca aliomba Mwongozo.

Mwongozo wa Spika ulioombwa na Mheshimiwa Jesca David Kishoa kuhusu kutojibiwa kikamilifu maswali ya nyongeza katika swali lake la msingi la 131.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 20 Aprili, 2026, katika kikao cha 12 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Tatu, Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki aliuliza maswali mawili ya nyongeza katika swali lake la msingi Na. 131.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maswali yake ya nyongeza kujibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu), Mheshimiwa Kishoa aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 79 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 kutokana na kutoridhishwa na majibu ya Serikali. Swali la msingi la Mheshimiwa Kishoa lilikuwa kama ifuatavyo: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa soko kubwa la mazao ya kilimo Wilaya ya Mkalama kama ilivyoahidi kwenye Ilani?

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu), alijibu kwa kueleza kuwa, "*Serikali inatambua umuhimu wa kujenga soko hilo. Vilevile, hata kiwanja kimepatikana na kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na tathmini ya mazingira inaendelea kufanyika.*" Aidha, alieleza kuwa, baada ya hapo bajeti ya ujenzi wa soko itatengwa.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na jibu hilo, Mheshimiwa Kishoa aliuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza alitaka kujua hatua iliyofikiwa katika mchakato wa ujenzi wa soko kwa kuzingatia kuwa nyaraka zote muhimu zimekabidhiwa kwenye mamlaka husika lakini hakuna kinachoendelea. Swali la pili liliitaka Serikali kutoa *commitment*, soko hilo lini litajengwa ili kuongeza mapato ya ajira kwa wananchi?

Waheshimiwa Wabunge, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika maswali ya nyongeza yalikuwa kama ifuatavyo: -

> *"Tunafahamu kuna uhitaji wa kujenga soko la mazao na ndiyo maana tayari timu ya wataalamu iko site tunavyoongea sasa, na kabla Juni tutakuwa tumepata design yote na usanifu wa kina na baada ya hapo tunatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Hakuna nyaraka ambayo haijafanyiwa kazi, ndiyo maana timu iko pale site. Nikuhakikishie wewe na wananchi wa Mkalama kwamba jambo hilo linakwenda kufanyika."*

Waheshimiwa Wabunge, kiti kimepata *Hansard* kama kilivyoahidi na kujiuliza je, maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kishoa hayakupata majibu ya kuridhisha?

Waheshimiwa Wabunge, kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kujenga soko la mazao katika Kata ya Nduguti, Makao Makuu ya Halmashauri ya Mkalama. Aidha, alifafanua kwamba nyaraka zilizoandaliwa kwa ajili ya mradi huo zinafanyiwa kazi. Mheshimiwa

Naibu Waziri alithibitisha kwamba timu ya wataalamu wa Serikali inaendelea na mchakato wa awali ambapo ukikamilika bajeti ya ujenzi wa soko itatengwa na ujenzi utaanza.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kuwa timu ya wataalamu iko *site* na kabla ya mwezi Juni mchakato wa kuandaa michoro na usanifu wa soko utakuwa umekamilika. Majibu hayo yalimfanya Mheshimiwa Kishoa atume maafisa wake kwenda Ofisi ya Halmashauri Mkalama pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ili kupata usahihi wa majibu yaliyotolewa. Baada ya hilo, ikabainika kuwa tangu mwaka 2024 hakukuwa na mwendelezo wa ujenzi wa soko.

Waheshimiwa Wabunge, uchambuzi wa suala hili umeonesha kwamba mradi wa ujenzi wa soko unafanyiwa kazi. Hili linaungwa mkono na maelezo ya Mheshimiwa Kishoa aliyekiri kwamba zipo nyaraka za ujenzi wa mradi zimeandaliwa na kuwasilishwa Serikalini ambazo ni barua, andiko la mradi, pamoja na *environmental and social impact assessment*.

Waheshimiwa Wabunge, katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri alilithibitishia Bunge kuwa nyaraka hizo zimepokelewa na zinatumika katika kuandaa michoro ya ujenzi, usanifu na uandaaji wa bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, wakati akijibu, Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kuwa wataalamu wako *site*. Ukiangalia kwa ujumla maelezo ya Naibu Waziri na yale ya Mheshimiwa Kishoa unapata jibu kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri alimaanisha wataalamu wanaendelea na hatua za awali za ujenzi. Kazi hiyo ya wataalamu inaweza kufanyika hata kama hawapo katika eneo la mradi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, maelezo hayo yapo katika ufafanuzi wa Mheshimiwa Naibu Waziri alipoeleza kuwa kutoka sasa hadi mwezi Juni au kabla ya Juni michoro ya ujenzi itakuwa imekamilika, na baada ya hapo Serikali itapanga bajeti ya ujenzi wa soko.

Waheshimiwa Wabunge, tafsiri ya maneno hayo ilichukuliwa tofauti na Mheshimiwa Kishoa ambaye alitafsiri kuwa wataalamu wa Serikali wapo kwenye eneo la miradi hiyo na aliwatuma maafisa wake kwenda kuthibitisha.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo, nimejiridhisha kwamba majibu ya Naibu Waziri yalikuwa ya kuridhisha kwa sababu yalifafanua kutosheleza kuhusu hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa mradi wa soko kama ilivyoulizwa na Mheshimiwa Kishoa.

Waheshimiwa Wabunge, imedhihirika kwamba Mheshimiwa Kishoa alisisitiza kuhusu umuhimu wa Serikali kukamilisha ujenzi wa soko na kwamba ujenzi wa soko umechukua muda mrefu.

Waheshimiwa Wabunge, upande wa Serikali umeahidi kuwa kabla ya mwezi Juni hatua za mandalizi za mradi huo zitakuwa zimekamilika na bajeti ya mradi itapangwa.

Waheshimiwa Wabunge, matumaini yangu ni kuwa Serikali itatekeleza ahadi hiyo kwa wakati ili kuwawezesha wananchi wa Mkalama kunufaishwa na soko litakalojengwa. Hivyo, Mheshimiwa Kishoa avute subira kwani muda uliobaki ni mfupi kutoka sasa. Huo ndiyo Mwongozo wa Spika, umetolewa leo tarehe 22 Aprili, 2026.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 179

**Changamoto ya Ajira kwa Vijana**

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa muda mfupi na wa kati wa kupunguza changamoto ya ajira kwa Vijana hususan Wahitimu wa Vyuo Vikuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kuwawezesha vijana, hususan wahitimu wa vyuo vikuu, ili kupunguza tatizo la ajira. Miongoni mwa hatua hizo ni kuandaa Mwongozo wa Taifa wa Mafunzo ya Uzoefu Kazini wa Mwaka 2017 unaoratibu utoaji wa mafunzo kwa kushirikisha sekta ya umma na binafsi, pamoja na kutekeleza programu ya mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano.

Mheshimiwa Spika, kupitia programu hiyo, jumla ya wahitimu 32,194 wamenufaika kwa kupata ujuzi, maadili ya kazi na uzoefu unaowawezesha kuajiriwa au kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeanzisha programu maalum za kuwawezesha vijana katika sekta zenye ajira nyingi kama kilimo *(BBT)*, madini *(MBT)* na uvuvi *(BBT-LIFE)*, sambamba na kuunganisha Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi kupitia mikataba na Qatar, Saudi Arabia, *UAE* na Iran, ambapo vijana 6,559 wamenufaika kati ya Julai, 2025 hadi Machi, 2026.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mikopo yenye masharti nafuu imeendelea kutolewa. Mwaka 2024/2025 shilingi bilioni 36.64 zilitolewa kwa vikundi 2,827, na mwaka 2025/2026 zimetengwa shilingi bilioni 200 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Regina Malima.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali na ninatambua namna

ambavyo Serikali imeendelea kuwekeza katika elimu ya juu hasa vyuo na vyuo vikuu. Ninaipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na nitakuwa na swali moja dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua, je, ni sekta zipi zimepewa kipaumbele katika mipango hiyo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameisema hapa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO:** Mheshimiwa Spika, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Regina kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, lakini mtakumbuka tangu Mheshimiwa Rais ameingia madarakani ukiacha siku 100 za Mheshimiwa Rais ambapo tulitoa ajira 12,000 mpaka kufikia mwezi huu wa nne tarehe 11 Serikali imeshaajiri vijana 25,238.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kikubwa cha Serikali tumepeleka vijana kwenye maeneo ya afya na elimu ambapo kulikuwa kuna pengo kubwa la watumishi, na tunaendelea kufanya hivyo kwenye sekta nyingine.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi hiyo hiyo ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Salum Khamis Salum.

Na. 180

**Ujenzi wa Soko la Mnada wa Mifugo – Meatu**

**MHE. THOMAS K. MAGANGA K.n.y. MHE. SALUM K. SALUM** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la Mnada wa Mifugo ili kuwa na Soko lenye hadhi na kuongeza mapato ya Halmashauri katika Jimbo la Meatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khamis Salum, Mbunge wa Jimbo la Meatu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu inayo minada ya awali minne ya Bukundi, Itinje, Mwanhuzi na Tindabuligi ambayo inahitaji kuboreshwa ili kuweka mazingira mazuri ya kuuza na kununua mifugo katika wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu kupitia mapato ya ndani ilitoa shilingi milioni 14.3 kwa ajili ya kuboresha minada hiyo kwa kujenga machinjio, choo na kutwaa eneo la kujenga mnada wa kisasa lenye ukubwa wa ekari nane katika Kijiji cha Bukundi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Halmashauri imetenga shilingi milioni 12 kwa ajili ya kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa uzio wa mnada katika eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa mnada wa kisasa wakati taratibu za kutafuta fedha za ujenzi wa mnada huo zikiendelea. Ujenzi wa uzio huo unatarajiwa kuanza Mei, 2026.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kampala, kwa niaba.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka Mizani kwenye minada hiyo ili kuwasaidia wakulima kuuza mifugo yao kwa kilo kuliko inavyokisiwa kwa sasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni utaratibu wa Serikali, na kwa mujibu sheria, mauzo ya mifugo yanatakiwa kufanyika kwa kufuata taratibu za kuwa na mizani ya kupima uzito wa mifugo hiyo. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Wizara husika, Viwanda na Biashara, na Wizara ya Mifugo, tutahakikisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tunawasiliana na kuweka utaratibu wa pamoja ili kuhakikisha kwamba eneo la minada hii linakuwa na mizani kwa ajili ya kupimia mizigo na biashara iende vizuri zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mnada wa Tinde ulioko katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ni mnada ambao uko barabarani njia kuu ya kwenda Burundi, Rwanda pamoja na Uganda na hauna uzio. Nini mkakati wa Serikali kutuwekea uzio katika ule Mnada wa Tinde kupunguza ajali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Dkt. Christina kwamba Mnada wa Tinde ni mnada mkubwa na unahudumia wafanyabiashara wengi na uko kwenye barabara kuu. Kwa kweli tunahitaji kuwa na uzio ili kwanza kuboresha usalama, lakini pia kuboresha huduma za mnada huo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga waanze kutenga fedha za mapato ya ndani ya halmashauri kwa awamu kuanza ujenzi wa uzio huo kwa hatua, wakati Serikali Kuu pia ikiangalia namna nzuri ya kupata fedha na kuweza kuunga mkono juhudi hizo ili mnada ule uboreshwe kuwa wa kisasa zaidi.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikali Kiti*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante. Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itaboresha ujenzi wa Mnada wa Kateshi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya Serikali ni kwamba maeneo yote yenye uhitaji wa shughuli za kiuchumi na za kijamii yakiwemo masoko, stendi na minada, ni kipaumbele katika mipango ya halmashauri, lakini pia ni kipaumbele katika mipango ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Asia Halamga kwamba hoja hiyo tumeichukua, lakini nasisitiza pia kupitia Halmashauri ya Hanang, Mkurugenzi aanze kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kuanza kuboresha mnada huo wakati Serikali inaendelea na hatua zinazotakiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante. Tunaendelea, ninamwita sasa Mheshimiwa Omari Marcus Msigwa, Mbunge wa Madaba aulize swali lake.

Na. 181

**Hitaji la Watumishi wa Sekta ya Afya – Madaba**

**MHE. OMARY M. MSIGWA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaongeza Watumishi wa Sekta ya Afya wakiwemo Wataalamu wa Mionzi katika Jimbo la Madaba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Marcus Msigwa, Mbunge wa Jimbo la Madaba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutenga bajeti na kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya nchini. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2025/2026 jumla ya watumishi wa kada mbalimbali za afya 37,921 wameajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Serikali imeajiri jumla ya wataalam wa kada mbalimbali za afya 5,000 na kuwapanga katika halmashauri zenye upungufu ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Madaba iliyopangiwa watumishi 84.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu na huduma katika vituo vya afya ngazi ya msingi hali iliyopelekea mahitaji ya wataalam wa kada za afya ikiwemo wataalam wa mionzi kuongezeka ambapo wanaohitajika ni 1,159 na kwa sasa wapo 338 sawa na 29%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuajiri wataalam wa mionzi pamoja na kuwaendeleza wataalam wa kada nyingine 56 wakiwemo watumishi wawili kutoka Halmashauri ya Madaba wanaopata mafunzo ya muda mfupi ya mionzi katika Chuo cha Afya Hydom.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omary Marcus Msigwa maswali ya nyongeza.

**MHE. OMARY M. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali la nyongeza. Je, ni lini utakuwa tayari kuja kuona Vituo vya Afya Mtyangimbole, Lituta na Matetereka katika Halmashauri mpya ya Jimbo la Madaba ambapo kuna upungufu mkubwa wa watumishi sekta ya afya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama ambavyo katika ajira za siku 100 za kwanza za uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Halmashauri ya Madaba ilipata watumishi 84 na tunatambua kwamba kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika halmashauri hiyo. Kila kibali cha ajira inapotoka tutahakikisha Halmashauri ya Madaba inapewa kipaumbele ili kuongeza watumishi katika vituo vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie kwamba nipo tayari kuambatana naye, tutapanga baada ya Bunge hili ili twende Madaba kupitia kwenye vituo hivyo vya afya alivyovitaja pamoja na kuona hali ya utumishi na kuona namna nzuri zaidi ya kuboresha huduma za afya.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, Jimbo la Same Mashariki lina vituo vya afya vitatu, ninaishukuru Serikali, lakini vituo vitatu vya afya vyote havina watumishi wa kutosha. Ukiangalia zahanati za jimbo zima, kila zahanati unakuta ina mganga mmoja tu au wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi Mheshimiwa Waziri aje kwangu, bali ninaomba akaketi ofisini, aangalie vizuri na aone kwamba kuna umuhimu wa kuniletea watumishi. Je, ataniletea watumishi hao lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Jimbo la Same Mashariki katika zahanati na vituo vya afya kuna upungufu wa watumishi, lakini Serikali imekuwa kila ikitoa kibali cha ajira tunahakikisha watumishi wanapelekwa Jimbo la Same Mashariki kama ambavyo tumekuwa tukipeleka kwenye majimbo mengine kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwamba Serikali inatambua uhitaji wa watumishi, na kila kibali cha ajira kinapojitokeza, tutahakikisha watumishi wanaopelekwa halmashauri hiyo inakuwa ni kipaumbele cha hali ya juu ili kuendelea kupunguza pengo la watumishi na kuendelea kuboresha huduma kwa wananchi wa Jimbo la Same Mashariki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Mji Nanyamba ina vituo vya kutolea huduma ya afya viwili; Kituo cha Afya Dinyecha na Hospitali ya Mji Nanyamba zenye *X-Ray machine,* lakini halmashauri hiyo haina mtaalamu wa mionzi hata mmoja. Je, Serikali itapeleka mtumishi huyo haraka ili ikatoe huduma inayokusudiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunavyo vituo vya afya ambavyo Serikali kwa kujali afya za wananchi tulinunua mitambo na mashine za *X-Ray* vikiwemo Vituo vya Afya viwili katika Halmashauri ya Nanyamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Abdallah Chikota kwamba Serikali inatambua hatuna watumishi wa *X-Ray* katika halmashauri hiyo, na hivi sasa tumeanzisha utaratibu wa kupeleka watumishi wanaotoka makazini kwenda kwenye vyuo ambavyo vinafundisha *short courses* za masuala ya *X-Ray* na hivi sasa tuna watumishi zaidi ya 150 wanaendelea na kozi hizo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kuhitimu wataalamu hao tutahikikisha maeneo yale ambayo ya mashine za *X-Ray* na wataalamu hawapo, tunapeleka wataalamu ili

tuhakikishe kwamba huduma za *X-Ray* na *Ultra Sound* na huduma nyinginezo za vipimo zinafanyika vizuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Zuberi Mfaume.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Ninapenda kumwuliza Naibu Waziri kwamba ni lini sasa watumishi wa kada ya afya, katika maabara watakuwa wakipandishwa ngazi za madaraja sambamba kama wenzao wa kada ya famasi pamoja na manesi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taratibu za utumishi wa umma, na kwa taratibu ambazo zimeendelea kutekelezwa kila kada, ina utaratibu wake, kwanza wa madaraja, pia na utaratibu wake wa kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka mitano iliyopita imevunja rekodi ya kupandisha madaraja kwa watumishi wa kada zote; madaktari, wauguzi, walimu na watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba wale wenye sifa na wanaostahili kupandishwa madaraja, wanapandishwa madaraja yao kwa wakati ili kudumisha utumishi bora katika sekta ya afya, na pia katika sekta zote hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza. Halmashauri ya Mji wa Bunda ina mahitaji ya watumishi kwenye sekta ya afya 854. Waliopo ni 384, upungufu 470 wakiwepo watano kwa ajili ya mionzi. Ni lini sasa Serikali itatupatia

wataalamu hawa ili wananchi wangu wawe na uhakika wa kupata huduma nzuri ya afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba Serikali inatambua kuna upungufu wa watumishi katika vituo vyake vya huduma katika Jimbo la Bunda Mjini, na upungufu huu umetokana na sababu kubwa mbili. Sababu ya kwanza, ni kwa sababu Serikali imejenga vituo vya afya, zahanati na hosptali za wilaya kwa wingi ndani ya miaka mitano. Kwa hiyo, *automatically* imeleta mahitaji makubwa zaidi ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunafahamu safari ni hatua, tumeanza kwa kujenga, kupeleka vifaa tiba na sasa tunakwenda kupeleka watumishi kama ambavyo watumishi 5,000 wameajiriwa miezi miwili iliyopita na tutaendela kuhakikisha kwamba tunapeleka watumishi katika Halmashauri ya Bunda Mjini na wataalamu wa *X-Ray*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, wapo kwenye mafunzo, tunaendelea kuwapeleka kwa awamu na tutahakikisha maeneo yote yenye mitambo ya *X-Ray, Ultrasound* na mitambo mingine tunapata wataalamu ili vipimo kwa wagonjwa wetu viwe bora na uhakika zaidi.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Sasa tunahamia Wizara ya Uchukuzi. Ninamwita Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 182

**Malipo wa Fidia kwa Wananchi wa Kilwa Masoko**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa fidia kwa Wananchi wa Kilwa Masoko waliopisha upanuzi wa eneo la Uwanja wa Ndege?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha zoezi la uthamini wa mali za wananchi wanaopaswa kupisha utekelezaji wa mradi wa ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko. Hatua hii ni muhimu katika kuhakikisha kuwa haki na stahiki za wananchi husika zinatambuliwa ipasavyo kabla ya utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi hao, kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya kisheria inayosimamia ulipaji wa fidia nchini. Serikali ina dhamira ya kuhakikisha kuwa fidia stahiki inalipwa kwa wakati kadri rasilimali zitakavyopatikana, ili kuwezesha utekelezaji wa mradi huo muhimu kwa maendeleo ya sekta ya usafiri wa anga na uchumi wa eneo husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasnain Dewji maswali ya nyongeza.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ahadi hii ya fidia ilitamkwa na Mheshimiwa Rais Mkoani Lindi wakati amekuja kuomba kura, na ahadi ya Rais ni kama maelekezo, na kwa kuwa Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo wananchi wangu walipwe fidia, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aharakishe hilo jambo kwa kuwa wananchi wangu wanateseka sana, hawana mpango

wowote, huku fidia hawajapata na huku mvua zinanyesha. Kwa hiyo, ninaomba sana fidia ipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ninamwomba Naibu Waziri aje Kilwa kuona, tukae nao wanateseka sana, mvua hizi ni kubwa, hawana pa kwenda huku fidia hawajapata, huku hawajijui wanakwenda wapi? Kwa hiyo, ninamwomba sasa Naibu Waziri aje aongozane na mimi, tufuatane, aone kabla...

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa, umeshauliza maswali mawili. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Dewji kwa namna ambavyo ana-*sympathize* na wananchi wa Kilwa Kusini kutokana na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali inatambua umuhimu wa kuendeleza kiwanja hiki, na lazima nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba yako mambo makuu matatu ambayo tunayazingatia sana katika upangaji wa bajeti. La kwanza, tunatazama Ilani ya CCM; la pili, tunatazama dira ya 2050; na la tatu, maelekezo ya viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye mwenyewe ameshasema na amekumbushia kwa niaba ya wananchi kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameonyesha dhamira ya dhati kwa kuhakikisha kwamba uwanja huu unajengwa. Pale Kilwa siyo tu uwanja, pia alionyesha dhamira ya dhati kuhakikisha kwamba bandari ya uvuvi inajengwa na ninyi mnashuhudia bandari ya uvuvi sasa inakwenda kuzinduliwa. Nimhakikishie hata hili anakwenda kulifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira, Serikali kupitia Wizara yetu ya Uchukuzi pamoja na Wizara ya Fedha tumeshamaliza uthamini, hatua iliyobaki ni kulipa. Tutakwenda kuharakisha kama alivyoomba ili wananchi hao wanaoteseka waweze kupata fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ameuliza kuhusiana na kuwa tayari kwenda, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa Mnyaa, nitakuwa tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kwenye eneo kuzungumza na kuwaeleza nia dhahiri ya Serikali ili watuvumilie tunapoendelea kujipanga kwa ajili ya kulipa fidia hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi wanaozunguka Uwanja wa Ndege wa Masasi katika Kata ya Mwenge Mtapika, Kijiji cha Mbonde ambapo tathmini yake na uhakiki ilifanyika mwaka 2023? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Uwanja gani amesema?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hokororo, ninaomba urudie swali lako.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi wanaozunguka Uwanja wa Ndege wa Masasi, Kata ya Mwenge Mtapika, Kijiji cha Mbonde ambao tathmini yake na uhakiki ulishakamilika tangu 2023?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, Mtwara, kwa swali lake la nyongeza juu ya wananchi wa Masasi. Ninamwomba kama ninavyowaomba na Waheshimiwa Wabunge watupe subira kidogo, kwani tumefanya tathmini viwanja takribani 14 nchi nzima na tunalipa awamu kwa awamu. Kwa kuja kwenye swali lake kulingana na upatikanaji wa fedha tutakwenda kulipa wananchi hao, watuvumilie.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa kiwanja cha ndege kilichopo maeneo ya Sanzale, Kata ya Magomeni Bagamoyo ukizingatia Mji wa Bagamoyo sasa umekuwa mji wa ikolojia ya bahari na usafiri fungamanishi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anataka kufahamu ni lini Serikali inakwenda kujenga uwanja ulipo pale Bagamoyo? Ni kweli Serikali inayo dhamira ya kuujenga uwanja huo, lakini ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba uwanja huo ambao unakwenda kujengwa ni sehemu ya mradi mkubwa sana wa kiuchumi wa Bagamoyo ambao ndani yake una bandari pamoja vitu vingine vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, sasa hivi tupo kwenye mipango mbalimbali Serikalini kuhakikisha kwamba tunafanikisha, na tutakapokuwa tayari, tutakwenda kujenga uwanja huo.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Agnesta Kaiza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri ninatambua chini ya uongozi wa Mama Samia Suluhu Hassan, wananchi 737 kati ya wananchi 1,825 wameshalipwa fidia katika Kata ya Kipawa ndani ya Mtaa wa Kipunguni Mashariki kwa ajili ya wale waliopisha upanuzi wa uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kwa Serikali. Ni lini sasa Serikali italipa zile fidia kwa wananchi 1,088, fidia ambayo imekaa kwa muda mrefu sana? Zingatia, ni lini, Mheshimiwa Naibu Waziri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Agnesta, Mbunge wa Segerea kwa

swali lake hilo ambalo ameliuliza. Ni dhamira ya Serikali kuanzia mwaka 1967 kufanya uthamini katika uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam pale *JNIA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ni Rais huyu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan baada ya kuona wamekaa muda mrefu wananchi hawa mwaka 2022 akalekeza, tukafanya uthamini upya, ambapo ilibainika tunahitaji takribani shilingi bilioni 144, Mheshimiwa Rais ameshaanza kulipa kwa wananchi hao, takribani shilingi bilioni 66.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, wananchi waliobaki 1,000 ni dhamira ya Serikali kulipa kidogo kidogo, wanakwenda kulipwa Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji. Sasa ninamwita Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, Mbunge wa Viti Maalum, aulizr swali lake.

Na. 183

**Kufikisha Maji ya Ziwa Victoria kwa Wananchi - Simiyu**

**MHE. TINNAR A. CHENGE** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani kufikisha huduma ya Maji Safi na Salama kutoka Ziwa Victoria kwa Wananchi wanaoishi umbali zaidi ya Km 12 kutoka Bomba Kuu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Mkoa wa

Simiyu ambapo utekelezaji wa mradi huo utahusisha pia Vijiji 103 ambavyo viko katika umbali wa kilometa 12 kutoka bomba kuu kila upande katika Wilaya za Busega, Bariadi na Itilima. Mradi huo umefikia wastani wa 58% za utekelezaji ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuendelea kufanya upanuzi wa mradi huo mara utakapokamilika ili kufikisha huduma kwenye vijiji vyote ambavyo vitakuwa havijafikiwa na huduma ya majisafi na salama kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tinnar Chenge.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na niendelee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mradi huu kubwa sana wa maji, na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jamii ya wananchi wa Mkoa wa Simiyu ni wafugaji na wakulima, je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga bomba lingine sambamba na hili la majighafi kwa ajili ya shughuli za mifugo pamoja na kilimo cha umwagiliaji ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mkoa wa Simiyu una wilaya tano, na kati ya wilaya hizo wilaya yenye changamoto kubwa sana sana ya maji ni Wilaya ya Meatu. Je, Serikali haioni kwamba kuna sababu za msingi za kuingiza Wilaya ya Meatu kwenye awamu ya kwanza ya ujenzi wa Bomba la Ziwa Victoria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swali muhimu sana na la msingi linalobeba matamanio ya wananchi wa Mkoa wa Simiyu, lakini pia niendelee kumpongeza na kumshukuru kwa kutoa ushirikiano mzuri sana kwa Wabunge wa majimbo katika Mkoa wa Simiyu. Vilevile, ninampongeza kwa kutafsiri kwa uhalisia majukumu ya Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni mkubwa sana. Ni mradi wa takribani shilingi bilioni 440 ambapo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa kwa ajili ya wananchi wa Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, katika kuhakikisha kwamba tunakabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kurejesha uoto wa asili, Serikali imepanga kupanda miti na nyasi katika maeneo ya wilaya zote tano za Bariadi, Busega, Itilima, Maswa na Meatu, lakini tunayo maeneo ambayo tuna ekari karibia 11,200 ambapo mpaka sasa tumeshafikia 30% ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunao mpango wa kukarabati mabwawa ili kuhakikisha sasa kwenye suala la umwagiliaji, basi iweze kufanyika bila kuwa na changamoto yoyote. Upande wa Meatu, ni kweli kabisa katika wilaya ambazo zina ukame, Meatu kwa Mkoa wa Simiyu inaongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, usanifu wa mradi huu ambapo tunajenga tanki letu kwenye *intake* yetu pale Nyashimo, pia tunajenga mtambo wa kutibu maji na kuyasafisha. Pia, tuna ujenzi wa matanki karibia sita ambayo yamebeba kwa upana wake mahitaji ya wilaya zote tano ikiwemo Meatu. Kwa kile kilima kilichoko Ibumba pale Itilima, kuna tanki la lita milioni 10 ambalo ndilo litakalochukua maji kutoka pale Itilima kupeleka katika Wilaya za Meatu pamoja na Maswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tunaamini kwamba *phase* ya kwanza itakapokamilika, *phase* ya pili itabaki sasa ni kusambaza maji katika Wilaya ya Meatu pamoja na Maswa na mradi utakuwa umekamilika kwa 100%, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Adonis Alfred, uliza swali dogo la nyongeza.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Ningependa kufahamu Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi yake ya muda mrefu ya kufikisha huduma ya majisafi na salama katika Kata za Mayondwe na Muhutwe katika Wilaya ya Muleba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni ahadi ambayo imetolewa na Serikali ya Awamu ya Tano, na utekelezaji ulishafanyika katika Kata za Kemondo na Kanazi kwa Wilaya ya Bukoba. Kwa hiyo, ilikuwa inasubiriwa kwamba mradi huu utafika katika Wilaya ya Muleba katika kata hizo.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Muleba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za Serikali, sambamba na ahadi kutokana na Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ndiyo msingi wa utekelezaji, ndiyo msingi wa mipango yetu; mpango wa mwaka mmoja, na miaka mitano. Ndiyo msingi wa kutenga bajeti kuhakikisha sasa ahadi hizo zinaenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, ahadi ya Serikali ambayo ilitolewa, aidha na viongozi wakuu wa Kiserikali, ama kwenye Ilani ya uchaguzi, ama kiongozi yeyote ambaye alifika katika eneo husika na kutoa hiyo ahadi, ahadi hizo zitatekelezwa na bila kuwa na changamoto yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna juhudi ambazo tayari zimeshafanyika katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge, na tunaamini kwamba miradi iliyopo katika hatua mbalimbali, tutaikamilisha, na baada ya hapo, tutaangalia kama kutakuwa na changamoto nyingine. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea. Ninamwita sasa Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, aweze kuuliza swali lake.

Na. 184

**Kukamilika kwa Mradi wa Maji Rorya – Tarime**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Miji 28 ya Rorya – Tarime utakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Jimbo la Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Miji 28 wa Rorya - Tarime uliopo Mkoa wa Mara kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 134.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa dakio *(intake)* katika Ziwa Victoria lenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 29 kwa siku, ujenzi wa mtambo wa kutibu maji *(treatment plant)* wenye uwezo wa kutibu maji lita milioni 28 kwa siku, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 110, ujenzi wa matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 10 sanjari na ujenzi wa kituo kimoja cha kusukuma maji *(booster station)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 16% na unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2026/2027 kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo mradi huo utanufaisha wananchi wapatao 460,885 waishio katika Wilaya za Rorya na Tarime.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Wambura, maswali ya nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na majibu ya kwamba mradi huu unatakiwa kukamilika ndani ya mwaka 2026/2027, lakini ninadhani wewe unafahamu kwamba mradi huu umesimama, mkandarasi hayuko *site*, na anadai zaidi ya shilingi bilioni saba ili aweze kurudi kuendelea kukamilisha kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mara ya tatu sasa ninasimama ndani ya Bunge hili kuulizia kuhusu mradi huu na mkandarasi hayuko *site* mpaka sasa. Ninataka nijue Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini mkandarasi huyu atalipwa hiyo shilingi bilioni saba ili aweze kurudi *site* aweze kukamilisha mkataba huu kwa muda ambao amepewa kwa mujibu wa mkataba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ni kwamba Wilaya ya Rorya imezungukwa na maji zaidi ya 77%, nchi kavu ni sehemu ya 23% peke yake, lakini katika vijiji 86, vijiji vyenye miundombinu ya maji ni 47 pekee yake, vijiji 39 havina miundombinu, na havina maji yoyote. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba Wilaya ya Rorya kwa ujumla wake sasa inapata miradi ya maji ili kuwanufaisha wananchi kwa ujumla wake?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri na kwa kuwasemea wana Rorya, na kwa mradi huu atakuwa anawasemea Wanarorya na Wanatarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu unatekelezwa kwa mfumo wa *design and build*. Maana yake ni kwamba, inapofikia upande wa ku-*design*, siyo lazima mkandarasi awe *site*, anaweza akaendelea ku-*design* wakati akiwa eneo lingine, baada ya kukamilisha kipande ambacho anaki-*design*

anahamia *site* kwa ajili ya kutekeleza. Kinachofanyika mpaka sasa, Wizara ya Maji ndani ya wiki mbili hizi mkandarasi tumemlipa shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inatambua umuhimu wa mradi huu na ndiyo maana tayari imeshatoa hizo fedha. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira ili mradi huu utekelezwe kwa ubora stahiki, lakini na thamani ya pesa. Tunafahamu kwamba kuna hamu na kiu ya wananchi wake kupata huduma hii ya majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria. Tutahakikisha kwamba watapata hayo majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Vijiji vya Rorya kama ambavyo amesema kwamba 77% vimezungukwa na maji, ni kweli kabisa. Nimtoe hofu, tunavyo vijiji 1,575, vikiwemo hivi vijiji 39 na tumeshaanza kuweka mpango kuanza kuhakikisha kwamba vijiji hivi ambavyo viko katika mpango wa miaka mitano, kila mwaka tutakuwa tunapunguza vijiji kadhaa, mpaka tutakapofikia katika *target* yetu ya mwaka 2030, tutakuwa tumekamilisha vijiji vyote ambavyo vitakuwepo Rorya na nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Nuru Kashakari aulize swali lake la nyongeza.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wilaya ya Uvinza, Jimbo la Kigoma Kusini, kuna miradi mikubwa minne ambayo imegharimu kiasi cha shilingi bilioni 15 ambayo ni Kijiji cha Kazuramimba, Kijiji cha Makizega, Kijiji cha Ilagala, na Kalenge. Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya majimbo yaliyokuwa na changamoto kubwa sana katika upande wa maji, Jimbo la Uvinza lilikuwa na changamoto kubwa sana. Kwa uwekezaji mkubwa katika jimbo hili na katika kijiji ambacho

amekitaja, Kijiji cha Kazuramimba, ambapo mimi nilifika katika tanki ambalo lilikuwa limejengwa likaachia. Tukarejea tena kufanya *design* nyingine na tukajenga tanki ambalo mpaka sasa liko imara kabisa na limeshaanza kutoa huduma ya majisafi na salama katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri ni kwamba katika eneo la Kazuramimba nilizunguka katika ile mitaa yote, nikajionea mpaka kwenye zile shule, na ninafahamu namna hali ilivyokuwa na sasa ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu katika maeneo ambayo yamebaki hayana majisafi na salama, tunao mkakati wa kuhakikisha sasa tunaenda kuyafungua maji ya lile Tanki la Kazuramimba ili maeneo yote ya shule yanayozunguka pale yapate huduma ya majisafi na salama, na miradi mingine ambayo tayari tumeiingiza kwenye bajeti, itaenda kuhakikisha kwamba inapunguza kwa ukubwa sana changamoto ya majisafi na salama katika Jimbo la Uvinza. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa *Eng.* Ramadhani Hamza Singano.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mji wa Soni ni miongoni mwa miji yenye changamoto ya maji, lakini kwa kuwa kuna chanzo cha uhakika cha Mto Mkuzu, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kumaliza changamoto hii mara moja?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasikia vizuri swali lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ramadhani Singano, tafadhali uliza tena swali lako. Ongeza sauti kidogo ili Mheshimiwa aweze kukusikiliza.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu ni kwamba, Mji wa Soni, Bumbuli, ni miongoni mwa miji yenye changamoto kubwa ya huduma ya maji, lakini kuna chanzo kikubwa cha uhakika cha Mto Mkuzu. Ni lini Serikali itaona umuhimu wa kumaliza changamoto hii kwa kutumia chanzo hiki cha uhakika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Singano kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya, lakini pia kwa kuendelea kutushauri yeye akiwa mdau wa Wizara ya Maji. Akiwa mtumishi wa Wizara ya Maji ameendelea kutupatia ushirikiano mzuri sana hasa kutatua changamoto katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu katika eneo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge ameligusia, tunayo mipango ya kuhakikisha kwamba tunaenda kutatua changamoto hiyo, lakini suala la lini, tutaenda kuingiza kwenye mpango wa bajeti ya mwaka 2026/2027 ili tuone namna ya kwenda kutatua tatizo hilo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Tarime una mahitaji wa lita za ujazo wa maji 4,830 lakini yaliyopo sasa hivi ni 2,175 tu, sawa na 45%. Hivyo, tulikuwa tunategemea kuna mradi wa muda mrefu wa Ziwa Victoria. Muda mfupi tuliomba, mwaka huu wa fedha milioni shilingi 140 ili kuweza kuongeza mtandao wa maji kwa Mtaa ya Saba Saba, Majengo na Ronsoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa kati tuliomba shilingi milioni 617 ili kuweza kuweka chujio kwenye chanzo cha Nyandurumo ambako mvua ikinyesha wale wanaopata maji, 45% maji ni machafu sana lakini mpaka sasa hivi wametuletea milioni 278 tu. Ile shilingi milioni 140 ya muda mfupi hawajaileta kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninauliza ni lini fedha hizi zitaenda, ili sasa huu mradi wa muda mfupi na muda wa kati uweze kukamilika, watu wa Mji wa Tarime wapate maji wakisubiria mradi huu wa Ziwa Victoria? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Mbunge ni suala la kisera la kuhakikisha kwamba wananchi wanapata majisafi na salama. Ili wapate majisafi na salama ni lazima tuwe na mtambo wa kuchuja ili kuhakikisha kwamba maji yanatibiwa na kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba tunayo miradi mingi inayoendelea kutekelezwa. Tutahakikisha tunapeleka fedha awamu kwa awamu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amekiri kwamba mpaka sasa Serikali imeshapeleka shilingi milioni 200 na kitu. Nimtoe hofu, kwa dhamira ya Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunafahamu kwamba wananchi wote na Wabunge wote wanayo mahitaji yao ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuweka vipaumbele katika miradi ambayo inaenda kugusa matokeo ya moja kwa moja ili iweze kutoa matokeo na kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba upatikanaji wa maji haya hasa kipindi cha masika *turbidity* inakuwa kubwa sana na hilo tunalitambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo msingi huo huo tulioutumia kuhakikisha kwamba angalau tunapeleka fedha kwanza za kuanza mradi huo ili ukiwa unaendelea, na mkandarasi akiwa anatoa hati za madai, na sisi tutaendelea kulipa bila kuwa na changamoto yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na imani na subira, wakati tunalifanyia

kazi, na litakapokamilika wananchi wake watakuwa na furaha ya kutumia majisafi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa tunaendelea, Wizara ya Viwanda na Biashara. Ninaomba nimwite Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 185

**Kufufua Kiwanda Musoma**

**MHE. MGORE M. KIGERA** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya kufufua viwanda vilivyotelekezwa muda mrefu ili kuleta ajira kwa Watu wa Musoma?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara ninaomba nijibu swali namba 185 kutoka kwa Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara ni moja ya mikoa ya kipaumbele katika suala zima la ufufuaji wa viwanda na ujenzi wa viwanda vipya. Katika mkoa huo, hasa Wilaya ya Musoma Mjini, kuna viwanda viwili ambavyo vilikuwa vinamilikiwa na Serikali ambavyo havifanyi kazi. Viwanda hivyo ni *MUTEX* na Kiwanda cha *Musoma Dair*y.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba viwanda hivi vinarudi katika uzalishaji, Serikali inaendelea kuangalia namna bora ya kufanya, ambapo baada ya tathmini ya kina ama mazungumzo, imekubalika kwamba kiwanda cha *MUTEX* kirejeshwe kwa mwekezaji wa awali kwa mkataba na masharti mapya. Majadiliano hayo yamefanyika na mkataba

uliowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye pia amefanya maboresho na kurejesha kwa Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho hayo yanaenda sambamba na tathmini ya kina kufanyiwa kazi, na ikikamilika, mwekezaji atakabidhiwa kiwanda ili mkataba mpya uanze kazi na shughuli za uzalishaji ziendelee. Aidha, Kiwanda cha *Musoma Dairy*, aliyekuwa mwekezaji wa awali ametuma maombi Serikalini akiomba arejeshewe kiwanda hicho ili aweze kuendeleza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa maombi hayo yanafanyiwa tathmini ya kina na mazungumzo yanaendelea ili yakikamilika tuangalie namna ya kufufuliwa kwa shughuli za Kiwanda hicho cha *Musoma Dairy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgore Miraji, maswali ya nyongeza.

**MHE. MGORE M. KIGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Musoma Mjini, kama ambavyo dhamira ya Serikali ni kukuza sekta ya viwanda kutoka 4.8% mpaka asilimia tisa ifikapo 2030, je, Serikali inatoa *commitment* gani kwa wananchi wa Musoma Mjini kwamba mwekezaji huyo atakapokabidhiwa kiwanda hicho, ataenda kufanya uzalishaji haraka iwezekanavyo ili wananchi hao waweze kupata ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wengi wamekuwa wakipata viwanda hivyo na kuvitumia kama *collateral,* na dhamira ya dhati ya kuwekeza viwanda hivyo inakuwa haipo, na Serikali inashindwa kutatua changamoto za ajira pamoja na uchumi kwa wananchi kwa maeneo yaliyo mengi hasa ya Musoma Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, mwekezaji wa Kiwanda cha Musoma *Dairy*, tangu aliponyang'anywa kiwanda hicho na Serikali mwaka 2018, leo ni miaka tisa, katika kiwanda

hicho kumefanyika wizi na ubadhirifu mkubwa sana, na kusema kumrudishia kiwanda hicho ili aweze kufanya *investment* ni kwamba tunadanganyana kwa sababu kiwanda hicho kwanza kina mkopo ambao mwekezaji alikopa *TIB Bank* na *PTA Bank*…

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa.

**MHE. MGORE M. KIGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni ni muhimu kushirikiana na mwekezaji huyo kutafuta *strategic investor* ambaye atakuwa na mtaji mkubwa wa kuwekeza katika kiwanda hicho?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera kwa jitihada kubwa ambazo anazifanya kuunga mkono sera ya ukuzaji wa viwanda katika nchi yetu na ongezeko la thamani ya mazao hasa katika Mkoa wa Mara hususan katika Wilaya ya Musoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameomba *commitment* ya Serikali kuhusiana na suala zima la uzalishaji pale ambapo mwekezaji huyu mpya atakapokabidhiwa kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikichukua kiwanda hiki kwa sababu ya kusuasua na kusimama kwa shughuli za uzalishaji. Mazungumzo ambayo tumeyafanya ni kuingia mkataba mpya wenye masharti mapya, ambayo yanamwelekeza mwekezaji huyu kuwa *committed* na hasa kwa upande wake pale ambapo hatatimiza makubaliano na Serikali, ambayo ni kuanza kwa uzalishaji pale ambapo atakabidhiwa kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninampa faraja Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali iko makini. Masharti ya mkataba huu mpya yanaenda kumlazimisha muwekezaji huyu kuanza shughuli za uzalishaji wa kiwanda hiki mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la *Musoma Dairy,* Serikali haina taarifa ya wizi na ubadhirifu, lakini kama upo,

hatuwezi kushirikiana na wezi na wabadhirifu katika kujadiliana namna bora ya kufufua kiwanda hiki. Sheria zipo na tathmini inaendelea kujua athari ambazo zimesababishwa na uwekezaji katika kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili liko kwa Msajili wa Hazina. Wizara ya Viwanda na Biashara inafuatilia kwa karibu kuona ni namna gani shughuli za kiwanda hiki cha maziwa zinarudi, ili kuongeza thamani ya mazao pale katika Mji wa Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru kwa majibu yako kwa maswali Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Sasa ninamwita Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 186

**Ufuatiliaji wa Maendeleo ya Wanafunzi Wanaofanya Vizuri Kitaifa**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufuatilia maendeleo ya Wanafunzi wanaofanya vizuri kitaifa ili kuhakikisha wanakuwa rasilimali muhimu kwa maendeleo ya Taifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inathamini na kufuatilia maendeleo ya wanafunzi wanaofaulu vizuri katika mitihani ya Kitaifa kwa kuwa, ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya nchi. Katika kutekeleza jitihada hizo, Serikali imeweka mpango mahsusi wa kubaini na kufuatilia maendeleo yao, sambamba na kuwaendeleza kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kupitia Mpango wa *Samia Scholarship* Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 imetoa ufadhili kwa wanafunzi 936 waliofaulu vizuri katika mitihani ya Kidato cha Sita, hususan katika masomo ya Sayansi na Hisabati. Lengo ni kuwaendeleza katika maeneo ya kimkakati katika sayansi, teknolojia, uhandisi na tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia ufadhili wa *Samia Scholorship Extended* jumla ya wanafunzi 50 wamepelekwa katika Chuo Kikuu cha Johannesburg, Afrika Kusini na Chuo Kikuu cha Limerick, nchini Ireland, kwa ajili ya kusomea masomo ya Sayansi ya Kompyuta, Hisabati ya Juu na Akili Unde *(Artificial Intelligence)*. Serikali itaendelea kuongeza wigo wa kufuatilia na kuwaendeleza wanafunzi wanaofanya vizuri katika mitihani ya Kitaifa ili waweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Taifa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juliana Shonza, maswali ya nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua jitihada kubwa ambazo zimefanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, hasa kupitia *Samia Scholarship*. Swali langu, nataka kujua kuhusu wale ma-*TO,* kwa maana ya wale wanafunzi ambao wanaibuka kuwa vinara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni baada ya mimi kuguswa sana na taarifa ya *TO* wa Mwaka 2006, Elias Kihombo, ambaye kwa bahati mbaya kwa sasa hivi ni Marehemu. Elias Kihombo alifanya kazi kubwa sana ya kuzunguka kwenye shule nyingi kufundisha na vilevile kufundisha *tuition* nyingi, lakini inaonekana alivyofika chuo, hakufanya vizuri, hali iliyosababisha ku-*disco*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaweza kuona kwamba, mtu ambaye ni *TO,* lakini akifika chuo ana-*disco*. Kwa hiyo, nataka nijue tu kwamba, ukiachana na hii *Samia Scholarship* toka mwaka 2000 mpaka sasa hivi, je, Serikali wana kanzidata ya *TO's* wangapi? Vilevile, je, wanajua kwamba, wako wapi na wanafanya nini? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunao wanafunzi wa kidato cha sita na vyuo vikuu ambao wanafanya vizuri zaidi kila mwaka. Serikali hii kwa kutambua umuhimu wao na kuwatumia katika ujenzi wa Taifa letu, imekuwa ikiwatambua, kwanza kwa kutoa zawadi mbalimbali na *certificates*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuhakikisha kwamba wanatambuliwa na kupewa ufadhili maalum katika vyuo vikuu kote nchini, na pia katika vyuo vikuu bora kabisa duniani, ili wapate utaalam mbalimbali ambao unakuja kusaidia ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2017 mpaka mwaka huu wa fedha 2025/2026 jumla ya wanafunzi waliofanya vizuri sana Kitaifa 1,113 wamepelekwa kwenye vyuo bora nje ya nchi na wanaendelea na masomo mbalimbali kwa lengo la kupata utaalam adhimu na kuja kutumia utaalam huo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza Serikali inatambua na inawafuatilia wanafunzi wote wanaofanya vizuri ili kuhakikisha wanapata fursa nzuri ya kujiendeleza na kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, Mheshimiwa Mbunge anahitaji kuona kanzidata ya mwaka 2020 mpaka sasa, ninaomba hili nilichukue na nitafute, kwa sababu, ni suala la

takwimu. Nitampa Mheshimiwa Mbunge, ili kuweza kutambua ni wangapi? Wako wapi? Wanafanya shughuli gani? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilikuona Mheshimiwa Najma Giga, swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu ya juu ni suala la Muungano. Je, Serikali ina mpango gani kwa wanafunzi ambao wanafanya vizuri sana kwa upande wa Zanzibar? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, suala la elimu ni la Muungano na ndiyo maana fursa hizi za wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi, wanaopelekwa kwenye vyuo vikuu bora kabisa duniani, wanatoka pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kupitia *Samia Scholarship*, ambayo imeleta ukombozi mkubwa sana kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo yao, imeendelea kuchukua wanafunzi kutoka pande zote za Muungano. Tutaendelea kuhakikisha kwamba, tunatoa fursa hizo ili wanafunzi wa pande zote waweze kunufaika na kujenga Taifa letu kwa ufanisi mkubwa zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea na Swali Na. 187. Sasa ninamwita, kwa niaba, Mheshimiwa Daniel Awack, Mbunge wa Karatu, aweze kuuliza swali.

Na. 187

**Kuanzisha Mkoa wa Kikodi, Wilaya ya Karatu**

**MHE. DANIEL A. TLEMAI K.n.y. MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanzisha Mkoa wa Kikodi katika Wilaya ya Karatu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, lililowasilishwa na Mheshimiwa Daniel Awack, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakupongeza sana kwa kazi nzito na nzuri unayoendelea kuifanya na pia kwa kazi nzuri ya kuwahudumia wananchi wa Karatu kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo. Hii dhana ya jimbo langu, jimbo langu, Karatu ninaona haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Mkoa wa Kikodi katika maeneo mbalimbali, ikiwemo Wilaya ya Karatu, hufanyika kwa kuzingatia vigezo vya kiutawala na kiuchumi ikiwa ni pamoja na kiasi cha mapato kinachokusanywa, idadi ya walipakodi, rasilimali zilizopo, pamoja na mahitaji ya huduma katika eneo husika. Lengo kuu ni kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongeza ufanisi na kusogeza huduma kwa walipakodi, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* imezipandisha hadhi baadhi ya wilaya za kikodi kuwa mikoa ya kikodi, ikiwemo Mkoa wa Kikodi wa Ilala, Kinondoni, Temeke, Kariakoo, Kahama, Tegeta na Pemba. Wilaya hizo zilizopewa hadhi ya mikoa ya kikodi, zina wastani wa jumla ya walipakodi, kwa mfano Ilala ni 906,399, Kinondoni 734,984, Temeke 563,568, Kariakoo 67,996, Kahama 82,054, Tegeta 136,164, na Pemba walipa kodi 28,076.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika katika mwaka 2023/2024 na 2024/2025 wilaya hizo zilikuwa na wastani wa mapato ya kodi shilingi bilioni 862 kwa Ilala, shilingi bilioni 774 kwa Kinondoni, shilingi bilioni 190 kwa Temeke, shilingi bilioni 136 kwa Kariakoo, shilingi bilioni 25.89 kwa Kahama, shilingi bilioni 101 kwa Tegeta na shilingi bilioni 16.36 kwa Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muundo wa kikodi wa sasa, Wilaya ya Karatu inatambulika kama Wilaya ya Kikodi, chini ya Mkoa wa kikodi wa Arusha, ndani ya Idara ya Kodi za Ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Aidha, Wilaya ina jumla ya walipakodi 4,672 ambao kwa kiasi kikubwa wanachangia ukusanyaji wa mapato ya kodi kutoka katika vyanzo za utalii, madini na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, takwimu zinabainisha ukuaji wa asilimia tisa nukta nne nane wa mapato ya kodi katika wilaya hiyo, kwa kuzingatia makusanyo yenye jumla ya shilingi bilioni 10.07 kwa mwaka 2023/2024 na shilingi bilioni 11.12 kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huu, Serikali kupitia *TRA*, itaendelea kutathmini na kufuatilia kwa karibu ukuaji huu wa mapato, ongezeko la idadi ya walipakodi na shughuli nyingine za kiuchumi katika Wilaya ya Karatu, ili vigezo vya kupewa hadhi ya Mkoa wa Kikodi vitakapokamilika, hatua stahiki ziweze kuchukuliwa, ikiwemo kutafuta rasimali muhimu za kufanikisha suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha inatambua kwamba, swali lako linalenga kudumisha na kuimarisha mapato ya kodi ya nchi hii kwa kupanua wigo na kuimarisha ufanisi wa vyanzo vilivyopo. Ninakupongeza kwa hatua hiyo, lakini Wizara ya Fedha itaendelea kuangalia uwezekano wa kuanzisha Mkoa wa Kikodi kwenye Wilaya ya Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Awack, maswali ya nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mwezi Oktoba, 2025, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliwaahidi wananchi wa Jimbo la Karatu na kuwaambia, kwa maombi ya Wanakaratu sasa itakuwa Mkoa wa Kikodi. Kwa kuwa, Karatu ni eneo la katikati ya utalii kwa watalii wanaoelekea Ngorongoro, Manyara na Serengeti na mwaka 2024/2025 Serikali kupitia *TRA*, katika Wilaya ya Karatu, wamekusanya shilingi bilioni 11.12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri imeonekana kwamba, Mkoa wa Kikodi wa Pemba wamekusanya shilingi bilioni 16 katika mwaka wa 2024/2025. Ukilinganisha inaonekana kwamba, inaweza kufananafanana kidogo, Karatu kuwa Mkoa wa Kikodi. Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2025 katika Jimbo la Karatu kwa wananchi wa Jimbo la Karatu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufasaha. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kwa mujibu wa takwimu inaonyesha kwamba, shilingi bilioni 11.12 zimekusanywa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na inakaribia kabisa yale mapato ambayo yamekusanywa na Pemba ya shilingi bilioni 16. Ahadi za viongozi, ikiwemo ahadi ya Mheshimiwa Rais pamoja na maelekezo yake, ni vipaumbele vya Serikali kiutekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, wako kwenye *threshold* inavyoonekana, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Karatu, jambo hili kwa kuwa liko katika hatua za mwisho za tathmini, nina imani, na mimi nitasimamia uanzishwaji wa Mkoa wa Kikodi pale Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua wingi wa watalii wanaopita pale Karatu na mapato ambayo pengine tunayakosa kutokana na kutokuwa na Mkoa wa Kikodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu yako. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Sasa ninamwita Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 188

**Malipo kwa Mkandarasi wa Barabara ya Mlandizi – *Ruvu Station***

**MHE. HAMOUD A. JUMAA** aliuliza: -

Je, lini Serikali italipa fedha za kuanza kazi kwa Mkandarasi wa ujenzi wa Barabara ya Mlandizi hadi *Ruvu SGR Station*, ili ujenzi uanze rasmi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mlandizi hadi Stesheni ya *Ruvu SGR*, yenye urefu wa kilomita 23, inaunganisha Barabara Kuu ya Morogoro, yaani *TANZAM,* katika eneo la Mlandizi na Stesheni ya *SGR* ya Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali imeingia mkataba na mkandarasi wa ujenzi wa barabara hiyo kwa utaratibu wa sanifu na jenga, yaani *design and build,* ambapo ujenzi wa barabara hiyo unatarajia kukamilika

mwezi Januari, 2028. Kwa sasa, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kumlipa mkandarasi malipo ya awali, ili aweze kuanza kazi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, maswali ya nyongeza.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini kuna swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, bado Serikali haijapata fedha, na kawaida wakati unakuwa na mambo makubwa; unakuwa na mpango wa muda mrefu na mpango wa muda mfupi. Sasa, barabara yetu hii kwa sasa haipitiki na ni barabara ambayo tunaitegemea kiuchumi. Je, Serikali ina mpango gani kwa sasa kuitengeneza hii barabara, ili iweze kupitika kwa muda wote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, barabara nyingi hasa ambazo zimejengwa kwa kiwango cha changarawe zimekuwa na changamoto katika kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamkumbusha Mheshimiwa Mbunge pia kwamba, barabara hii ilikuwa na vipande viwili. Kilomita hizi nyingine nane zilikuwa zinahudumiwa na wenzetu wa *TARURA* ambapo sasa zimeunganishwa kwa pamoja, na kuwa zinakwenda kujengwa na *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninatoa maelekezo kwa Meneja wa Mkoa wa Pwani kwamba, kwa kuwa stesheni ya *Ruvu SGR* wananchi wengi wanaitumia hasa wa Mkoa wa Pwani maeneo ya Kibaha na Mlandizi, ahakikishe barabara hii inapitika muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana leo ama kesho aweze kuitembelea hiyo barabara, ili maeneo yote ambayo yanaifanya isipitike aweze kuyasimamia na kuweka mkandarasi kwa haraka, ili wananchi ambao wanatumia hicho kituo cha *Ruvu SGR* waweze kupata hiyo huduma. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya mchepuko, kilomita 16, ndani ya Jimbo la Songea Mjini wananchi bado hawajalipwa fidia. Je, ni lini Serikali italipa fidia, ili ujenzi wa barabara hiyo uweze kuanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna barabara ya kilomita 16 ambayo sisi tunasema ni *Songea Bypass*. Barabara hii inajengwa na Serikali ya Tanzania kwa kusaidiana na *World Bank*. Tayari tumeshafanya uthamini wa wananchi ambao watapisha mradi huo ambao ni zaidi kidogo ya shilingi bilioni Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Ndumbaro pamoja na wananchi wa Songea kwamba tunategemea Serikali kulipa fidia hiyo ambayo tayari ipo Hazina ili mradi huo uanze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hiyo barabara ya *bypass* pia mkandarasi huyo ndiye atakayejenga kutoka Songea kilometa 100 kuelekea Njombe hadi Lutukira tayari ameshaanza kazi, yuko kwenye hatua za awali kwa maana ya *mobilization*, atakapokuwa anaendelea, basi tukishalipa ataanza pia kujenga hicho kipande cha *bypass* ili magari mengi yanayopita hapo na hasa ya makaa ya mawe kwenda huko Mtwara yasiweze kupita Songea Mjini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Zuena Bushiri, ajiandae Mheshimiwa Paschal Chinyele, ajiandae Mheshimiwa Asha Baraka.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Lembeni – Nyumba ya Mungu inayokwenda katika mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe haijawekwa lami. Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuweka lami katika barabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inatafuta fedha ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, tunachofanya ni kuhakikisha kwamba hiyo barabara inapitika. Kwa hiyo, ninamwagiza Meneja wa *TANROADS* kuhakikisha kwamba barabara hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge inapitika katika kipindi hiki hasa kwa dharura, lakini baada ya mvua kwisha, basi barabara hii iweze kujengwa katika hali ambayo inaweza ikapitika kwa muda wote. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Paschal Chinyele.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Serikali ipo katika hatua za mwisho za kufanya upanuzi wa barabara tatu zinazokwenda Mikoa ya Iringa - Singida pamoja na Arusha. Hata hivyo, Serikali bado hawajalipa fidia wakazi wa Jiji la Dodoma hasa katika Kata za Kikuyu, Mkonze, Mnadani, Nala, Chamwino, Mnadani pamoja na Miyuji. Je, Serikali ina mpango gani kuwalipa wakazi hao kabda ya upanuzi wa barabara hizi haujaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Chinyele kwa kufuatilia ulipaji wa fidia wa wananchi wake kwa wale hasa ambao watapitiwa na miradi ya kupanua barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ipo kwenye hatua za mwisho kuanza kujenga barabara ya njia nne

kutoka katikati ya Jiji kwenda njia ya Dar es Salaam, kwenda njia ya Arusha, na pia kwenda njia ya Iringa ili kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tumeshaanza kufanya uthamini kwa maana ya wananchi watakaopisha mradi, na tutahakikisha kwamba hatumbomolei mwanachi yeyote ambaye amefuatwa na barabara kabla hatujamlipa fidia. Kama kuna changamoto mahali popote kwenye Kata yoyote, Mheshimiwa Mbunge tunaomba tuwasiliane ili tuweze kufika na kuondoa changamoto kwa sababu ni utaratibu mwananchi yeyote anapopisha ujenzi wa barabara, anastahili kulipwa fidia, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Baraka.

**MHE. ASHA R. BARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Barabara Kibaha *DC* yenye kilometa 34 ni barabara ambayo haipitiki, siyo rafiki na ina vitu muhimu sana. Kuna Kituo cha Afya cha Halmashauri na kuna shule ya *Primary* yenye watoto wenye mahitaji maalum na pia kuna uwanja mkubwa sana ambao mikutano yote inafanyika hapo ya Kibaha *DC*, na shughuli zote ikiwemo na burudani. Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami? Ni lini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yake nimeyaelewa, lakini barabara aliyoitaja ndiyo sijaisikia vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Baraka, taja tu barabara.

**MHE. ASHA R. BARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inaitwa kwa jina maarufu Makofia – Mlandizi yenye kilometa 34 ambayo inaunganisha hospitali kubwa *dispensary* kubwa ambayo wanatumia watu wa Mlandizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa ameshakusikia. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Makofia – Mlandizi nadhani itakuwa ni swali la tatu ama la nne katika *session* hii ya Bunge kuulizwa. Barabara hii tumeijibu na tutaendelea kujibu kwamba ni barabara ambayo ni muhimu sana kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tulikuwa tumefanya tathmini ya fidia awali, lakini ikaonekana muda umepita. Tumefanya tena uthamini upya ambao jedwali la malipo ya fidia iko Hazina kwa ajili ya kuwalipa hao wananchi ambao watapisha barabara ili hii barabara iweze kujengwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itaunganisha kwa lami kati ya Kijiji cha Ihemi na Kijiji cha Mgama ambapo kuna kilometa kama sita hivi zilizobaki? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili pia liliulizwa na Mbunge wa Kilolo ambayo nadhani hiyo barabara ikitoka Ihemi – Mgama inaenda pia na Kilolo. Ni barabara ambayo inahudumiwa na wakala wetu na iko kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunatafuta fedha ya kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, tunachoweza kumwahidi Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tutahakikisha kwanza inapitika kwa kipindi chote cha mwaka wakati Serikali inatafuta fedha ili kuweza kukamilisha usanifu na kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa aweze kuuliza swali lake.

Na. 189

**Ujenzi wa Barabara ya Makongolosi hadi Rungwa**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa barabara kutoka Makongolosi hadi Rungwa kwa kiwango cha lami utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Makongolosi – Rungwa (km 176.51) ni sehemu ya barabara ya Mbeya – Rungwa (Km 288.9). Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa ujenzi wa sehemu ya Mbeya - Makongolosi (km 112.39) kwa kiwango cha lami umekamilika. Kwa sehemu iliyobaki, yaani Makongolosi – Rungwa (km 176.51) Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, swali la nyongeza. Waheshimiwa mliowasha *mic* tafadhali tunaomba mzime wote.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Serikali ambapo kila mwaka wakati swali hili linapoulizwa, majibu ni haya haya. Kipande cha barabara ambacho kinazungumzwa sasa hivi ambacho kimeshajengwa kuanzia Mbeya – Chunya – Makongolosi kilishakamilika takribani miaka 10 imeshapita, kwa sasa hivi barabara hiyo imeshaanza kuharibika hasa kipande cha Mbeya – Lwanjilo kina mashimo mengi na kimeanza kuwekewa viraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, swali la msingi, ni lini Serikali itaanza kujenga kipande cha barabara kuanzia Makongolosi –

Rungwa, barabara hii inayounganisha Mkoa wa Mbeya, Singida pamoja na Tabora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, barabara ya kuanzia Igawa inayopita Mbeya Mjini – Tunduma, imechakaa, imekwisha na ni barabara mbaya sana. Tutambue barabara hii ndiyo barabara moja Tanzania kwa maana *T1* inayopitisha mizigo takribani asilimia 40 inayotoka Bandari ya Dar es Salaam. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa barabara hii na kutoa fedha ili barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara tunayoisema ya Mbeya – Makongolosi – Rungwa – Itigi na Rungwa – Ipole hadi Tabora ni moja ya barabara ndefu katika nchi yetu ambazo ni *trunk*. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi la Serikali, ni kwamba tumeanza kuijenga kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbeya tumeshajenga hizo kilometa 112, lakini barabara hiyo inakwenda Singida, ambapo tunavyoongea sasa hivi wako wakandarasi wameanza Singida kutoka Mkiwa Manyoni wakija Naronga ambapo mwelekeo ni kwenda Rungwa kuja Makongolosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mbunge kwamba Serikali tunatafuta chanzo ambacho kitakuwa cha uhakika ili kuweza kuunganisha mikoa hiyo mitatu ya Tabora, Singida na Mbeya. Kwa sasa kabla hatujapata chanzo cha uhakika kujenga barabara yote, ndiyo maana tunakwenda kwa awamu, tukiwa na uhakika kwamba tunatafuta chanzo cha uhakika ambacho tutaijenga hiyo barabara yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, ni kweli kwamba barabara kubwa katika nchi yetu ni *T1* TanZam, Dar es Salaam – Morogoro – Iringa – Mbeya – Tunduma. Barabara hii iko kwenye mipango hasa kipande cha Igawa – Mbeya – Tunduma ni barabara ambayo tumeamua kuijenga kwa ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoongea sasa hivi, Serikali ipo kwenye majadiliano ya mwisho na watu ambao wameonesha utayari wa kusaidiana na Serikali kujenga hiyo barabara ya Igawa – Mbeya – Tunduma njia nne kwa utaratibu wa ubia. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mbunge, Serikali inalifanyia kazi na tuna hakika tutafika pazuri ili barabara hiyo iweze kujengwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilikuona Mheshimiwa Hawa Chakoma, ajiandae Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, na Mheshimiwa Amosy Maganga.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya Bungu – Nyamisati ni barabara ya muda mrefu, ina historia na inaunganisha Majimbo matatu; Jimbo la Mafia, Jimbo la Kibiti na Jimbo la Mkuranga. Ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii tumeshakamilisha usanifu wa kina, Bungu – Nyamisati na ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na kuunganisha, lakini barabara hii ndiyo inayopeleka watu wa Kisiwa cha Mafia. Kwa hiyo, Serikali tumeshafanyia usanifu na tusubiri bajeti tuone tutakuwa tumeipangia nini kwa maana ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Barabara ya Tabora – Mambali – Shinyanga, barabara hii ujenzi wake umekuwa ukisuasua na hususan kwenye kipande cha kutoka Tabora Mjini kuelekea Bukene. Umuhimu wa barabara hii kwa wananchi wangu wa Kata ya Misha, Kalunde pamoja na Kata ya Kabila ni mkubwa sana. Ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii ili iweze kunufaisha wananchi wa maeneo wa hayo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hii barabara ya Tabora – Mambali – Bukene Nzega ni kweli tumeanza kufanya kwa kiwango kidogo japo tulianza upande wa Bukene, lakini ni barabara ambayo hata ukienda kwenye vitabu vyetu vya bajeti, tumeitambua na tukaipangia kuwa kwenye mpango wa kuijenga. Sasa kitakachojitokeza ni bajeti, ikiruhusu, basi tutaanza kwa sababu tayari ipo kwenye mipango yetu ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Amosy Maganga.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi hii. Barabara ya kutoka Ipole – Rungwa imekuwa kwenye ahadi ya Serikali ya kujengwa kwa kiwango cha lami kwa zaidi ya miaka 30 sasa. Hebu Serikali sasa iwaambie wananchi hao wa Kata za Ngoywa, Kitunda, Kiloli, Kirumbi pamoja na Kipili kwamba sasa kwa mwaka wa fedha ujao 2026/2027, Serikali sasa inaenda kutekeleza ahadi hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ni sehemu ya barabara ambayo ipo kwenye swali la msingi ambayo ni Mbeya – Makongolosi – Rungwa – Kitunda – Ipole na hiki kipande alichokitaja nadhani nimekielezea kwamba tunatafuta fedha kuunganisha Mkoa wa Tabora kuja Rungwa, Singida kuja Rungwa na kwenda Makongolosi kilometa hizo 172 Ipole – Rungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama nilivyosema wakati najibu swali la mwuliza swali la msingi, ni kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa kweli kuijenga hiyo barabara. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba hata katika bajeti itakayokuja, tutakuja na mapendekezo ya kuomba ianze kujengwa kwa kiwango cha lami, kipande hicho cha Ipole – Rungwa na kwenda Makongolosi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Regina Mikenze, swali dogo la nyongeza.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niulize swali la nyongeza. Wilaya ya Nyang'hwale ndiyo Wilaya pekee katika Mkoa wa Geita ambayo haina barabara yoyote ya kiwango cha lami inayounganisha Wilaya hiyo na Wilaya nyingine ikiwemo Makao Makuu ya Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lini Serikali itatujengea barabara kwa kiwango cha lami katika Wilaya hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge na ninatambua kwamba hili swali tumelijibu mara kadhaa kuhusu barabara ya lami aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge. Barabara hii ipo kwenye utaratibu kwa sasa wa kuisanifu kuanzia Busisi – Ngoma - Nyang'hwale hadi Nyambura na pia kutoka Nyang'hwale kwenda Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha usanifu, gharama zitajulikana, na sasa ndiyo tutakuja na mpango wa kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia na swali letu la mwisho linaloelekezwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Sasa ninamwita Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mbunge wa Serengeti aweze kuuliza swali lake.

Na. 190

**Fidia kwa Waathirika wa Wanyamapori**

**MHE. MARY D. SURATI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fidia kwa wakati kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary, Mbunge wa Serengeti kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikilipa kifuta jasho na kifuta machozi kama mkono wa pole au faraja kwa wananchi wanaopata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu, kwa lengo la kuimarisha mtazamo chanya kwa wananchi juu ya shughuli za uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori nchini. Malipo hayo yamekuwa yakifanyika kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za Mwaka 2011 na marekebisho yake ya mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha utaratibu wa kushughulikia masuala ya wanyamapori wakali na waharibifu, Serikali imeanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa *PAIS (Problem Animal Information System),* ambao utawezesha kurahisisha ukusanyaji na uwasilishaji wa taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa wakati, kuongeza kasi ya uchakataji na uhakiki wa taarifa zinazowasilishwa, kuwezesha malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi kufanyika kwa wakati, na kupunguza udanganyifu wa taarifa zinazowasilishwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Daniel, swali la nyongeza.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa juhudi zote ambazo zimekuwa zikifanyika kutokana na changamoto ya wanyamapori hao, hasa Simba. Hata hivyo, nilikuwa nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, kutokana na takwimu za Wizara ya Maliasili na Utalii, ambazo zinatamka wazi kwamba, wananchi wanaopatikana katika Hifadhi ya Serengeti ndiyo ambao wanaathiriwa zaidi na wanyamapori kuliko hifadhi nyingine zote, ukizingatia tuna Ikorongo *Game Reserve*, Grumeti, Ilona pamoja na Serapa, je, kwa sasa hivi ambavyo nyumbu wanaanza sasa kurudi huku kutoka Maasai Mara, Wizara

imejiandaaje kutusaidia magari ya Sepali maana tembo wale wote huwa hawapendi ule mlio wa wale nyumbu na wanaanza kurudi kwenye makazi ya wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu namba mbili. Kumekuwa na ucheleweshwaji wa malipo ya fedha za *open area,* ambapo Vijiji vya Makundusi pamoja na Robanda havijapewa fedha hizo za malipo ya *open area* kuanzia Julai, 2025 mpaka hivi sasa tunavyozungumza. Hii inasababisha wananchi kutaka kurudushiwa maeneo yao ili waendelee kufanya shughuli zao za kiuchumi, hali ambayo inaweza ikazoofisha shughuli zetu za uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anaenda kulijibu swali hili kwamba…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa swali, umeshauliza maswali.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini wananchi hawa wanakwenda kulipwa fedha hizo? Ninaomba akumbuke Hifadhi ya Serengeti…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mary, maana salamu yake siku zote ni ufuatiliaji wa suala hili. Kwa hiyo, ninampongeza sana kwa ufuatiliaji wake. Mara zote basi yeye unamkuta yupo Ofisini kwa ajili ya kufuatilia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nikiri kuwa ni kweli kwa alichokisema Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hii imechelewa kwa kipindi fulani. Ninaomba nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge, fedha hii kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha inaenda kulipwa na Serikali ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu uhaba wa vitendea kazi ambao ameuzungumza, Serikali imeanzisha juhudi

mbalimbali. Hivi ninavyozungumza, Serikali imenunua gari maalum ambalo linajulikana kama *Mobile Veterinary Clinic*. Gari hilo litapelekwa katika sehemu zote ikiwemo eneo la Serengeti. Vilevile tutaongeza idadi ya ndege nyuki ili kuhakikisha kwamba wale wanyama wakali na waharibifu wanarejeshwa katika sehemu yao ya hifadhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Ninaomba kuwataarifu kwamba Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Waziri wa Madini ndiye anayekaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni kuanzia leo tarehe 24 Aprili, 2026. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwaletee tangazo la wageni waliopo Bungeni asubuhi ya leo. Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, kwanza ni wageni sita wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Mkoa wa Manyara ambao ni Ndg. Fredrick Gidano, Ndg. Sophia Adam, Ndg. Agatha Sighis, Ndg. Petronila Joseph, Ndg. Paskali Saragu, na Ndg. Haqwan Shabadi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Dkt. Juma Zuberi Homera, Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni Ndg. Eliakim Maswi, Katibu Mkuu; Ndugu Dkt. Franklin Rwezimula, Naibu Katibu Mkuu; Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama; Mheshimiwa Eva Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama; Ndugu Victor Kategere, Mtendaji wa Mahakama ya Rufani; Mheshimiwa George Herbert, Msajili wa Mahakama ya Rufani; Ndg. Sylivester Mwakitalu, Mkurugenzi wa Taifa wa Mashtaka; Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali; na Mheshimiwa Winifrida Korosso, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania.

Wengine ni Prof. Sist Mramba, Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo *(Law School of Tanzania);* Mheshimiwa Dkt. Mary Levira (Jaji), Mwenyekiti wa Baraza la Chuo cha Uongozi

wa Mahakama, Lushoto; Dkt. Paul Kihwelo, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto. Karibuni sana. (Makofi)

Vilevile tunao Ndugu George Mandepo, Katibu Mtendaji Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Ndugu Samweli Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ndugu Frank Kanyusi, Mtendaji Mkuu na Kabidhi Wasii wa Mawakala wa Ufilisi na Udhamini *(RITA);* Ndugu Patience Ntwina, Katibu Mtendaji Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Ndugu Rehema Katuga, Kaimu Mwandishi Mkuu wa Sheria; na Mheshimiwa Odo Mwisho, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Ruvuma.

Wengine ni Mheshimiwa Hemed Chale, *MNEC,* Mkoa wa Ruvuma; Ndugu Mary Makondo, Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma; Mheshimiwa Ngollo Malenya, Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo; na Ndugu Philimoni Magesa, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo. Karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Tunao Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Jasmine Homera, mke wa Mheshimiwa Waziri. Karibu sana wifi yetu. *(Makofi)*

Vilevile tunao Ndugu Jian Homera, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Jihanprinsess Homera, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Jureen Homera, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Afreen Homera, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Naureen Homera, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Elizabeth Mallya, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Siraju Ponera, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Mwajuma Homera, dada wa Mheshimiwa Waziri. Karibuni sana familia ya Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni. *(Makofi)*

Tunao Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ambao ni Wawakilishi kutoka *British High Commission, UNDP, UN Women* na *UNICEF* kutoka Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Wawakilishi kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Chama cha Wanasheria Tanganyika *(TLS)*. Karibuni. *(Makofi)*

Tunayo pia Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi ya Wilaya ya Namtumbo. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninajulishwa kwamba hapa Mheshimiwa Winifrida Korosso, Mheshimiwa Paul Kihwelo na Mheshimiwa Levira, hawa ni Majaji wa Mahakama ya Rufani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge, tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini, Ndugu Abedi Mollel, mpiga kura wake kutoka Longido Mkoani Arusha. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni 16 wa Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, ni wapiga kura wake wakiongozwa na Mwenyekiti wa CHAUMA, Ndugu Syrus Mwongi kutoka Segerea Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Tunao Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanafunzi 101 na walimu sita wa Shule ya Sekondari ya Wasichana *St. Monica* kutoka Jijini Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanachama 60 wa Shirika la *International Peace Information* wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Shirika Dkt. Judith Mollel kutoka Mkoani Dr es Salaam. Karibuni Wageni wetu wote hapa Bungeni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuwasilisha Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria Bungeni, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, kwa kuniruzuku uhai na afya njema iliyoniwezesha kusimama hapa leo katika Bunge lako Tukufu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria, Mahakama ya Tanzania pamoja na taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti zilizochambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na kujadili, kupitisha Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba Sheria na taasisi zake pamoja na Mahakama ya Tanzania kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Ninaahidi kuitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na unyenyekevu kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Ninamwomba Mwenyezi Mungu anijalie hekima, busara, ujasiri ili niweze kutimiza wajibu huu mkubwa niliopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, ninatoa pole kwako katika Bunge lako kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu waliotangulia mbele ya haki, ambao ni Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, na Mbunge wa Jimbo la Isimani. Pia Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Mheshimiwa Halima

Iddi Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Mwakilishi wa Wawafanyakazi kutoka vyama vya wafanyakazi Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika sekta ya sheria pia tumeondokewa na Mheshimiwa Julie Catherine Manning aliyekuwa Mwanamke wa Kwanza Tanzania kusoma Shahada ya Sheria na aliyewahi kuwa katika nafasi ya Waziri wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa na Watanzania ili kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatua inayoonyesha imani waliyonayo kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nimpongeze kwa uongozi wake mahiri, thabiti na wenye maono ya mbali uliowezesha mafanikio katika sekta mbalimbali, hususan sekta ya sheria, kwa kuweka mifumo thabiti ya kisera, kisheria, na kitaasisi. Mifumo ambayo imewezesha kuimarika kwa utoaji na upatikanaji wa haki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tuendelee kumwombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, amjalie afya njema, hekima, na busara katika kuendelea kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Uongozi na maelekezo yao thabiti yanaimarisha zaidi utekelezaji wa majukumu ya sekta ya sheria kuwa kichocheo cha maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake iliyoweka msingi imara wa mwelekeo wa kisera kwa Taifa letu kwa mwaka

wa fedha 2026/2027. Sambamba na pongezi hizi, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote waliotangulia kuwasilisha hotuba zao hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, ninakupongeza kwa kuchaguliwa na Bunge kuwa Mwenyekiti wa Bunge katika Bunge hili Tukufu. Aidha, ninaomba nimpongeze pia Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Damas Daniel Ndumbaro kwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa George Mchechu Masaju kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. Uteuzi wake unadhihirisha umahiri na uzoefu alionao katika sekta ya sheria kwa ujumla ikiwemo mhimili wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninamshukuru sana Mheshimiwa Hamza Said Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa jinsi anavyonipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya Wizara pamoja na utaratibu na usimamizi wa sekta ya sheria kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Zainab Athmani Katimba, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, nitumie fursa hii tena kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala,

Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hizi zinafanya kazi kubwa za kuchambua na kushauri Mpango ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfumo wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2026/2027 katika kutambua na kuthamini mchango wa Kamati hizi katika kuhakikisha kuwa sekta ya sheria inabaki kuwa kiungo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maono na mageuzi katika sekta ya sheria, hotuba hii inawasilisha mbele yako leo katika Bunge lako Tukufu imebeba ujumbe, msingi wa mustakabali wa Taifa letu. Ujumbe huo umeanisha masuala ya msingi katika Sekta ya Sheria nchini yatakayoichangia katika kufikia matarajio yanayoainishwa katika Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ujumbe huo, tunaamini kwamba hakuna maendeleo endelevu bila mfumo imara wa kisheria, hakuna uchumi shindani bila utawala wa sheria, pia hakuna Taifa lenye utulivu bila haki kwa wote. Kwa mantiki hiyo, Sekta ya Sheria siyo tu ni mhimili wa utawala bora, bali ni miundombinu inayoonekana inayoshikilia misingi ya uchumi, uwekezaji, na umoja wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, mwelekeo wa Sekta ya Sheria ni kusimama katika nafasi ya kimkakati kama mlinzi mkuu wa utawala wa kikatiba, utawala wa sheria na haki, na kichocheo cha maendeleo ya uchumi wa Taifa katika kufikia malengo ya Dira 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba inayowasilishwa leo haiainishi tu takwimu za kibajeti, inabainisha dira yenye mfumo wa mageuzi ya Sekta ya Sheria nchini, mwelekeo wa kiitifaki wa kujenga Serikali imara inayozingatia utawala wa sheria, na mkakati wa kuifanya Sekta ya Sheria kuwa mhimili mkuu wa maendeleo ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hotuba hii ni mwelekeo wa kimkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kuitumikia na kuipa

nafasi Sekta ya Sheria nchini ili ichangie kikamilifu kwenye ujenzi wa Taifa letu kwa maslahi mapana ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zama hizi za ushindani wa Kimataifa na uchumi wa kisasa, nguvu ya Taifa haipimwi tena kwa rasilimali zake za asili pekee, bali inapimwa kwa uimara wa taasisi zake, ufanisi wa mifumo yake ya utoaji haki, na uwezo wake wa kusimamia sheria katika kuleta amani, utulivu, maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii hususan katika upatikanaji haki kwa wakati na kwa watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, Sekta ya Sheria inachukua nafasi mpya kabisa katika historia ya Taifa letu. Siyo tena kama msimamizi wa sheria pekee, bali kama injini ya uthabiti wa Taifa na kichocheo cha maendeleo ya uchumi katika kufikia Dira ya Maendeleo ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwelekeo mpya na mageuzi katika Sekta ya Sheria, ninaomba kutumia fursa hii kutoa shukrani za dhati na za kipekee kwa uongozi wa juu wa Taifa letu ambao umeendelea kuweka msingi imara wa mageuzi tunayoyazungumzia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna moja au nyingine, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake madhubuti wenye dira, na wenye uelewa mpana wa nafasi ya sheria katika maendeleo ya Taifa letu. Mheshimiwa Rais ameweka msingi wa mageuzi ya kweli kwa mfumo katika Sekta ya Sheria kama ilivyooneshwa katika Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuanza kwa kusisitiza kwamba, msingi mkuu wa Dira 2050 ambao ni utawala, amani, usalama, na utulivu, na siyo kauli ya mapambo ya sera, bali ni uamuzi wa kimkakati wa Taifa letu uliofanywa kwa ujasiri na uongozi wa juu wa nchi hii. Huu ni msingi unaobeba hatima ya Tanzania ya kesho tuitakayo. Ni msingi unaotofautisha Taifa linalokua kwa bahati na Taifa linalojengwa kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muktadha huo, bajeti ya mwaka 2026/2027 inayowasilishwa leo siyo tu chombo cha kugawa rasilimali, bali ni nyenzo muhimu ya kutekeleza falsafa hii ya Taifa ya kujenga Tanzania juu ya misingi isiyotetereka ya utawala wa sheria, amani endelevu, usalama wa uhakika, na utulivu wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Bunge lako Tukufu litambue kuwa kwa mara ya kwanza katika historia ya maendeleo ya Taifa letu, Sekta ya Sheria imewekwa katikati ya mjadala wa uchumi wa Taifa. Hii ni hatua ya kihistoria. Tumetoka katika mtazamo wa kuiona sekta hii kama mtumiaji wa rasilimali, na sasa tunaijenga kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi nchini, mlinzi wa uwekezaji, nguzo ya kuaminika ya utulivu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna uchumi wa kisasa unaoweza kustawi bila uhakika wa sheria, hakuna mwekezaji anayeweza kuwekeza bila ulinzi wa haki, na hakuna maendeleo ya kweli bila mifumo ya haki inayofanya kazi kwa ufanisi na kwa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi huu wa Dira 2050 unataka tufanye mageuzi ya kina na mifumo. Serikali inaendelea kuimarisha taasisi za utoaji haki, kuongeza upatikanaji wa huduma za kisheria kwa wananchi wote ili kuharakisha matumizi ya teknolojia katika mfumo wa sheria ili kuongeza uwazi, ufanisi, na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tutaendelea kuimarisha na kusimamia uwazi, ufanisi, na uwajibikaji na tutaendelea kusimamia mifumo mbadala ya Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala *(Altenative Disputes Resolution - ADR)* ili kupunguza mzigo katika Mahakama na kuharakisha haki kwa wananchi. Hayo yote ni sehemu ya kujenga Taifa ambalo sheria siyo kikwazo, bali ni daraja la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia utawala, amani, usalama, na utulivu tunazungumzia pia ujenzi wa imani ya wananchi kwa Taifa lao. Taifa lenye utulivu siyo lile lisilo na changamoto, bali ni lile lenye mifumo imara ya kushughulikia

changamoto hizo kwa haki na kwa wakati. Kupitia bajeti hii, Serikali inalenga kuimarisha mshikamano wa Taifa, kulinda haki za wananchi, na kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anahisi uwepo wa Dola inayomtambua, inayomlinda, na inayomhudumia kwa usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu pia kusisitiza kuwa msingi huu wa Dira 2050 siyo jukumu la Serikali pekee, ni wajibu wa pamoja unaohusisha Bunge lako Tukufu, Mahakama, Sekta Binafsi, asasi za kiraia, na taasisi za dini. Taifa lenye amani na utulivu hujengwa kwa misingi ya maadili, kuheshimu sheria, na uwajibikaji wa pamoja. Hivyo, utekelezaji wa msingi huu unahitaji mshikamano wa Kitaifa, dhamira na malengo ya pamoja, na uongozi thabiti unaoongozwa na msingi wa haki na uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uongozi wa juu wa Taifa tayari umefanya uamuzi huu wa kihistoria wa kujenga Tanzania imara kupitia utawala wa sheria, sasa ni jukumu letu kuhakikisha kuwa uamuzi huu unatekelezwa kwa vitendo, kwa uthabiti, na kwa matokeo yanayoonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ninaomba Bunge lako Tukufu liunge mkono bajeti hii, siyo tu kama bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, bali kama chombo cha Taifa cha kulinda na kuimarisha msingi wake mkuu wa maendeleo. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeweka jiwe la msingi imara kuelekea Tanzania yenye amani ya kudumu, usalama wa uhakika, utawala bora, na maendeleo jumuishi ifikapo mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dira na dhima ya kauli mbiu yetu. Dira ya Wizara ya Katiba na Sheria ni kuwa na Taifa linalozingatia haki, jumuishi, na lenye ustahimilivu ambapo usawa na uadilifu na utawala wa sheria vitatawala kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dhima ya Wizara; kuweka mifumo madhubuti ya Kikatiba na kisheria, kuendeleza upatikanaji wa haki, kulinda haki za binadamu, na kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali asilia kwa maendeleo ya kijamii, kiuchumi ya Tanzania. Vilevile, Wizara ina Kauli mbiu ya "Haki, Usawa, na Utawala wa Sheria kwa Wote."

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria yameainishwa kwenye Ibara ya 24 na 25 katika Kitabu cha hotuba yangu. Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ulizingatia dira, miongozo mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 26 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kipaumbele yaliyobainishwa katika bajeti ya mwaka 2025/2026 yameainishwa kwenye Ibara ya 27 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mwenendo wa bajeti ya fedha iliyopokelewa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Makusanyo ya maduhuli katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara, Mhimili wa Mahakama, pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 15,680,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 – Machi, 2026, Mhimili wa Mahakama, na taasisi za zimekusanya jumla ya shilingi bilioni 5.32 sawa na 33.9% ya lengo la makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026, na 45.3% kwa lengo la kipindi cha miezi tisa. Sababu ya kutofikiwa lengo la makusanyo ya maduhuli ni kupungukiwa kwa washtakiwa waliohukumiwa na kutozwa faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, Mhimili wa Mahakama, na taasisi za Wizara, iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 687.69 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha ya hizo, shilingi bilioni 135.99 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 389.46 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na shilingi bilioni 132.24 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizopokelewa katika kipindi cha Julai, 2025/2026, Mhimili wa Mahakama na taasisi za Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 526.62 sawa na 77% ya bajeti ya shilingi bilioni 687.69 iliyoainishwa. Katika fedha hizo, shilingi bilioni 105.64 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, shilingi bilioni 297 ni

kwa ajili ya matumizi mengineyo, na shilingi bilioni 123.71 ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 umezingatia vipaumbele vilivyowekwa na Wizara katika mwaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuimarika kwa huduma za msaada wa kisheria kwa watu wenye uhitaji. Msaada wa kisheria ni nguzo muhimu katika kulinda haki za wananchi na kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wote, hususan kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za uwakilishi katika vyombo vya utoaji wa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 – Machi, 2026, jumla ya wananchi 7,462,387 walifikiwa na kupatiwa huduma za msaada wa kisheria. Aidha, kupitia afua hiyo, jumla ya migogoro 5,209 ilipokelewa ambapo kati ya hiyo migogoro 2,545 ilihitimishwa, na 2,664 iliendelea kufanyiwa kazi katika vyombo mbalimbali vya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 – Machi, 2026, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria katika maeneo ya vizuizi kwenye mikoa minne; Mara, Mwanza, Shinyanga, na Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji huu ulibainisha kuwa, kupitia utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria, kati ya wafungwa na mahabusu 3,847 waliofikiwa katika magereza 18 katika mikoa tajwa, jumla ya wafungwa na mahabusu 1,377 waliachiwa ndani ya kipindi cha miezi minne kupitia huduma ya *parole* au kupatiwa adhabu mbadala nje ya gereza baada ya kukamilisha taratibu kwa mujibu kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa kampeni ya msaada wa kisheria *(Mama Samia Legal Aids Campaign)* awamu ya kwanza, Wizara imekamilisha mkakati wa utekelezaji wa Awamu ya Pili wa *MSLAC*

*II* utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2026/2027 – 2029/2030).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu unalenga kuimarisha mafanikio yaliyopatikana na kushughulikia changamoto zilizojitokeza katika awamu ya kwanza. Hakika msaada wa kisheria tutakwenda nchi nzima kuhakikisha kwamba wananchi wananufaika na Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kushughulikia masuala ya kikatiba pamoja na kutoa Elimu ya Katiba na Uraia kwa Umma; Wizara inatambua kuwa, msingi imara wa utawala bora, haki, na maendeleo endelevu ya Taifa letu unategemea uwepo wa mfumo madhubuti wa Kikatiba unaoeleweka na unaoheshimiwa na wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha Julai 2025 – Machi 2026, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) imechopeka maudhui ya Katiba na uraia katika mitaala ya shule za awali, msingi, na sekondari, kwa ajili ya kuendelea kufundisha. Aidha, Wizara imeandaa Hati ya Makubaliano na Chuo Kikuu Mzumbe kwa lengo la kuandaa maudhui ya Kikatiba na maadili katika mitaala ya chuo hicho ili yaanze kufundishwa katika Somo la Katiba na Maadili Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi imekamilisha uandaaji wa maudhui ya Elimu ya Katiba na Uraia yatakayofundishwa katika vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi katika somo la Stadi za Maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mwongozo wa kuifundishia Elimu ya Katiba na Uraia na nyenzo za ufuatiliaji na tathmini vimeandaliwa. Vilevile, jumla ya wakufunzi 26 na walimu 80 kutoka katika kanda zote tisa za *VETA* wamepatiwa mafunzo. Somo hili limeanza kufundishwa rasmi Machi, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Mifumo ya Haki Jinai inaimarika, Serikali imeendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume ya kuangalia namna ya kuboresha Taasisi

za Haki Jinai Nchini. Maboresho hayo yamejikita katika kuhakikisha kuwa mifumo ya kisheria, kimuundo, na kitaasisi inaboreshwa ili Taasisi za Haki Jinai ziweze kutekeleza majukumu yaliyoainishwa kwa ufanisi na kwa weledi mkubwa. Hivyo, Haki Jinai inapatikana kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 – Machi, 2026, Wizara imeandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Haki Jinai pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera. Ni matarajio ya Serikali kuwa, sera hiyo itatoa mwongozo wa jumla kuhusu namna ya kufanyia kazi masuala ya haki jinai ili kuimarisha utawala bora na hivyo kufikia malengo ya Serikali yaliyomo kwenye mipango ya Kimataifa na Kitaifa ambayo Serikali imeridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa Wizara umeboreshwa kwa kuanzisha Divisheni ya Ulinzi wa Watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi. Lengo la kuanzishwa kwa divisheni hiyo ni kutoa ulinzi na motisha na kulipa fidia kwa watoa taarifa fiche za uhalifu na mashahidi ili kuwaongezea imani, kuimarisha usalama, na hivyo kuwezesha ushahidi kupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali inajenga Mfumo Jumuishi wa TEHAMA wa Haki Jinai *(Criminal Justice Single Window System)* kwa lengo la kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inasomana kulingana na majukumu ya kila mdau wa Haki Jinai, na hivyo kurahisisha utendaji wa majukumu ya kuimarisha uwazi miongoni mwa Taasisi za Haki Jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imefanya mapitio ya muundo wake na kuanzisha kitengo kinachoshughulikia Taasisi za Haki Jinai kama ilivyopendekezwa na Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo hicho kimeanza kutekeleza majukumu yake ambapo katika kipindi cha Julai, 2025 – Machi, 2026, jumla ya malalamiko 69 yanayohusu ucheleweshwaji wa mashauri ya jinai, kunyimwa dhamana, na matumizi mabaya ya madaraka yalipokelewa. Malalamiko hayo yameendelea kufanyiwa kazi ili kuyahitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kubainisha na kutatua migogoro ya kisheria kwa wananchi na wadau wengine, Wizara imejikita katika kuimarisha mifumo ya utoaji haki nchini na haki madai ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi, na Udhamini ilipokea migogoro zaidi ya 32 ya bodi za wadhamini ambapo migogoro sita ilitatuliwa kwa njia ya majadiliano, na migogoro 26 ipo katika hatua mbalimbali za usuluhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 – Machi, 2026, Wizara imepokea malalamiko 1,527 kupitia Kituo cha Huduma kwa Mteja, ambapo kati ya hayo malalamiko 1,322 sawa na 86.5% yamefanyiwa kazi na kuhitimishwa na malalamiko 205 yanaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali za utatuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeanzisha Programu Maalumu ya 'Sema na Waziri' ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 17 Machi, 2026. Programu hii inalenga kutoa fursa kwa wananchi kupiga simu na kuhudumiwa moja kwa moja na Mheshimiwa Waziri katika masuala mbalimbali ya kisheria, kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi, pamoja na kurahisisha utatuzi wa migogoro papo kwa papo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 – Machi, 2026, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilipokea malalamiko 143 na kuyafanyia kazi. Malalamiko haya yalihusu migogoro ya ardhi, uchafuzi wa mazingira, ukamataji na mauaji ya mifugo, fidia ya mali, kutolipwa mafao, kushushwa cheo kiuonevu, kubomolewa nyumba, na matumizi mabaya ya madaraka. Katika malalamiko hayo, 96 yalifungwa na 47 yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha mifumo ya utoaji haki ipatikane kwa wote, Wizara pamoja na taasisi zake imeendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki kwa kufanya mageuzi ya kisheria, kimuundo na kiutendaji kwa lengo la kuhakikisha haki inapatikana kwa watu wote na kwa usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 – Machi, 2026, Wizara imepokea maombi 63 ya nyongeza ya muda wa kufungua mashauri Mahakamani, ambapo maombi 49 yamehitimishwa na 14 yanaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, maombi 36 kuwaachilia huru wahalifu wenye changamoto ya afya ya akili yamepokelewa, ambapo amri za kuachiliwa huru kwa wahalifu 36 zinaandaliwa na kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara ilipokea maombi manne ya kuwaachia huru wafungwa waliowekwa kizuizini chini ya uangalizi wa Rais kutokana na umri mdogo, ambapo amri za kuwaachilia huru wafungwa wawili zimetolewa na nyingine mbili bado zinafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuharakisha usikilizaji wa mashauri Mahakamani ni moja ya vipaumbele muhimu vya Mahakama ya Tanzania katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata haki kwa wakati. Katika kipindi cha Julai, 2025 – Machi, 2026, kulikuwa na jumla ya mashauri 205,038 Mahakamani. Kati ya hayo, mashauri 166,553 yalisikilizwa na kuhitimishwa, na mashauri 38,485 yanaendelea katika hatua mbalimbali katika Mahakama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usikilizaji na umalizaji wa haraka wa mashauri yaliyomo Mahakamani una mchango mkubwa kwa Taifa kiuchumi na kijamii. Mathalani, katika zoezi maalumu la kusikiliza mashauri ya kiuchumi na kibiashara iliyofanywa na Mahakama, katika kibindi cha Oktoba hadi Novemba, 2025, mashauri 2,973 yalihitimishwa. Kuhitimishwa kwa mashauri hayo kuliwezesha kuachilia jumla ya shilingi trilioni 13.1 zilikuwa zimeshikiliwa kutokana na mashauri hayo na hayo kuingia kwenye mzunguko wa uchumi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi na usimamizi wa shughuli za kimahakama katika ngazi ya Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo kwa Kanda 20 za kimahakama umefanyika kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukaguzi huo yamewezesha kuongeza kasi ya umaliziaji mashauri Mahakamani, kwa kuwa kuambatana na kuongezeka kwa kasi ya umaliziaji mashauri katika Mahakama na ukaguzi wa jalada moja baada ya lingine. Vilevile, magereza 129 kati ya 130 yaliyopo yalikaguliwa, sawa na 98.8%, kuboreka kwa mfumo wa kitaifa kuzingatia mifumo ya kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria, inajukumu la kusimamia na kuratibu masuala ya haki za binadamu nchini, ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa mikataba na itifaki za kikanda na Kimataifa ambazo nchi imeridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imeandaa Rasimu ya Taarifa ya Nchi ya Hali ya Haki za Binadamu ya Mzunguko wa Nne kwa Mfumo wa Mapitio ya Kipindi Maalum *(UPR)* ambayo inapima na kuonesha maendeleo ya nchi katika utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu. Aidha, kwa mara ya kwanza Taasisi za Kidini *(Faith Based Organizations – FBOs)* zimeishirikisha Serikali katika maandalizi ya Taarifa yao Kivuli *(Shadow Report)* kuhusu masuala ya haki za binadamu. Taarifa hizo zitawasilishwa Umoja wa Mataifa Julai, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeandaa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo 187 yaliyotolewa kwa Tanzania katika mzunguko wa *UPR* wa mwaka 2021, kwa ajili ya kuonesha namna nchi ilivyotekeleza mapendekezo ili kulinganishwa na taarifa itakayotolewa na nchi katika mzunguko wa nne wa *UPR*. Taarifa hiyo imewasilishwa Umoja wa Mataifa tarehe 10 Aprili, 2026 kama taarifa kivuli *(shadow report)* kutoka Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, Wizara na Taasisi zake imeshiriki katika mikutano mbalimbali yenye malengo mahsusi ya kuboresha mifumo ya haki jinai na haki madai, mikutano hiyo imebainishwa katika Ibara ya 64 katika kitabu cha hotuba yetu ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza programu ya kutumia lugha ya Kiswahili kwenye utoaji wa haki na kuwawezesha wananchi kuzielewa sheria za nchi, Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, imekamilisha kutafsiri sheria kuu 433 kwa lugha ya Kiswahili ili ziweze kutumika Mahakamani na kutangazwa rasmi kupitia Tangazo la Serikali Na. 659 la 2025. Sheria hizo pamoja na sheria 13 zilizotungwa katika lugha ya Kiswahili zinafanya jumla ya sheria zote 446 kuwa katika Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwezesha utekelezaji wa sheria kuu zilizotafsiriwa katika lugha ya Kiswahili, Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria inaendelea na zoezi la tafsiri ya sheria ndogo, ambapo katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya Sheria Ndogo 229 zimetafsiriwa kutoka katika lugha ya Kiingereza na kwenda kwenye lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuimarika kwa mifumo ya kisheria na kitaasisi katika utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Wizara inatambua na kuthamini nafasi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro katika kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wakati, kupunguza gharama na kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imepokea maombi 332 ya wataalamu wa utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Kati ya maombi hayo, maombi 205 yameidhinishwa baada ya kukidhi vigezo vya jopo la ithibati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya watatuzi migogoro kwa njia mbadala 881 wamesajiliwa. Aidha, jumla ya watoa huduma za utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala 813 wamepatiwa mafunzo wakiwemo Wasuluhishi *(Arbitrators)* 362, Wapatanishi *(Mediators),* 286, Waendesha Maridhiano *(Reconciliators)* 101 na Waendesha Majadiliano *(Negotiators)* 132.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imesimamia majadiliano ambayo

yamesababisha kuhitimishwa kwa migogoro nje ya Mahakama. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, jumla ya migogoro ya madai 143 imefanyiwa kazi, ambapo kiasi kilichodaiwa kabla ya majadiliano ni shilingi trilioni 2.83.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia majadiliano hayo, kiasi kilicholipwa ni shilingi trilioni 2.18. Hivyo, Serikali imeokoa shilingi bilioni 646.22. Katika kuimarisha utendaji kazi na kulinda maslahi ya Taifa, imeweka mikakati ya kutoa mafunzo ya kisheria kwa Viongozi wa Umma. Jitihada hizi zinalenga kuzuia migogoro, kuokoa rasilimali za umma, na kujenga uwezo wa kisheria katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2025, Mahakama Kuu Kituo cha Usuluhishi ilikuwa na jumla ya Mashauri 37. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 mashauri 238 yamepokelewa na kufanyiwa kazi jumla ya mashauri kuwa 275. Kati ya Mashauri hayo, mashauri 242 yamesuluhishwa na Mashauri 33 yanaendelea katika hatua mbalimbali za usuluhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarika kwa usimamizi wa mikataba na utajiri asili wa maliasili, ulinzi na usimamizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi, ni wajibu wa kikatiba, ni msingi wa uhai wa uchumi wetu. Hivyo, Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia masuala ya utajiri asili na maliasilia za nchi. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ilipokea mikataba 140 ya uwekezaji katika sekta ya utajiri asili na maliasilia na kuifanyia mapitio ili kuhakiki uzingatiwaji wa misingi ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara iliwajengea uwezo wataalamu 72 kutoka Wizara za Kisekta, Idara, Taasisi na Wakala za Serikali zinazohusika na ulinzi na usimamizi wa maliasilia za nchi. Vilevile, viongozi na watendaji 244 wa Serikali walijengewa uwezo kuhusu faida na changamoto za mikataba ya kukuza na kulinda uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara imeandaa Mwongozo wa Tathmini na Ufuatiliaji wa Uzingatiwaji wa Misingi ya Sheria za Usimamizi wa Utajiri Asili na Maliasilia Nchi. Lengo la Mwongozo huo ni kufanya tathmini ya

uzingatiwaji wa utekelezaji wa sera, Sheria na Kanuni za kisekta kwa kuhakikisha kuwa nchi inapata mapato stahiki yanayotokana na uwekezaji katika miradi ya utajiri asili na maliasilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuimarisha Usimamizi, Ufuatiliaji na Majadiliano ya Mikataba, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jukumu la kuimarisha upekuzi, usimamizi, majadiliano na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanya upekuzi wa Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa 2,562. Upekuzi huu umeimarisha ulinzi wa maslahi ya Serikali, kupunguza hatari za hasara za kifedha, kuongeza masilahi ya Serikali, kupunguza hasara za kifedha za Serikali, kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma, na kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa kuzingatia sheria na mikataba yenye tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Ofisi ilikamilisha upekuzi wa Hati za Makubaliano *(Memoranda of Understanding)* 396. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imesimamia mikataba 2,821 iliyosainiwa kati ya Serikali na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ofisi ilipokea maombi ya kuvunja mikataba saba ambapo ilishauri mikataba mitano ivunjwe kwa mujibu wa masharti ya mikataba husika na mikataba miwili ilishauriwa isivunjwe badala yake utekelezaji uendelee kwa mujibu wa masharti ya kimkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imesimamia majadiliano yaliyofanikisha kusainiwa kwa mikataba tisa yenye jumla ya thamani ya shilingi trilioni 7.48 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuimarika kwa mifumo ya uandishi, utafsiri na urekebu wa sheria. Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imeendelea na majukumu yake ya

kuandaa miswada ya sheria, kuhakiki na kusimamia uchapishaji wa sheria ndogo, kutafsiri na kurekebisha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imeandaa Miswada ya Sheria minne. Kati ya Miswada hiyo, miwili imesomwa kwa mara kwanza; ambayo ni Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 na Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinaohamishika kwa Mwaka wa Fedha 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imeandaa, kuhakiki na kuchapisha jumla ya Sheria Ndogo 447. Sheria hizo zinajumuisha Kanuni 107, Notisi 145, Amri 125, Sheria Ndogo 62, Hati saba na Mwongozo mmoja. Mchanganuo wa sheria hizo umeainishwa kwenye kiambatanisho namba tano, kwenye ukurasa wa 164 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imekamilisha kutoa Toleo la Urekebu la Nyongeza la Mwaka 2025 ambalo limejumuisha Sheria kuu 71 zilizorekebishwa. Aidha, sheria hizo zimetangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 637A la 2025. Vilevile Sheria Ndogo 265 zimefanyiwa urekebu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pamoja na taasisi zake imeweka kipaumbele hususani katika kutoa uelewa kwa watendaji wa Serikali kuhusu huduma zinazotolewa kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali, ili kuhakikisha utekelezaji wa majukumu unazingatia misingi ya haki, uwajibikaji na weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini imetoa elimu ya usimamizi wa Bodi za Wadhamini, Udhamini wa Umma na Usajili wa ndoa za kimila kwa watumishi 370. Wakiwemo Wakuu wa Wilaya 42, Makatibu Tawala 56, Maafisa Tarafa 218, viongozi wa dini 54 katika mikoa ya Singida, Morogoro, Iringa, Dodoma, Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wajumbe wa Bodi za Wadhamini 585 wamepatiwa Mafunzo ya Usimamizi wa Bodi za Wadhamini kwa kuzingatia Sheria katika mikoa tajwa. Vilevile, wakala umetoa elimu ya usajili wa vizazi na vifo, ndoa, udhamini wa umma na mirathi kwa wananchi kupitia vipindi vya redio 560, vipindi vya runinga 170, maudhui 487 katika mitandao ya kijamii, maudhui 74 katika blogu na maudhui 85 katika magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, ilitoa elimu ya masuala ya kisheria katika Maonesho ya Kitaifa ya Saba Saba na Nane Nane ambapo jumla ya wananchi 745,693 walifikiwa. Vilevile, Tume iliandaa na kurusha vipindi vya runinga, redio na kusambaza vipeperushi 5,860.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 57 kupitia runinga, vipindi vitano vya redio na vipindi 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imetoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali, ikiwemo ya Jumbe Fupi *(Bulk SMS)* kupitia simu za mkononi ambapo jumbe moja inawafikia takribani wananchi 87,557.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, jumla ya nakala 19,555 za vipeperushi zilisambazwa kwa wananchi, klabu 25 za haki za binadamu zilianzishwa katika Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu, na kufanya jumla ya vilabu 389.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilitoa mafunzo kwa wadau 2,088 wakiwemo Maafisa wa Jeshi la Polisi 827, Waandishi wa Habari 354 na wananchi 907. Mafunzo hayo yalitolewa katika mikoa 14 ya Tanzania Bara na mitano Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa Mawakili wa Serikali 596 kutoka katika Wizara, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na taasisi mbalimbali kuhusu uendeshaji na usimamizi wa mashauri ya madai na usuluhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarika kwa utafiti, tathmini na mapitio ya sheria. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imefanya Utafiti wa Mifumo ya sheria zinazosimamia Biashara ya Hewa ya Ukaa, Matumizi ya Akili Unde, Usajili wa Mawakili Tanzania, na Mfumo wa Sheria za kupinga maamuzi ya kiutawala nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Tume imefanya Tathmini ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi katika Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura 449; Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura 450; na Sheria ya Ugaidi, Sura 19. Vilevile Tume imefanya Mapitio ya Sheria ya Usuluhishi, Sura 15; Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Sura 295; Sheria ya Bima za Vyombo vya Moto (Magari), Sura 169; na Sheria ya Bima, Sura 394.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi zinalenga kujenga msingi imara wa maboresho ya sheria pale inapobidi, kuandaa mapendekezo ya kutungwa kwa sheria mpya zitakazowezesha uwepo wa mifumo ya sheria inayokidhi mahitaji ya maendeleo ya sasa na ya baadaye baada ya kubaini kiwango cha ufanisi wa utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuendesha mashtaka ya jinai na kuimarisha shughuli za utenganishaji wa mashtaka na upelelezi. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi za jinai 17,612 katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, kesi 14,522 sawa na 82% zilihitimishwa mahakamani, Kati ya kesi zilizohitimishwa, 10,640 sawa na 73% zilihitimishwa kwa watuhumiwa kutiwa hatiani. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi

Machi, 2026, Jumla ya kesi 2,491 ziliendeshwa katika Kanda za Mahakama Kuu. Kati ya kesi zilizoendeshwa, kesi 864 sawa na 34.7% zilihitimishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya rufaa na maombi 389 ya Mkurugenzi wa Mashtaka yalisikilizwa. Jumla ya rufaa na maombi 139 sawa na 35.7% yalisikilizwa na kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, rufaa na maombi 250 sawa na 64.3% yanaendelea kusikilizwa. Jumla ya rufaa na maombi 2,773 dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka yalisikilizwa katika Mahakama Kuu. Aidha, jumla ya rufaa na maombi 1,368 sawa na 49.3% yalitolewa ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendelea na zoezi la utaifishaji wa mali zinazotokana na uhalifu mara baada ya kesi kuhitimishwa. Mali zilizotaifishwa ni pamoja na nyumba 10 na viwanja 16, hati fungani zilizopo Benki Kuu ya Tanzania zenye thamani ya shilingi 490,000,000, fedha taslimu shilingi 8,543,350 na Dola za Marekani 1,800 sawa na shilingi 4,626,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mali hizi zilizopatikana kwa njia za uhalifu (mazalia ya uhalifu) ama zilizotumika kutenda uhalifu zilitaifishwa kuwa mali za Serikali. Hatua hii ya utaifishaji ilidhihirisha dhamira ya Serikali kwamba hakuna mwananchi atakayenufaika na mali zitokanazo na uhalifu. Hivyo, nitoe wito kwa wananchi kuzingatia sheria na kuepuka kutenda uhalifu kwa kuwa uhalifu haulipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, imeendelea kutenganisha huduma za mashtaka na upelelezi pamoja na kusogeza huduma za kimashtaka kwa wananchi katika ngazi za mikoa na wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, ofisi ilifungua Ofisi za Wilaya katika Wilaya 10 ambazo ni Kakonko (Kigoma), Liwale (Lindi), Mkinga (Tanga), Kibiti na Kisarawe (Pwani), Sikonge na Uyui (Tabora), Nyasa na Namtumbo

(Ruvuma) na Mbogwe (Geita). Hivyo kuwa na jumla ya ofisi za wilaya 118 kati ya wilaya 139 zilizopo nchini. Aidha, jumla ya Mawakili wa Serikali 78 wameajiriwa ili kukabiliana na upungufu wa watumishi katika ofisi za mikoa na wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha jumla ya mashauri ya madai 10,401, katika kuendesha mashauri hayo; Mashauri 641 yalihitimishwa, katika ya mashauri yaliyohitimishwa ofisi imeshinda mashauri 565 sawa na 88.1% ya mashauri yaliyomalizika na kuokoa shilingi bilioni 316.28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha jumla ya mashauri ya usuluhishi 251. Aidha, mashauri 18 yalihitimishwa yakiwemo 17 ya usuluhishi wa Kitaifa na moja la usuluhishi wa Kimataifa. Kutokana na kumalizika kwa mashauri hayo, Serikali imeokoa shilingi bilioni 6.81 na Dola za Kimarekani milioni 418.17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika sekta ya sheria; katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, ujenzi wa majengo mbalimbali ya Mahakama umeendelea ukijumuisha vituo Jumuishi vya Utoaji Haki tisa, katika mikoa ya Geita, Lindi, Katavi, Njombe, Simiyu, Ruvuma, Songwe, Singida na Kusini Pemba, ambapo baadhi ya majengo yamekamilika kwa 100%, na mengine yapo katika hatua za mwisho za umaliziaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa majengo haya umewezesha kuanzishwa kwa masijala za Mahakama Kuu katika Mikoa ya Njombe, Katavi, Singida, Lindi na Songwe ambapo hapo awali wananchi walikuwa wanapata huduma za Mahakama Kuu kupitia mikoa jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ya majengo ya Mahakama ni pamoja na kuendelea na, ujenzi wa Mahakama za Wilaya 18 na Mahakama za Mwanzo 71 katika mikoa mbalimbali. Vilevile, Mahakama inaendelea na ukarabati wa majengo ya zamani ya Mahakama Kuu Dodoma, Mwanza, Dar es Salaam na Iringa, na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imekamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi Makao Makuu - Dodoma na Ofisi tano za mikoa ya kimashtaka ya Morogoro, Tanga, Njombe, Geita na Mbeya na hivyo kufikisha majengo ya Ofisi za mikoa ya kimashtaka kufika 12 kati ya mikoa 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa ujenzi wa majengo haya kumesaidia kuboresha na kusogeza huduma zaidi kwa wananchi. Aidha, Ofisi inaendelea ujenzi wa majengo ya Ofisi za Mikoa na Wilaya katika mikoa nane ya kimashtaka ya Kinondoni, Temeke, Simiyu, Lindi, Singida, Kigoma, Songwe na Kilimanjaro. Aidha, ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wilaya sita unaendelea katika Wilaya za Bahi, Manyoni, Hai, Kigamboni, Nzega na Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa majengo ya Vituo Jumuishi vya Taasisi za Serikali zinazotoa Huduma za Kisheria katika mikoa ya Mwanza umefikia 74% na Arusha 50%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusimamia na kuendeleza elimu na taaluma ya sheria nchini; Wizara kupitia Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo *(The Law School of Tanzania - LST)* na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto *(Institute of Judicial Administration - IJA)* imeendelea kutoa elimu ya taaluma ya Sheria nchini na mafunzo endelevu ya kimahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika matokeo ya mitihani ya Septemba, 2025/2026 Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania jumla ya wahitimu 697 walifaulu kwenye vipengele vyao vyote na wengine walifaulu kwenye vipengele vya masomo baadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Chuo cha Uongozi wa Mahakama kimesajili jumla ya wanafunzi 822 sawa na 82.2% ya lengo la udahili wa wanafunzi 1,000. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya wanafunzi 815 walihitimu mafunzo ya ngazi ya Astahashada na Stashahada ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezeshaji wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu na kusimamia masuala ya ufilisi na udhamini, Wizara kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA)* unaendelea na utekelezaji wa programu mbalimbali za usajili wa matukio muhimu ya binadamu ikiwemo usajili wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano, na hadi miaka 17 na watu walio na umri wa miaka 18 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa Wizara kwa mwaka 2026/2027 na mwelekeo wa sekta ya sheria katika mwaka 2026/2027; katika mwaka 2026/2027, Wizara inalenga kujenga sekta ya sheria inayotoa haki kwa wakati, yenye ufanisi mkubwa, inayotumia teknolojia, na inayochochea maendeleo ya katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya uamuzi wa kimkakati kwa uamuzi huo ni wa kuijenga upya sekta ya sheria Tanzania ili kuwezesha taasisi yenye ufanisi inayoshirikisha wadau wote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nisome vipaumbele vya bajeti 2026/2027:-

(i) Mageuzi ya Mfumo wa Kisheria;

(ii) Ujenzi wa miundombinu ya upatikanaji haki;

(iii) Kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya jinai;

(iv) Kuimarisha huduma za Msaada wa Kisheria;

(v) Kuimarisha haki za binadamu na utawala bora;

(vi) Kuimarisha masuala ya Kikatiba na kielimu;

(vii) Kuimarisha uwezo kwa wataalam wa sekta ya sheria;

(viii) Kuimarisha huduma za ufilisi na udhamini; na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukurani. Ninapenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Makamu Mwenyekiti; na Kamati Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa maelekezo na ushauri wao ambao umeleta mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa uchambuzi wa kina katika bajeti hii. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wao umesaidia sana kutekeleza bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Namtumbo kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao Bungeni pamoja na Viongozi na Wanachama wa Chama cha Mapinduzi na wananchi kwa ujumla katika Mkoa wetu wa Ruvuma, akiwemo Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Ruvuma, Katibu wa CCM wa Mkoa wa Ruvuma, Mjumbe wa *NEC* wa Mkoa wa Ruvuma, Katibu na Viongozi wengine wote wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninawashukuru pia Viongozi wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ambao Kamati ya Siasa ya Wilaya ikiongozwa na ndugu yangu Mzee Said Lihui kwa kuendelea kulilinda jimbo ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru pia Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Jaji wa Tanzania, na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama kwa kazi kubwa anayoifanya ya kusimamia na pia na Katibu wake wa Tume ambaye ni Prof. Elisante Ole Gabriel. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru kipekee Mheshimiwa Hamza Saidi Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wake katika kusimamia sekta ya sheria. Ukweli ni kwamba anatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi wenzangu wakiwemo Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Bwana Eliakim Chacha Maswi, Katibu Mkuu; na Bwana Samwel Marco Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu. Pia, shukurani za dhati nimpe ndugu yetu Dkt. Franklin Jasson Rwezimula, Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa shukrani za dhati kwa viongozi wengine wa Mhimili wa Mahakama akiwemo Mheshimiwa Dkt. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania; Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; na Mheshimiwa Eva Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru Wenyeviti wa Bodi za Taasisi za Wizara ambao ni Mheshimiwa Dkt. Mary Caroline Levira, Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Mheshimiwa Winifrida Beatrice Korosso, Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; pamoja na Mheshimiwa Mathew Pauwa Mwaimu, Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu na aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na Mheshimiwa Mohamed Khamis Hamad, aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hao, ninapenda pia kuwashukuru viongozi wengine wa Taasisi za Wizara ambao ni Mheshimiwa Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka; Dkt. Ally Saleh Possi, Wakili Mkuu wa Serikali; Bwana Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria; Mheshimiwa Dkt. Paul Faustine Kihwelo, Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Bwana Frank Kanyusi, Kabidhi Wasii Mkuu na Mkurugenzi Mkuu wa *RITA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni akina Patience Kilanga Ntwina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na Prof. Sist Joseph Mramba, Mkuu *LST School*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishukuru mashirika mbalimbali. *(GIZ)* Shirika la Maendeleo la Watu wa Ujerumani; Shirika la *Irish Rule of Law International;* Benki ya Dunia; Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto *(UNICEF);* na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia usawa wa kijinsia, *(UN Women)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishukuru familia yangu; wake zangu wawili. Kipekee, ninarudia, ninaomba niishukuru familia yangu; Bi. Imani Juma Homera na Bi. Jasmine Juma Homera kwa kunipa usingizi mwororo na kunisaidia niweze kufanya kazi vizuri za Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninawashukuru wazazi wangu Mzee Zuberi Rajabu Homera pamoja na Mama yangu mzazi Amina Mohamed Mango kwa kuendelea kuniombea popote walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, ninawashukuru watoto wangu, waliopo leo wamewakilisha tu, wapo kama tisa hivi. Leo wamewakilishwa tu. Yuko Noureen, Jureen, Afrin, Gian, na Princess. Hawa ni watoto wangu ambao leo wamewakilisha kwa niaba ya wenzao wengine ambao wamebaki nyumbani. Mwingine Marleen na Junaitha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 774.79 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mafungu tisa ambayo: Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12) shilingi bilioni 8.15; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16) shilingi bilioni 61.09; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Fungu 19) shilingi bilioni 41. 31; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (Fungu 35) shilingi bilioni 162.52; Mahakama ya Tanzania (Fungu 40) shilingi bilioni 287.63; Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41) shilingi bilioni 160.32; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) shilingi bilioni 17.41; Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Fungu 59)shilingi bilioni 12.11; na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (Fungu 101) shilingi bilioni 24.24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027 Wizara ya Katiba na Sheria, Mhimili wa Mahakama na Taasisi zake unaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 774.79. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 152.46 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, shilingi bilioni 484.91 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 137.42 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ninaomba urudie Fungu la Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Fungu 59) ili *Hansard* i-*record* vizuri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Fungu 59) shilingi bilioni 12.11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027 Wizara ya Katiba na Sheria, Mhimili wa Mahakama na Taasisi zake unaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 774.79. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 152.46 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, shilingi bilioni 484.91 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 137.42 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina na mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu yameainishwa kwenye vitabu vya Randama za mafungu husika ambavyo vimegawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge kupitia Mfumo wa Kielektroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. JUMA ZUBERI HOMERA (MB.), WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti zilizochambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; pamoja na kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria, Taasisi zake pamoja na Mahakama ya Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniruzuku uhai na afya njema iliyoniwezesha kusimama hapa leo katika Bunge lako kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mahakama ya Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

3. ***Mheshimiwa Spika***, kwa heshima na taadhima ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Ninaahidi kuitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na unyenyekevu kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu anijalie hekima, busara na ujasiri ili niweze kutimiza wajibu huu.

***Salamu za Pole***

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa ninatoa pole kwako na Bunge lako kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu waliotangulia mbele ya haki ambao ni Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Isimani; Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na mwakilishi wa

wafanyakazi kutoka Vyama vya Wafanyakazi Tanzania Bara. Aidha, katika Sekta ya Sheria pia tumeondokewa na Mheshimiwa Julie Catherine Manning aliyekuwa mwanamke wa kwanza Tanzania kusoma Shahada ya Sheria na aliyewahi kuhudumu katika nafasi ya Waziri wa Sheria akiwa ni Mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo. Vilevile, aliweka rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa Jaji wa Mahakama Kuu katika Afrika Mashariki na Kati.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha hivi karibuni, wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na maafa yaliyotokana na mafuriko katika mikoa mbalimbali. Baadhi ya Mikoa hiyo ni Dodoma, Arusha, Mwanza, Mbeya, Iringa, Singida, Shinyanga, Lindi, Manyara, Pwani, Ruvuma, Kigoma, Tanga, Dar es Saalam, Kilimanjaro na Morogoro. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo. Aidha, ninatoa pole kwa waathirika na manusura wa matukio yote yaliyotokea nchini katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026 zikiwemo ajali mbalimbali za vyombo vya barabarani na kwenye maji. Ninawaombea majeruhi wote uponyaji wa haraka na marehemu wote wapate pumziko la amani, AMINA.

***Pongezi***

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na taadhima ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa na Watanzania ili kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hatua inayoonesha imani waliyonayo kwake. Aidha, nimpongeze kwa uongozi wake mahiri, thabiti na wenye maono ya mbali uliowezesha mafanikio katika sekta mbalimbali hususan Sekta ya Sheria, kwa kuweka mifumo thabiti ya kisera, kisheria na kitaasisi ambayo imewezesha kuimarika kwa utoaji na upatikanaji haki, huduma za msaada wa kisheria na utawala bora. Ninaomba tuendelee kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema amjalie afya njema, hekima na busara katika kuendelea kuliongoza Taifa letu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Uongozi na maelekezo yao thabiti yataimarisha zaidi utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Sheria kuwa kichocheo cha maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake iliyoweka msingi imara wa mwelekeo wa kisera kwa Taifa letu kwa Mwaka wa Fedha 2026/ 2027. Vilevile, ninampongeza kwa uongozi wake mahiri na hodari katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako tukufu.

Sambamba na pongezi hizi, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote waliotangulia kuwasilisha hotuba zao.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nikupongeze kwa kuchaguliwa na Bunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.), kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuaminiwa kwenu na Wabunge kunaonesha umahiri na uwezo mlionao wa kuliongoza Bunge letu katika kuwatumikia Watanzania. Vilevile, niwapongeze Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga; na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa George Mcheche Masaju, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. Uteuzi wake unadhihirisha umahiri na uzoefu alionao katika Sekta ya Sheria kwa ujumla ikiwemo Mhimili wa Mahakama. Aidha, ninamshukuru sana Mhe.

Hamza Saidi Johari (Mb.), Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa jinsi anavyonipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya Wizara pamoja na uratibu na usimamizi wa Sekta ya Sheria kwa ujumla.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba (Mb.), kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki (Mb.) kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Kamati hizi zimefanya kazi kubwa ya kushauri na kuchambua Mpango na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Hakika tunatambua na kuthamini mchango wa Kamati hizi katika kuhakikisha kuwa sekta ya sheria inabaki kuwa kiungo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Maoni na ushauri wao umekuwa ni msaada mkubwa kwa Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia Watanzania. Napenda niwahakikishie kuwa Wizara yangu ina imani kubwa katika uongozi wao na itaendelea kuwapatia ushirikiano unaostahili.

### *Maono ya Mageuzi Katika Sekta ya Sheria*

12. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii ninayoiwasilisha mbele ya Bunge lako imebeba ujumbe wa msingi kwa mustakabali wa Taifa letu. Ujumbe huo umeainisha masuala ya msingi katika Sekta ya Sheria nchini yatakayochangia katika kufikia matarajio yaliyoainishwa katika DIRA 2050. Kutokana na ujumbe huo, tunaamini kwamba hakuna maendeleo endelevu bila mfumo imara wa kisheria, hakuna uchumi shindani bila utawala wa sheria na pia hakuna Taifa lenye utulivu bila haki kwa wote. Kwa mantiki hiyo, Sekta ya Sheria siyo tu ni Mhimili wa utawala bora bali ni miundombinu isiyoonekana (*invisible infrastructure*) inayoshikilia misingi ya uchumi, uwekezaji na umoja wa kitaifa. Hivyo, mwelekeo wa Sekta ya Sheria ni kusimama katika nafasi ya kimkakati kama mlinzi mkuu wa utawala wa kikatiba, utawala wa

sheria na haki, na kichocheo cha maendeleo ya uchumi wa Taifa katika kufikia malengo ya DIRA 2050.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba ninayoiwasilisha haiainishi tu takwimu za kibajeti, inabainisha dira \yenye mfumo wa mageuzi ya Sekta ya Sheria nchini; mwelekeo wa kitaifa wa kujenga Serikali imara inayozingatia utawala wa sheria; na mkakati wa kuifanya Sekta ya Sheria kuwa Mhimili mkuu wa maendeleo ya uchumi wa Taifa letu. Aidha, hotuba hii ni mwelekeo wa kimkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kuitumia na kuipa nafasi Sekta ya Sheria nchini ili ichangie kikamilifu kwenye ujenzi wa Taifa letu kwa maslahi mapana ya kizazi cha sasa na kijacho.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** katika zama hizi za ushindani wa kimataifa na uchumi wa kisasa, nguvu ya Taifa haipimwi tena kwa rasilimali zake za asili pekee, bali inapimwa kwa uimara wa taasisi zake; ufanisi wa mifumo yake ya utoaji haki; na uwezo wake wa kusimamia sheria katika kuleta amani, utulivu, maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii hususan katika upatikanaji haki kwa wakati kwa watu wote. Kwa mantiki hiyo, Sekta ya Sheria inachukua nafasi mpya kabisa katika historia ya Taifa letu. Siyo tena kama msimamizi wa sheria pekee, bali kama injini ya uthabiti wa Taifa na kichocheo cha maendeleo ya uchumi katika kufikia malengo ya DIRA 2050.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwelekeo mpya na mageuzi katika Sekta ya Sheria, ninaomba kutumia fursa hii kutoa shukrani za dhati na za kipekee kwa uongozi wa juu wa Taifa letu ambao umeendelea kuweka msingi imara wa mageuzi tunayoyazungumzia leo. Kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake madhubuti, wenye dira, na wenye uelewa mpana wa nafasi ya sheria katika maendeleo ya Taifa letu. Mhe. Rais ameweka msingi wa mageuzi ya kweli ya kimfumo katika Sekta ya Sheria kama ilivyooneshwa kwa uwazi katika DIRA 2050.

16. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuanza kwa kusisitiza kwamba msingi mkuu wa DIRA 2050 ambao ni *Utawala, Amani, Usalama na Utulivu* si kauli ya mapambo ya sera, bali ni uamuzi wa

kimkakati wa Taifa letu uliofanywa kwa ujasiri na Uongozi wa Juu wa nchi. Huu ni msingi unaobeba hatima ya Tanzania ya kesho tuitakayo; ni msingi unaotofautisha Taifa linalokua kwa bahati na Taifa linalojengwa kwa makusudi. Katika muktadha huu, bajeti ya mwaka 2026/2027 tunayoijadili leo siyo tu chombo cha kugawa rasilimali, bali ni nyenzo muhimu ya kutekeleza falsafa hii ya Taifa ya kuijenga Tanzania juu ya misingi isiyotetereka ya utawala wa sheria, amani endelevu, usalama wa uhakika na utulivu wa kudumu.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** ni muhimu Bunge lako Tukufu litambue kuwa kwa mara ya kwanza katika historia ya maendeleo ya Taifa letu, Sekta ya Sheria imewekwa katikati ya mjadala wa uchumi wa Taifa. Hii ni hatua ya kihistoria. Tumetoka katika mtazamo wa kuiona sekta hii kama mtumiaji wa rasilimali, na sasa tunaijenga kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi, mlinzi wa uwekezaji, na nguzo ya kuaminika ya utulivu wa Taifa. Hakuna uchumi wa kisasa unaoweza kustawi bila uhakika wa sheria; hakuna mwekezaji anayeweza kuwekeza bila ulinzi wa haki; na hakuna maendeleo ya kweli bila mifumo ya haki inayofanya kazi kwa ufanisi na kwa haki.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** msingi huu wa DIRA 2050 unatutaka tufanye mageuzi ya kina na ya kimfumo. Serikali itaendelea kuimarisha taasisi za utoaji haki, kuongeza upatikanaji wa huduma za kisheria kwa wananchi wote, na kuharakisha matumizi ya teknolojia katika mifumo ya sheria ili kuongeza uwazi, ufanisi na uwajibikaji. Aidha, tutaendelea kuimarisha na kusimamia mifumo mbadala ya Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala (*Altenative Disputes Resolution - ADR*) ili kupunguza mzigo katika mahakama na kuharakisha haki kwa wananchi. Haya yote ni sehemu ya kujenga Taifa ambalo sheria si kikwazo, bali ni daraja la maendeleo.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** tunapozungumzia Utawala, Amani, Usalama na Utulivu, tunazungumzia pia ujenzi wa imani ya wananchi kwa Taifa lao. Taifa lenye utulivu si lile lisilo na changamoto, bali ni lile lenye mifumo imara ya kushughulikia changamoto hizo kwa haki na kwa wakati. Kupitia bajeti hii, Serikali inalenga kuimarisha mshikamano wa Taifa, kulinda haki za

wananchi, na kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anahisi uwepo wa dola inayomtambua, inayomlinda, na inayomhudumia kwa usawa.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** ni muhimu pia kusisitiza kuwa msingi huu wa DIRA 2050 si jukumu la Serikali pekee. Ni wajibu wa pamoja unaohusisha Bunge lako Tukufu, Mahakama, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, na Taasisi za Dini. Taifa lenye amani na utulivu hujengwa kwa misingi ya maadili, kuheshimu sheria, na uwajibikaji wa pamoja. Hivyo, utekelezaji wa msingi huu unahitaji mshikamano wa kitaifa, dhamira na malengo ya pamoja, na uongozi thabiti unaoongozwa na misingi ya haki na uadilifu.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa Uongozi wa Juu wa Taifa tayari umefanya uamuzi huu wa kihistoria wa kuijenga Tanzania imara kupitia utawala wa sheria, sasa ni jukumu letu kuhakikisha kuwa uamuzi huu unatekelezwa kwa vitendo, kwa uthabiti na kwa matokeo yanayoonekana. Hivyo basi, naomba Bunge lako Tukufu liunge mkono bajeti hii siyo tu kama bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, bali kama chombo cha Taifa cha kulinda na kuimarisha msingi wake mkuu wa maendeleo. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeweka jiwe la msingi imara kuelekea Tanzania yenye amani ya kudumu, usalama wa uhakika, utawala bora na maendeleo jumuishi ifikapo mwaka 2050.

## B. DIRA, DHIMA NA KAULI MBIU

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Dira ya Wizara ya Katiba na Sheria ni "*Kuwa na Taifa linalozingatia haki, jumuishi na lenye ustahimilivu ambapo usawa, uadilifu na utawala wa sheria vinatawala kwa wote*". Dira hii inalenga kujenga Taifa lenye haki, amani, utulivu, ushirikishwaji, nguvu ya kukabiliana na changamoto, na Taifa linaloongozwa kwa misingi ya usawa, maadili, na sheria.

23. **Mheshimiwa Spika,** Dhima ya Wizara ni "Kuweka mifumo madhubuti ya Kikatiba na kisheria, kuendeleza upatikanaji wa haki, kulinda haki za binadamu, na kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali asilia kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Tanzania". Dhima hii inaeleza jukumu kuu au kazi inayopaswa kufanywa ili kufikia maendeleo ya Taifa. Aidha,

inalenga kujenga mfumo imara wa sheria na haki, kulinda haki za binadamu, na kutumia rasilimali vizuri ili kuleta maendeleo endelevu ya Taifa na kufikia Dira ya Wizara. Vilevile, Wizara ina Kauli mbiu ya "Haki, Usawa na Utawala wa Sheria kwa Wote." Kauli mbiu hii inasisitiza jamii yenye haki, isiyo na ubaguzi, na inayoendeshwa kwa kufuata sheria.

## C. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mhimili wa Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Taasisi nyingine ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Hati Idhini ambayo ilitolewa katika Gazeti la Serikali Na. 686 la tarehe 19 Desemba, 2025, Wizara ya Katiba na Sheria ilipewa usimamizi na uratibu wa majukumu yafuatayo: -

(i) Kutunga sera zinazohusu masuala ya sheria na kusimamia utekelezaji wake;
(ii) Kushughulikia masuala ya kikatiba;
(iii) Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki;
(iv) Uandishi wa sheria;
(v) Kuendesha mashtaka;
(vi) Kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi;
(vii) Usuluhishi wa migogoro ya kibiashara, sheria za kimataifa na mikataba;
(viii) Kuratibu masuala ya haki za binadamu na utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria;
(ix) Kusimamia shughuli za ufilisi na udhamini;
(x) Kuratibu tathmini na maboresho ya sheria;
(xi) Kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sheria za utajiri na maliasilia za nchi;
(xii) Kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai;

(xiii) Utendaji na maendeleo ya rasilimali watu iliyo chini ya Wizara; na
(xiv) Kuratibu majukumu ya taasisi, mipango na miradi chini ya Wizara.

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

26. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ulizingatia Dira na miongozo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ambayo ni pamoja na; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (2030); Mpango wa Maendeleo wa Afrika (2063), Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026 na Mpango Elekezi wa Muda Mrefu 2011/2012 – 2025/2026. Hotuba hii pia imezingatia masuala ya Sekta ya Sheria kama yalivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020; Ahadi za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akihutubia Bunge la 12; Maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na Mipango Mikakati ya Wizara na Taasisi zake.

27. ***Mheshimiwa Spika***, katika bajeti ya mwaka 2025/2026, Wizara ilibainisha masuala ya kipaumbele kama ifuatavyo: -

(i) Kuimarisha huduma za msaada wa kisheria kwa watu wenye uhitaji;
(ii) Kushughulikia masuala ya kikatiba pamoja na kutoa elimu ya Katiba na Uraia kwa umma;
(iii) Kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini;
(iv) Kubainisha na kutatua migogoro ya kisheria kwa wananchi na wadau wengine;
(v) Kuimarisha mifumo ya utoaji haki ili haki ipatikane kwa wote na kwa wakati;
(vi) Kuboresha mfumo wa kitaifa na kuzingatia mifumo ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za binadamu na utawala bora;

(vii) Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika masuala ya haki jinai na haki madai;
(viii) Kuwezesha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Sekta ya Sheria nchini;
(ix) Kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi katika Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala;
(x) Kuimarisha usimamizi wa mikataba ya utajiri asili na maliasilia za nchi ambazo Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zimeingia na wawekezaji;
(xi) Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na majadiliano ya mikataba;
(xii) Kuimarisha mfumo wa uandishi, ufasiri na urekebu wa sheria;
(xiii) Kuongeza uelewa kwa Watendaji wa Serikali na Wananchi kuhusu Sheria za Nchi;
(xiv) Kuimarisha utafiti, tathmini na mapitio ya sheria;
(xv) Kuendesha mashtaka ya jinai na kuimarisha shughuli za utenganishaji wa mashtaka na upelelezi;
(xvi) Kuimarisha uratibu, usimamizi na uwakilishi katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi;
(xvii) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika sekta ya sheria;
(xviii) Kusimamia na kuendeleza elimu na taaluma ya Sheria nchini;
(xix) Kuwezesha usajili wa matukio muhimu ya binadamu na kusimamia masuala ya ufilisi na udhamini;
(xx) Kuwezesha ajira, uteuzi, kuimarisha nidhamu na maadili ya watumishi wa Mahakama;
(xxi) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha huduma za kisheria nchini; na
(xxii) Kuendeleza rasilimali watu katika Sekta ya Sheria.

## E. MWENENDO WA BAJETI NA FEDHA ZILIZOPOKELEWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### *Makusanyo ya Maduhuli*

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara, Mhimili wa Mahakama ipamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya Shilingi

**15,676,199,000.00** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo ni pamoja na ada ya usajili wa Mashirika yanayotoa Huduma za Msaada wa Kisheria, ada za usajili wa Watatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala, ada za kusajili mashauri, faini zinazotokana na mashauri mbalimbali ya Mahakama pamoja na pango la ofisi. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara na Taasisi zake imekusanya jumla ya Shilingi **5,322,561,848.37** sawa na asilimia **33.9** ya lengo la makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2025/2026 na asilimia **45.3** kwa lengo la kipindi cha miezi 9 kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na.1**.

***Bajeti Iliyoidhinishwa***

29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **687,698,489,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha ya hizo, Shilingi **135,995,670,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi, Shilingi **389,464,032,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **162,238,787,000.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo Shilingi **79,671,467,000.00** ni fedha za ndani na Shilingi **82,567,320,000.00** ni fedha za nje (**Kiambatisho Na.2).**

***Fedha Zilizopokelewa***

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imepokea jumla ya Shilingi **532,858,152,735.34** sawa na asilimia **77** ya Bajeti ya Shilingi **687,698,489,000** iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **105,309,573,726.22** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi, Shilingi **303,841,906,611.65** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **123,706,672,397.50** ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha Shilingi **79,085,746,157.50** fedha za ndani na Shilingi **44,620,926,240.00** fedha za nje. Muhtasari wa mchanganuo wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha fedha kilichopokelewa na Wizara na Taasisi kwa kipindi hicho zimeainishwa katika **Kiambatisho Na. 3a na 3b.**

## F. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KUZINGATIA VIPAUMBELE

31. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mpango na bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 umezingatia vipaumbele vilivyowekwa na Wizara kama ifuatavyo: -

**(i) Kuimarisha Huduma za Msaada wa Kisheria kwa Watu Wenye Uhitaji**

32. ***Mheshimiwa Spika,*** msaada wa kisheria ni nguzo muhimu katika kulinda haki za wananchi na kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wote, hususan kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za uwakilishi katika vyombo vya utoaji haki. Upatikanaji wa huduma hii umeendelea kupunguza ukosefu wa usawa mbele ya sheria, kuimarisha utawala wa sheria na kuongeza imani ya wananchi kwenye mifumo ya utoaji haki. Huduma za msaada wa kisheria, zimeendelea kutolewa kupitia afua mbalimbali ikiwemo kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara na wadau mbalimbali wakiwemo watoa huduma za msaada wa kisheria, Taasisi zinazotoa elimu na mafunzo ya Sheria.

33. ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya wananchi **7,462,387** (wanaume **3,611,286** na wanawake **3,851,101**) walifikiwa na kupatiwa huduma za msaada wa kisheria kupitia maonesho ya kitaifa na majukwaa mbalimbali ikiwemo Siku ya Wanawake Duniani, wiki ya vijana na wiki ya Utumishi wa Umma; Madawati ya Msaada wa Kisheria**;** Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria; huduma za msaada wa kisheria magerezani; Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo; na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Aidha, kupitia afua hizo, jumla ya migogoro **5,209** ilipokelewa ambapo kati ya hiyo, migogoro **2,545** ilihitimishwa na **2,664** inaendelea kufanyiwa kazi katika vyombo vya maamuzi. Tathmini ya migogoro iliyopokelewa inaonesha kuwa migogoro ya ardhi ni asilimia **32**; madai asilimia **15**; matunzo ya Watoto asilimia **14**; ndoo asilimia **13**; mirathi asilimia **8**; ukatili wa kijinsia asilimia **4**; jinai asilimia **3**; ajira **3**; na mengineyo asilimia **8**.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa utoaji wa huduma za msaada wa kisheria katika maeneo ya vizuizi kwenye mikoa minne (**4**) ya Mara, Mwanza, Shinyanga na Simiyu. Ufuatiliaji huo ulibainisha

kuwa, kupitia utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria, kati ya wafungwa na mahabusi **3,847** (wanaume **3,684** na wanawake **163)** waliofikiwa katika magereza **18** katika mikoa tajwa, jumla ya wafungwa na mahabusi **1,377** (wafungwa **414** na mahabusi **953)** waliachiwa ndani ya kipindi cha miezi minne (**4**) kupitia huduma ya *parole* au kupatiwa adhabu mbadala nje ya gereza baada ya kukamilisha taratibu za kisheria. Pia, Wizara ilifanya ufuatiliaji katika magereza **40** yaliyopo mikoa ya Dodoma (**6**), Mara (**5**), Kigoma (**5**), Ruvuma (**6**), Mtwara (**5**), Lindi (**6**), na Pwani (**5**), Morogoro (**1**) na Singida (**1**). Tathmini hiyo ilibaini kupungua kwa msongamano wa mahabusi na wafungwa, kuimarika kwa matumizi ya adhabu mbadala kwa mujibu wa sheria, kuzingatiwa kwa haki za binadamu, pamoja na matumizi ya mifumo ya kidijitali kama Mahakama Mtandao na eCMS ambayo yamerahisisha usikilizaji wa mashauri na upatikanaji wa nyaraka kwa wakati.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, jumla ya Wanasheria **544** wakiwemo Mawakili wa Serikali **373** na Mawakili wa Kujitegemea **171** walibainishwa katika ngazi za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mikoa yote **26** ya Tanzania Bara, ili kushiriki kikamilifu katika utoaji wa huduma za Msaada wa Kisheria. Kati yao, Mawakili **220** (Mawakili wa Serikali **49** na Mawakili wa Kujitegemea **171**) wamepatiwa mafunzo maalum kuhusu masuala ya huduma za msaada wa kisheria na mbinu za utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wasaidizi wa Kisheria **243** na Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria **47** walisajiliwa na kufanya jumla ya Wasaidizi wa Kisheria kufikia **2,448** na Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria kufikia **430.** Katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 walisajiliwa Wasaidizi wa Kisheria **91** na Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria **183** sawa na ongezeko la asilimia **6.2** kwa Wasaidizi wa Kisheria waliosajiliwa. Aidha, katika kipindi husika, jumla ya Wasaidizi wa Kisheria **404** (wanaume **247** na wanawake **157**) walipatiwa mafunzo kuhusu masuala ya kisheria na msaada wa kisheria ikilinganishwa na Wasaidizi wa Kisheria **216** waliopatiwa mafunzo katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025 sawa na ongezeko la **46.5%.** Ongezeko hili limetokana

na kuimarika kwa mifumo ya upatikanaji haki ikiwemo ushirikishwaji wa wadau katika huduma za msaada wa kisheria.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeandaa rasimu ya Sera ya Kitaifa ya Huduma za Msaada wa Kisheria pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo. Aidha, Mpango Kazi wa Kitaifa wa Msaada wa Kisheria wa miaka mitano (2026/2027–2030/2031) umeandaliwa. Vilevile, Wizara imeandaa miongozo minne (**4**) ambayo ni: Mwongozo wa Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria Maeneo ya Vizuizini; Mwongozo wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Awamu ya Pili; Mwongozo wa Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria; Mwongozo wa Matumizi ya Mawakili wa Serikali katika Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria; na Mwongozo wa Utendaji Kazi wa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria katika Kutekeleza Majukumu ya Uwakili wa mwaka 2026 (GN. Na. 70/2026). Lengo la Sera, Miongozo na Mkakati huo ni kuweka misingi ya kuimarisha upatikanaji na uendelevu wa huduma za msaada wa kisheria ngazi ya kijamii. Pia, Wizara imeingia makubaliano na Chuo Kikuu cha Dodoma kuimarisha utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kupitia kliniki za msaada wa kisheria na tafiti, pamoja na kushirikiana na *Legal Services Facility* (LSF) kuboresha huduma za wasaidizi wa kisheria ngazi ya jamii.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Awamu ya Kwanza, Wizara imekamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Awamu ya Pili (MSLAC II) utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2026/2027 - 2029/2030). Mkakati huu unalenga kuimarisha mafanikio yaliyopatikana na kushughulikia changamoto zilizojitokeza, kwa kuweka msisitizo katika kuyafikia maeneo na makundi yenye uhitaji mkubwa; kuboresha ubora na ufanisi wa huduma; pamoja na kuanzisha na kuimarisha mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini, usimamizi wa mashauri na mifumo endelevu ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria katika ngazi zote za utawala na mnyororo wa upatikanaji haki.

### (ii) Kushughulikia Masuala ya Kikatiba Pamoja na Kutoa Elimu ya Katiba na Uraia kwa Umma

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua kuwa msingi imara wa utawala bora, haki na maendeleo endelevu ya taifa letu unategemea uwepo wa mfumo madhubuti wa kikatiba unaoeleweka na kuheshimiwa na wananchi wote. Wananchi wanapofahamu misingi ya Katiba na Utawala bora, hujenga tabia ya kuheshimu sheria, taasisi za umma na viongozi waliopo madarakani. Hali hii hupunguza migogoro isiyo ya lazima na kuimarisha amani na utulivu wa nchi katika juhudi za kujenga taifa lenye misingi imara ya uzalendo.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara imeendelea kuchukua hatua mahsusi kwa kutoa mafunzo ya elimu ya uraia na utawala bora kwa Wananchi **9,906** sawa na ongezeko la asilimia **94** ikilinganishwa na Wananchi **5,111** waliopatiwa mafunzo katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2024/2025. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo Wananchi kuhusu uelewa wa haki na wajibu wao kwa kuzingatia Katiba na sheria za nchi.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) imechopeka (*insert*) maudhui ya Katiba na uraia katika mitaala ya shule za awali, msingi na sekondari kwa ajili ya kuendelea kufundishwa. Aidha, Wizara imeandaa Hati ya Makubaliano na Chuo Kikuu  Mzumbe kwa lengo la kuandaa maudhui ya Katiba na maadili katika Mitaala ya Chuo hicho ili yaanze kufundishwa katika somo la Katiba na Maadili.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi-VETA imekamilisha uandaaji wa maudhui ya elimu ya Katiba na uraia yatakayofundishwa katika vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi katika somo la Stadi za Maisha. Aidha, Mwongozo wa kufundishia elimu ya katiba na uraia na nyenzo za ufuatiliaji na tathmini vimeandaliwa. Vilevile, jumla ya wakufunzi **26** na walimu **80** kutoka katika Kanda zote tisa (**9**) za VETA wamepatiwa mafunzo. Somo hili limeanza kufundishwa rasmi Machi, 2026.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha misingi ya utawala bora, demokrasia na utawala wa sheria ndani na nje ya mipaka

ya nchi yetu, Wizara ilishiriki katika misheni za uangalizi wa chaguzi zinazoandaliwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC. Aidha, Wizara ilishiriki katika chaguzi zilizofanyika katika visiwa vya Jamhuri ya Ushelisheli Septemba, 2025 na Jamhuri ya Malawi Oktoba, 2025. Ushiriki wa Wizara katika misheni hizi una nafasi ya kipekee katika kuendeleza na kulinda misingi ya kidemokrasia inayotambuliwa kimataifa.

**(iii) Kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa mfumo wa Haki Jinai unaimarika Serikali imeendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Namna ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini. Maboresho hayo yamejikita katika kuhakikisha kuwa mifumo ya kisheria, kimuundo na kitaasisi inaboreshwa ili Taasisi za Haki Jinai ziweze kutekeleza majukumu yaliyokasimiwa kwao kwa ufanisi na weledi na hivyo haki jinai kupatikana kwa wote na kwa wakati.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imeandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Haki Jinai pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera. Ni matarajio ya Serikali kuwa, Sera hiyo itatoa mwongozo wa jumla kuhusu namna ya kufanyia kazi masuala ya haki jinai ili kuimarisha utawala bora na hivyo kufikia malengo ya Serikali yaliyomo kwenye mipango ya kitaifa na kimataifa ambayo Serikali imeridhia. Vilevile, Mwongozo wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa majukumu ya mfumo wa Taasisi za Haki Jinai nchini umeandaliwa. Lengo la mwongozo huu ni kuhakikisha kuwa Taasisi za Haki Jinai zinatekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria, usawa na kwa wakati.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** muundo wa Wizara umeboreshwa kwa kuanzisha Divisheni ya Ulinzi wa Watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi. Lengo la kuanzishwa kwa divisheni hiyo ni kutoa ulinzi, motisha na kulipa fidia kwa watoa taarifa fiche za uhalifu na mashahidi ili kuwaongezea imani, kuimarisha usalama na hivyo kuwezesha ushahidi kupatikana kwa wakati.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali inajenga Mfumo Jumuishi wa TEHAMA wa Haki Jinai *(Criminal Justice Single Window System)*. Ujenzi huo ni jitihada za kuhakikisha Mifumo ya TEHAMA inasomana kulingana na majukumu ya kila mdau wa Haki Jinai na hivyo kurahisisha utendaji wa majukumu na kuimarisha uwazi miongoni mwa Taasisi za Haki Jinai. Ujenzi wa Mfumo unaendelea na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2026.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imefanya mapitio ya muundo wake na kuanzisha Kitengo kinachoshughulikia Taasisi za Haki Jinai kama ilivyopendekezwa na Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini. Kitengo hicho kimeanza kutekeleza majukumu yake ambapo katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026 jumla ya malalamiko **69** yanayohusu ucheleweshwaji wa mashauri ya jinai, kunyimwa dhamana na matumizi mabaya ya madaraka yalipokelewa. Malalamiko hayo yanaendelea kufanyiwa kazi ili kuyahitimisha.

**(iv) Kubainisha na Kutatua Migogoro ya Kisheria kwa Wananchi na Wadau Wengine**

49. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imejikita katika kuimarisha mifumo ya utoaji haki jinai na haki madai ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wote na kwa wakati. Aidha, Serikali inatambua upatikanaji wa haki kwa usawa, uwazi na kwa wakati ni nguzo muhimu ya utawala bora, inayoleta amani na maendeleo endelevu ya Taifa.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini imeendelea kubainisha na kufanyia kazi migogoro ya kisheria inayotokana na usajili na usimamizi wa bodi za wadhamini na udhamini wa umma, mirathi, ufilisi na udhamini. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wakala ulipokea migogoro **32** ya bodi za wadhamini ambapo migogoro sita **(6)** ilitatuliwa kwa njia ya majadiliano na migogoro **26** ipo katika hatua mbalimbali za usuluhishi.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imepokea malalamiko **1,527** kupitia Kituo cha Huduma kwa Mteja ambapo kati ya hayo, malalamiko **1,322** sawa na asilimia **86.5** yamefanyiwa kazi na kuhitimishwa na malalamiko **205** yanaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali za utatuzi. Katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025 yalipokelewa malalamiko **1,024** ambapo **584** yalihitimishwa sawa na asilimia **57**. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha Kituo cha Huduma kwa Mteja ambapo imepita katika mikoa **14** ambayo ni Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Tabora, Geita, Bukoba, Kigoma, Mwanza, Mara, Simiyu na Dodoma kwa lengo la kuhamasisha kupitia vyombo vya habari ili wananchi wakifahamu na kukitumia kituo ipasavyo katika kuwasilisha malalamiko na changamoto mbalimbali za kisheria. Vilevile, Wizara imeanzisha programu maalum ya ***SEMA NA WAZIRI*** ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 17 Machi, 2026. Programu hii inalenga kutoa fursa kwa wananchi kupiga simu na kuhudumiwa moja kwa moja na Mheshimiwa Waziri katika masuala mbali mbali ya kisheria, kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi pamoja na kurahisisha utatuzi wa changamoto.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wananchi wanafanya shughuli zao za kijamii na kiuchumi kwa amani, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeendelea kupokea na kufanyia kazi malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Tume ilipokea malalamiko **143** na kuyafanyia kazi, malalamiko hayo yalihusu migogoro ya ardhi, uchafuzi wa mazingira, ukamataji na mauwaji ya mifugo, fidia ya mali, kutolipwa mafao, kushushwa cheo kiuonevu, kubomolewa nyumba na matumizi mabaya ya Madaraka. Katika malalamiko hayo **96** yalifungwa na **47** yanaendelea kufanyiwa kazi, ikilinganishwa kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2024/2025 malalamiko **113** yalipokelewa na **45** yalifungwa sawa na ongezeko la asilimia **53.12**.

### (v) Kuimarisha Mifumo ya Utoaji Haki ili Haki Ipatikane kwa Wote na kwa Wakati

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pamoja na Taasisi zake imeendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki kwa kufanya mageuzi ya kisheria, kimuundo na kiutendaji kwa lengo la kuhakikisha haki inapatikana kwa wote kwa usawa na kwa wakati. Jitihada hizi zinahusisha uboreshaji wa sheria, kuimarisha taasisi, pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa kutumia mbinu na teknolojia za kisasa ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imepokea maombi **63** ya nyongeza ya muda wa kufungua mashauri mahakamani ambapo maombi **49** yamehitimishwa na **14** yanaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, maombi **36** ya kuwaachilia huru wahalifu wenye changamoto ya afya ya akili yamepokelewa ambapo amri ya kuachiliwa huru kwa waalifu 36 ziliandaliwa na kutolewa. Vilevile, Wizara ilipokea maombi manne **(4)** ya kuwaachia huru wafungwa waliowekwa kizuizini chini ya uangalizi wa Rais kutokana na umri mdogo ambapo Amri za kuachilia huru wafungwa wawili zimetolewa na nyingine mbili **(2)** hazijatolewa kwa kuwa maombi hayo hayajakidhi vigezo vya kisheria.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** suala la kuharakisha usikilizaji wa mashauri mahakamani ni moja ya vipaumbele muhimu vya Mahakama ya Tanzania katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata haki kwa wakati. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 kulikuwa na jumla ya mashauri **205,038** mahakamani; kati ya hayo **45,187** tulianza nayo mwaka 2024/ 2025 yaani yalikuwepo kabla ya tarehe 30 Juni, 2025 na mashauri **159,851** yalifunguliwa katika mwaka wa fedha 2025/2026. Kati ya mashauri **205,038** yaliyokuwepo, mashauri **166,553** yalisikilizwa na kuhitimishwa na mashauri **38,485** yanaendelea katika hatua mbalimbali. Aidha, mashauri yenye umri mrefu mahakamani ni **3,675**. Muda unaotafsiriwa kama ni umri mrefu kwa mashauri ni yale yanayozidi miaka miwili **(2)** kwa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu; mwaka mmoja **(1)** kwa Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya; na miezi sita **(6)** kwa Mahakama za Mwanzo. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kasi ya uondoshaji wa mashauri Mahakamani *(case clearance rate)* ni asilimia **104** ikilinganishwa na asilimia **105** katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Uwezo wa umalizaji wa mashauri *(disposal rate)* ni asilimia

**81** ikilinganishwa na asilimia **85** kwa kipindi kama hicho mwaka 2024/2025**.**

56. ***Mheshimiwa Spika,*** usikilizaji na umalizaji wa haraka wa mashauri yaliyopo mahakamani una mchango mkubwa kwa Taifa kiuchumi na kijamii. Mathalan, katika zoezi maalum la kusikiliza mashauri ya kiuchumi na kibiashara lililofanywa na Mahakama Oktoba na Novemba, 2025 lilifanikisha umalizaji wa mashauri **2,973.** Kuhitimishwa kwa mashauri hayo kuliwezesha kuachilia jumla ya shilingi **trilioni 13.1** zilizokuwa zimeshikiliwa na mashauri hayo kuingia kwenye mzunguko wa Uchumi.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** ukaguzi na usimamizi wa shughuli za kimahakama katika ngazi ya Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo kwa Kanda **20** za kimahakama umefanyika kwa asilimia **100** ikilinganishwa na Ukaguzi wa kipindi kama hiki kwa mwaka 2024/2025 uliofanyika kwa asilimia **99.7**. Matokeo ya ukaguzi huo, yamewezesha kuongeza kasi ya umalizaji mashauri mahakamani kwa kuwa huambatana na ukaguzi wa jalada moja baada ya jingine. Vilevile, magereza **129** kati ya **130** yaliyopo yalikaguliwa, sawa na asilimia **98.8** ikilinganishwa na ukaguzi wa kipindi kama hiki katika mwaka 2024/2025 uliofanyika kwa asilimia **80.2.**

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Mahakama ya Tanzania imeendelea kushirikiana na wadau wake katika mnyororo wa haki jinai ili kuhakikisha mashauri yanamalizika kwa wakati. Tarehe 12 na 13 Machi 2026 Mahakama iliitisha kikao kazi cha pamoja kilichohusisha wadau kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Chama cha Wanasheria Tanganyika, Idara ya Ustawi wa Jamii, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza pamoja na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Kupitia kikao hicho, wajumbe walijadili taarifa ya hali ya mashauri ya mlundikano hadi kufikia Desemba, 2025, hali ya mahabusi magerezani na mikakati ya kupunguza mlundikano pamoja na kuongeza matumizi ya TEHAMA kwenye usikilizaji wa rufaa na maombi. Kikao hiki kimesaidia kupata ufumbuzi wa pamoja wa changamoto mbalimbali, ikiwemo

kuongeza kasi ya umalizaji wa mashauri mahakamani, na kila mdau kutekeleza wajibu wake kwa wakati.

**(vi) Kuboresha Mfumo wa Kitaifa na Kuzingatia Mifumo ya Kikanda na Kimataifa Kuhusu Haki za Binadamu na Utawala Bora**

59. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Katiba na Sheria ina jukumu la kusimamia na kuratibu masuala ya haki za binadamu nchini, ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa mikataba na itifaki za kikanda na kimataifa ambazo nchi imeridhia. Aidha, Wizara inaendelea kuimarisha mifumo ya kitaifa ya uwajibikaji, ikiwa ni pamoja na uratibu wa taarifa, ukusanyaji wa takwimu, ushahidi, na kuhakikisha kila taasisi inawajibika kikamilifu katika utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali imeandaa rasimu ya Taarifa ya Nchi ya Hali ya Haki za Binadamu ya Mzunguko wa Nne (**4**) wa Mfumo wa Mapitio ya Kipindi Maalum (UPR) ambayo inapima na kuonesha maendeleo ya nchi katika utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu. Aidha, kwa mara ya kwanza Taasisi za Kidini (*Faith Based Organizations – FBOs*) zimeishirikisha Serikali katika maandalizi ya Taarifa yao Kivuli (*Shadow Report*) kuhusu masuala ya haki za binadamu. Taarifa hizo zitawasilishwa Umoja wa Mataifa Julai, 2026. Aidha, Wizara imeandaa taarifa mbili (**2**) za utekelezaji wa Mkataba, ambayo ni mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981 na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa mwaka 2006. Taarifa hizi zinabainisha uwazi na uwajibikaji wa Serikali, zinaongeza ufuatiliaji wa utekelezaji wa haki za binadamu na kuimarisha uwajibikaji wa Taifa katika jumuiya za kikanda na kimataifa. Taarifa hizi za utekelezaji wa mikataba na itifaki zipo katika hatua ya ukamilishaji na zinatarajiwa kuwasilishwa kwenye Kamati za Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika zinazosimamia utekelezaji wa Mikataba Juni, 2026.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeandaa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo **187** yaliyotolewa kwa Tanzania katika mzunguko wa UPR wa

mwaka 2021, kwa ajili ya kuonesha namna nchi ilivyotekeleza mapendekezo ili kulinganishwa na taarifa itakayotolewa na nchi katika mzunguko wa nne (**4)** wa UPR. Taarifa hiyo imewasilishwa Umoja wa Mataifa tarehe 10 Aprili 2026 kama taarifa kivuli (*shadow report*) kutoka Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu (*National Human Rights Institution – NHRI*). Aidha, THBUB iliandaa taarifa ya utekelezaji wa mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981 kwa kipindi cha miaka miwili (**2**) (2023 -2025), taarifa hiyo iliwasilishwa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Oktoba 2025. Taarifa hizi zinabainisha uwazi na uwajibikaji wa Serikali, zinaongeza ufuatiliaji wa utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu na kuimarisha uwajibikaji wa Taifa katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeshiriki katika majukwaa mbalimbali ya haki za binadamu ikiwemo kikao cha **60** na **61** cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa vilivyofanyika Geneva nchini Uswisi. Kikao cha **60** kilifanyika tarehe 08 Septemba hadi 08 Oktoba 2025 na kikao cha 61 kilichofanyika kuanzia Februari 23 hadi 31 Machi 2026. Vilevile, Wizara imeshiriki katika kikao cha **85** cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kilichofanyika tarehe 21 hadi 30 Oktoba, 2025, katika mji wa Banjul, nchini Gambia. Ushiriki wa Tanzania katika vikao hivyo hutoa ushahidi wa hatua mbalimbali ambazo nchi imechukua katika kulinda, kukuza na kuheshimu haki za binadamu.

**(vii) Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika Masuala ya Haki Jinai na Haki Madai**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika masuala ya kisheria ikiwemo uhalifu unaovuka mipaka, kubadilishana wahalifu watoro, ushirikiano katika masuala ya kisheria *(Mutual Legal Assistance)* na kubadilishana uzoefu katika masuala mbalimbali ya kisheria, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, Wizara na Taasisi zake imeshiriki katika mikutano mbalimbali yenye malengo mahsusi ya kuboresha mifumo ya haki jinai na haki madai. Baadhi ya mikutano na vikao hivyo ni: -

(a) Kikao cha kimataifa cha *United Nations Convention Against Corruption (UNCAC)* kilichofanyika kuanzia tarehe 1 hadi 5 Septemba, 2025 mjini Vienna nchini Austria. Kupitia kikao hicho, Tanzania ilipongezwa kwa kufanikiwa kuondolewa kwenye orodha ya nchi zinazoshukiwa kuwa na vitendo vya utakatishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na silaha za maangamizi *(Gray List Countries)*. Hatua hii ni ishara ya kuimarika kwa mifumo ya kisheria na kitaasisi ya kudhibiti uhalifu wa kifedha;

(b) Kikao cha tatu cha mkutano wa kikanda kilichofanyika kuanzia tarehe 25 hadi 26 Novemba, 2025 mjini Nairobi nchini Kenya. Kupitia kikao hicho, nchi wanachama zilikubaliana kuunda Jumuiya ya Ulinzi wa Mashahidi barani Afrika itakayosimamia masuala yote ya ulinzi wa watoa taarifa na mashahidi na kuwa na ushirikiano wa kikanda. Aidha, taratibu za kusaini tamko rasmi la pamoja zinaendelea;

(c) Mkutano wa 11 wa Mawaziri wa Kamati Maalum ya Sheria na Haki ya Umoja wa Afrika uliofanyika Jijini Nairobi, Kenya tarehe 08-15 Desemba, 2025. Katika Mkutano huo jumla ya Sheria **12** zilipitishwa na kuwasilishwa katika Mkutano Mkuu wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika. Miongoni mwa Sheria hizo ni Sheria ya Kuanzanisha Taasisi ya Fedha Afrika, Sheria nane (8) zinazosimamia Soko Huru la Biashara Afrika. Aidha, zote 12 ziliridhiwa na Wakuu wa Nchi na Serikali ili zianze kutumika;

(d) Mkutano wa 63 wa *Asian Africa Legal Consultative Organisation (AALCO*) uliofanyika Kampala, Uganda kuanzia tarehe 8 hadi 12 Septemba, 2025. Kupitia ushiriki huo, Tanzania ilinufaika kwa kupata maarifa ya kimataifa katika kuboresha Sera na sheria za ndani, pamoja na kujengewa uwezo wa kitaalamu kwa washiriki;

(e) Kongamano la 9 la Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika *(9th Tokyo International Conference on African Development - TICAD 9)*, nchini Japan kuanzia tarehe 18

hadi 23 Agosti, 2025. Kupitia kongamano hilo, Tanzania ilisaini Hati ya Ushirikiano (MoC) na Japani katika masuala ya Sheria;

(f) Kikao kazi cha wataalam kilichohusu kujifunza mbinu za kuandaa Mkataba Kifani wa Uwili wa Majadiliano ya Uwekezaji na Biashara. Kikao hicho kilichofanyika nchini India kuanzia tarehe 26 hadi 28 Agosti 2025, kwa lengo la kujifunza na kupata uzoefu kuhusu namna ya kuandaa mkataba kifani wa kuongoza majadiliano ya uwekezaji kati ya Tanzania na Nchi nyingine;

(g) Kikao cha Majadiliano ya Mkataba wa Kulinda na Kukuza Uwekezaji baina ya Tanzania na Canada kwa malengo ya kuingia mkataba mpya wa uwili kati ya Tanzania na Canada ili kuvutia uwekezaji wa kigeni. Kikao hicho kilifanyika tarehe 12 hadi 14 Novemba, 2025 nchini Canada; na

(h) Kongamano la Kikanda kuhusu Kuimarisha Mifumo ya Asili/Jadi ya Utatuzi wa Migogoro (*International Conference on Strengthening Traditional Dispute Resolution for Access to Justice*) kwa ajili ya Upatikanaji wa Haki Barani Afrika. Kongamano hili lilifanyika tarehe 25 – 26 Machi, 2026 Jijini Addis Ababa, Ethiopia. Aidha, Tanzania iliwasilisha namna ilivyo na mifumo ya kisheria ushughulikiwaji na utatuzi wa Migogoro kwa njia mbadala pamoja na kujifunza mifumo ya nchi nyingine ili kubadilishana uzoefu.

**(viii) Kuwezesha Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Sekta ya Sheria Nchini**

65. ***Mheshimiwa* Spika,** katika kutekeleza programu ya kutumia lugha ya Kiswahili kwenye utoaji wa haki na kuwawezesha wananchi kuzielewa sheria za nchi, Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imekamilisha kutafsiri sheria kuu **433** kwa lugha ya Kiswahili na kutangazwa rasmi kupitia Tangazo la Serikali Na. 659 la 2025. Sheria hizo pamoja na sheria **13** zilizotungwa katika lugha ya Kiswahili zinafanya jumla ya sheria

zote **446** kuwa katika Kiswahili. Aidha, uzinduzi wa Juzuu za Toleo la Sheria zilizofanyiwa tafsiri unatarajiwa kufanywa mwezi Julai, 2026 na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

66. ***Mheshimiwa* Spika,** katika kuwezesha utekelezaji wa sheria kuu zilizotafsiriwa katika lugha ya Kiswahili, Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria inaendelea na zoezi la tafsiri ya sheria ndogo, ambapo katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya Sheria Ndogo **229** zimetafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili ***(Kiambatisho Na. 4).***

**(ix) Kuimarisha Mifumo Kisheria na Kitaasisi katika Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala**

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua na kuthamini nafasi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro katika kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wakati, kupunguza gharama na kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa kijamii jambo linaloendana na maono ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Katika mwelekeo huo, Wizara imeendelea kuchukua hatua thabiti za kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuhakikisha njia hizi zinakuwa jumuishi, zenye ufanisi na chachu ya maendeleo endelevu ya Taifa.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imepokea maombi **332** ya wataalam wa utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Kati ya maombi hayo, maombi **205** yameidhinishwa baada ya kukidhi vigezo vya jopo la ithibati ikilinganishwa na maombi **227** yaliyopokelewa na maombi **170** yaliyoidhinishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia **21** la maombi yaliyoidhinishwa**.** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya watatuzi migogoro kwa njia mbadala **881** wamesajiliwa. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imehuisha maombi **31** ya vyeti vya watoa huduma za utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Pia, wananchi **162** wamepatiwa elimu kuhusu utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala kupitia Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Sabasaba. Aidha, jumla ya watoa huduma za utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala **881** wamepatiwa mafunzo

wakiwemo Wasuluhishi (*Arbitrators*) **362**, Wapatanishi (*Mediators*), **286**, Waendesha Maridhiano (*Reconcilators*) **101** na Waendesha Majadiliano (*Negotiators*) **132.**

69. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeboresha muundo wake kwa kuanzisha Kitengo cha Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala. Lengo la kuanzishwa kwa kitengo hicho ni kuimarisha upatikanaji haki kwa wananchi; kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani; kuimarisha huduma za usuluhishi na upatanishi; na kuimarisha uratibu wa huduma za utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imefanya ukaguzi wa watoa huduma za utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala, ambapo jumla ya wataalam **86** wa utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala pamoja na taasisi tano **(5)** zilikaguliwa. Ukaguzi huo ulibaini changamoto mbalimbali ikiwemo uelewa mdogo wa wananchi kuhusu fursa ya kutumia huduma za utatuzi migogoro kwa njia mbadala.

70. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imesimamia majadiliano ambayo yamesababisha kuhitimishwa kwa migogoro nje ya Mahakama. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya migogoro ya madai **143** yenye thamani ya Shilingi **2,828,720,740,317.35** imefanyiwa kazi. Kutokana na majadiliano kiasi Kilichodaiwa ni Shilingi **2,182,498,274,413.82,** hivyo, Serikali iliokoa Shilingi **646,222,465,903.53.** Aidha, Katika kuimarisha utendaji kazi na kulinda maslahi ya Taifa, Ofisi imeweka mikakati ya kutoa mafunzo ya kisheria kwa Viongozi wa Umma. Jitihada hizi zinalenga kuzuia migogoro, kuokoa rasilimali za umma, na kujenga uwezo wa kisheria ndani ya Serikali.

71. ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya Wajumbe **344** wa Bodi za Usuluhishi wa Ndio katika Kata zote zilizopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Wilaya ya Karagwe, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba; na Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba. Kati ya Wajumbe hao wanaume ni **205** na Wanawake ni **l39**

72. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 30 Juni 2025, Mahakama Kuu Kituo cha Usuluhishi ilikuwa na jumla ya Mashauri

**37.** Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 mashauri **238** yamepokelewa na hivyo kufanya jumla ya mashauri kuwa **275**. Kati ya Mashauri hayo, mashauri **242** yamesuluhishwa na Mashauri **33** yanaendelea katika hatua mbalimbali za usuluhishi. Mashauri yanapomalizika kwa njia ya usuluhishi yana faida kubwa, ikiwepo kuokoa muda ambao wadaawa wangeendelea na shauri Mahakamani, pamoja na kupunguza mrundikano wa mashauri Mahakamani. Aidha, upatanishi na usuluhishi unarudisha mahusiano yaliyopotea, na hivyo kuimarisha mahusiano katika jamii. Katika jitihada za kutoa elimu kuhusu masuala ya usuluhishi na upatanishi, tarehe 9 Aprili 2026 Wiki ya Usuluhishi ilizinduliwa jijini Dar es Salaam. Baada ya zunduzi huo, tarehe 13 hadi 17 Aprili 2026 Mahakama kwa kushirikiana na wadau iliendesha wiki ya usuluhishi katika mikoa yote nchini ambapo wananchi walipatiwa elimu, pamoja na huduma ya usuluhishi bila malipo.

**(x) Kuimarisha Usimamizi wa Mikataba ya Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi ambazo Wizara, Idara na Taasisi za Serikali Zimeingia na Wawekezaji**

***Mheshimiwa Spika,*** ulinzi na usimamizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi ni wajibu wa kikatiba na msingi wa uhai wa uchumi wetu. Hivyo, Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia masuala ya utajiri asili na maliasilia za nchi kwa kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinalindwa na kutumiwa kwa namna ambayo inaleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ilipokea mikataba **140** ya uwekezaji katika sekta ya utajiri asili na maliasilia na kuifanyia mapitio ili kuhakiki uzingatiwaji wa misingi ya sheria hizo. Hatua hii inalenga kuhakikisha kuwa mikataba hiyo inalinda maslahi ya Taifa na kuchangia ipasavyo katika kufikia maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Aidha, Wizara iliwajengea uwezo wataalamu **72** kutoka Wizara za Kisekta, Idara, Taasisi na Wakala za Serikali zinazohusika na ulinzi na usimamizi wa maliasilia za Nchi ili kuimarisha uelewa wa pamoja katika usimamizi wa rasilimali hizo. Vilevile, viongozi na watendaji **244** wa Serikali walijengewa uwezo kuhusu faida na changamoto za mikataba ya kukuza na kulinda uwekezaji (BITs).

74. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara imeandaa Mwongozo wa Tathmini na Ufuatliaji wa Uzingatiwaji wa Misingi ya Sheria za Usimamizi wa Utajiri Asili na Maliasilia Nchi. Lengo la Mwongozo huo ni kufanya tathmini ya uzingatiwaji wa utekelezaji wa sera, Sheria na Kanuni za kisekta kwa kuhakikisha kuwa nchi inapata mapato stahiki yanayotokana na uwekezaji katika miradi ya utajiri asili na maliasilia, wananchi wanashirikishwa ipasavyo katika miradi ya uwekezaji na makampuni yanatekeleza wajibu wake kwa jamii. Pia, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uendeshaji wa Kamati na Mabaraza ya Usimamizi wa Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi kuanzia ngazi ya Taifa hadi Kijiji.

75. **Mheshimiwa Spika,** suala la ulinzi na usimamizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi ni mtambuka na linahitaji uratibu jumuishi na uelewa wa pamoja miongoni mwa wadau. Kwa kutambua hilo, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara iliwajengea uwezo maafisa viungo kutoka Wizara Idara na Taasisi za Kisekta wapatao **250** katika masuala yanayohusu umuhimu wa kuzingatia misingi ya Sheria Sura 449 na 450 katika uwekezaji kwenye utajiri asili na maliasilia za za nchi'; Aidha, katika kipindi hicho Jumla ya wananchi **509** walipata elimu kuhusu maudhui ya Sheria Sura 449 na 450 na namna wanavyoweza kushikriki katika fursa zinazopatikana katika uwekezaji kwenye utajiri asili na maliasilia za nchi. Vilvile, katika kipindi hicho viongozi na watendaji **352** wa Serikali walijengewa uwezo kuhusu faida na changamoto za mikataba ya kukuza na kulinda uwekezaji (BITs) pamoja na mbinu mbalimbali za usimamizi wa rasilimali, kwa lengo la kukuza uzalendo na utaifa katika kulinda maslahi ya Taifa.

### (xi) Kuimarisha Usimamizi, Ufuatiliaji na Majadiliano ya Mikataba

77. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jukumu la kuimarisha upekuzi, usimamizi, majadiliano na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba. Jukumu hilo linalenga kuimarisha uthabiti katika utekelezaji wa mikataba hiyo; kulinda thamani ya fedha ili kuleta matokeo yanayokusudiwa; kupunguza na kudhibiti vihatarishi; na kutambua mapema

uwezekano wa kuvunjika kwa mikataba isiyo na manufaa ambayo inaweza kuisababishia Serikali hasara.

78. ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanya upekuzi wa Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa **2,562** ikilinganishwa na Mikataba **2,311** iliyofanyiwa upekuzi katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia **10**. Upekuzi huo umeimarisha ulinzi wa maslahi ya Serikali, kupunguza hatari za hasara za kifedha, kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma, na kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa kuzingatia sheria na mikataba yenye tija kwa wananchi. Vilevile, Ofisi ilikamilisha upekuzi wa Hati za Makubaliano (*Memoranda of Understanding*) **396** ikilinganishwa na hati **514** zilizofanyiwa upekuzi katika kipindi hicho kwa mwaka 2024/2025**.** Hatua hii imeimarisha diplomasia ya kisheria, kuhakikisha ushirikiano wa kimataifa unaleta manufaa ya kiuchumi na kijamii, na kupunguza vihatarishi vinavyoweza kujitokeza katika utekelezaji wa makubaliano hayo.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya mikataba **2,562** iliyofanyiwa upekuzi, mikataba **443** ilithaminishwa katika sarafu mbalimbali ambapo, Mikataba **354** ilikuwa na thamani ya Shilingi **Trilioni 4.74**; Mikataba **72** ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani **2,200,246,254.54** sawa na Shilingi **Trilioni 6.4**; Mikataba **13** ilikuwa na thamani ya Fedha ya Jumuiya ya Ulaya (Euro) **1,114,102,270.38** sawa na Shilingi **Trilioni 3.3** na Mikataba minne (**4**) ilikuwa na thamani ya fedha ya Pauni (GBP) **881,138,752.00** sawa na Shilingi **Trilioni 3.04**. Mikataba iliyofanyiwa upekuzi ilihusisha masuala ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo, utoaji huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, hospitali na barabara.

80. ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imesimamia mikataba **2,821** iliyosainiwa kati ya Serikali na wadau mbalimbali. Aidha, Ofisi ilipokea maombi ya kuvunja mikataba saba **(7)** ambapo ilishauri mikataba mitano **(5)** ivunjwe kwa mujibu wa masharti ya mikataba husika na mikataba miwili **(2)** ilishauriwa isivunjwe badala yake utekelezaji uendelee kwa mujibu wa masharti ya mikataba. Hatua hii imesaidia mikataba kukamilika kwa wakati au kuhitimishwa salama kwa kufuata

utaratibu wa kimkataba. Hivyo, kuokoa gharama ambazo zingeweza kutokea kutokana na uvunjaji wa mikataba usiozingatia taratibu.

81. ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imesimamia majadiliano yaliyofanikisha kusainiwa kwa mikataba tisa (**9**) yenye jumla ya thamani ya Shilingi **7,476,011,507,615.00**. Aidha, Ofisi inaendelea kusimamia majadiliano ya Mikataba ya miradi ya kimkakati ikiwemo Mradi wa Uchakataji Gesi Asilia (LNG) na Mradi wa Makaa ya Mawe na Chuma wa Liganga na Mchuchuma ili kulinda maslahi ya umma.

82. ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuimarisha misingi ya utawala bora na kufuata sheria, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali, Wakala wa Serikali, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Wananchi. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, Ofisi imetoa ushauri wa kisheria kwa maombi **1,243** yaliyopokelewa. Ushauri huu umeongeza uhalali wa maamuzi ya Serikali, kupunguza migogoro, kuimarisha utawala bora, na kusaidia taasisi za umma kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria. Kati ya maombi **1,243**, maombi **207** yalitoka Serikali Kuu (Wizarani), maombi **386** yalitoka Taasisi za Serikali, maombi **69** yalitoka kwenye Mashirika ya Umma, maombi **127** yalitoka Mamlaka za Serikali, maombi **130** Wakala wa Serikali, maombi **252** yalitoka Mamlaka za Serikali za Mtaa na maombi **72** yalitoka kwenye Makampuni.

### (xii) Kuimarisha Mfumo wa Uandishi, Ufasiri na Urekebu wa Sheria

83. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imeendelea na majukumu yake ya kuandaa miswada ya sheria; kuandaa, kuhakiki na kusimamia uchapishaji wa sheria ndogo; kutafsiri na kurekebu sheria ili kuhakikisha zinaendana na wakati uliopo na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kimazingira na kiteknolojia.

84. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imeandaa miswada ya sheria minne **(4).** Miswada hiyo ni Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali zinazotumika katika Mfumo wa Haki Jinai wa Mwaka 2026, unaojumuisha marekebisho mbalimbali katika Sheria **16**; Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026, unaojumuisha marekebisho katika Sheria **19;** Muswada wa Sheria ya Ahueni za Biashara wa Mwaka 2026; na Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026. Kati ya miswada hiyo, miwili **(2)** imesomwa kwa Mara ya Kwanza, ambayo ni Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026; na Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imeandaa, kuhakiki na kuchapisha jumla ya Sheria Ndogo **447**. Sheria hizo zinajumuisha Kanuni **107**, Notisi **145**, Amri **125**, *Sheria Ndogo* **62,** Hati saba (**7**) na Mwongozo mmoja (**1**) kama ilivyoainishwa katika ***Kiambatisho Na.5.***

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa sheria zote za nchi zinaendana na wakati na kuwarahisishia watumiaji katika kufanya rejea ya sheria husika hususan wakati wa utoaji wa haki na utekelezaji wa wajibu ikiwemo huduma za kimahakama na ukusanyaji mapato, Wizara kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imekamilisha kutoa Toleo la Urekebu la Nyongeza la Mwaka 2025 ambalo limejumuisha sheria kuu **71** zilizorekebishwa (***Kiambatisho Na.6***). Aidha, sheria hizo zimetangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 637A la 2025. Vilevile, Ofisi imefanya urekebu wa sheria ndogo **265** kama zinavyoonekana katika ***Kiambatisho Na.7***.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa sheria zinakuwa bora, wazi, na zinazotekelezeka kwa ufanisi, Wizara kupitia Ofisi Mwandishi Mkuu wa Sheria imeandaa miongozo mbalimbali ya uandishi wa sheria ikiwa ni pamoja na Mwongozo wa Urekebu wa Sheria; Mwongozo wa Ufasiri wa Sheria; Toleo la Pili la Istilahi za

Kisheria ambalo linajumuisha misamiati ya Kisekta; Mwongozo wa Uandishi wa Sheria Toleo la Pili la Mwaka 2025; Orodha ya Majina ya Sheria Kuu kwa lugha ya Kiswahili; na Mwongozo wa Uhakiki Ubora.

### (xiii) Kuongeza Uelewa kwa Watendaji wa Serikali na Wananchi kuhusu Sheria za Nchi

88. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pamoja na taasisi zake imeweka kipaumbele mahsusi katika kutoa uelewa kwa watendaji wa Serikali kuhusu huduma zinazotolewa kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali, ili kuhakikisha utekelezaji wa majukumu unazingatia misingi ya haki, uwajibikaji na weledi. Aidha, Wizara pamoja na taasisi zake imeendelea kuweka mkazo katika utoaji wa elimu kwa umma kuhusu huduma zinazotolewa kwa lengo la kuwajengea wananchi uelewa wa haki zao, wajibu wao pamoja na taratibu sahihi za kufuata ili kupata huduma hizo. Elimu hii huchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza migogoro, kuzuia ukiukwaji wa sheria na kuimarisha upatikanaji wa haki hivyo kuchochea maendeleo ya jamii yenye misingi ya utawala bora na amani.

89. ***Mheshimiwa Spika*;** Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini imeendelea kutoa elimu kwa watendaji wa Serikali na wananchi kuhusu sheria zinazosimamia usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wakala umetoa elimu ya usimamizi wa bodi za udhamini, udhamini wa umma na usajili wa ndoa za kimila kwa Watumishi **456** ambao wanahusika na utoaji wa huduma za Wakala ikiwemo Wakuu wa Wilaya **63**, Makatibu Tawala wa Wilaya **77**, Maafisa Tarafa **316** na viongozi wa dini **54** katika mikoa ya Singida, Morogoro, Iringa, Dodoma, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Njombe, Tabora na Kigoma. Aidha, wajumbe wa bodi za wadhamini **585** wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wa bodi za wadhamini kwa kuzingatia Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura 318 pamoja na sheria zinazosimamia utakatishaji wa fedha katika mikoa husika. Vilevile, Wakala umetoa elimu ya usajili wa vizazi na vifo, ndoa, udhamini wa umma na mirathi kwa wananchi kupitia vipindi vya redio **560**,

vipindi vya luninga **170**, maudhui **487** katika mitandao ya kijamii, maudhui **74** katika blogu na maudhui **85** katika magazeti.

90. ***Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, ilitoa elimu ya masuala ya kisheria katika Maonesho ya Kitaifa ya Sabasaba na Nanenane ambapo jumla ya wananchi **745,693** walifikiwa. Aidha, kupitia maonesho hayo jumla ya wadau **388** walitoa maoni na mapendekezo ya maboresho ya sheria mbalimbali. Vilevile, Tume iliandaa na kurusha vipindi vya luninga, redio na kusambaza vipeperushi **5,860** vinavyogusa maeneo **10** ya sheria (Sheria ya Kazi, Sheria ya Ardhi, Utambulisho wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sheria ya Mazingira, Hakimiliki na Hakishiriki, Usuluhishi katika Mabaraza ya Kata, Ulinzi wa Watoa Taarifa na Mashahidi, Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Uwakilishi katika Mahakama za Mwanzo na Sheria ya Ukomo wa muda).

91. ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imechukua hatua madhubuti katika kuongeza uelewa wa sheria na haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa watendaji wa Serikali na wananchi kwa ujumla. Lengo la elimu hiyo ni kujenga jamii inayotambua thamani ya utu, usawa na haki. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya vipindi **57** viliandaliwa na kurushwa kupitia vyombo vya habari ikiwemo runinga vipindi vitano **(5)** na redio vipindi **52** katika Mikoa **14** ya Tanzania bara na mitano **(5)** ya Zanzibar ambapo takribani wananchi **298,300** walipata elimu hiyo**,** ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/2025 takribani wananchi **64,550** walifikiwa.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi machi 2026 Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeendelea na utaratibu wa kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali, ikiwemo ya Jumbe Fupi *(Bulk SMS)* kupitia simu za mkononi ambapo jumbe moja inawafikia takribani wananchi **87,557.**

Aidha jumla ya nakala **19,555** za vipeperushi zimesambazwa kwa Wananchi, klabu **25** za haki za binadamu zimeanzishwa katika shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu, na

kufanya kuwa na jumla ya klabu **389**, ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/2025 kulikuwa na klabu **364**. Lengo la jitihada hizi ni kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu sheria za nchi, kuimarika kwa utawala wa sheria, na kukuza ushiriki wa wananchi katika kulinda haki zao, jambo linaloonesha dhamira thabiti ya Serikali katika kujenga jamii yenye haki, uwazi na uwajibikaji.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilitoa mafunzo kwa wadau **2,088** wakiwemo maafisa wa Jeshi la Polisi **827**, waandishi wa habari **354** na wananchi **907**. Mafunzo hayo yalitolewa katika mikoa **14** ya Tanzania bara na mitano **(5)** Zanzibar. Aidha, mafunzo yalilenga kuwajengea uelewa kuhusu wajibu na umuhimu wa kuheshimu haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi hicho, Wizara imetoa mafunzo kwa Maafisa Uchunguzi na Wapelelezi **50** kutoka katika mikoa saba (**7**) ambayo ni Dar es Salaam, Morogoro, Arusha, Mbeya, Dodoma, Mwanza na Songwe kuhusu umuhimu wa Ulinzi wa watoa taarifa na mashahidi kwa lengo la kuwajengea uwezo katika masuala ya uchunguzi na upelelezi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa Mawakili wa Serikali **596** kutoka katika Wizara, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na taasisi mbalimbali kuhusu uendeshaji na usimamizi wa mashauri ya madai na usuluhishi. Lengo la mafunzo hayo, ni kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika ngazi mbalimbali ili kupunguza matukio ya Serikali kushtakiwa pamoja na kuimarisha usimamizi wa mikataba na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi.

### (xiv) Kuimarisha Utafiti, Tathmini na Mapitio ya Sheria

96. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kufanya mapitio, tathmini na utafiti wa sheria mbalimbali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuhakikisha sheria zinaendana na mahitaji ya wakati, mabadiliko ya kijamii,

kiuchumi na kiteknolojia. Jitihada hizi zinalenga kujenga mfumo wa sheria unaochochea uwekezaji, unaolinda rasilimali za Taifa na kuimarisha utawala bora.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imefanya Utafiti, Tathmini na Mapitio ya sheria mbalimbali ikiwemo; Utafiti wa Mfumo wa sheria zinazosimamia Biashara ya Hewa ya Ukaa; Matumizi ya Akili Unde; Usajili wa Mawakili Tanzania; na Mfumo wa Sheria za kupinga maamuzi ya kiutawala nchini. Aidha, imefanya Tathmini ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi katika Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura 449; Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura 450 na Sheria ya Ugaidi, Sura 19. Vilevile, imefanya Mapitio ya Sheria ya Usuluhishi, Sura 15; Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Sura 295; Sheria ya Bima za Vyombo vya Moto (Magari), Sura 169; na Sheria ya Bima, Sura 394. Hatua hizi zinalenga kujenga msingi imara wa maboresho ya sheria na pale inapobidi, kuandaa mapendekezo ya kutungwa kwa sheria mpya zitakazowezesha uwepo wa Mifumo ya Sheria inayokidhi mahitaji ya maendeleo ya sasa na ya baadaye pamoja na kubaini kiwango cha ufanisi wa utekelezaji wa Sheria husika.

**(xv) Kuendesha Mashtaka ya Jinai na Kuimarisha Shughuli za Utenganishaji wa Mashtaka na Upelelezi**

98. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza jukumu la kuendesha kesi za jinai katika Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, kanda mbalimbali za Mahakama Kuu na kusikiliza rufaa na maombi katika ngazi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Aidha, Wizara kupitia OTM imeendelea kutekeleza Mpango wa Kutenganisha Shughuli za Mashtaka na Upelelezi ili kuimarisha utawala wa sheria na kuboresha utoaji wa haki jinai kwa wananchi kwa kuhakikisha kwamba upelelezi wa makosa ya jinai na uendeshaji wa mashtaka unafanywa na taasisi tofauti, huru na zinazowajibika. Lengo kuu ni kuimarisha utawala wa sheria, kujenga imani ya wananchi katika vyombo vya haki, kupunguza uwezekano wa ukiukwaji wa haki za binadamu, kuongeza ubora na weledi katika uendeshaji wa mashtaka na kupunguza msongamano wa

mahabusi kwa kufungua mashauri ya jinai yenye ushahidi wa kutosha pekee.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi za jinai **17,612** katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi nchini ikilinganishwa na kesi **22,813** zilizoendeshwa katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Katika kipindi hicho, kesi **14,522** sawa na asilimia **82** zilihitimishwa mahakamani ikilinganishwa na kesi **14,776** zilizohitimishwa katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Kati ya kesi zilizohitimishwa, **10,640** sawa na asilimia **73** zilihitimishwa kwa watuhumiwa kutiwa hatiani ikilinganishwa na kesi **10,438** sawa na asilimia **70.6** zilizohitimishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/2025. Aidha, Kesi **3,090** sawa na asilimia **17.5** zinaendelea mahakamani zikiwa katika hatua mbalimbali za usikilizwaji ikilinganishwa na kesi **8,037** zilizokuwa zinaendelea mahakamani katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mahakama za Watoto, Ofisi iliendesha kesi **377** ikilinganishwa na kesi **555** zilizoendeshwa katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Kati ya kesi zilizoendeshwa, kesi **336** sawa na asilimia **89.1** zilihitimishwa mahakamani ikilinganishwa na kesi **401** zilizohitimishwa katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Kati ya kesi zilizohitimishwa, **280** sawa na asilimia **83.3** zilihitimishwa kwa watuhumiwa kutiwa hatiani ikilinganishwa na kesi **312** sawa na asilimia **77.8** zilizohitimishwa kipindi kama hicho mwaka 2024/2025 na kesi **41** sawa na asilimia **10.9** zipo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji katika Mahakama za Watoto nchini ikilinganishwa na kesi **154** zilizokuwa zinaendelea katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi za jinai, na kusikiliza rufaa na maombi ya jinai katika kanda mbalimbali za Mahakama Kuu. Jumla ya kesi **2,491** ziliendeshwa katika Kanda za Mahakama Kuu ikilinganishwa na kesi **2,068** zilizoendeshwa katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Kati ya kesi zilizoendeshwa, **864** sawa na asilimia **34.7** zilihitimishwa ikilinganishwa na kesi **600** sawa na

asilimia **65.3** zilizohitimishwa katika kipindi kilichopita na kesi **1,627** zinaendelea katika hatua mbalimbali za kusikilizwa mahakamani ikilinganishwa na kesi **1,468** zilizokuwa zinaendelea katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Kesi **194** ziliendeshwa katika ngazi ya Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ikilinganishwa na kesi **71** zilizoendeshwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Kati ya kesi zilizoendeshwa, **34** sawa na asilimia **17.5** zilihitimishwa ikilinganishwa na kesi **40** zilizohitimishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025 na kesi **160** sawa na asilimia **82.5** zinaendelea mahakamani ikilinganishwa na kesi **31** sawa na asilimia **77.5** zilizokuwa zinaendelea katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya rufaa na maombi **389** ya Mkurugenzi wa Mashtaka yalisikilizwa ikilinganishwa na rufaa na maombi **288** yaliyosikilizwa katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Jumla ya rufaa na maombi **139** sawa na asilimia **35.7** yalisikilizwa na kutolewa maamuzi ikilinganishwa na rufaa na maombi **85** sawa na asilimia **29.5** yaliyosilizwa katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Aidha, rufaa na maombi **250** sawa na asilimia **64.3** yanaendelea mahakamani katika hatua mbalimbali za usikilizwaji ikilinganishwa na **203** sawa na asilimia **70.5** yaliyokuwa yanaendelea katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/2025.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya rufaa na maombi **2,773** dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka yalisikilizwa katika Mahakama Kuu ikilinganishwa na rufaa na maombi **2,226** yaliyokuwepo katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Aidha, jumla ya rufaa na maombi **1,368** sawa na asilimia **49.3** yalitolewa maamuzi ikilinganishwa na Rufaa na maombi **1,187** sawa na asilimia **53.3** yaliyotolewa maamuzi katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Aidha, rufaa na maombi **1,405** sawa na asilimia **50.7** dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka yanaendelea kusikilizwa mahakamani katika hatua mbalimbali za usikilizwaji ikilinganishwa na Rufaa na Maombi **1,039** sawa na asilimia **46.7** yaliyokuwa yanaendelea kusikilizwa katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Mahakama ya Rufani ilisikiliza jumla ya rufaa na maombi **1,280** ikilinganishwa na rufaa na maombi **1,654** ya kipindi kilichopita kwa mwaka 2024/2025. Kati ya rufaa na maombi yaliyosikilizwa, **108** sawa na asilimia **8.4** yalikuwa ya Mkurugenzi wa Mashtaka ikilinganishwa na rufaa na maombi **245** sawa na asilimia **14.8** yaliyosikilizwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Aidha, rufaa na maombi **1,172** sawa na asilimia **91.6** yalikuwa dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ikilinganishwa na rufaa na maombi **1,409** sawa na asilimia **85.2** dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Vilevile, rufaa na maombi **155** sawa na asilimia **12.1** yalisikilizwa na kuhitimishwa ikilinganishwa na rufaa na maombi **655** sawa na asilimia **39.6** yaliyosikilizwa na kuhitimishwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 na rufaa na maombi **1,125** yanaendelea kusikilizwa katika vikao mbalimbali vya Mahakama ya Rufani nchini ikilinganishwa na rufaa na maombi **132** yaliyokuwa yanaendelea kusikilizwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendelea na zoezi la utaifishaji wa mali zitokanazo na uhalifu mara baada ya kesi kuhitimishwa na Mahakama. Katika kipindi hiki, mali zilizotaifishwa ni pamoja na nyumba **10** na viwanja **16**, hati fungani zilizopo Benki kuu ya Tanzania zenye thamani ya Shilingi **490,000,000.00**, fedha taslimu Shilingi **8,543,350.00** na Dola za Marekani **1,800** sawa na Shilingi **4,626,000.00** Mali hizi zilizopatikana kwa njia ya uhalifu (mazalia ya uhalifu) ama zilizotumika kutenda uhalifu zilitaifishwa kuwa mali za Serikali. Hatua hii ya utaifishaji inadhihirisha dhamira ya Serikali kwamba hakuna mwananchi atakayenufaika na mali zitokanazo na uhalifu. Hivyo, nitoe wito kwa wananchi kuzingatia Sheria na kuepuka kutenda uhalifu kwa kuwa uhalifu haulipi.

107. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kukagua magereza na vituo vya polisi. Lengo la ukaguzi huu ni kuainisha changamoto za kiutendaji na kiupelelezi na kutoa maelekezo stahiki ya kutatua changamoto hizo kwa mujibu wa sheria. Katika kipindi cha

kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, jumla ya Magereza **94** na Vituo vya Polisi **483** vilikaguliwa ambapo mahabusi **918** waliachiwa huru kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ushahidi hafifu. Hatua hii imesaidia kupunguza mlundikano wa mahabusi katika Vituo vya Polisi na Magereza nchini.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilifanya ukaguzi wa mahabusi za watoto waliokinzana na sheria katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mbeya na Dar es salaam. Lengo lilikuwa kuangalia uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mtoto, Sura 13 na Miongozo ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Katika ukaguzi huo, watoto **19** walikutwa katika mahabusu hizo wakituhumiwa na makosa mbalimbali yasiyokuwa na dhamana kama mauaji, madawa ya kulevya na unyang'anyi wa kutumia silaha. Kupitia ukaguzi huo, jumla ya majalada **59** yalifanyiwa mapitio.

Kati ya hayo, Majalada **43** yaliandaliwa hati za mashtaka, Saba (**7**) yalirudishwa kwa upelelezi zaidi na majalada tisa (**9**) yalifungwa. Hii ilisaidia kuharakisha upelelezi na uendeshaji wa kesi hizo mahakamani. Aidha, Jumla ya mashauri **17** washtakiwa walitiwa hatiani, watatu (**3**) waliachiliwa huru na mashahuri **21** yanaendelea mahakamani katika hatua mbalimbali. Taarifa ya magereza na vituo vya polisi vilivyokaguliwa katika kipindi hiki ni kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na.8.***

109. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, imeendelea kutenganisha huduma za mashtaka na upelelezi pamoja na kusogeza huduma za kimashtaka kwa wananchi katika ngazi za mikoa na wilaya. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi ilifungua Ofisi za Wilaya katika Wilaya **10** ambazo ni Kakonko (Kigoma), Liwale (Lindi), Mkinga (Tanga), Kibiti na Kisarawe (Pwani), Sikonge na Uyui (Tabora), Nyasa na Namtumbo (Ruvuma) na Mbogwe (Geita) na hivyo kuwa na jumla ya Ofisi za wilaya **118** kati ya Wilaya **139** zilizopo nchini. Aidha, jumla ya Mawakili wa Serikali **78** wameajiriwa ili kukabiliana na upungufu wa watumishi katika ofisi za Mikoa na Wilaya.

**(xvi) Kuimarisha Uratibu, Usimamizi na Uwakilishi katika Kuendesha Mashauri ya Madai na Usuluhishi**

110. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendelea kuiwakilisha Serikali katika kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi yaliyopo na yatakayofunguliwa katika Mahakama na Mabaraza ya Usuluhishi ndani na nje ya nchi. Lengo la uwakilishi huo ni kulinda maslahi ya umma katika mashauri yanayofunguliwa na au dhidi ya Serikali ndani na nje ya nchi.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha jumla ya mashauri ya Madai **10,401,** ikilinganishwa na mashauri **9,013** yaliyoendeshwa katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi**, 2025** sawa na ongezeko la asilimia **15.4.** Kati ya mashauri hayo, **9,663** ni ya madai ya kitaifa, **34** ni ya madai ya kimataifa na **704** ni ya kikatiba na haki za binadamu. Katika kuendesha mashauri hayo, mashauri **641** yalihitimishwa. Kati ya mashauri yaliyohitimishwa, **536** ni ya madai ya kitaifa na **105** ni ya kikatiba na haki za binadamu. Katika mashauri yaliyohitimishwa Ofisi imeshinda mashauri **565** sawa na asilimia **88.1** ya mashauri yaliyomalizika kwa kipindi husika na kuokoa Shilingi **316,280,153,699.70** ambazo Serikali ingelipa endapo ingeshindwa mashauri hayo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **313,476,117,530.43** zimetokana na kuhitimishwa kwa mashauri **526** kwenye Mahakama na Shilingi **2,804,036,169.27** zimetokana na kuhitimishwa kwa mashauri **45** kwa njia ya majadiliano nje ya Mahakama.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha jumla ya mashauri **76** ya uchaguzi yakipinga matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba, 2025. Kati ya mashauri hayo **44** ni ya ubunge na **32** ni ya udiwani. Aidha, mashauri **33** yalifunguliwa Zanzibar na **43** Tanzania Bara. Mashauri **33** yaliyofunguliwa Zanzibar yapo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Vilevile, kwa mashauri **43** yaliyofunguliwa Tanzania Bara, mashauri **39** yamemalizika na **4** yanaendelea (**2** Ubunge na **2** Udiwani). Kwa mashauri **39** yaliyomalizika, Serikali ilishinda mashauri yote. Mashauri **37** bado yanaendelea katika Mahakama mbalimbali Tanzania Bara na Zanzibar. Pia, mbali na mashauri ya uchaguzi yaliyofunguliwa moja kwa moja, jumla ya mashauri **13** ya Mapitio ya Kimahakama

yaliwasilishwa katika Mahakama mbalimbali, mashauri haya hayapingi uchaguzi wa Udiwani/Ubunge moja kwa moja bali yanatokana na Uchaguzi Mkuu.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha jumla ya mashauri ya usuluhishi **251** ikilinganishwa na mashauri **209** yaliyoendeshwa katika kipindi cha Julai **2024** hadi Machi, **2025** sawa na ongezeko la asilimia **20.1.** Kati ya mashauri hayo, **221** ni ya usuluhishi wa kitaifa na **30** ni ya usuluhishi wa kimataifa. Aidha, mashauri **18** yalihitimishwa yakiwemo **17** ya usuluhishi wa kitaifa na moja **(1)** la usuluhishi wa kimataifa. Vilevile, mashauri **17** ya usuluhishi wa kitaifa yaliyohitimishwa, matatu **(3)** yalihitimishwa kwenye Mabaraza ya Usuluhishi, mawili **(2)** kwa Msuluhishi binafsi na **12** kwenye Mahakama. Pia, shauri moja **(1)** la usuluhishi wa kimataifa lilihitimishwa kwa njia ya majadiliano nje ya Baraza la Usuluhishi. Kutokana na kumalizika kwa mashauri hayo, Serikali imeokoa Shilingi **6,813,014,544.27** na Dola za Marekani **418,172,414.13,** ambazo Serikali ingelipa endapo ingeshindwa mashauri hayo.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kusimamia, kufuatilia na kupitia taratibu za uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ikiwemo kufanyia kazi notisi za siku **90** ambayo huipa Serikali nafasi ya kumaliza mgogoro bila kufika mahakamani. Ufuatiliaji huu wa mashauri unazingatia falsafa ya 4R ya Mheshimiwa. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikilenga zaidi mapatano nje ya Mahakama au mabaraza ya usuluhishi. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi imefanyia kazi notisi **765** za siku **90** zenye nia ya kuishtaki Serikali kwa kuwasiliana na taasisi husika pamoja na kufanya vikao vya majadiliano vikijumuisha wadaawa ili kufikia muafaka. Aidha, katika madai ambayo Serikali inautetezi na majadiliano ya awali yameshindikana Ofisi hutaarifu taasisi daiwa kuandaa utetezi iwapo mdai atawasilisha madai yake mahakamani baada ya muda wa notisi kuisha. Vilevile, Ofisi hufanya ufuatiliaji kuhakikisha kuwa kila shauri linalofunguliwa mahakamani kabla ya muda wa notisi kuisha linapingwa. Hatua hii imesaidia Serikali kuepuka kulipa gharama kubwa za mashauri, riba na faini ambazo zingeweza

kutokea endapo Serikali ingeshindwa mashauri mahakamani. Kumaliza mashauri nje ya mahakama kumesaidia kuvutia wawekezaji kwa kuonyesha utayari wa serikali katika kutatua migogoro kwa njia ya mazungumzo na weledi.

**(xvii) Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu katika Sekta ya Sheria**

115. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuwekeza katika kuimarisha miundombinu ya taasisi za utoaji haki, ili kusogeza huduma za haki karibu na wananchi, na kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa taasisi hizo. Katika mwaka 2025/26, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama, na ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika mikoa na wilaya mbalimbali.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, ujenzi wa majengo mbalimbali ya Mahakama unaendelea ukijumuisha vituo Jumuishi vya Utoaji Haki tisa **(9)**, katika mikoa ya Geita, Lindi, Katavi, Njombe, Simiyu, Ruvuma, Songwe, Singida na Kusini Pemba, ambapo baadhi ya majengo yamekamilika kwa asilimia **100**, na mengine yapo katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Ujenzi wa majengo haya umewezesha kuanzishwa kwa masijala za Mahakama Kuu katika mikoa ya Njombe, Katavi, Singida, Lindi na Songwe ambapo hapo awali Wananchi walikuwa wanapata huduma za Mahakama Kuu kupitia mikoa jirani. Miradi mingine ya majengo ya Mahakama ni pamoja na kuendelea na, ujenzi wa Mahakama za Wilaya **18** na Mahakama za Mwanzo **71** katika mikoa mbalimbali. Vilevile, Mahakama inaendelea na ukarabati wa majengo ya zamani ya Mahakama Kuu Dodoma, Mwanza, Dar es Salaam na Iringa, na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu. Hali halisi ya utekelezaji wa miundombinu ya Mahakama imeoneshwa katika ***Kiambatisho Na.9.***

117. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imekamilisha ujenzi wa jengo la ofisi Makao Makuu - Dodoma na Ofisi tano **(5)** za mikoa ya kimashtaka ya Morogoro, Tanga, Njombe, Geita na Mbeya na hivyo kufikisha majengo ya Ofisi za mikoa ya kimashtaka **12** kati ya **30.** Kukamilika kwa ujenzi wa majengo haya

kumesaidia kuboresha na kusogeza huduma zaidi kwa wananchi. Aidha, Ofisi inaendelea ujenzi wa majengo ya Ofisi za Mikoa na Wilaya katika mikoa nane (**8**) ya kimashtaka ya Kinondoni, Temeke, Simiyu, Lindi, Singida, Kigoma, Songwe na Kilimanjaro. Aidha, ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wilaya sita (**6**) unaendelea katika Wilaya za Bahi, Manyoni, Hai, Kigamboni, Nzega na Mufindi. Hali ya ujenzi wa majengo haya ni kama ilivyobainishwa katika ***kiambatisho Na.9.***

118. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea na ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Taasisi za Serikali Zinazotoa Huduma za Kisheria (*Government Legal Institutions Integrated Centers* - GLIICs). Vituo Jumuishi vinajumuisha kuwepo na jengo moja linalojumuisha Taasisi za Serikali zinazotoa Huduma za Kisheria ambazo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na wadau muhimu kulingana na mahitaji. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa majengo ya Vituo Jumuishi vya Taasisi za Serikali Zinazotoa Huduma za Kisheria katika mikoa ya Mwanza umefikia asilimia **75** na Arusha asilimia **50** (***Kiambatisho Na.9***).

**(xviii) Kusimamia na Kuendeleza Elimu na Taaluma ya Sheria Nchini**

119. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo *(The Law School of Tanzania - LST)* na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto *(Institute of Judicial Administration - IJA)* imeendelea kutoa elimu ya taaluma ya Sheria nchini na mafunzo endelevu ya kimahakama kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuimarisha weledi, ufanisi na utoaji wa haki ili kuandaa wataalamu wabobevu wenye weledi na maadili katika sekta ya Sheria.

120. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (The Law School of Tanzania – LST) iliendelea kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo kwa wanafunzi wa kundi (cohort) la **39**

walipata matokeo, kundi la **40** walikuwa kwenye mafunzo ya uwandani na kundi la **41** walikuwa wakipata uzoefu kutoka kwa wataalamu darasani. Aidha, katika matokeo ya mitihani ya Septemba 2025 jumla ya watahiniwa **697** walifaulu kwenye vipengele vyote vya masomo na wengine kwenye baadhi ya vipengele vya masomo. Vilevile, katika kipindi tajwa, Taasisi ilisimamia utoaji wa mafunzo na mitihani kwa wanafunzi Wasaidizi wa Kisheria (Paralegals), katika ngazi ya cheti cha msingi cha Sheria kwa wasaidizi wa sheria ngazi ya nne *(NTA level 4)* na cheti cha elimu ya ufundi wa sheria kwa wasaidizi wa sheria ngazi ya tano *(NTA level 5)*. Watahiniwa wote wa ngazi ya cheti cha msingi cha Sheria walifaulu mitihani na kutunukiwa Cheti cha Astashahada ya Usaidizi wa Kisheria. Pia, watahiniwa wote wa ngazi ya cheti cha elimu ya ufundi wa sheria kwa wasaidizi wa sheria ngazi ya tano walifaulu na kuruhusiwa kuendelea na mafunzo ya mwaka wa pili.

121. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo imeboresha mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Maktaba *Library Management Information System (LIBMIS)*, mfumo huo unawezesha wanafunzi na wadau mbalimbali kusoma vitabu na kupata huduma za maktaba kidijitali muda na mahali popote wanapokuwa. Mfumo huo utaongeza upatikanaji wa taarifa za kisheria kwa wakati, kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za maktaba kwa njia ya kielektroniki na kuongeza ufanisi. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya vitabu **212** viliingizwa kwenye Mfumo huo ambapo jumla ya wasomaji **15,634** kutoka makundi mbalimbali ya wanafunzi na wadau wengine walihudumiwa kupitia maktaba. Idadi hiyo imeongezeka kwa asilimia **50.6** kutoka wasomaji **10,381** katika kipindi kama hicho 2024/2025.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeendelea kutoa elimu ya Sheria katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ya Sheria kwa lengo la kuandaa wataalamu wenye weledi na maadili katika masuala ya sheria na Utawala wa Haki. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Chuo kimesajili jumla ya wanafunzi **822** sawa na asilimia **82.2** ya lengo la Udahili wa wanafunzi **1,000.** Aidha, katika kipindi hicho jumla ya wanafunzi **815** walihitimu mafunzo ya ngazi

ya Astahashada na Stashahada ya Sheria ukilinganisha na wahitimu **766** waliohitimu katika mwaka **2024/2025** ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia **6.4.**

123. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeendelea Kusimamia, kuratibu na kuendeleza elimu na taaluma ya Sheria nchini kwa kushirikiana taasisi za ndani, mashirika ya kitaifa na kimataifa kama vile *Irish Rule of Law International*, *Shirika la GIZ Tanzania, Laws Africa, na* Chuo Kikuu cha *Sant' Anna School of Advanced Studies* cha nchini Italia yenye lengo la kuimarisha weledi, uelewa, na ufanisi wa maafisa wa Mahakama katika utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Chuo kiliendesha na kuratibu mafunzo ya aina mbalimbali na kuwanufaisha jumla ya washiriki **1,673** wakiwemo Waheshimiwa majaji **37** wa Mahakama ya Rufani, Waheshimiwa Majaji **104** wa Mahakama Kuu, Naibu wasajili **86**, Waheshimiwa mahakimu **1,060**, waendesha Mashtaka **75**, maafisa Ustawi wa jamii **20,** maafisa Bima **16**, wasaidizi wa kisheria **80,** maafisa misitu nane **(8),** maafisa **11** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na madalali na wasambaza nyaraka za Mahakama **157.**

**(xix) Kuwezesha Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Kusimamia Masuala ya Ufilisi na Udhamini**

124. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) unaendelea na utekelezaji wa programu mbalimbali za usajili wa matukio muhimu ya binadamu ikiwemo usajili wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano, usajili wa watoto walio na umri wa miaka 5 hadi 17 na watu walio na umri wa miaka 18 na kuendelea. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wakala umesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa **1,195,207** (Wanaume **667,970** na Wanawake **590,432**) ikilinganishwa na vyeti vya kuzaliwa **1,338,618** (Wanaume **667,970** na Wanawake **670,648**) vilivyotolewa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025. Usajili huo umegawanyika katika makundi yafuatayo: -

***a. Usajili na Utoaji vyeti vya Kuzaliwa kwa Watoto Walio na Umri Chini ya Miaka Mitano***

125. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 imesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa **377,780** (wakiume **187,757** na wakike **190,023**) kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano ikilinganishwa na vyeti vya kuzaliwa **653,841** (wakiume **327,574** na wa kike **326,267**) vya watoto wa kundi hilo vilivyotolewa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025.

***b. Usajili wa Watoto Walio na Umri wa Miaka 5 hadi 17 Waliopo Shuleni***

126. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wakala umesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa **261,577** (wakiume **130,265** na wakike **131,311**) sawa na ongezeko la asilimia tisa **(9)** ikilinganishwa na vyeti vya kuzaliwa **239,672** (wakiume **119,357** na wakike **120,315**) vya watoto wa kundi hilo vilivyotolewa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025.

***c. Usajili wa Watu Wenye Umri wa Miaka 18 na Kuendelea***

127. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wakala umesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa **555,850** (wanaume **278,370** na wanawake **277,480**) sawa na ongezeko la asilimia **25** ikilinganishwa na vyeti vya kuzaliwa **445,105** (wanaume **222,998** na wanawake **222,107**) vya watu wa kundi hilo vilivyotolewa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, Wakala umefanya uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa **471,824** kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wanaoomba mikopo kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu pamoja na wananchi kupata huduma za bima ya afya.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala ulifanya uzinduzi wa kutoa vyeti vya kuzaliwa na vifo ndani ya saa 48 mwezi Desemba 2025. Tangu uzinduzi ufanyike hadi Machi, 2026 Wakala umepokea jumla ya maombi **445,512** (**434,412** ya vizazi na **11,100** ya vifo). Kati ya maombi yaliyopokelewa **420,863** (**412,577** ya vizazi na **8,286** ya vifo) yalifanyiwa kazi na vyeti kutolewa ndani ya saa 48 sawa na asilimia **94** ya maombi yaliyopokelewa. Wakala

utaendelea kuhakikisha wananchi wanaotimiza masharti katika maombi yao wanapata vyeti ndani ya saa 48.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wakala umesajili na kutoa vyeti vya vifo **34,637** ikilinganishwa na vyeti vya vifo **35,163** vilivyotolewa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, Wakala umefanya uhakiki wa vyeti vya vifo **29,467** kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wanaoomba mikopo kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu pamoja na wananchi kupata huduma za bima ya afya. Vilevile, Wakala umesajili marejesho ya shahada za Ndoa **44,889** zilizofungwa ikilinganishwa na marejesho ya shahada za ndoa **35,052** zilizosajiliwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025. Pia, jumla ya leseni mpya **2,994** za kufungisha ndoa zilitolewa kwa viongozi wa dini na leseni **397** za kufungisha ndoa zilihuishwa. Katika kuimarisha usajili wa ndoa hususani za kimila Wakala umeanza kutoa elimu kwa Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala na Maafisa Tarafa ili watekeleze wajibu wao wa kusajili ndoa za kimila kwa kuzingatia Sheria ya Ndoa, Sura 29.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wakala umesajili na kutoa vyeti **468** vya talaka ikilinganishwa na vyeti **675** vilivyotolewa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, Wakala umesajili na kutoa vyeti **25** vya kuasili watoto ikilinganishwa na vyeti **29** vya kuasili watoto vilivyotolewa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/ 2025. Kutokana na takwimu za talaka natoa wito kwa viongozi wote waliopewa dhamana ya kufungisha ndoa, wazazi na walezi kuendelea kutoa elimu ya maadili kwa wanandoa, na kujenga utamaduni wa kuvumiliana na kutatua changamoto zinazojitokeza kwa njia ya majadiliano ili kupunguza talaka zinazo athiri malezi ya watoto kwa mustakabali wa haki zao na kusajili ndoa zilizovunjwa kwa amri ya Mahakama ili kulinda haki za kisheria.

131. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara kupitia Wakala umesajili jumla ya bodi za wadhamini **101** ikilinganishwa na bodi za wadhamini **113** zilizosajiliwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025 na kufanya jumla ya bodi zinazosimamiwa kufikia **5,306** za vyama vya siasa; vilabu

vya michezo; taasisi za kijamii; taasisi za kifamilia; na taasisi za kidini zenye mali na fedha yenye thamani ya zaidi ya shilingi **trilioni 10**. Aidha, katika kipindi husika Wakala ulipokea jumla ya maombi ya huduma za bodi za wadhamini **1,550** ambapo maombi **1,156** yalihitimishwa na **394** yanaendelea kufanyiwa kazi kama yalivyobainishwa katika ***kiambatisho Na.10***. Wakala unaendelea kufanya mageuzi ya usimamizi wa bodi za wadhamini ili kuhakikisha mali za taasisi wanazosimamia zinatumika kwa manufaa ya wanachama na wanufaika.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wakala ulipokea mirathi mipya **15** kutoka amri za Mahakama za kumwelekeza Kabidhi Wasii Mkuu kuwa msimamizi wa mirathi ikilinganishwa **14** iliyopokelewa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025 na kufanya jumla ya mirathi inayosimamiwa kufikia **129**. Katika kipindi husika mirathi moja **(1)** imefungwa baada ya kugawa mali kwa wanufaika na **128** inaendelea kufanyiwa kazi**.** Aidha, katika kipindi husika, Wakala umeandika na kutunza wosia **136** ikilinganishwa na wosia **109** zilizoandaliwa na kutunzwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia **25**. Wakala unaendelea na maboresho ya kuimarisha uandishi, uhamasishaji na uhifadhi wa wosia ili kuondoa migogoro inayojitokeza katika usimamizi wa mirathi nchini.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wakala kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali umeendesha mashauri **83** ya mirathi na usimamizi wa bodi za wadhamini katika Mahakama mbalimbali pamoja na mabaraza mbalimbali ambapo mashauri **37** yamehitimishwa na mashauri **46** yanaendelea kufanyiwa kazi ikilinganishwa na mashauri **59** ambapo **33** yalihitimishwa na **26** yanaendelea kufanyiwa kazi kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025.

### (xx) Kuwezesha Ajira, uteuzi, Kuimarisha Nidhamu na Maadili ya Watumishi wa Mahakama

134. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Utumishi wa Mahakama ina jukumu la msingi katika kusimamia rasilimali watu

ndani ya Mahakama hususan katika masuala ya ajira, teuzi, nidhamu na maadili ya watumishi. Katika kutekeleza majukumu haya Tume inalenga kuwa na watumishi wa Mahakama wenye weledi, uadilifu, uwajibikaji na wanaozingatia misingi ya utawala bora.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Tume imefanya uteuzi wa kujaza nafasi nane **(8)** za viongozi mbalimbali kwa ajili ya Mahakama wakiwemo Wakuu wa Vitengo wawili **(2)** na Wakurugenzi Wasaidizi sita **(6).** Aidha, watumishi **114** wa Mahakama walithibitishwa kazini na watumishi **1,117** waliajiriwa. Kati yao, **173** ni Mahakimu Wakazi na **944** ni watumishi wa kada mbalimbali. Vilevile, Watumishi **755** walipandishwa vyeo vya kimuundo.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia maadili ya watumishi wa Mahakama, Tume imeshughulikia Mashauri mbalimbali ya Maafisa Mahakama na Wasio Maafisa Mahakama na kutolewa uamuzi. Aidha, katika kuhakikisha Kamati za Maadili za Mkoa na Wilaya zinatekeleza majukumu yake, Tume imefanya ufuatiliaji katika mikoa ya Geita na Kagera na wilaya zake kwa lengo la kuangalia namna Kamati zinavyotekeleza jukumu la kusimamia maadili ya Maafisa Mahakama na kushauri juu ya uendeshaji wa Kamati hizo.

**(xxi) Kuimarisha Mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya Kuboresha Huduma za Kisheria Nchini**

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pamoja na Taasisi zake inaendelea kujenga mifumo mipya, kuboresha mifumo iliyopo na kuunganisha mifumo hiyo na mifumo ya Taasisi zingine za umma na sekta binafsi kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa katika sekta ya sheria nchini. Hatua hizi ni utekelezaji wa Sera ya Serikali Mtandao ya mwaka 2016 kuelekea uchumi wa kidijitali na kuhakikisha haki inapatikana kwa usawa, kwa wakati, na kwa ufanisi zaidi.

138. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea na ujenzi wa Mfumo wa Kitaifa wa Huduma za Kisheria ujulikanao kama *National Legal Information System* (NaLIS) ambao unatarajiwa kuzinduliwa Julai, 2026. Mfumo huo

utakuwa jukwaa kuu la kuunganisha huduma zote za kisheria katika mfumo mmoja jumuishi utakaorahisisha upatikanaji haki, kuongeza uwazi na kupunguza gharama na muda kwa wananchi katika kuifikia haki. Aidha, mfumo huu utawezesha kutoa elimu ya haki za binadamu na usaidizi wa kisheria kwa wananchi kwa kutumia teknolojia zinazoibukia ikiwemo Akili Unde.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Serikali inajenga Mfumo Jumuishi wa Haki Jinai *(Criminal Justice Single Window)* unaolenga kuunganisha Taasisi zote za Haki Jinai. Mfumo huo utawezesha kubadilishana taarifa, kuongeza uwajibikaji wa Taasisi za Haki Jinai, kupunguza ucheleweshwaji wa mashauri ya jinai na kuwawezesha Wananchi kufuatilia mwenendo wa mashauri hayo. Vilevile, jumla ya Kompyuta mpakato **470** zimenunuliwa kwa ajili ya watendaji katika baadhi ya Taasisi za Haki Jinai na Taasisi zinazotoa huduma za msaada wa kisheria nchini ikiwemo Wizara **(260)**, Mahakama ya Tanzania **(150)** na Sekretarieti za Mikoa **(60)**. Vitendea kazi hivi ni muhimu katika kuimarisha huduma za utoaji haki kwa wananchi.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** Mahakama ya Tanzania imeendelea kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mashauri (*eCMS*), Mfumo wa Kunukuu na Kutafsiri Mwenendo wa Mashauri (*TTS*); Mfumo wa Takwimu (*Data Hub*); Mfumo wa Taarifa za Sheria Tanzania (*TAnzLII*); na Mahakama Mtandao katika utoaji wa huduma. Katika kipindi cha Julai,2025 hadi Machi, 2026 Mahakama imeunganisha mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mashauri na mifumo ya taasisi mbalimbali ambazo ni Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Jeshi la Magereza, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Matokeo ya ujenzi, uunganishaji na matumizi ya mifumo hiyo ni pamoja na: -

(i) Kuongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri kupitia mfumo wa TTS, ambao unaondoa muda ambao Jaji ama Hakimu alikuwa anatumia kuandika mwenendo wa shauri kwa mkono;

(ii) Mfumo wa *e-CMS* umewezesha kuongeza ufanisi, na unafuu kwa wananchi kwa kuwawezesha kutolazimika kwenda

Mahakamani kufungua shauri, pamoja na kupata taarifa za shauri, na nakala za hukumu bila kwenda Mahakamani na hivyo kuokoa fedha na muda;

(iii) Mfumo wa Mahakama Mtandao *(virtual Court)* unasaidia kuharakisha usikilizaji wa mashauri, hususan kuwezesha wadaawa, na mashahidi kuhudhuria shauri bila kulazimika kufika mahakamani. Hii inaokoa muda na gharama za kufika Mahakamani kwa wadaawa, pamoja na Magereza; na

(iv) Mfumo wa *TAnzLII* unaongeza uwazi katika shuhguli za mahakama kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa, na kusaidia mahakama za chini kuboresha maamuzi kupitia upatikanaji wa haraka wa maamuzi yote ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani.

141. ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka 2025/2026, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea na maboresho ya Mfumo wa *OAGMIS II* katika *module* za *e-vetting*; *econtract management* na *e-archive*. Maboresho haya ni pamoja na kuunganisha mfumo huo na Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma *(NeST)* utakaowezesha kupokea, kuchambua na kuweza kutoa ushauri wa mikataba ya ununuzi wa Taasisi zote za Umma. Mfumo huo utawezesha masuala mbalimbali ikiwemo: -

(i) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Taasisi nunuzi kujiridhisha kuwa Ushauri wa Kisheria uliotolewa umefanyiwa kazi kabla ya hatua ya kusainiwa kwa mkataba husika;
(ii) Kurahisisha upatikanaji wa huduma za ushauri wa kisheria kwa haraka;
(iii) kupunguza urasimu na gharama za usafiri;
(iv) kuongeza uwazi na upatikanaji wa taarifa kwa wakati;
(v) kupunguza migogoro inayotokana na makosa ya Kisheria; na
(vi) kuimarisha usimamizi wa kumbukumbu, uchambuzi na upekuzi wa mikataba kwa usahihi na usalama zaidi.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini inaendelea kujenga mfumo mmoja utakaokuwa na moduli za huduma zote. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wakala umekamilisha kuandaa moduli ya vizazi na vifo na

usimamizi wa bodi za wadhamini. Aidha, katika kipindi husika huduma za usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Bodi za Wadhamini zimewezeshwa kupatikana kidijitali kupitia *eRITA* ambapo mwananchi anaweza kutuma maombi popote alipo bila kufika ofisi za Wakala na kuchagua Ofisi ya Mkuu wa Wilaya iliyo karibu kwa ajili ya kuchukua nyaraka za huduma aliyoomba. Aidha, Wakala umeunganisha mifumo yake na mifumo ya Taasisi **10** hivyo kufanya jumla ya taasisi **39** kuunganishwa na kubadilishana taarifa na Wakala. Kuunganisha mifumo hiyo kumewezesha uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa na vifo kufanyika kimfumo na wananchi kupata majibu papo hapo.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Chuo cha Uongozi wa Mahakama kimekamilisha ujenzi wa Studio ya mafunzo pamoja na Mfumo wa Utoaji Mafunzo Kielektroniki *(IJA eLMs)*. Mfumo huu utaongeza kasi ya Utoaji wa mafunzo kwa wanafunzi na watumishi wengi popote walipo na kupunguza gharama. Pia, utasaidia kuboresha mafunzo kupitia matumizi ya nyenzo za kisasa na kurahisisha ufuatiliaji wa maendeleo ya washiriki wa Mafunzo hayo. Aidha, Mfumo huu pia utachangia katika kuongeza ufanisi wa Chuo na wigo wa wanafunzi kujifunza, kusaidia mafunzo endelevu kwa watumishi bila kuathiri majukumu yao ya kazi, usimamizi wa mafunzo, uhifadhi na usambazaji wa maudhui kidijitali.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea na maboresho ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mashauri (CIMS) kwa kuongeza moduli ya usajili mashauri na barua, uratibu na ufuatiliaji wa mawasiliano ya kawaida; moduli ya kutoa taarifa; moduli ya kusajili mashauri ya zamani na moduli ya kutengeneza jalada**.** Lengo la maboresho hayo ni kuuwezesha mfumo huo kutoa taarifa sahihi, kwa wakati na kusomana na mifumo ya Taasisi nyingine za utoaji haki. Pia, Ofisi imeboresha Mfumo wa Maktaba Mtandao (*e-Library*) unaosaidia kuongeza upatikanaji wa taarifa za kisheria kwa wakati kwa kuunda *pocket library* inayowezesha watumishi kufikia machapisho nje ya mtandao (*offline*).

145. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika maktaba mtandao, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imehamia kwenye toleo jipya la *Dspace* ambalo limeboresha kasi, usalama na urahisi wa

usimamizi wa maktaba kieletroniki. Vilevile, mfumo huu umeunganisha huduma za maktaba na kanzidata za kimataifa zenye machapisho ya kiwango cha juu *Ebscohost, Emerald Insight, Oxford Journals, Sage na jusMundi* ili kuwawezesha watumishi kupata rejea sahihi na za kuaminika na zilizosawazishwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya watumiaji **187,930** wamepitia maktaba mtandao, sawa na wastani wa watumiaji **1,200** kwa siku. Hii inaonyesha kukua na kuimarika kwa matumizi ya maktaba mtandao.

146. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, imeunganisha mfumo wa *NPS-CMIS* na mfumo wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mahakama ya Tanzania, Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) unaowezesha kubadilishana taarifa. Lengo la kuunganisha mfumo huu na wadau wa haki jinai ni kurahisisha ubadilishanaji taarifa katika utoaji haki jinai kwa wakati.

147. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeendelea na maboresho ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Malalamiko (*Complaints Management Information System - CMIS*) ambao utawezesha kuchakata malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora kutoka kwa wananchi. Mfumo huu utawawezesha wananchi kuwasilisha malalamiko yao kwa urahisi na kupata taarifa juu ya kupokelewa na kufanyiwa kazi kwa malalamiko yaliyopokelewa, mfumo utaanza kutumika kwa ufanisi kwa mwaka 2026/2027 baada ya maboresho kukamilika.

### (xxii) Kuendeleza Rasilimali Watu Katika Sekta ya Sheria

148. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua kuwa rasilimali watu ndio kiungo muhimu kwa utoaji wa huduma bora za kisheria na usimamizi wa haki nchini. Katika kufikia azma ya kuwa na sekta ya sheria yenye ufanisi, uwazi na inayojibu mahitaji ya wananchi, Wizara na Taasisi zake inaendela kuajiri na kuendeleza watumishi wake kwa kuwajengea uwezo, kuimarisha weledi, na kukuza

maadili ya utumishi wa umma kupitia programu mbalimbali za mafunzo ya ndani na nje ya nchi.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha utendaji kazi wa watumishi katika sekta ya sheria, Wizara imefanya maboresho ya Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya Kada zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria. Katika maboresho hayo, Kada zimeongezeka kutoka kada moja (**1**) iliyokuwepo hadi kada **11**. Kada hizo ni Mawakili wa Serikali; Maafisa Sheria; Waandishi wa Sheria; Makatibu Sheria; Maafisa Uchunguzi; Maafisa Usajili; Makatibu Sheria Wasaidizi; Maafisa Usajili Wasaidizi; Warekebu Sheria Wasaidizi; Maafisa Sheria Wasaidizi; na Wasaidizi wa Sheria. Aidha, kuidhinishwa kwa Miundo ya Maendeleo ya Kada chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kutawezesha kuwepo kwa kada mbalimbali za kisheria hususan Kada ya Wasaidizi wa Sheria ambao watakuwa wakitekeleza majukumu hadi kwenye ngazi ya Vijiji na hivyo kurahisisha na kusogeza upatikanaji wa huduma za kisheria kwa Wananchi.

### *a. Wizara ya Katiba na Sheria*

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Katiba na Sheria ina jumla ya watumishi **643**, katika mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara imeajiri watumishi **45**, imewathibitisha kazini watumishi **449**, imepandisha cheo watumishi sita **(6),** watumishi watatu **(3)** wameteuliwa kwenye nafasi za uongozi, watumishi **10** wamehamia kutoka taasisi mbalimbali, watumishi **21** wamehama kwenda taasisi mbalimbali. Aidha, Wizara imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi **32** katika fani mbalimbali ikiwemo: - utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala; Stashahada ya Juu ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo; haki za binadamu; na Sheria kwenye Akili Unde. Pia, Wizara imewawezesha watumishi **56** kushiriki mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi **31** na nje ya nchi **25**.

### *b. Mahakama ya Tanzania*

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia Machi, 2026, Mahakama ina watumishi **6,894**. Kati ya hao, Majaji ni **141** (Mahakama ya Rufani **37** na Mahakama Kuu **104**); Naibu wasajili **78**, Mahakimu **1,596** na watumishi wengine **5,079**. Aidha, Mahakama imewezesha jumla

ya watumishi **2,736** kushiriki mafunzo ambapo watumishi **320** ni mafunzo ya muda mrefu na watumishi **2,416** mafunzo ya muda mfupi.

### *c. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

152. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Watumishi **15** wa kada mbalimbali waliajiriwa, Watumishi **21** walihamia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Watumishi **10** walipandishwa vyeo, Watumishi watatu (**3**) walibadilishwa kada, na Watumishi watatu (**3**) waliteuliwa kwa nafasi mbalimbali za uongozi. Hadi kufikia Machi, 2026 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa na jumla ya watumishi **210**. Vilevile, watumishi **17** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu (**15** mafunzo ndani ya nchi na **2** mafunzo nje ya nchi), Watumishi **192** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi (**117** mafunzo ndani ya nchi na **75** mafunzo nje ya nchi) na Watumishi **42** walipatiwa mafunzo elekezi.

### *d. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka*

153. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeajiri watumishi **182** wakiwemo Mawakili wa Serikali **127**, Makatibu Sheria **36** na Kada nyingine **19** hivyo kuwa na jumla ya watumishi **1,195.** Kati ya hao, Mawakili wa Serikali ni **813**, Makatibu Sheria ni **166** na kada nyingine watumishi **216**. Watumishi **19** wamehamia; watumishi wanne (**4**) wamehama; mtumishi mmoja (**1**) amestaafu na watumishi **77** wamethibitishwa kazini. Vilevile, watumishi **10** wamepandishwa vyeo. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imewezesha watumishi **223** katika mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi katika fani za upelelezi wa makosa ya mtandao, Sheria za makosa ya mtandao, Utaalam wa makosa ya alama na maandishi. Pia, jumla ya watumishi **261** walishiriki katika mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi.

### *e. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali*

154. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2026, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina jumla watumishi **258.** Kati ya hao, **139** ni Mawakili wa

Serikali, **18** ni Makatibu Sheria na **101** ni watumishi wa kada nyingine. Kati ya hao, watumishi saba **(7)** ni ajira mpya. Aidha, katika kipindi husika watumishi **23** walishiriki mafunzo ya muda mrefu na watumishi **74** walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika maeneo ya kimkakati. Maeneo hayo ni pamoja na usimamizi wa kimataifa wa mikataba ya ujenzi *(FIDIC)*; usuluhishi katika mikataba ya ujenzi na migogoro inayosimamiwa na Baraza la Taifa la Ujenzi *(NCC)*; usuluhishi katika mikataba ya uwekezaji kimataifa; na usuluhishi katika nyanja ya mikataba ya kibiashara na uwekezaji; na stashahada ya usuluhishi wa kimataifa. Vilevile, watumishi **162** waliwezeshwa kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kitaaluma.

***f. Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria***

155. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2026, Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria ina jumla ya Watumishi **80** ambapo kati ya hao **56** ni Waandishi wa Sheria na Mawakili wa Serikali, na **24** ni kada nyingine. Kati ya watumishi waliopo, saba **(7)** wamehamia kutoka Taasisi nyingine za Serikali. Aidha, Ofisi imewawezesha Waandishi wa Sheria watano (**5**) kuhudhuria masomo ya muda mrefu katika Shahada ya Uzamili katika fani za Uandishi wa Sheria pamoja na Kodi, na Waandishi wa Sheria tisa (**9**) kushiriki mafunzo mahsusi ya Uandishi wa Sheria yaani *Postgraduate Diploma in Legislative Drafting* yanayotolewa na Taasisi ya Uandishi wa Sheria Nchini Zambia.

***g. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora***

156. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ina jumla ya watumishi, **215** wa kada mbalimbali kati ya watumishi hao, watumishi **31** wameajiriwa na sita **(6)** wamehamia kutoka taasisi nyingine. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 Watumishi **37** wamewezeshwa kushiriki mafunzo mbalimbali kati ya hao nane **(8)** walishiriki mafunzo ya muda mrefu, **29** mafunzo ya muda mfupi katika fani za Sheria katika fani za haki za binadamu. Vilevile, watumishi tisa **(9)** walithibitishwa vyeo na **25** walithibitishwa kazini.

***h. Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania***

157. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ina jumla ya Watumishi **73** wa kada mbalimbali, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 watumishi nane (**8**) wameajiriwa, saba (**7**) wamehamia, **22** wamethibitishwa kwenye vyeo vya muundo na sita (**6**) wamepandishwa vyeo. Aidha, watumishi **36** wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi **15** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu, ambapo kati ya hao watumishi watatu **(3)** ni ngazi ya Shahada ya kwanza katika fani za Maktaba na usimamizi wa Taarifa; Utawala wa Biashara katika Usimamizi wa Rasilimali Watu; na Utawala wa Umma. Vilevile, watumishi **12** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika fani za sheria; haki za binadamu; utawala wa biashara katika usimamizi wa makampuni; ununuzi na ugavi; usimamizi wa rasilimali watu na teknolojia ya habari na mawasiliano.

***i. Tume ya Utumishi wa Mahakama***

158. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Utumishi wa Mahakama, ina jumla ya watumishi **31.** Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Tume imepandisha vyeo watumishi wawili **(2),** kuwapatia mafunzo ya uzamili watumishi watatu **(3),** watumishi sita **(6)** wamewezeshwa kushiriki mafunzo ya muda mfupi na watumishi wanne (**4)** wamewezeshwa kuhudhuria semina za kitaaluma.

***j. Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini***

159. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini - RITA una jumla ya watumishi **268**. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 watumishi **61** wameajiriwa, wanne **(4)** wamepandishwa vyeo, wanne **(4)** wamethibitishwa kwenye vyeo, watatu **(3)** wamebadilishwa kada, mmoja **(1)** amehamia, **(1)** amehama na saba **(7)** wamestaafu. Aidha, watumishi **129** wamewezeshwa kushiriki mafunzo ikiwemo **120** mafunzo ya muda mfupi na tisa **(9)** mafunzo ya muda mrefu. Kati ya watumishi waliopatiwa mafunzo ya muda mrefu watumishi wawili wamesomea fani za kimkakati ikiwemo shahada ya uzamili ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala na shahada ya uzamili wa sheria ya kampuni na biashara.

***k. Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo***

160. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ina jumla ya watumishi **75**. Kati ya hao, Wakufunzi wa ndani ni **12** na watumishi waendeshaji ni **63** katika fani mbalimbali. Aidha, Taasisi ina Wakufunzi wa muda **80** kulingana na mfumo wa ufundishaji. Katika kipindi hicho watumishi wawili **(2)** waliajiliwa, watatu **(3)** walihama, wawili **(2)** walihamia na mmoja (**1**) amestaafu. Aidha, jumla ya watumishi tisa **(9)** wameendelea na mafunzo ya muda mrefu katika Shahada ya uzamivu **(4)**, Shahada ya Uzamili **(3)**, Shahada ya Sayansi ya Usimamizi wa Maktaba **(1)** na Shahada ya Rasilimaliwatu **(1). Pia,** watumishi **28** waliwezeshwa kushiriki mafunzo ya muda mfupi. Ili kuifanya Taasisi za Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo kuwa Kitovu cha Ubora (*Centre of Excellency*) Taasisi imekuwa na ushirikiano na Taasisi za nje ya nchi zinazotoa mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo kama vile *Law Development Centre* ya Uganda na *Business Professional People (BPP)* ya London Uingereza na itaendeleza ushirikiano huo ili kupata uzoefu wa kimataifa kwenye maeneo mbalimbali.

### *I. Chuo cha Uongozi wa Mahakama – Lushoto*

161. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo Cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kina jumla ya Watumishi **105** wa fani mbalimbali kati ya hao, Wakufunzi ni **22** na watumishi waendeshaji ni **83**. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, jumla ya watumishi **13** walihama, mmoja **(1)** alihamia, nafasi moja **(1)** ya uongozi ilijazwa na watano **(5)** walipandishwa vyeo. Aidha, watumishi **105** walipatiwa mafunzo ya Muda mfupi na watumishi **10** wanaendelea na Mafunzo ya Muda mrefu katika fani za Sheria, uhasibu, uongozi na ustawi wa jamii.

## G. FURSA NA MIKAKATI

### *Fursa zilizopo*

162. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2025/26 hadi kufikia Machi, 2026 fursa kadhaa zimebainika ikiwemo: -

(i) Kuongezeka kwa hamasa kutoka kwa Viongozi na Wananchi wanaohitaji elimu ya Katiba na Uraia ili kuongeza uelewa na ushiriki wa wananchi katika utawala bora na wakidemokrasia;

(ii) Kuongezeka kwa uelewa wa umma kuhusu Sheria za Nchi na haki za banadamu hivyo kupunguza matukio ya uhalifu, uvunjaji wa haki za binadamu, kuimarika kwa utawala bora na uwajibikaji kwa wote;

(iii) Kuongezeka kwa uhitaji wa kufungamanisha mifumo ya TEHAMA ya Taasisi mbalimbali ili kuboresha upatikanaji haki kwa wakati;

(iv) Kuwepo kwa ongezeko la Wananchi wanaohitaji huduma za kisheria ikiwemo msaada wa kisheria kutokana na wigo wa elimu ya msaada wa kisheria kuongezeka;

(v) Uhitaji wa kujenga uwezo katika fani za kimkakati kwenye Sekta ya Sheria ikiwemo masuala utatuzi wa Migogoro kwa njia Mbadala, haki za binadamu, Katiba, uchambuzi wa mikataba;

(vi) Uhitaji wa kuboresha mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuwezesha mageuzi katika sekta ya sheria;

(vii) Kuwepo kwa utashi wa kisiasa wa kuimarisha na kuendeleza mifumo ya kutunga na kusimamia utawala wa sheria; na

(viii) Kuwepo kwa utayari wa wadau kushirikiana na Wizara na taasisi za sekta ya Sheria katika utoaji wa huduma za kisheria kwa Umma.

***Mikakati ya Kutumia Fursa***

163. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutumia fursa tajwa, Wizara imebuni mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na: -

(i) Kuandaa na kutoa programu za elimu ya Katiba na Uraia kwa umma kupitia vyombo vya habari, semina, warsha na mikutano ya hadhara;

(ii) Kuanzisha na kutekeleza programu na vipindi mbalimbali kwa ajili ya kutoa elimu ya masuala ya kisheria na haki za binadamu kwa umma;

(iii) Kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) kujenga, kuboresha na kufungamanisha mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Sheria;

(iv) Kuimarisha mifumo ya kitaasisi ya upatikanaji huduma za kisheria kwa wananchi wote ikiwemo huduma ya msaada wa kisheria;

(v) Kuanzisha programu maalum ya **SEMA NA WAZIRI** ili kutatua kwa haraka changamoto za kisheria kwa Wananchi;

(vi) Kujenga uwezo katika fani za kimkakati kwenye Sekta ya Sheria ikiwemo masuala ya utatuzi wa Migogoro kwa njia Mbadala, haki za binadamu, Katiba, uchambuzi wa mikataba;

(vii) Kuimarisha mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi ili kuifanya sekta ya sheria ichangie kikamilifu katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu;

(viii) Kuandaa na kutekeleza programu za mageuzi katika Sekta ya Sheria; na

(ix) Kuendelea kuimarisha ushirikiano uliopo na kubainisha ushirikiano mpya na wadau mbalimbali katika Sekta ya Sheria.

**H. MPANGO WA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027**

***a. Mwelekeo wa Sekta ya Sheria katika Mwaka 2026/2027***

164. ***Mheshimiwa Spika,*** mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2026/27 umeandaliwa kwa kuzingatia misingi ifuatayo ya kimkakati: -

(i) DIRA 2050 inayosisitiza utawala bora, haki na mifumo imara ya kisheria kama msingi wa uchumi imara;

(ii) Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2025 inayoelekeza kuimarishwa kwa upatikanaji wa haki na mifumo ya sheria;

(iii) Mpango wa Taifa wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV);

(iv) Mpango Mkakati wa Wizara na Mipango Mkakati ya Taasisi za Wizara kwa kipindi cha 2026/2027 – 2030/2031; na

(v) Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria (*Legal Sector Transformation Programme – LSTP*)**.**

165. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2026/2027, Wizara inalenga kujenga Sekta ya Sheria inayotoa haki kwa wakati, yenye ufanisi mkubwa, inayotumia teknolojia, na inayochochea maendeleo ya uchumi wa Taifa. Aidha, Wizara imejipanga kuibadilisha Sekta ya Sheria kuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi na uwekezaji, badala ya kuwa sekta ya huduma tu. Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imeainisha maeneo **15** ya kimkakati ambayo ni:-

(i) **Kuimarisha Ukuu na Maendeleo ya Katiba** kwa kuwezesha Katiba kufahamika, kutekelezwa na kuchangia kuleta maendeleo endelevu na utawala bora.

(ii) **Kuongeza wigo wa Upatikanaji Haki kwa Wananchi** kwa kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi nchini ili kufikisha huduma hadi ngazi ya kata na vijiji.

(iii) **Kuimarisha Mifumo ya Utoaji Huduma za Msaada wa Kisheria** kwa kuongeza wigo wa utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia *(MSLAC)* na kuunganisha mifumo ya Serikali katika ngazi zote hadi ngazi ya msingi.

(iv) **Kuanzisha Mfumo wa Ulinzi wa Mashahidi na Watoa Taarifa za Uhalifu** kwa kuanzisha divisheni maalum ya ulinzi na kujenga miundombinu salama ya ulinzi.

(v) **Kuimarisha Mfumo wa Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala *(ADR)*** kwa kuongeza matumizi ya usuluhishi, upatanishi, majadiliano na maridhiano na kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani.

(vi) **Kufanya maboresho ya mifumo ya Sheria ili kuwezesha utekelezaji wa DIRA 2050** kwa kuweka mifumo ya kisheria imara, inayotabirika na hivyo kuchochea uwekezaji na kulinda rasilimali za Taifa.

(vii) **Kuimarisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka** kwa kuongeza uwezo wa kusimamia mashauri ya kimataifa na kulinda Serikali dhidi ya athari hasi za kisheria.

(viii) **Kuimarisha Mifumo ya kidijitali katika Sekta ya Sheria** kwa kujenga, kuboresha na kuunganisha mifumo ya TEHAMA.

(ix) **Kuimarisha Ubora wa Utungaji wa Sheria** kwa kuendeleza ujuzi na weledi kwa wataalam wa uandishi wa Sheria ili sheria zichangie kufikia malengo ya DIRA 2050.

(x) **Kuimarisha Taasisi za Utawala Bora** kwa kujenga uwezo wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na kuimarisha uwajibikaji wa Taasisi.

(xi) **Kuimarisha Mafunzo na Utaalam wa Sekta ya Sheria** kwa kuendeleza wataalam katika maeneo ya ubobezi na kuwa na Kituo cha umahiri katika Sekta ya Sheria.

(xii) **Kuimarisha Usimamizi wa Mali za Wadhamini *(Public Trustee)*** na kuboresha huduma za mirathi na ufilisi na kulinda mali za wanufaika.

(xiii) **Kuimarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E)** kwa kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kupima utendaji katika Sekta ya Sheria.

(xiv) **Kuimarisha Ushirikiano na Taasisi zisizokuwa za Kiserikali** katika utoaji wa huduma za kisheria na kusimamia maadili na utawala bora.

(xv) **Kuimarisha Nidhamu na Uwajibikaji wa Taasisi za Umma katika Sekta ya Sheria** kwa kuweka mifumo madhubuti ya uwajibikaji na Kupunguza rushwa na matumizi mabaya ya madaraka.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali itatekeleza kwa nguvu mpya Awamu ya Pili ya *Mama Samia Legal Aid Campaign (MSLAC II)*, tukisisitiza kwamba huu siyo mpango wa kawaida wa utoaji huduma, bali ni mageuzi ya msingi ya mfumo wa haki nchini yanayolenga kuifanya haki ipatikane kwa kila Mtanzania bila ubaguzi wa eneo, kipato au hali ya kijamii. Kupitia Mpango huu, tunajenga mfumo jumuishi, unaofikiwa na Wananchi wote, unaounganisha Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Wadau wa Maendeleo, na jamii kwa ujumla ili kuhakikisha kuwa hakuna Mtanzania anayebaki nyuma katika kupata haki. Aidha, nitoe wito kwa Watendaji wote wa Serikali kuelewa na kuishi dhamira hii ya kitaifa kwamba; ***haki kwa wananchi siyo huduma ya hiari ni wajibu wa msingi wa Serikali***, na hivyo utekelezaji wa MSLAC II utasimamiwa kwa uwajibikaji, weledi na matokeo yanayopimika, ili kuimarisha utawala wa sheria, amani na maendeleo ya Taifa letu kuelekea DIRA 2050.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa maelekezo haya na utekelezaji *MSLAC II*, Wizara ya Katiba na Sheria inachukua hatua ya kihistoria na ya kimapinduzi katika kujenga mfumo wa haki unaowafikia wananchi wote. Tunadhamiria kwa dhati kugeuza msaada wa kisheria kutoka kuwa huduma ya hiari kwenda kuwa haki ya msingi ya kila Mtanzania, bila kujali mahali alipo au hali yake ya kiuchumi. Kupitia hatua hii, tunaweka msingi wa Taifa lenye haki, usawa na utulivu, ambapo sheria inakuwa nguzo ya mshikamano wa kitaifa na chachu ya maendeleo endelevu. Hatua hii inaweka msingi imara wa utekelezaji wa DIRA 2050, kwa kutambua kuwa hakuna maendeleo ya kweli bila upatikanaji wa haki kwa wote. Hivyo, ninaomba Bunge lako Tukufu liunge mkono juhudi hizi za kihistoria ili kwa pamoja tujenge Tanzania yenye haki kwa wote leo na kwa vizazi vijavyo.

168. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara na Taasisi za Wizara inapendekeza bajeti inayoweka vipaumbele

katika ujenzi wa mifumo ya TEHAMA, ulinzi wa mashahidi, Msaada wa kisheria, mafunzo ya rasilimali watu; na mapitio na marekebisho ya Sheria ili kuwezesha utekelezaji wa DIRA 2050.

169. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ufanisi na uwajibikaji wa utoaji wa huduma za msaada wa kisheria, Serikali inaelekeza kuanzishwa kwa mfumo wa kidigitali wa kitaifa wa *e-Legal Aid* ndani ya kipindi kisichozidi siku120. Mfumo huu utakuwa chombo muhimu cha kisasa kitakachowezesha usajili wa kesi kwa njia ya kidigitali, ufuatiliaji wa huduma zinazotolewa kwa wananchi, pamoja na uchambuzi wa takwimu kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi ya kisera na kiutendaji. Aidha, mfumo huu utaunganishwa na *Dashboard* ya Taifa itakayowezesha ufuatiliaji wa matokeo kwa wakati halisi, kuongeza uwazi, na kuimarisha uwajibikaji wa watendaji katika ngazi zote. Kupitia hatua hii, Serikali inalenga kujenga mfumo wa haki unaotumia teknolojia kama nyenzo ya kuhakikisha kila Mtanzania anapata haki kwa haraka, kwa ufanisi, na kwa usawa.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake pamoja na Mhimili wa Mahakama kwa mwaka 2026/2027 haukusudii tu kutekeleza shughuli za Serikali, bali umeandaliwa mahsusi ili kuzalisha matokeo ya kimkakati yanayopimika yenye mchango wa moja kwa moja katika utekelezaji wa DIRA 2050. Kwa mantiki hiyo, Wizara itajikita katika falsafa mpya ya uendeshaji wa Sekta ya Sheria kutoka Mfumo wa Sekta ya Sheria Unaotumia Rasilimali Bila Kutoa Matokeo Yanayoonekana (*input-based governance*) kwenda mfumo wa Sekta ya Sheria Unaohakikisha Haki inapatikana na Matokeo yanaonekana (*resultsbased legal governance*). Hivyo, mafanikio ya bajeti hii hayatapimwa kwa kiasi cha fedha kilichotumika, bali kwa kiwango cha matokeo yaliyopatikana kwa Wananchi, Serikali na Taifa kwa ujumla.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imefanya uamuzi wa kimkakati na uamuzi huo ni wa kuijenga upya Sekta ya Sheria Tanzania ili iwe ya kisasa, yenye ufanisi, inayotabirika, na inayoweza kushindana katika viwango vya kikanda na kimataifa. Huu ni mwelekeo unaolenga kujenga mfumo wa haki unaopatikana kwa wote,

kujenga mazingira bora ya uwekezaji, kuimarisha utawala bora na uwajibikaji na kuhakikisha Taifa linaendelea kuwa na amani na utulivu wa kudumu. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti hii inatarajiwa kuleta matokeo yafuatayo: -

(i) Kuongezeka kwa imani ya wananchi kuhusu mfumo wa haki;
(ii) Kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji nchini;
(iii) Kupungua kwa migogoro na gharama za kisheria; na
(iv) Kuongezeka kwa utawala bora na uwajibikaji.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba Bunge lako Tukufu liendelee kuisimamia na kuisadia Wizara ya Katiba na Sheria kwa ukaribu; itambue umuhimu wa kimkakati wa Sekta ya Sheria nchini; na kuiunga mkono bajeti hii kwa mtazamo wa muda mrefu kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Katika kipindi hiki cha ushindani wa kimataifa wa uwekezaji, ni lazima Taifa liwe na uwezo wa kulinda maslahi yake kupitia sheria. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha uchambuzi wa mikataba ya kimkakati (*legal due diligence*);
(ii) Kujenga uwezo wa Serikali katika majadiliano ya mikataba (*negotiation capacity*);
(iii) Kuimarisha usimamizi wa migogoro ya kimataifa ya uwekezaji; na
(iv) Kuweka mifumo ya kudhibiti athari za kisheria (*legal risk management systems*)

173. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2026/2027 umejengwa katika muktadha mpana wa kimkakati wa Taifa (*national strategic repositioning*) unaolenga kuiwezesha Tanzania kufikia hadhi mpya ya maendeleo, utulivu na ushindani wa kimataifa kuelekea DIRA 2050. Katika uchambuzi wa kina uliofanywa, Serikali imebaini ukweli usiopingika kuwa, hakuna Taifa linaloweza kufikia Dira ya muda mrefu bila kuwa na mfumo thabiti wa kisheria unaoongoza, kulinda na kuelekeza matumizi ya rasilimali kwa maendeleo ya Taifa hilo.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** katika historia ya mataifa yote yaliyofanikiwa, kuna ukweli usiopingika kuwa, hakuna Taifa lililopiga hatua ya maendeleo bila kuwa na mfumo imara wa sheria unaoaminika, unaotekelezeka, unaotabirika na unaotoa haki kwa wakati. Hivyo, katika Hotuba hii, Waheshimiwa Wabunge mliopo katika Ukumbi huu mna nafasi ya kipekee ya kuwa sehemu ya uamuzi wa kihistoria wa kuiwezesha Sekta ya Sheria kuwa msingi mkuu wa utekelezaji wa DIRA 2050. Maamuzi mtakayoyafanya ya kuidhinisha Mpango na Bajeti hii: -

(i) Yataboresupatikanaji haki kwa mamilioni ya Watanzania;
(ii) Yataongeza uwezo wa Taifa kulinda rasilimali zake;
(iii) Yataboresha mazingira ya uwekezaji na uchumi wa Taifa; na
(iv) Yataongeza zaidi imani ya wananchi kwa Serikali yao.

175. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima kubwa na kwa kuzingatia nafasi ya Bunge lako Tukufu katika ujenzi wa Taifa letu, ninaomba Bunge lako liangalie Mpango na Bajeti hii kwa jicho la kimkakati kwa kutambua kuwa uwekezaji katika Sekta ya Sheria ni uwekezaji katika msingi wa Taifa lenye haki, utulivu na maendeleo endelevu.

176. ***Mheshimiwa Spika,*** niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa Wizara ya Katiba na Sheria ipo tayari kutekeleza mpango huu kwa ufanisi wa hali ya juu; kuhakikisha uwajibikaji wa rasilimali za umma; na kufanikisha mageuzi ya kimfumo ya Sekta ya Sheria.

***b. Vipaumbele vya Wizara***

177. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara, Taasisi zake na Mhimili wa Mahakama itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za kisheria na utoaji haki kwa umma ili kuendana na Mipango ya Sekta ya Sheria nchini; na Mipango ya Kikanda na Kimataifa ili kufikia malengo yaliyopangwa kwa kipindi husika. Katika kufikia azma hiyo maeneo mahsusi ya kipaumbele yameainishwa kama ifuatavyo: -

(i) Mageuzi ya Mfumo wa Kisheria katika Haki Jinai na Haki Madai;
(ii) Ujenzi wa Miundombinu ya Upatikanaji Haki;
(iii) Kuimarisha Usimamizi na Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai na Madai;

(iv) Kuimarisha huduma za Msaada wa Kisheria kwa Wananchi;
(v) Kuimarisha Haki za Binadamu na Utawala Bora;
(vi) Kuimarisha Masuala ya Kikatiba na Elimu ya Uraia;
(vii) Kuimarisha Uwezo kwa Wataalam wa Sekta ya Sheria;
(viii) Kuimarisha Huduma za Ufilisi na Udhamini;
(ix) Kuendeleza Matumizi ya Kiswahili katika Sekta ya Sheria;
(x) Kuimarisha Mfumo wa Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala;
(xi) Kuimarisha Ulinzi wa Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi pamoja na Kulinda Maslahi ya Taifa;
(xii) Kuimarisha Uwajibikaji na Utendaji katika Sekta ya Sheria;
(xiii) Mageuzi ya Kidigitali katika Sekta ya Sheria;
(xiv) Ulinzi wa Watoa Taarifa na Mashahidi;
(xv) Mageuzi ya Sheria kwa Ajili ya Uwekezaji na Uchumi;
(xvi) Kusimamia ajira, uteuzi, nidhamu na maadili ya watumishi wa Mahakama; na
(xvii) Kuimarisha Mapitio, Tafiti na Tathmini za Sheria ili kurahisisha utekelezaji wa DIRA, 2050.

***c. Kazi Zitakazotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2026/2027***

178. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41) katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni pamoja na: -

(i) Kutoa huduma za msaada wa kisheria hadi ngazi ya msingi/kijamii na kuweka mifumo ya uendelevu wa huduma za msaada wa kisheria nchini;
(ii) Kuandaa Sera ya Taifa ya Haki Madai;
(iii) Kuandaa Mpango Kabambe wa Sekta ya Sheria;
(iv) Kutoa elimu kwa wadau kuhusu Sera ya Taifa ya Haki Jinai na Sera ya Taifa ya Msaada wa Kisheria;
(v) Kutoa elimu ya Katiba na Uraia kwa Viongozi, Watendaji na Umma kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(vi) Kutekeleza Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu, Mkakati wa Elimu ya Haki za Binadamu na Mpango Kazi wa Haki za Binadamu na Biashara;
(vii) Kuimarisha mfumo wa Utatuzi wa Migogoro kwa njia Mbadala;
(viii) Kuandaa mikataba ya usafirishaji wa watuhumiwa kati ya nchi na nchi *(extradition)*;
(ix) Kuwajengea uwezo maafisa viungo kutoka Wizara na Taasisi zinazohusika na masuala ya utajiri asili na maliasilia katika masuala yanayohusu usimamizi jumuishi wa rasilimali asilia za nchi;
(x) Kufanya usajili na usimamizi wa mirathi, bodi za wadhamini na mali za udhamini wa umma;
(xi) Kuhamasisha umma katika uandishi, uhifadhi na usajili wa wosia pamoja na kuanzisha rejista ya usajili wa watoa huduma za ufilisi nchini; na
(xii) Kutoa mafunzo ya ubobezi katika maeneo ya kimkakati ili kuchochea mageuzi katika Sekta ya Sheria.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12) katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha Mfumo wa TEHAMA wa ajira, maadili na nidhamu;
(ii) Kuimarisha Ajira na uteuzi kwa watumishi wa Mahakama;
(iii) Kuimarisha Nidhamu na Maadili ya watumishi wa Mahakama;
(iv) Kuimarisha uwezo wa Taasisi wa kutoa huduma bora pamoja na ustawi wa watumishi; na
(v) Kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya Taasisi.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16) katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha mfumo wa utoaji wa huduma za ushauri kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea,
Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali, Wakala wa Serikali, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Wananchi;

(ii) Kutoa elimu ya masuala ya kisheria na mikataba kwa Viongozi wa Umma wakiwemo Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iii) Kuimarisha majadiliano ya utatuzi wa migogoro mbalimbali nje ya Mahakama.

(iv) Kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mikataba iliyosainiwa;

(v) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha huduma za kisheria nchini ukiwemo Mfumo wa Legal Sector Management Information System;

(vi) Kuimarisha huduma za maktaba na Utafiti wa masuala ya kisheria;

(vii) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali, Wakala wa Serikali, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Wananchi; na

(viii) Kuimarisha maendeleo ya Watumishi na Usimamizi wa Rasilimali Watu.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Fungu 19) katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni pamoja na: -

(i) Kuimarisha uwakilishi na usimamizi katika kuendesha mashauri ya madai, yakiwemo mashauri ya Katiba na Haki za Binadamu, Uchaguzi, Biashara na Ardhi, yaliyopo na yatakayofunguliwa na au dhidi ya Serikali ndani na nje ya nchi;
(ii) Kuimarisha uwakilishi na usimamizi katika kuendesha mashauri ya usuluhishi yanayotokana na sekta mbalimbali yatayofunguliwa na au dhidi ya Serikali katika Mahakama na Mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi;
(iii) Kuimarisha uratibu katika kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi yaliyopo na yatakayofunguliwa na au

dhidi ya Serikali katika mahakama na mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi;

(iv) Kuanzisha na kuimarisha Ofisi za Wakili Mkuu wa Serikali katika mikoa iliyo na Masjala za Mahakama Kuu ili kusogeza huduma karibu na wadau;

(v) Kuboresha Mifumo na matumizi ya TEHAMA katika maeneo mbalimbali ili kuongeza ufanisi na ubora wa utoaji huduma;

(vi) Kuboresha mazingira ya kazi na maendeleo ya rasilimali watu; na

(vii) Kuimarisha mahusiano na mawasiliano na wadau kuhusu masuala ya kisheria katika uendeshaji wa mashauri na majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (Fungu 35) katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni pamoja na: -

(i) Kuimarisha uendeshaji mashtaka na usimamizi wa kesi za jinai;

(ii) Kuimarisha uratibu na usimamizi wa upelelezi wa makosa ya jinai;

(iii) Kuimarisha mfumo wa utaifishaji, usimamizi na urejeshwaji wa mali zinazotokana na uhalifu;

(iv) Kuimarisha ushirikiano wa masuala ya kisheria baina ya taasisi, kitaifa na kimataifa;

(v) Kuimarisha uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kutoa huduma bora pamoja na ustawi wa watumishi; na

(vi) Kuimarisha Mfumo Jumuishi wa TEHAMA wa Taasisi za Haki Jinai.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni pamoja na: -

(i) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu;

(ii) Kuimarisha uwezo katika Ukaguzi na Usimamizi wa shughuli za Mahakama;

(iii) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;
(iv) Kuboresha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma;
(v) Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai na madai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki;
(vi) Kuimarisha maendeleo ya rasilimaliwatu, ikiwa ni pamoja na mafunzo, nidhamu na maslahi kwa watumishi; na
(vii) Kuendelea kukamilisha uanzishwaji Masjala ndogo Mpya za Mahakama Kuu katika mikoa ya Simiyu, Njombe, Lindi, Katavi, Singida na Songwe.

184. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni pamoja na: -

(i) Kufanya uchunguzi wa malalamiko **150** (Mapya **100** na ya zamani **50**) yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika malalamiko **25** yaliyofanyiwa uchunguzi;
(ii) Kuimarisha na kuhamasisha elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika mikoa **20** ya Tanzania bara na Zanzibar, kurusha vipindi **130** vya redio na runinga, kuanzisha klabu za haki za binadamu katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo;
(iii) Kuimarisha na kuhamasisha matumizi ya Mifumo ya TEHAMA;
(iv) Kufungua kesi tano (**5**) za uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;
(v) Kufanya ukaguzi wa magereza **78,** vituo **37** vya polisi, shule za maadilisho moja **(1)** na mahabusu ya watoto moja (**1**) na maeneo mengine wanamozuiliwa watu katika Mikoa **20;**
(vi) Kufungua kesi tano **(5)** za uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora; na
(vii) Kuwezesha kufanyika kwa utafiti mmoja **(1)** wa kutathmini hali ya Ukatili wa Kijinsia dhidi ya Wanawake na watoto katika mikoa mitano **(5)** ya Tanzania Bara.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Fungu 59) katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni pamoja na:-

(i) Kufanya Mapitio, Tafiti na Tathmini za Sheria ili kurahisisha utekelezaji wa DIRA 2050;
(ii) Kutangaza shughuli za Tume na Kutoa elimu ya sheria kwa umma kupitia vipindi vya radio, runinga, vipeperushi, mikutano na majarida;
(iii) Kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kimataifa na kikanda;
(iv) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kutekeleza majukumu makuu ya Tume; na
(v) Kuwajengea uwezo watumishi kupitia Mpango wa Mafunzo wa miaka mitano (2025/2030) sambamba na kuboresha mazingira ya kazi na upatikanaji wa vitendea kazi.

186. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (Fungu 101) katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni pamoja na: -

(i) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika Uandishi wa Sheria;
(ii) Kuwezesha utekelezaji wa kisheria wa Dira 2050 kwa kuandaa miswada ya sheria ili kufikia malengo na shabaha zilizopangwa;
(iii) Kutoa Toleo la Urekebu wa Sheria Ndogo la Mwaka 2027;
(iv) Kutoa Toleo la Ufasiri wa Sheria Ndogo la Mwaka 2027;
(v) Kuwajengea uwezo watumishi wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria;
(vi) Kuimarisha ubora katika maandalizi ya miswada ya sheria na sheria zinazotungwa; na
(vii) Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

## I. SHUKRANI KWA WATENDAJI NA WADAU

187. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb.),

Mwenyekiti wa Kamati na Mhe. Edwin Enosy Swalle (Mb.), Makamu Mwenyekiti na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki (Mb.) Mwenyekiti wa Kamati, na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King (Mb.) Makamu Mwenyekiti kwa maelekezo na ushauri wao ambao umeleta mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Nitoe shukrani zangu pia, kwa wajumbe wa Kamati kwa uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kwa kupitisha kwa kauli moja Randama ya Makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Ninapenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa ushauri, maelekezo na maoni yote yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika maandalizi ya bajeti hii. Nawashukuru sana kwa uongozi wao na ushirikiano wanaotupatia.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Namtumbo kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao Bungeni pamoja na Viongozi na Wanachama wa Chama cha Mapinduzi katika Mkoa wa Ruvuma, akiwemo Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Katibu wa CCM Mkoa, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Namtumbo na Katibu wa CCM Wilaya ya Namtumbo. Ninawashukuru sana kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili pamoja na kuratibu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika Mkoa huo na Jimbo la Namtumbo.

189. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Jaji Mkuu wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama kwa kazi kubwa anayoifanya ya kusimamia na kuimarisha mifumo ya utoaji wa haki. Jitihada zake zimekuwa chachu ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati kwa Watanzania wote bila ubaguzi.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru Viongozi wenzangu akiwemo Mhe. Hamza Saidi Johari (Mb.), Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mhe. Zainab Athuman Katimba (Mb.), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Bw. Eliakim Chacha Maswi, Katibu Mkuu; Bw. Samwel Marco Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na Dkt. Franklin Jasson

Rwezimula, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa shughuli za Wizara.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa shukrani za dhati kwa viongozi wengine wa Mhimili wa Mahakama akiwemo Mhe. Dkt. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania; Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; na Mhe. Eva Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na wasaidizi wao.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwashukuru Wenyeviti wa Bodi za Taasisi za Wizara ambao ni Mhe. Dkt. Mary Caroline Levira, Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Mhe. Winifrida Beatrice Korosso, Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Mhe. Mathew Pauwa Mwaimu, Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu na aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Mhe. Bw. Mohamed Khamis Hamad, aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. 193.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hao, ninapenda pia kuwashukuru Viongozi wengine wa Taasisi za Wizara ambao ni Bw. Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka; Dkt. Ally Saleh Possi, Wakili Mkuu wa Serikali; Bw. Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria; Mhe. Dkt. Paul Faustine Kihwelo, Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Bw. Frank Kanyusi Frank, Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini; Bw. George Nathaniel Mandepo, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Bw. Patience Kilanga Ntwina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na Prof. Sist Joseph Mramba, Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania.

194. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kutumia nafasi hii kuwashukuru Watendaji Wakuu wa Taasisi za Wizara wakiwemo Bi. Bibiana Joseph Kileo, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka; Bi. Alice Edward Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali; Bi. Irene Joseph

Lesulie, Naibu Kabidhi Wasii Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini.

195. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, ninaishukuru familia yangu hususan Wake zangu vipenzi Bi. Imani Juma Homera na Bi. Jasmine Juma Homera na watoto wangu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kunivumilia na kunitia moyo wakati ninapokuwa natekeleza majukumu yangu ya kulitumikia Taifa. Aidha, ninawashukuru wazazi wangu Baba Mzazi, Zuberi Rajabu Homera na Mama Mzazi, Amina Mohamedi Mango kwa malezi yao na ushauri wanaonipatia mara kwa mara.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho ila siyo kwa umuhimu, ninaomba kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Pia, ninaomba nichukue fursa hii kuwashukuru wadau wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaotupatia katika utekelezaji wa majukumu ambayo Wizara imekasimiwa na Serikali.

197. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/2026 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani ikiwemo Shirika la Maendeleo la watu wa Ujerumani (GIZ), Shirika la *Irish Rule of Law International,* mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, Taasisi za fedha za Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Benki ya Dunia, Asasi za Kiraia (AZAKI), Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake (UNWOMEN), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), *Danish Institute for Human Rights* (DIHR), Jumuiya ya Madola na Maendeleo ya Uingereza (FCDO), Taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau ushiriki wa Wananchi katika kutii na kuheshimu Katiba na Sheria za nchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, ninazishukuru taasisi za elimu ya juu vikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), na Chuo Kikuu

Mzumbe (MU) kwa ushirikiano wao katika kuboresha masuala ya kisheria kitaaluma.

199. Pia, ninaishukuru Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania pamoja na makampuni ya simu yakiwemo *Halotel, Airtel Tanzania, TTCL, Vodacom Tanzania* na *MIC Tanzania (Yas)* kwa ushirikiano na michango yao endelevu katika kuimarisha huduma za kisheria na msaada wa kisheria kupitia miundombinu na huduma za mawasiliano.

Aidha, nazipongeza taasisi za kibenki ikiwemo *NMB Bank, CRDB Bank* na *Tanzania Postal Bank* kwa mchango wao katika kuwezesha huduma za kifedha na kuunga mkono juhudi za Wizara katika kufanikisha malengo yake. Ushirikiano huu umeendelea kuwa chachu ya mafanikio ya sekta na ustawi wa wananchi kwa ujumla.

## J. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/2027

### *a. Makusanyo ya Maduhuli*

199. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara, Taasisi zake na Mhimili wa Mahakama inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi **15,676,000,000.00** ikiwa ni maduhuli kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 1.**

***Jedwali Na. 1: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha, 2026/2027***

| Na. | Mafungu | Lengo la Mwaka |
|---|---|---|
| 1 | Fungu 35 | 60,000,000.00 |
| 2 | Fungu 40 | 15,571,000,000.00 |
| 3 | Fungu 41 | 45,000,000.00 |
| **JUMLA** | | **15,676,000,000.00** |

### *b. Makadirio ya Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2026/2027*

200. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **774,789,136,714** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti kwa mafungu tisa **(9)** ya Wizara na taasisi zake ni kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi Zake kwa Mwaka wa Fedha, 2026/2027**

| Fungu la Matumizi | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 152,459,788,000 |
| Matumizi Mengineyo | 484,909,718,714 |
| Miradi ya Maendeleo - Fedha za Ndani | 132,882,763,000 |
| Miradi ya Maendeleo - Fedha za Nje | 4,536,867,000 |
| **JUMLA** | **774,789,136,714** |

201. ***Mheshimiwa Spika***, kiasi hicho cha fedha kinaombwa kupitia mafungu ya bajeti yaliyo chini ya Wizara ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama**

| | |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 1,017,424,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 7,130,120,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **8,147,544,000.00** |

**Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

| | |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 4,809,900,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 52,281,434,000.00 |

| | |
|---|---|
| Miradi ya Maendeleo - Fedha za Ndani | 4,000,000,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **61,091,334,000.00** |

**Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

| | |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 5,095,940,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 36,217,836,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **41,313,776,000.00** |

**Fungu 35: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

| | |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 22,251,348,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 124,405,864,000.00 |
| Miradi ya Maendeleo - Fedha za Ndani | 15,866,110,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **162,523,322,000.00** |

**Fungu 40: Mahakama ya Tanzania**

| | |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 95,303,465,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 169,638,278,714.00 |
| Miradi ya Maendeleo - Fedha za Ndani | 18,601,200,000.00 |
| Miradi ya Maendeleo - Fedha za Nje | 4,090,000,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **287,632,943,714.00** |

**Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria**

| | |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 15,721,630,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 49,738,345,000.00 |

| | |
|---|---|
| Miradi ya Maendeleo Fedha za Ndani | 94,415,453,000.00 |
| Miradi ya Maendeleo Fedha za Nje | 446,867,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **160,322,295,000.00** |

**Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

| | |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 4,115,311,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 13,291,446,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **17,406,757,000.00** |

**Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania**

| | |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 1,556,429,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 10,555,230,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **12,111,659,000.00** |

**Fungu - 101: Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria**

| | |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 2,588,341,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 21,651,165,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **24,239,506,000.00** |

202. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027 Wizara ya Katiba na Sheria, Mhimili wa Mahakama na Taasisi zake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi **774,789,136,714.00.** Kati ya fedha hizo shilingi **152,459,788,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi, Shilingi **484,909,718,714.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi **137,419,630,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

203. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina na mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu yameainishwa kwenye vitabu vya Randama za mafungu husika ambavyo vimegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Bunge.

204. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, hoja imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba yako ya bajeti. *(Makofi)*

Sasa ninaomba nimwite, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Kwa niaba yake, ninaomba nimwite Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda. *(Makofi)*

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kuniweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kwa niaba ya Mwenyekiti na Wajumbe wote niwasilishe taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, ninaomba taarifa ya Kamati iwekwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa Mezani kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuwasilisha taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 kwa kugawanyika katika sehemu kuu tano kama iliyoainishwa katika ukurasa wa kwanza hadi ukurasa wa pili wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Kamati kufanya uchambuzi na Maoni ya Kamati juu ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2026/2027 unaotokana na masharti ya Kanuni ya 121(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hiyo imeweka masharti yanayoelekeza Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kwa mwaka unaofuata wa fedha kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafungu yaliyochambuliwa, Kamati ilichambua bajeti za mafungu nane (8) ambayo ni: -

(i) Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria;
(ii) Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
(iii) Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;
(iv) Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama;
(v) Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;
(vi) Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania;
(vii) Fungu 19 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; na mwisho;
(viii) Fungu 101 - Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, uchambuzi wa Kamati umeangazia maeneo makuu manne ambayo ni: -

(i) Makusanyo ya maduhuli kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(ii) Upatikanaji wa fedha za Bajeti kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(iii) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026; na

(iv) Uzingatiaji wa Maazimio ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makusanyo ya maduhuli hadi Februari, 2026, Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi milioni 108.3. Kati ya fedha hizo, Fungu 41, Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya shilingi 45,000,000; Fungu 35, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ililenga kukusanya shilingi 60,000,000; na Fungu 16, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ililenga kukusanya shilingi milioni 3.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli hayo hadi kufikia Februari, 2026 unaonesha Wizara kupitia mafungu ilikusanya jumla ya shilingi milioni 88.8 sawa na 81.97% ya lengo, hivyo kuvuka lengo la 66.7% iliyopanga kufikia mwezi Februari, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hicho Wizara ya Katiba na Sheria imekusanya shilingi milioni 32.80; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imekusanya shilingi 56,000,000; na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali haikuweza kukusanya kiasi chochote. Maelezo zaidi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli yanapatikana katika ukurasa wa tano hadi wa sita wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi na upatikanaji wa fedha za bajeti. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026 kwa kila fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ni kama ifuatavyo: -

(i) Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 97.7. Katika kiasi hicho, shilingi bilioni 45.2 ni matumizi ya kawaida ikujumuisha shilingi bilioni 14.2 kwa ajili ya Mishahara *(PE)* na shilingi bilioni 30.9 kwa ajili ya *OC*.

Aidha, fedha za maendeleo zilitengwa, jumla ya shilingi bilioni 52.6 ambazo shilingi bilioni 44.4 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 8.14 ni fedha za nje. Hadi kufikia Februari, 2026 fedha za

matumizi ya kawaida zilizopokelewa ni shilingi bilioni 27.4 sawa na 61% ya bajeti iliyoidhinishiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hicho kinajumuisha mishahara shilingi bilioni 9.9 na *OC* shilingi bilioni 14.7. Aidha, fedha za maendeleo zilizopokelewa ni shilingi bilioni 36.04 sawa na 68.58% ya fedha zilizoidhinishwa. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi bilioni 35.8 fedha za ndani sawa na 80.65% na shilingi milioni 224.23 fedha za nje sawa na asilimia mbili nukta saba tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inaonyesha kuwa kiwango cha mapokezi ya fedha za maendeleo kwa upande wa fedha za nje siyo cha kuridhisha, kwani zimepokelewa asilimia mbili nukta saba tano tu badala ya 66.7%. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo za ndani, hali ya mapokezi ilikidhi matakwa ya bajeti na zilipokelewa 80.65%. Kupokelewa kwa fedha hizo kumeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ikiwemo utekelezaji na kutoa huduma ya msaada wa kisheria unaojulikana kama *Mama Samia Legal Aid Campaign*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia msaada wa kisheria wananchi wengi, hususan wanyonge wasioweza kumudu huduma za ada za mawakili, walitatuliwa shida zao na hivyo kupunguza kero na malalamiko kwa jamii. Maelezo zaidi kuhusu mapokezi ya fedha za bajeti ya Fungu 41 yanapatikana ukurasa wa saba hadi wa tisa wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 16, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 40.9. Kati ya hizo fedha, shilingi bilioni 40.2 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha shilingi bilioni 35.5 kwa ajili ya *OC* na shilingi bilioni 4.7 kwa ajili ya mshahara. Aidha, shilingi milioni 788.7 zilitengwa kwa ajili ya maendeleo ambapo zote ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2026, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ilipokea fedha za matumizi ya kawaida jumla ya shilingi bilioni 24.5 sawa na 61% ya bajeti iliyoidhinishwa. Fedha hizo zinajumuisha shilingi bilioni 21.7 kwa ajili ya *OC* na shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya mshahara. Aidha, kwa upande wa fedha za

maendeleo, ofisi ilipokea kiasi cha shilingi milioni 179.3 sawa na 22% ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inaonesha kuwa kiasi cha fedha kilichopokelewa, kwa ajili ya maendeleo siyo cha kuridhisha kwani kilipokelewa kwa 22.74% tu badala ya 66.7%. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kupokelewa kwa kiasi hicho kisichoridhisha kuna uwezekano mkubwa wa kukwamisha miradi ambayo ilikusudiwa, hususan ujenzi wa ofisi Mkoani Arusha. Ili mradi ukamilike kwa wakati, Kamati inashauri fedha zilizotengwa zitolewe kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu 35, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka hii iliidhinishiwa shilingi bilioni 145.9 ambapo shilingi bilioni 130.1 ni matumizi ya kawaida, ikijumuisha shilingi bilioni 20.3 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 109.7 kwa ajili ya OC. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa zilikuwa ni shilingi bilioni 15.9 zote zikiwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya mapokezi ya fedha hizo inaonesha kuwa, hadi kufikia Februari, 2026, fedha za matumizi ya kawaida zinazojumuisha mishahara na *OC* zilizopokelewa ni shilingi bilioni 95.3 sawa na 73.27% ya bajeti iliyoidhinishwa, ambapo shilingi bilioni 79.7 ni kwa ajili ya *OC* na shilingi bilioni 15.7 kwa ajili ya mishahara. Aidha, fedha za maendeleo zilizopokelewa ni shilingi bilioni 12.8 sawa na 80.5% ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya mapokezi ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni ya kuridhisha ambapo imesaidia ofisi hii kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kushtaki na kuendesha mashauri ya jinai kwa kiasi cha kuridhisha. Aidha, licha ya mafanikio hayo, Kamati ilielezwa kuwa kufuatia ofisi kuanzisha ofisi za mashtaka za wilaya katika wilaya mbalimbali isipokuwa wilaya 21 tu, ofisi hii inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vitendea kazi muhimu kama vile magari, kompyuta pamoja na mashine za kudurufu. Maelezo zaidi ya mapokezi ya fedha hizi ya bajeti ya

Fungu 35 yanapatikana katika ukurasa wa 11 hadi 13 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu 12, Tume ya Utumishi wa Mahakama iliidhinishiwa kutumia shilingi bilioni 6.9, fedha zinazojumuisha *OC* shilingi bilioni 5.8 na mshahara shilingi bilioni 1.1. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2026, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilipokea jumla ya shilingi bilioni 3.9 sawa na 55.9% ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo, *OC* iliyopokelewa ni shilingi bilioni 3.3 sawa na 56.78%, mshahara ni shilingi milioni 555.97 sawa na 49.41%. Tathmini hii inaonesha kuwa hali ya mapokezi ya fedha kwa Fungu 12 ilikuwa ya wastani. Maelezo zaidi kuhusu mapokezi ya fedha za bajeti kwa Fungu 12 yanapatikana katika ukurasa 13 hadi ukurasa 15 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Fungu 55, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliidhinishiwa kutumia shilingi bilioni 11.7 kiasi kinachojumuisha mishahara shilingi bilioni 3.5 na OC shilingi bilioni 8.3. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Tume hii ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 9.013 kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na 76.75% ya fedha zilizoidhinishwa. Kiasi hicho kinajumuisha mishahara shilingi bilioni 2.43 sawa na 70.30% ya fedha za *OC*, shilingi bilioni 6.6 sawa na 79.44%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inaonesha kuwa, hali ya mapokezi ya fedha kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilikuwa ni ya kuridhisha, kwani ilifikia zaidi ya lengo la 66.7% na hivyo kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake ikiwemo kushughulikia na kuhitimisha malalamiko 76 yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Licha ya mafanikio hayo, Tume inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa ofisi za mkoa kwani ina ofisi katika mikoa mitano tu kati ya mikoa 31 iliyopo Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii imesababisha Tume kushindwa kuwahudumia wananchi katika mikoa 26 kadiri

ilivyotarajiwa. Maelezo zaidi kuhusu mapokezi ya fedha za bajeti kwa Fungu 55 yanapatikana katika ukurasa wa 15 hadi 17 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu 59, Tume ya Kurekebisha Sheria iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 7.4, kiasi kinachojumuisha mishahara ya shilingi bilioni 1.8 na fedha za *OC* shilingi bilioni 5.6. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Tume ya Kurekebisha Sheria ilipokea kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 3.9 sawa na 53% ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zinajumuisha mishahara ya shilingi milioni 845.8 na *OC* shilingi bilioni 3.05. Maelezo zaidi kuhusu mapokezi ya fedha za bajeti ya Fungu 59 yanapatikana katika ukurasa wa 17 na 18 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu 19, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 38.5 kiasi kinachojumuisha mishahara ya shilingi bilioni 4.8 na *OC* shilingi bilioni 33.7. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Ofisi ya Wakili Mkuu ilipokea jumla ya shilingi bilioni 22.8 sawa na 59.12% ya fedha zilizoidhinishwa. Katika kiasi hicho, mishahara ni shilingi bilioni 3.2 sawa na 67.29% na fedha za *OC* ni shilingi bilioni 19 sawa na 57.96%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inaonesha kuwa mapokezi ya fedha kwa Ofisi ya Wakili Mkuu yalikuwa ya wastani kwani fedha zilizopokelewa zilikuwa ni 59.12% badala ya 66.7%. Kupitia fedha hizo, ofisi hii imetekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kuendesha mashauri ya madai 1,398 katika kipindi cha Julai, 2025 hadi mwezi Februari, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mashauri hayo, mashauri yaliyomalizika katika kipindi hicho ni 604 sawa na asilimia tano nukta nane moja ya mashauri yote. Kamati ina mtazamo kuwa idadi ya mashauri yaliyomalizika iko chini na hivyo ofisi hii ibuni mikakati mahususi itakayowezesha mashauri mengi kumalizika mahakamani kwa wakati bila kuathiri ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, pamoja na kazi hizo, Kamati ilielezwa kuwa ofisi hii inakabiliwa na changamoto ya kukosekana

kwa majengo ya ofisi katika baadhi ya mikoa na hivyo kulazimika kutumia gharama kubwa kulipa kodi ya pango katika mikoa na kuleta ugumu wa utekelezaji wa majukumu ya kiofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa ofisi hii inasimamia na kuendesha mashauri yote ya madai mahakamani yanayohusu Serikali za Mikoa, ikiwemo mashauri ya mashirika mbalimbali ya umma na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa bila kutoza gharama yoyote, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ihakikishe Ofisi ya Wakili Mkuu inawezeshwa kwa kupewa ofisi katika hiyo mikoa pasipo na kulazimu ofisi hiyo kulipia kodi ya pango. Maelezo zaidi kuhusu mapokezi ya fedha za bajeti ya Fungu 19 yanapatikana katika ukurasa wa 18 hadi 21 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu Na. 101, Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, iliidhinishiwa kutumia shilingi bilioni 17.4, kiasi kinachojumuisha shilingi bilioni 16.5 kwa ajili ya OC na shilingi milioni 928.8 kwa ajili ya mshahara. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, ofisi ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 11.24 sawa na 65% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10.2 ni kwa ajili ya OC na shilingi bilioni 1.06 kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na ofisi kupokea fedha kiasi cha kuridhisha ni kufasiri Sheria Ndogo 172 kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili na kurekebisha Sheria Ndogo 265.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, idadi ya kanuni zilizopo ni kubwa, ili kuendana na ukubwa huu, Kamati ina maoni kuwa, kazi ya kufasiri kanuni hiyo iongezeke. Aidha, kwa kuwa kazi ya kufasiri sheria ilikamilika, Kamati inashauri kuwa sheria zitangazwe rasmi na kusambazwa kwa watumiaji wa jamii, ili waweze kunufaika na kutumia sheria kama lugha inayofahamika kwa kujulikana na jamii iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa 2025/2026. Kamati ilitembelea kukagua miradi miwili iliyopo katika Mkoa wa Singida

na Mwanza inayotekelezwa na Wizara hii. Mradi wa Singida unahusu ujenzi wa Ofisi ya Mashtaka ya Mkoa unatekelezwa vizuri kama Taarifa ya Kamati inavyoeleza katika ukurasa wa 26 hadi 27 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi mwingine unasuasua. Mradi huu unahusu ujenzi wa jengo la ghorofa tatu, kwa ajili ya kituo jumuishi cha taasisi ya kisheria unaojengwa katika kata ya Buswelu, Wilaya ya Ilemela, Mkoa wa Mwanza. Taasisi hizo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mkabidhi Wasii, yaani *RITA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 26 Aprili, 2022 na ulitakiwa kukamilika tarehe 25 Oktoba, 2023. Gharama za utekelezaji wa mradi huu ilikuwa ni shilingi bilioni 3.4 ambapo shilingi bilioni 3.3 ni gharama za mkandarasi, yaani *SUMA JKT*, na shilingi milioni 85 ni gharama za mshauri elekezi, Wakala wa Majengo, yaani *TBA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe 16 Machi, 2026, utekelezaji ulikuwa umefikia 74%. Aidha, jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 2.9 sawa na 87.35% ya gharama ya mradi ilikuwa imelipwa kwa mkandarasi anayetekeleza mradi huu, ambapo *SUMA JKT* ilikuwa imelipwa kiasi cha shilingi bilioni 2.9 sawa na 88% na *TBA* shilingi milioni 55.5 sawa na 65%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mradi huu kutokamilika, tarehe 25 Oktoba, 2023, kama ilivyokubalika wakati wa kuanzishwa kwa mradi huu Oktoba, 2022, mshitiri amekuwa akiongeza muda kwa nyakati tofauti, ambapo nyongeza ya muda iliyotolewa kwa sasa inamalizika tarehe 30 Mei, 2026. Kamati ilielezwa kuwa, kuchelewa kukamilika kwa mradi huu kulisababishwa na uwepo wa mawe kwenye ardhi yaliyogundulika wakati wa uchimbaji wa msingi, hivyo ilisababisha ujenzi wa msingi kuchukua muda mrefu na ucheleweshaji wa malipo ya fedha kutoka Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, uwepo wa mawe katika eneo siyo sababu ya kuchelewa

kwa mradi kama hivi inavyoelezwa. Hii inatokana na ukweli kwamba, Kamati hii ilipotembelea na kukagua mradi mwezi Machi, 2023 wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo na mradi ulikuwa umefikia 45% ambapo msingi na boma ulikuwa tayari vimeshajengwa. Hivyo basi, tangu mwezi Machi, 2023 hakukuwa na kazi ya kujenga msingi na hivyo basi, siyo sababu tena ya mradi huu kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuhusu sababu ya kuchelewa kwa malipo kutoka Wizara ya Fedha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, nayo siyo sababu kwani wakati Kamati ilipokagua mradi huu malipo yaliyolipwa na Serikali kwa Mkandarasi *SUMA JKT* yalikuwa ni 88% wakati kazi imefikia 74%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokagua mradi huu mwezi Machi, 2023 ilielezwa kuwa, utekelezaji wake ulikuwa umefikia 45% na ilipokagua tena mwezi Machi, 2026 mradi huu ulikuwa umefikia 74% chini ya Mkandarasi *SUMA JKT*. Hali hii inaashiria kasi ndogo sana ya ujenzi wa mradi huu. Ili kuunusuru mradi huu na kuondokana na kuongezeka kwa muda mara kwa mara, muda wa utekelezaji wa mradi, Serikali ichukue hatua za makusudi za haraka katika kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa wakati. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo yanapatikana katika ukurasa 25 hadi 30 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Katiba na Sheria katika mafungu nane inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 487.2. Katika kiasi hicho, shilingi bilioni 372.4 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha shilingi bilioni 57.2 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 315 kwa ajili ya *OC*. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 114.8 kinachoombwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa ulinganisho wa bajeti ya mwaka 2025/2026 na bajeti ya mwaka 2027, bajeti inayofuata imeongezeka kwa wastani wa 32.15% ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha ya matumizi ya bajeti ya mwaka 2026/2027 imeongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 74.9 sawa na 22.22% ukilinganisha na ya mwaka wa fedha 2025/2026 ambapo bajeti ilikuwa ni shilingi bilioni 297.428.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kiasi hicho mishahara imeongezeka kwa shilingi bilioni 5.8 sawa na 11.3%, na fedha za *OC* imeongezeka kwa shilingi bilioni 72.2 sawa na 29.7% ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, fedha za maendeleo zilitengwa jumla ya shilingi 52,540,000,000; shilingi 44,400,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 8,140,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2026, fedha na matumizi ya kawaida zilizopokelewa ni shilingi 27,400,000,000 sawa na 61% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kinajumuisha mishahara shilingi 9,900,000,000 na *OC* shilingi 14,700,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, fedha za maendeleo zilizopokelewa ni shilingi 36,040,000,000 sawa na 68.58% ya fedha zilizoidhinishwa. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi 35,800,000,000 fedha za ndani sawa na 80.65% na shilingi 224,230,000 fedha za nje sawa na 2.75%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inaonesha kuwa, kiwango cha mapokezi ya fedha za maendeleo kwa upande wa fedha za nje siyo cha kuridhisha, kwani zimepokelewa 2.75% tu badala ya 66.7%. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo za ndani, hali ya mapokezi ilikidhi matakwa ya bajeti na zilipokelewa 80.65%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupokelewa kwa fedha hizo kuliwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo utekelezaji na kutoa huduma ya msaada wa kisheria unaojulikana kama *Mama Samia Legal Aid Campaign*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia msaada wa kisheria, wananchi wengi, hususan wanyonge wasioweza kumudu huduma za ada za mawakili, walitatuliwa shida zao na hivyo kupunguza kero na malalamiko kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo zaidi kuhusu mapokezi ya fedha za bajeti ya Fungu 41 yanapatikana ukurasa wa saba hadi wa tisa wa Taarifa ya Kamati. Fungu 16, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 40,900,000,000. Kati ya hizo fedha, shilingi 40,200,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha shilingi 35,500,000,000 kwa ajili ya OC na shilingi 4,700,000,000 kwa ajili ya mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, shilingi 788,700,000 zilitengwa kwa ajili ya maendeleo, ambazo zote ni fedha za ndani. Hadi kufikia Februari, 2026, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ilipokea fedha za matumizi ya kawaida jumla ya shilingi 24,500,000,000 sawa na 61% ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zinajumuisha shilingi 21,700,000,000 kwa ajili ya OC na shilingi 2,800,000,000 kwa ajili ya mshahara. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, ofisi ilipokea kiasi cha shilingi 179,300,000 sawa na 22% ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za maendeleo bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 43.3, sawa na 61.12% ukilinganisha na bajeti ya maendeleo ya mwaka unaoisha ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 71.2. mchanganuo zaidi wa bajeti ya matumizi ya kawaida ya maendeleo, umeainishwa katika jedwali namba 12 na 13 lililopo katika ukurasa wa 34 hadi 38 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya ujumla inaonesha kuwa, bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeionggezeka katika fungu isipokuwa tu kwa fedha za maendeleo za nje. Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani na kuendana na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; ili kusaidia utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya jumla: Taasisi nyingi chini ya Wizara hii zinakumbwa na changamoto ya majengo yaani

ofisi, hususan Ofisi za Mikoa, kwa asilimia kubwa ya bajeti ya fedha za maendeleo inayohusu ujenzi wa ofisi hizo, imekuwa haitolewi kikamilifu. Ili kutatua changamoto hiyo na kufikisha huduma kwa wananchi, Serikali ihakikishe inatoa fedha za maendeleo kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mahsusi: Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa kuwa mradi wa msaada wa huduma za kisheria unaojulikana kama Mama Samia *Legal Aid Campaign* umekuwa na manufaa kwa wananchi hasa wa hali ya chini, kwa kuwapatia haki zao na kupunguza malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mradi huo uendelee kutoa tabasamu na matumaini kwa wananchi, Serikali iendeleze mradi huo kwa kuwafikia wananchi mbalimbali, hususan vijijini na maeneo mengine ya kimkakati yanayolalamikiwa na kukithiri kwa migogoro mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mshitiri wa ujenzi wa kituo jumuishi cha kisheria cha Mkoa wa Mwanza kilichoanza ujenzi mwaka 2022 na kutakiwa kukamilika 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilipofanya ukaguzi wa mradi Tarehe 18 Machi, 2026 ilikuta utekelezaji wake umefikia 74% licha ya Serikali kufanya malipo kwa kiasi cha 88%, licha ya kuhakikisha mradi huo unakamilika na umecheleweshwa zaidi ya miezi 29, Serikali ihakikishe inachukua hatua za kisheria, hatua za haraka za kunusuru mradi huu kwa kuhakikisha *SUMA JKT* anakamilisha mradi huo, licha ya mtindo wa utekelezaji wake unaosuasua.

**MWENYEKITI:** Ninaomba uhitimishe Mheshimiwa.

**MHE. YAHYA E. NAWANDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; ninapenda kumshukuru Spika, Naibu Spika, wewe binafsi na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa dhati kabisa ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria ambapo ushauri na ushirikiano umetuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi ya Bunge kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Juma Zuberi Homera, Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Naibu Waziri, Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wameendelea kutupatia kipindi chote cha Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwashukuru watendaji wa ofisi pamoja na taasisi zote kwa ushirikiano wanaotupatia Kamati, ukiongozwa na Katibu wa Wizara, Ndugu Eliakimu Chacha Maswi na Naibu Katibu Mkuu wake, Dkt. Franklin Jasson Rwezimula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**24 APRILI, 2026**

---

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

### 1.1 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 kwa kugawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, misingi na muundo wa taarifa hii;

(b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa fedha 2025/2026 katika maeneo yanayohusu makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

(c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(d) Sehemu ya Nne inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Ofisi hii na Serikali kwa ujumla; na

(e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi na Maoni ya Kamati juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2026/2027 unatokana na matakwa ya Kanuni ya 121(4) ikisomwa kwa pamoja na Kifungu 6(2)(e) na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni na vifungu hivyo vimeweka masharti yanayoelekeza Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu nane (8) ambayo ni: -

(a) **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria;

(b) **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(c) **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

(d) **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama;

(e) **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

(f) **Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania;

(g) **Fungu 19** - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; na

(h) **Fungu 101** - Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 2.1 Vipengele vya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** katika kikao cha Kamati kilichoketi tarehe 10 na 28 Machi, 2026, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria ikiwa na jumla ya mafungu nane (8) iliyohusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hiyo iliwasilishwa na **Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb)** Waziri wa Wizara hiyo. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hiyo umeangazia maeneo makuu manne ambayo ni: -

(a) Makusanyo ya maduhuli kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(b) Upatikanaji wa fedha za Bajeti za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(c) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kupitia Taarifa ya Kamati wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### *2.2 Makusanyo ya maduhuli hadi Februari, 2026*

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 108,332,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya **Shilingi 45,000,000.00**, **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ililenga kukusanya **Shilingi 60,000,000.00** na **Fungu 16** –

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ililenga kukusanya **Shilingi 3,332,000.00**.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli hayo hadi kufikia Februari, 2026 unaonesha kuwa: -

(a) **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria imekusanya zaidi ya lengo la **asilimia 66.7** kwani imekusanya **Shilingi 32,800,000.00** sawa na **asilimia 72.9** ya kiasi kilichoidhinishwa. Kamati ilielezwa kuwa, Sababu za kuvuka lengo la ukusanyaji maduhuli ni uwepo wa idadi kubwa ya maombi kwa ajili ya usajili na uhuishaji wa vyeti vya Wasuluhishi wa migogoro nje ya utaratibu wa mahakama (*Alternative Dispute Resolution*) na Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria**.**

(b) **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imekusanya kiasi cha **Shilingi 56,000,000.00** kati ya **Shilingi 60,000,000.00** sawa na **asilimia 93.33** ya lengo la Makusanyo. Makusanyo hayo yanatokana na wapangaji kuzingatiaji mikataba ya upangishaji wa majengo ya Ofisi hii kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

(c) **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali haikuweza kukusanya kiasi chochote cha fedha, hata hivyo lengo la makusanyo ya ofisi hiyo ni **Shilingi 3,332,000.00** kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati ilielezwa kuwa, Maduhuli hayo yaliyopangwa kukusanywa kutokana na huduma mbalimbali zinazotolewa na Ofisi hiyo kama vile kuuza nyaraka za zabuni, ada mbalimbali na urejeshwaji wa fedha za umma.

Kamati ina maoni kuwa, **ili kufikia lengo lililokusudiwa la makusanyo ya maduhuli, ni ushauri wa Kamati kuwa ni vyema Fungu 16 izingatie uhalisia wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa kuwianisha na uhalisia wa vyanzo vya makusanyo**.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa maduhuli kwa kila fungu unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

JEDWALI NA. 1 Makusanyo ya Madhuhuli 2025/2026

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO | MAKUSANYO HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2026 | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 45,000,000 | 32,800,000.00 | 109 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 60,000,000 | 56,000,000 | 93.33 |
| **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 3,332,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA KUU** | **108,332,000** | **88,800,000.00** | **81.97** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati.*

### 2.3 Uchambuzi wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** katika kushughulikia bajeti ya Wizara hii, Kamati imeangazia mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida ambayo inajumuisha mishahara (PE) na matumizi mengineyo (OC) pamoja na fedha kwa ajili ya maendeleo. Tathmini ya utekelezaji wa bajeti hadi februari, 2026 kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo: -

#### 2.3.1 Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 97,734,068,000.00**. Katika kiasi hicho, **Shilingi 45,175,295,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikujumuisha **Shilingi 14,182,689,000.00** kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Shilingi 30,992,606,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

Aidha, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo ni shilingi **52,558,773,000.00,** ambapo **shilingi 44,415,453,000.00** ni fedha za ndani na **shilingi 8,143,320,000.00** ni fedha za nje. Hadi kufikia Februari, 2026, Fungu 41 lilikuwa limepokea jumla ya **shilingi 63,405,563,112.50** sawa na **asilimia 64.87** ya kiasi chote kilichoidhinishwa. Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hizo unaonesha kuwa:-

(a) Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, hadi kufikia Februari, 2026 zilizopokelewa **Shilingi 27,361,153,760.61** sawa na **asilimia 61** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kinajumuisha mishahara Shilingi **9,917,208,329.47** sawa na asilimia **69.92,** na matumizi mengineyo **shilingi 17,443,945,431.14** sawa na asilimia **56** ya fedha zilizoidhinishwa.

(b) Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya **shilingi 36,044,409,351.89** zimetolewa sawa na **asilimia 68.58** ya fedha zilizoidhinishwa. Kiasi hicho kinajumuisha **shilingi 35,820,179,491.89** fedha za ndani, sawa na **asilimia 80.65** na **shilingi 224,229,860.00** fedha za nje, sawa na **asilimia 2.75**. Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 2 hapa chini.

**JEDWALI NA. 2:** Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Februari, 2026 Fungu 41

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa hadi Februari 2026 | Asilimia ya Mapokezi |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 30,992,606,000.00 | 17,443,945,431.14 | 56 |
| | Mishahara | 14,182,689,000.00 | 9,917,208,329.47 | 69.92 |
| **Jumla Ndogo** | | **45,175,295,000.00** | **27,361,153,760.61** | **61** |
| Maendeleo | Ndani | 44,415,453,000.00 | 35,820,179,491.89 | 80.65 |
| | Nje | 8,143,320,000.00 | 224,229,860.00 | 2.75 |
| **Jumla Ndogo** | | **52,558,773,000.00** | **36,044,409,351.89** | **68.58** |
| **JUMLA KUU** | | **97,734,068,000.00** | **63,405,563,112.50** | **64.87** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria kwa Fungu 41 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** Tathmini inaonesha kuwa, kiwango cha mapokezi ya fedha za maendeleo kwa upande wa fedha za nje si cha kuridisha, kwani zimepokelewa **asilimia 2.75** tu badala ya **asilimia 66.7**. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo za ndani, hali ya mapokezi ilikidhi matakwa ya kibajeti kwani zilipokelewa **asilimia 80.65**. Kamati ilielezwa kuwa, kupokelewa kwa fedha hizo, kumewezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ikiwemo kutekeleza mradi wa **Mama Samia Legal Aid Campaign**, jambo lililochangia kurudisha tabasamu kwa wananchi waliokuwa wamekosa matumaini na kupunguza chuki dhidi ya Serikali inayosababishwa na baadhi ya watu wanaopoka au kukandamiza haki za watu wanyonge.

### 2.3.2 Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 40,941,954,000.00**. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 40,153,250,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ikujumuisha **shilingi 35,481,434,000.00** kwa ajili ya matumizi Mengineyo na shilingi **shilingi 4,671,816,000.00** kwa ajili ya Mishahara. Aidha, kiasi cha **Shilingi 788,704,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambazo zote ni fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi katika mikoa ya Mwanza na Arusha.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mapokezi ya fedha hizo inaonesha kuwa:-

(a) Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, hadi kufikia Februari, 2026, Ofisi ilipokea kiasi cha **Shilingi 24,492,796,948.70** sawa na **Asilimia 61** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Fedha zilizopokelewa zinajumuisha Shilingi **21,653,209,016.70** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **2,839,587,932.00** kwa ajili ya Mishahara.

(b) Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Februari, 2026, Ofisi ilipokea kiasi cha **Shilingi 179,346,312.00** sawa na **Asilimia 22.74** ya fedha zilizoidhinishwa. Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 3 hapa chini.

**JEDWALI NA. 3:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 16

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa hadi Februari 2026 | Asilimia ya Mapokezi |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 35,481,434,000.00 | 21,653,209,016.70 | 61.03 |
| | Mishahara | 4,671,816,000.00 | 2,839,587,932.00 | 60.78 |
| **Jumla Ndogo** | | **40,153,250,000.00** | **24,492,796,948.70** | **61** |
| Maendeleo | Ndani | 788,704,000.00 | 179,346,312.00 | 22.74 |
| **JUMLA KUU** | | **40,941,954,000.00** | **24,672,143,260.70** | **60.26** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria kwa Fungu 16 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kuwa, hali ya mapokezi ya fedha za maendeleo si ya kuridhisha, kwani zilipokelewa **asilimia 22.74** tu badala ya **asilimia 66.7**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kutengwa kwa kiasi kidogo cha fedha kuna hatari ya kuathiri utekelezaji wa ujenzi wa majengo ya Ofisi, hususan jengo la Ofisi la Mkoa wa Arusha kutokukamilika kwa

kadiri ilivyopangwa. **Ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati, Kamati inashauri fedha zilizotengwa zitolewe kikamilifu.**

**2.3.3 Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 145,972,057,000.000.** Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 130,105,947,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ikijumuisha **shilingi 20,343,283,000.00** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 109,671,664,000.00** kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilitengwa kiasi cha **Shilingi 15,866,110,000.00** zote zikiwa ni fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mapokezi ya fedha hizo inaonesha kuwa:-

(a) Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Ofisi ilipokea jumla ya **Shilingi 95,323,562,030.08** sawa na **Asilimia 73.27** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 79,663,984,850.00** sawa na **asilimia 72.64** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 15,659,577,180.80** sawa na **asilimia 76.98** ni kwa ajili ya Mishahara.

(b) Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Februari 2026, zilipokelewa **shilingi 12,772,517,668.71** sawa na **asilimia 80.5** ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hizo unaonekana katika **jedwali namba 4** hapa chini.

**JEDWALI NA. 4:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026- Fungu 35

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya | OC | 109,671,664,000.00 | 79,663,984,850.00 | 72.64 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kawaida | Mishahara | 20,343,283,000.00 | 15,659,577,180.80 | 76.98 |
| **Jumla Ndogo** | | **130,105,947,000.00** | **95,323,562,030.08** | **73.27** |
| Maendeleo | Ndani | 15,866,110,000.00 | 12,772,517,668.71 | 80.5 |
| **JUMLA KUU** | | **145,972,057,000.00** | **108,096,079,698.79** | **74.06** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria kwa Fungu 35 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mapokezi kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa mwaka unaoisha ni ya kuridhisha, kwani katika kila sehemu ya bajeti, zilipokelewa zaidi ya **asilimia 66.7**. Kamati ilielezwa kuwa, kupokelewa kwa fedha kiasi cha kuridhisha kumesaidia ofisi kutekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kuendesha mashauri ya jinai nchini, ambapo kwa sasa mashauri yote ya jinai ya mahakama za wilaya na mahakama za juu yake zinaendeshwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kutumia wataalam wa sheria. Vilevile kiasi hicho kimewezesha Ofisi ya Mashtaka kufanya ufuatiliaji wa baadhi ya malalamiko yanayohusu masuala ya jinai hususan mashauri yanayoendeshwa katika baadhi ya mahakama za mwanzo ambako Ofisi hiyo haina usimamizi. Aidha, licha ya mafanikio hayo, Kamati ilielezwa kuwa bado Ofisi hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo uhaba wa magari na kompyuta. Changamoto hiyo imesababishwa na mahitaji kuwa makubwa kufuatia Ofisi hii kuanzisha Ofisi za Wilaya takribani wilaya zote zilizopo nchini, isipokuwa kwa wilaya ishirini na moja (21).

### 2.3.4 Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Tume iliidhinishiwa Bajeti ya **shilingi 6,966,967,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo **shilingi 5,841,720,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi 1,125,247,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2026 Tume ya Utumishi wa Mahakama ilipokea jumla ya **shilingi 3,873,051,966.00** sawa na **asilimia 55.59** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Matumizi Mengineyo ni **shillingi 3,317,081,966.00** sawa na **asilimia**

**56.78** na Mishahara **shilingi 555,970,000.00** sawa na **asilimia 49.41**. Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika **jedwali namba 5** hapa chini.

**JEDWALI NA. 5:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 12

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 5,841,720,000 | 3,317,081,966 | 56.78 |
| | Mishahara | 1,125,247,000 | 555,970,000 | 49.41 |
| **JUMLA KUU** | | **6,966,967,000** | **3,873,051,966** | **55.59** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria kwa Fungu 12 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kuwa, kiwango cha upokeaji wa fedha za bajeti ya matumizi ya kawaida hususan kwa upande wa fedha za matumizi mengineyo kipo chini ya **asilimia 66.7** inayotakiwa, kwani zilipokelewa kiasi sawa na **asilimia 49.41**. Kupokelewa kwa kiasi kisichofikia lengo kuna hatari ya kuathiri uendeshaji wa shughuli za kila siku za Tume, ikizingatiwa kuwa Tume hii inasamamia watalaam wenye jukumu la kutoa haki nchini ambao ni Majaji na Mahakimu.

### 2.3.5 Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 11,743,965,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,452,519,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Shilingi 8,291,446,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari 2026, Tume ilipokea kiasi cha **Shilingi 9,013,978,807.73** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 76.75** ya fedha zilizoidhinishwa ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 2,427,131,000.00** sawa na **asilimia 70.30** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Shilingi 6,586,847,807.73** sawa na **asilimia 79.44** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Kwa upande wa fedha za maendeleo, Tume hii haikudhinishiwa kiasi cha fedha. Hata hivyo, ilipokea jumla ya **Shilingi 62,900,125.00** kutoka taasisi

ya *Danish Institute for Human Rights* ikiwa ni Mradi wa kuandaa Mpango kazi wa Haki za Binadamu na Biashara. Fedha hizo zilitumika kutekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kuwezesha mkutano wa kitaifa wa majadiliano na wadau wa biashara katika sekta za kilimo, uzalishaji na usafirishaji kuhusu uimarishaji wa haki za binadamu na uhakiki.

Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 6 hapa chini.

**JEDWALI NA. 6:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026-Fungu 55

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa hadi Februari 2026 | Asilimia ya Mapokezi |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 8,291,446,000.00 | 6,586,847,807.73 | 79.44 |
| | Mishahara | 3,452,519,000.00 | 2,427,131,000.00 | 70.30 |
| **JUMLA KUU** | | **11,743,965,000.00** | **9,013,978,807.73** | **76.75** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizra ya Katiba na Sheria kwa Fungu 55 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kuwa, mapokezi ya fedha kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilikuwa ya kuridhisha. Kupitia fedha hizo, Tume ilitekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kushughulikia na kufunga **malalamiko 76** yaliyohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kuwezesha baadhi ya watumishi wa umma kulipwa haki zao ikiwemo haki ya kulipwa fedha za kusafirisha mizigo na madai ya kuumia kazini. Kulipwa huko kunatokana na Tume kufanya uchunguzi na kubaini kuwa watumishi hao wanahaki ya kulipwa na Serikali kutekeleza uamuzi wa Tume, licha ya kwamba mamlaka zao za ajira zilikuwa zimeshafanya uamuzi kuwa watumishi hao hawana haki ya kulipwa. Aidha, licha ya kazi hizo, Kamati imebaini kuwa Tume hii haina Ofisi kwenye mikoa 26 kati ya mikoa 31 ya Tanzania Bara na

Zanzibar. Kukosekana kwa ofisi hizo kunasababisha Tume kushindwa kupokea na kushughuliki malalamiko ya wananchi wanaoishi katika mikoa isiyokuwa na Ofisi za Tume

### 2.3.6 Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliidhinishiwa na Bunge kutumia kiasi cha **Shilingi 7,402,530,000.00** kwa ajili ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,775,350,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 5,627,180,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari 2026, Tume ya Kurekebisha Sheria ilipokea kiasi cha **Shilingi 3,894,346,699.61** sawa na **asilimia 53** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, **Shilingi 845,774,199.60** ni Mishahara na **Shilingi 3,048,572,500.01** ni Matumizi Mengineyo. Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 7 hapa chini.

**JEDWALI NA. 7:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 59

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa hadi Februari 2026 | Asilimia ya Mapokezi |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 5,627,180,000.00 | 3,048,572,500.01 | 54 |
| | Mishahara | 1,775,350,000.00 | 845,774,199.60 | 48 |
| **JUMLA KUU** | | **7,402,530,000.00** | **3,894,346,699.61** | **53** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria Fungu 59 na Usanifu wa Kamati.*

### 2.3.7 Fungu 19 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 38,497,754,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo kiasi cha **shilingi 4,779,918,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na kiasi cha **shilingi 33,717,836,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi

Mengineyo. Aidha, kwa mwaka unaoisha, Ofisi hii haikupangiwa bajeti ya fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2026 Ofisi imepokea kiasi cha **shilingi 22,758,629,755.29**, sawa na **asilimia 59.12** ya fedha zilizoidhinishwa. Katika kiasi hicho kilichopokelewa, **shilingi 3,216,386,756.00** sawa na **asilimia 67.29** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi 19,542,242,999.29** sawa na **asilimia 57.96** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, mbali na kupokea fedha zilizoidhinishwa, Ofisi pia ilipokea kiasi cha **shilingi 4,774,370,000.00** kwa ajili ya uratibu, usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya Uchaguzi Mkuu, uliofanyika Oktoba 2025, ambapo Ofisi ilisimamia uendeshaji wa **mashauri 75** ya uchaguzi yaliyofunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini. Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 8 hapa chini.

**JEDWALI NA. 8:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 19

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 33,717,836,000 | 19,542,242,999.29 | 57.96 |
| | Mishahara | 4,779,918,000 | 3,216,386,756 | 67.29 |
| **JUMLA KUU** | | **38,497,754,000** | **22,758,629,755.2 9** | **59.12** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mapokezi ya fedha kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilikuwa ya wastani, kwani zilipokelewa **asilimia 59.12** badala ya **asilimia 66.7**. Licha ya kiasi hicho, Ofisi imetekeleza kazi mbalimbali katika kipindi hicho. Baadhi ya kazi hizo ni kuendesha mashauri ya madai **10,398** yakihusisha madai ya kitaifa **9,585**, madai ya kimataifa **34**, mashauri ya uchaguzi **75** na mashauri ya Kikatiba na Haki za Binadamu **704**. Katika mashauri **10,398** yaliyosimamiwa na Ofisi hii, katika kipindi cha julai, 2025 hadi februari 2026 yalimalizika mashauri **604** sawa na asilimia **5.81** ya mashauri yote. Katika mashauri 604 yaliyomalizika, Ofisi ilishinda jumla ya mashauri **528** sawa na asilimia **87.42**. Mafanikio yaliyopatikana kupitia ushindi huo ni kuokoa fedha za

Serikali kiasi cha **shilingi 295,338,943,322.29**. Licha ya mafanikio haya, **ni mtazamo wa Kamati kwamba Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ibuni mkakati mahsusi utakaowezesha kasi ya umalizaji wa mashauri kuongezeka.** Kumalizika kwa mashauri mapema, kutapelekea wadau husika kufahamu haki zao kwa wakati na hivyo kupunguza malalamiko ya haki kucheleweshwa. Aidha, pamoja na kazi nyingi zinazotekelezwa na Ofisi hii, Kamati ilielezwa kuwa Ofisi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa majengo ya Ofisi kwenye ofisi za Mikoa. Changamoto hiyo imepelekea ofisi kupanga kwenye majengo mbalimbali kwa baadhi ya mikoa, na hivyo kuongeza gharama za matumizi na wakati mwingine kuleta ugumu katika kusimamia mashauri ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi hii kazi yake kuu ni kusimamia mashauri ya madai yanayoihusu Serikali kwa ujumla ikiwemo mashauri yanayozihusu taasisi, wakala, mashirika ya umma na TAMISEMI bila ya kutoza gharama zozote. **Ili kuondokana na changamoto ya Ofisi kwa baadhi ya mikoa, Kamati inashauri kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ihakikishe Ofisi hii inapewa vyumba kwa ajili ya ofisi za mikoa hiyo pasipo kulazimu Ofisi hii kulipia kodi ya pango**. **Aidha, Ofisi ibaki na jukumu la kulipia gharama za uendeshaji wa Ofisi kama vile umeme, maji, usafi na ulinzi**.

### 2.3.8 Fungu 101 - Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria

**Mheshimiwa Spika**; Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi 17,382,964,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 16,454,158,000.00** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 928,806,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Hadi kufikia Februari 2026, Ofisi imepokea kiasi cha **Shilingi 11,240,807,766.67** sawa na **Asilimia 65** ya bajeti iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo **Shilingi 10,183,150,766.67** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 1,057,657,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 9 hapa chini.

**JEDWALI NA. 9:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 101

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 16,454,158,000 | 10,183,150,766.67 | 61.89 |
| | PE | 928,806,000 | 1,057,657,000.00 | 113.88 |
| **JUMLA KUU** | | **17,382,964,000** | **11,240,807,766.67** | **65** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*.

**Mheshimiwa Spika**; Kwa kuwa kazi ya kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili imekamilika, Kamati inapendekeza sheria hizo zitangazwe rasmi na kusambazwa kwa watumiaji ili jamii iweze kuanza kunufaika nazo kama ilivyokusudiwa

**2.4 Tathmini ya jumla kuhusu Mapokezi ya fedha za Bajeti kwa Wizara ya Katiba na Sheria.**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba: -

(a) Kwa ujumla, Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2025/2026, hadi kufikia Februari, 2026 ilipokea **asilimia 66.56** ya bajeti iliyopitishwa na Bunge kipindi ambacho ilitakiwa kuwa **asilimia 75** ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa maana hiyo, mtiririko wa upatikanaji wa fedha ulipaswa kuboreshwa zaidi.

(b) Taasisi Mbili (2) kati ya Taasisi Nane (8) zilizopo chini ya Ofisi hii zimefanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa **asilimia 66.6** hadi kufikia Februari, 2026.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 10** na **Jedwali Na. 11.**

**JEDWALI NA. 10:** Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2025/2026 kwa Wizara na Taasisi zake

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2025/2026 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2026 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 45,175,295,000.00 | 27,361,153,760.61 | 61 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 40,153,250,000.00 | 24,492,796,948.70 | 61 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 130,105,947,000.00 | 95,323,562,030.08 | 73.27 |
| **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama | 6,966,967,000.00 | 3,873,051,966.00 | 55.59 |
| **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 11,743,965,000.00 | 9,013,978,807.73 | 76.75 |
| **Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania | 7,402,530,000.00 | 3,894,346,699.61 | 53 |
| **Fungu 19** - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 38,497,754,000.00 | 22,758,629,755.29 | 59.12 |
| **FUNGU 101** – Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria | 17,382,964,000.00 | 11,240,807,766.67 | 65 |
| **JUMLA KUU** | **297,428,672,000.00** | **197,958,327,734.69** | **66.56** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**JEDWALI NA. 11:** Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2025/2026

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|

| | 2025/2026 | FEBRUARI, 2026 | |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 52,558,773,000.00 | 36,044,409,351.89 | 68.58 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 788,704,000.00 | 179,346,312.00 | 22.74 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 15,866,110,000.00 | 12,772,517,668.71 | 80.5 |
| **JUMLA KUU** | **69,213,587,000.00** | **48,996,273,332.60** | **70.79** |

***Chanzo***: *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

### 2.5 Ukaguzi wa Miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 inaweka masharti kwa Kamati za kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha (2025/2026) kabla ya kuanza uchambuzi wa bajeti ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Katika kuzingatia masharti hayo, Kamati ilikagua miradi miwili (2) iliyopo katika mkao wa Singida na Mwanza inayotekelezwa na Wizara hii. Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

#### (i) Ujenzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Singida (Mradi Na 6389)

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 12 Machi, 2026 Kamati ilitembelea na kukagua ujenzi wa jengo la ghorofa moja kwa ajili ya Ofisi ya Mashtaka Mkoa wa Singida. Ujenzi wa mradi huu ulianza tarehe 10 Machi, 2025 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 10 Machi, 2026.

Jumla ya gharama za ujenzi wa mradi huo ni **shilingi 2,402,417,178.00** ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani (*VAT)*.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokagua mradi huu tarehe 12 Machi, 2026, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 38.2,** na malipo ya kiasi cha **shilingi 779,429,999.9** yalikuwa yamefanyika sawa na **asilimia 32** ya gharama zote za mradi. Gharama hizo zinajumuisha ujenzi wa boma, kibanda cha mlinzi, uzio, jengo kwa ajili ya jenereta na uwekaji wa umeme. Ilielezwa kuwa, gharama za mifumo ya TEHAMA pamoja na samani za ofisi si sehemu ya mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mradi huu kutakiwa kukamilika tarehe 30 Machi, 2026, utekelezaji wake haukukamilika katika muda huo na sasa unatarajia kukamilika mwezi Juni, 2026 baada ya kutolewa muda wa nyongeza wa miezi mitatu. Kamati ilielezwa kuwa, sababu kuu za mradi kutokukamilika kwa wakati ni kuchelewa kupata fedha za utekelezaji kutoka hazina. Ilielezwa kuwa, licha ya Mkataba kusainiwa tarehe **10 Machi, 2025**, fedha za malipo ya awali (advance payment) zilitolewa mwezi **Julai, 2025** na Mkandarasi alilipwa fedha hizo **mwezi Septemba, 2025**, na hivyo kupelekea mradi kuchelewa kuanza kwa muda miezi sita.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, muda halisia uliotumika kutekeleza mradi huu ni miezi minne, kwani ujenzi ulianza mwezi Septemba, 2025 badala ya mwezi Machi, 2025. Ujenzi kufikia **asilimia 38.2** katika kipindi cha miezi minne tu, ni hatua kubwa na nzuri ya utekelezaji wa mradi huu. **Ili kumuwezesha Mkandarasi kuendelea na kasi nzuri ya utekelezaji wa mradi huu, Kamati inashauri Serikali ihakikishe inatoa fedha za mradi huu kwa wakati**.

### (ii) Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha Taasisi za Kisheria - Buswelu, Ilemela- Mwanza (Namba ya Mradi 6389)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa Ofisi wa jengo la ghorofa tatu kwa ajili ya Ofisi za taasisi za kisheria za Serikali katika mkoa wa Mwanza. Taasisi hizo ni Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Kabidhi wasii (RITA).

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 26 Aprili, 2022 na ulitakiwa kukamilika tarehe 25 Oktoba, 2023. Gharama za utekelezaji wa mradi ni jumla ya **shilingi 3,368,671,233.81**, ambapo **shilingi 3,283,227,983.81** ni gharama za mkandarasi SUMA JKT anayetekeleza mradi huu, na **shilingi 85,443,250.00** ni kwa ajili ya Wakala wa Majengo (TBA) kwa ajili ya ushauri elekezi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe **16 Machi, 2026**, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 74**. Aidha, jumla ya kiasi cha **shilingi 2,942,687,466.81** sawa na **asilimia 87.35** ya gharama za mradi zilikuwa zimelipwa kwa wakandarasi wanaotekeleza mradi huu. Katika kiasi hicho, SUMA JKT ilikuwa imelipwa **shilingi 2,887,149,354.81** sawa na **asilimia 88** ya gharama za mkataba wa ujenzi, na TBA ilikuwa imeshalipwa **shilingi 55,538,112.00** sawa na **asilimia 65** ya gharama za Mkataba wa ushauri elekezi.

**Mheshimiwa Spika,** awali ujenzi wa mradi huo ulitakiwa kukamilika tarehe 25 Oktoba, 2023. Kutokana na kutokumalizika kwake, Serikali imekuwa ikiongeza muda kwa nyakati tofauti tofauti, ambapo nyongeza ya muda iliyotolewa kwa sasa inamalizika tarehe 30 Mei, 2026. Kuhusu sababu za kutokukamilka kwa mradi huo licha ya kuchelewa kwa muda wa miezi ishirini na tisa (29), Kamati ilielezwa kuwa kuchelewa huko kulisababishwa na uwepo wa mawe kwenye ardhi yaliyogundulika wakati wa uchimbaji wa msingi, na hivyo kusababisha ujenzi wa msingi kuchukua muda mrefu. Aidha, sababu nyingine iliyoelezwa ni ucheleweshaji wa malipo ya fedha kutoka Wizara ya fedha.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa uwepo wa mawe katika eneo hilo si sababu ya kuchelewa kwa mradi kama ilivyo elezwa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, Kamati hii ilipotembelea na kukagua mradi huu huu mwezi Machi, 2023 wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi, ilielezwa kuwa mradi ulikuwa umefikia **asilimia 45** ambapo msingi na boma vilikuwa tayari vimeshajengwa. Hivyo basi, kazi ya ujenzi wa msingi

ilikamilika tangu mwaka 2023, na hivyo uwepo wa mawe si sababu iliyosababisha mradi huo usikamilike kwa kipindi cha kuanzia mwezi Machi, 2023 hadi Kamati ilipotembelea na kukagua tena mradi huu tarehe 16 Machi, 2026. Aidha, kuhusu sababu ya kuchelewa kwa malipo kutoka Wizara ya fedha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa nayo si sababu ya kutokukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo katika muda wa nyongeza wa zaidi ya miezi ishirini na tisa. Hii inathibitishwa na ukweli kwamba, wakati Kamati ilipokagua mradi huu, malipo yaliyokuwa yamelipwa na Serikali kwa mkandarasi SUMA JKT yalikuwa ni **asilimia 88**, wakati kazi ilikuwa imefikia **asilimia 74**. Aidha, Kamati ilipohoji zaidi kuhusu mtiririko wa malipo ya fedha, Mkandarasi hakuwa na jawabu juu ya jambo hilo, na kukiri kuwa tayari alishalipwa **asilimia 88** ya gharama ya Mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kamati ilipokagua mradi huo mwezi Machi, 2023 utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 45**, na ilipoukagua tena mradi huo mwezi Machi, 2026 utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 74**, sawa na utekelezaji wa **asilimia 29** kwa kipindi cha muda wa miaka mitatu. Kwa mchanganuo huo, mkandarasi huyo anatekeleza mradi huo kwa kiwango cha **asilimia 9** kwa mwaka. Ikiwa hali itaendelea kuwa hivyo, mkandarasi mjenzi atahitaji kutumia muda wa miaka miwili na miezi nane kumaliza ujenzi uliobakia ambao ni sawa na **asilimia 26**.

**Mheshimiwa Spika,** katika mazingira hayo, tathmini inaonesha kuwa hali halisi ya utekelezaji wa mradi huu unaojengwa na SUMA JKT si ya kuridhisha. Aidha, kwa kuwa mkandarasi huyo alishalipwa kiasi kikubwa cha fedha kwa kinachozidi kazi aliyotekeleza, na kwa kuwa hakuna sababu nyingine iliyopo ya mkandarasi kuchelewesha mradi huo, ni mtazamo wa Kamati kuwa kazi hiyo imechelewa kutokana na aidha kwa sababu za uzembe wa Mkandarasi au kwa sababu mkandarasi hana uwezo wa kutekeleza kazi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo na ili kuunusuru mradi huo, **ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ichukue hatua za makusudi na za haraka za kuhakikisha mradi huo unakamilika,**

**na kama ikibidi kumnyang`anya mkandarasi kazi hiyo na kupewa mkandasi mwingine mwenye uwezo**.

### 2.6 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, mnamo tarehe 28 Machi, 2026; Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika maeneo makuu mawili ambayo ni Makadirio ya makusanyo ya maduhuli na makadirio ya matumizi. Tathmini ya uchambuzi kuhusu maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

### 3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 105,000,000.00** kutoka katika mafungu mawili ambayo ni Fungu 41-Wizara ya Katiba na Sheria jumla ya **shilingi 45,000,000.00** na Fungu 35-Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kiasi cha **shilingi 60,000,000.00**. Vyanzo vya maduhuli hayo ni malipo ya pango kwa kukodisha kumbi, makato kwa watumishi watakaoshindwa kurejesha taarifa ya matumizi ya fedha za masurufu yaliyopewa, ada za watoa huduma wa msaada wa kisheria na watatuzi wa migogoro kwa njia mbadala.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ulinganisho kati ya makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2025/2026 na 2026/2027, maduhuli yam waka ujao yamepungua kwa kiasi cha **shilingi 3,332,000.00** ikilinganishwa na mwaka unaoisha, ambao maduhuli yalikuwa **Shilingi 108,332,000.00**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kupungua kwa kiasi hicho kunatokana na Fungu 16-Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutokuwa na bajeti ya makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2026/2027, ilhali mwaka unaoisha Ofisi hiyo ilikuwa na makadirio ya maduhuli **shilingi 3,332,000.00.**

Wakati Kamati ilipokutana Serikali, ilielezwa kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa ikiweka bajeti ya makadirio ya maduhuli ikitegemea chanzo kikuu ambacho ni makato ya fedha kwa watumishi watakoshindwa kuwasilisha taarifa ya matumizi ya fedha za masurufu walizopewa, chanzo ambacho kwa sasa hakifanyi kazi kutokana na Serikali kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Aidha, kwa upande wa Fungu 35 na Fungu 41, makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yamebaki kama yalivyokuwa katika mwaka wa fedha 2025/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unaonesha kuwa, kati ya Mafungu manane (8) yaliyopo chini ya Wizara hii, ni Mafungu Mawili pekee ndiyo yenye Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Hali hiyo inatokana na asili na majukumu ya kila Fungu, ambapo mafungu mengi yamejikita katika kutoa huduma isiyokuwa na tozo, ada, na adhabu.

### 3.2 Makadirio ya Matumizi katika Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Katiba na Sheria katika mafungu yake nane inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 487,166,693,000.00**. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 372,427,763,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha **shilingi 57,156,323,000.00** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 315,271,440,000.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Aidha, kiasi cha **shilingi 114,738,930,000.00** kinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ulinganisho kati ya bajeti ya Mwaka 2025/2026 na bajeti ya mwaka 2026/2027, bajeti ya mwaka unaofuata imeongezeka kwa kiasi cha **shilingi 118,524,387,000.00** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka unaoisha ambayo ilikuwa ni **shilingi 368,642,306,000.00**. Ongezeko hilo ni wastani wa **asilimia 32.15**.

### 3.2.1 Mchanganuo wa Fedha za matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Aidha, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, bajeti yam waka 2026/2027 imeongezeka kwa kiasi cha **shilingi 74,999,091,000.00,** sawa na **asilimia 22.22**, ikilinganishwa na matumizi ya kawaida ya mwaka wa Fedha 2025/2026 ambayo ilikuwa ni **shilingi 297,428,672,000.00.** Katika kiasi hicho, mishahara imeongezeka kwa **shilingi 5,805,695,000.00** sawa na **asilimia 11.3** ikilinganishwa na mwaka unaoisha, na fedha za matumizi ya mengineyo (OC) zimeongezeka kwa kiasi cha **shilingi 72,193,350,000.00** sawa na **asilimia 29.7** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/2026. Mchanganuo wa bajeti ya Kawaida umeainishwa katika **jedwali Na12**

**JEDWALI NA. 12:** Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2026/2027

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 15,721,630,000.00 | 49,738,345,000.00 | 65,459,975,000.00 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 4,809,900,000.00 | 52,281,434,000.00 | 57,091,334,000.00 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 22,251,348,000.00 | 124,405,864,000.00 | 146,657,212,000.00 |
| **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama | 1,1017,424,000.00 | 7,130,120,000.00 | 8,147,544,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 4,115,311,000.00 | 13,291,446,000.00 | 17,406,757,000.00 |
| **Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania | 1,556,429,000.00 | 10,555,230,000.00 | 12,111,659,000.00 |
| **Fungu 19** - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 5,095,940,000.00 | 36,217,836,000.00 | 41,313,776,000.00 |
| **Fungu 101 –** Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria | 2,588,341,000.00 | 21,651,165,000.00 | 24,239,506,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **57,156,323,000** | **315,271,440,000.00** | **372,427,763,000.00** |

***Chanzo****: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

### 3.2.2 Mchanganuo wa Fedha za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za maendeleo, bajeti ya mwaka 2026/2027 imeongezeka kwa kiasi cha shilingi **43,525,296,000.00** sawa na **asilimia 61.12** ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo ya mwaka unaoisha ambayo ilikuwa shilingi **71,213,634,000.00.** Mchanganuo wa Miradi ya Maendeleo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 13**

**JEDWALI NA. 13:** Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2026/2027

| FUNGU | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 | |
|---|---|---|
| | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 94,425,953,000.00 | 446,867,000.00 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa | 4,000,000,000.00 | - |

| | | |
|---|---|---|
| Serikali | | |
| **FUNGU 35 –** Ofisi ya Taifa ya Mashitaka | 15,866,110,000.00 | - |
| **JUMLA NDOGO** | **114,292,063,000.00** | **446,867,000.00** |
| **JUMLA KUU** | **114,738,930,000.00** | |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya ujumla inaonesha kuwa bajeti yam waka 2026/2027 imeionggezeka katika kila kipengele, isipokuwa tu kwa fedha za maendeleo za nje. Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani. Kwa upande wa matumizi ya kawaida, Kamati ilielezwa kuwa, ongezeko katika matumizi ya kawaida linatokana na mabadiliko ya muundo wa utumishi na mishahara yaliyofanyika kwa baadhi ya taasisi ambpo mabadiliko hayo yataanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha unaofuata. Aidha, baadhi ya taasisi ziliongezewa fedha ili ziweze kuongeza kasi ya kutekeleza majukumu yake kwa lengo la kuendana na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050. Baadhi ya taasisi hizo ni Tume ya Kurekebisha Sheria ambayo inajukumu la kuchambua na kurekebisha sheria ili ziendane na matakwa ya Dira hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, fedha za maendeleo zimeongezeka kwa lengo la kutekeleza miradi ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa majengo ya Ofisi na kutekeleza mradi wa *Mama Samia Legal Aid Campaign*. Aidha, uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kwamba, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia majadiliano ya kina yaliyofanywa na Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka

2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ili kusaidia katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa Mafungu yote yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

(a) Taasisi nyingi chini ya Wizara hii zinakumbwa na changamoto ya majengo ya ofisi, hususan ofisi za mikoa. Aidha, kwa asilimia kubwa bajeti ya fedha za maendeleo inayohusu ujenzi wa ofisi hizo haikutolewa kikamilifu. Ili kutatua changamoto hiyo na kufikisha huduma kwa wananchi, Serikali ihakikishe inatoa fedha za maendeleo kikamilifu.

### 4.2 Ushauri Mahsus Fungu kwa Fungu

#### 4.2.1 Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

(a) Kwa kuwa mradi wa msaada wa huduma za kisheria unaojulikana kama *Mama Samia Legal Aid Campaign* umekuwa na manufaa kwa wananchi hasa wa hali ya chini kwa kuwapatia haki zao na hivyo kupunguza malalamiko, ili mradi huo uendelee kuleta tabasamu na matumaini kwa watu hao, Serikali iuendeleze mradi huo kwa kuwafikia wananchi mbalimbali hususan wananchi wa vijijini na maeneo mengine ya kimkakati yanayolalamikiwa kukithiri kwa migogoro mbalimbali.

#### 4.2.2 Fungu 16-Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

(a) Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mshitiri wa ujenzi wa kituo jumuishi cha kisheria katika mkoa wa Mwanza kilichoanza ujenzi mwaka 2022 na kutakiwa kukamilika mwaka 2023. Aidha, Kamati ilipofanya ukaguzi wa mradi huo tarehe 18 Machi, 2026 ilikuta utekelezaji wake umefikia **asilimia 74** licha ya Serikali kufanya malipo kwa kiasi cha **asilimia 88**, ili kuhakikisha mradi huo

unakamilika licha ya kuchelewa kwa zaidi ya **miezi 29**, Serikali ihakikishe inachukua hatua za haraka ili kuhakikisha SUMA JKT anakamilisha mradi huo licha ya mtindo wa utekelezaji wake unaosuasua.

### 4.2.3 Fungu 35- Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

(a) Ofisi ya Mashtaka imefanikiwa kuchukua jukumu la kusimamia na kuendesha mashauri ya jinai kote nchini kwa mashauri yanayofunguliwa mahakama za wilaya, mikoa, mahakama kuu na rufaa za mahakama ya rufani. Uwezekano huu umechangiwa na Ofisi hii kuanzisha Ofisi za mashtaka katika wilaya mbalimbali, isipokuwa kwa wilaya ishirini na moja tu (21). Kutokuwepo kwa Ofisi katika wilaya hizo 21 kuna athiri utekelezaji wa jukumu la kushtaki na kusimamia mashauri ya jinai katika wilaya hizo. Ili kuondokana na changamoto hiyo, Serikali ianzishe ofisi za mashtaka katika wilaya zilizobakia.

(b) Katika wilaya ambazo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeanzisha ofisi za mashataka za wilaya na kuteuwa wakuu wa mashtaka wa wilaya, kuna changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi muhimu ikiwemo magari na kopyuta, na hivyo kusababisha mazingira ya kufanya kazi katika wilaya hizo kuwa magumu. Ili watendaji waliopo katika ofisi hizo waweze kufanya kazi kwa ufanisi, Kamati inashauri kuwa Serikali inunue vitendea kazi muhimu ikiwemo magari, kompyuta na mashine za kudurufu.

### 4.2.4 Fungu 55- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

(a) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kuchunguza malalamiko yanayohusu uvunjifu wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora, na kufanikisha watu mbalimbali kupata haki zao. Licha ya mafanikio haya, Tume hii ina Ofisi katika mikoa mitano (5) tu kati ya mikoa 31 iliyopo nchini. Kukosekana kwa ofisi hizo, kumekuwa na athari za Tume kushindwa kufikiwa na wananchi wengi wa mikoa iliyobakia ili waweze kusaidiwa katika kupata haki zao. Ili kuondokana na changamoto hii, Serikali iiwezeshe Tume ili iweze kuanzisha Ofisi katika mikoa 26 iliyobakia.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Damas D.I Ndumbaro, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb - **M/Mweyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. - **Mjumbe**
4. Mhe. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - **Mjumbe**
5. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb - **Mjumbe**
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - **Mjumbe**
7. Mhe. Asha Hussein Saleh, Mb - **Mjumbe**
8. Mhe. Esther Edwin Malleko, Mb - **Mjumbe**
9. Mhe. Maryam Ussi Yahya, Mb - **Mjumbe**
10. Mhe. Nassoro Rashid Nassoro, Mb - **Mjumbe**
11. Mhe. Dkt. Neema Peter Majule, Mb - **Mjumbe**
12. Mhe. Nyamizi Simon Mhoja, Mb - **Mjumbe**
13. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb - **Mjumbe**
14. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb - **Mjumbe**
15. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb - **Mjumbe**
16. Mhe. Timida Mpoki Fyandomo, Mb - **Mjumbe**
17. Mhe. Dkt. Yahaya Esmail Nawanda, Mb - **Mjumbe**
18. Mhe. Yohana Stephen Msita, Mb - **Mjumbe**
19. Mhe. Zena Maulid Katambo, Mb - **Mjumbe**
20. Mhe. Hussein Nassoro Amar, Mb - **Mjumbe**

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru, **Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb)**) –Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria na Mhe. Zainabu Athuman Katiba (Mb)-Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wameendelela kuipatia Kamati yetu wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi hiyo pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Eliakim Chacha Maswi na Naibu Katibu Mkuu wake Dkt. Franklin Jasson Rwezimula.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leornard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
24 Aprili, 2026

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda kwa uwasilishaji wa taarifa ya Kamati, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa niaba yake Mheshimiwa Moses Bujaga.

**MHE. MOSES C. BUJAGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, nikitimiza wajibu huu kwa niaba ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama mbele yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa, napenda nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi, chini ya

Mwenyekiti wake Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kuwa mgombea wa Ubunge Jimbo la Sumve. Kwa kipekee kabisa, ninawashukuru wananchi wa Sumve kwa kunipa kura nyingi za kishindo katika uchaguzi mkuu, ninawaahidi uwakilishi uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, ninaomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Mfuko wa Mahakama, Fungu 40 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Ninaomba taarifa yote kama ilivyo iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Mahakama, Fungu 40 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania ni moja kati ya Mihimili mitatu ya Dola na majukumu yake makubwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ni kutafsiri sheria, kutolea maamuzi mashauri mbalimbali yanayoletwa mahakamani. Aidha, Ibara 107A(1) ya Katiba, imeipa Mahakama Mamlaka ya kuwa chombo pekee cha usimamizi wa utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 moja ya jukumu la Kamati ya Bajeti ni kuchambua makadirio ya bajeti ya Mahakama Fungu 40. Hivyo, katika kutekeleza takwa hilo la kisheria, tarehe 17 Machi, 2026 Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Juma Zuberi Homera, Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Mhandisi Mshamu Ali Munde, Naibu Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; pamoja na Profesa Elisante Ole Gabriel - Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kufanya majadiliano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya

Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Mahakama kuanzia tarehe Mosi Julai, 2025 hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2026, pamoja na vipaumbele vinavyopendekezwa kwenye mpango na bajeti ya Mfuko kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mfuko wa Mahakama uliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 291.1. Kati ya fedha hizo, shilingi 82,000,000,000 ni mishahara ya Mahakama, shilingi bilioni 2.6 ni mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na shilingi bilioni 143.4 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha za maendeleo zilizoidhinishwa ni shilingi 63,000,000,000 ambapo shilingi bilioni 18.6 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 44.4 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2026, Mfuko wa Mahakama ulikuwa umepokea jumla ya shilingi bilioni 220.8 sawa na 75.85% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 58.5 zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 106.9 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya shilingi bilioni 55.3 zilipokelewa katika kipindi hicho. Kati ya Fedha hizo shilingi 108,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 44.4 ni fedha za nje. Jedwali Namba Moja linaonesha mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa kipaumbele kwa Mfuko huu, kwa kuupatia rasilimali fedha ili uweze kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria. Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kugharamia mahitaji maalum ya Mahakama ambayo yana

maslahi mapana kwa uchumi na nchi kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na usikilizwaji wa mashauri ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Novemba hadi Desemba, 2025, Mahakama ilifanikisha usikilizaji na kutolea uamuzi mashauri ya kiuchumi yaliyokuwepo yenye thamani ya takribani shilingi trilioni 13.1. Uamuzi huu siyo tu ulipunguza idadi ya mashauri, lakini ulichochea mzunguko wa fedha kwenye uchumi kwa kuruhusu kiasi hicho cha fedha kuingia kwenye mzunguko, ambacho kilikuwa kinashikiliwa na Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kuipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua hii ya makusudi ambayo itachagiza katika kuvutia na kuongeza uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje. Kwani uimara wa Mahakama ya nchi ni moja ya kigezo muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na kuvutia uwekezaji katika nchi. Bila mfumo wa haki ulio thabiti, wawekezaji hukosa imani ya kuwekeza katika nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha maduhuli cha Mfuko wa Mahakama ni faini na ada za Mahakama. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mfuko wa Mahakama ulipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi bilioni 15.6. Hadi mwezi Februari, 2026, jumla ya shilingi bilioni 5.2 zilikusanywa sawa na 33.57% ya lengo, ufanisi huu mdogo ni kiashiria kuwa kumekuwa na ongezeko la kutii sheria nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio na changamoto ya utekelezaji wa majukumu ya Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; katika mwaka huo, Mfuko wa Mahakama umefanikiwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Usikilizaji wa mashauri; katika kipindi cha Mwezi Julai, 2025 hadi Februari, 2026, Mahakama ilikuwa na jumla ya mashauri 183,220. Kati ya mashauri hayo mashauri 45,187 ni mashauri yaliyokuwepo mwanzoni mwa Julai, 2025 na mashauri 138,033 ni mashauri mapya yaliyofunguliwa katika kipindi husika. Kati ya mashauri yote 182,220, mashauri

143,677 yameamuriwa katika kipindi tajwa na mashauri 39,543 yalikuwa yanaendelea kusikilizwa. Aidha, kati ya mashauri yote yaliyobaki Mahakamani, mashauri yenye umri mrefu kati ya miezi sita na miaka miwili kulingana na ngazi ya Mahakama ni 3,317 sawa na asilimia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafanikio hayo Mahakama ya Tanzania imeendelea kuongoza katika Ukanda wa Afrika kwa kuwa na kiwango cha chini cha asilimia nne cha mashauri ya muda mrefu. Hii imechagizwa na matumizi ya TEHAMA kutokana uwekezaji unaoendelea kufanywa na Serikali yetu Makini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya TEHAMA; Mahakama imeendelea kuimarisha na kutumia mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya mafanikio yaliyotokana na maboresho hayo ni pamoja Maamuzi 34,390 kuchapishwa katika maktaba mtandao, Maamuzi 7,174 kuchapishwa katika mfumo wa *TanzLII,* Jumla ya majalada 3,571 yenye kurasa 191,478 ya kumbukumbu za mashauri zilizozalishwa kipindi cha ukoloni, yamebadilishwa kwenda kwenye mfumo wa kidigitali na kutoa taarifa za mwenendo wa mashauri kupitia ujumbe mfupi wa meseji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya mifumo ya TEHAMA yamefanya Mahakama ya Tanzania kuwa miongoni mwa Mahakama zinazoongoza Afrika kwa kutumia mifumo ya TEHAMA katika kutekeleza majukumu yake. Matumizi ya TEHAMA yameonyesha mafanikio makubwa siyo tu katika kushughulikia mashauri, bali katika kuokoa muda, gharama pamoja na kurahisisha utendaji kazi. Aidha, mifumo imeongeza uwazi katika mnyororo wa utoaji haki na kukabiliana na changamoto ya watumishi wasio waadilifu.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha uwezo wa ukaguzi na usimamizi wa shughuli katika ngazi zote za Mahakama na Magereza; kwa kipindi cha Julai, 2025 mpaka Februari, 2026, ukaguzi wa shughuli za kimahakama ulifanyika katika Mahakama za chini kwa wastani wa 99.9%. Aidha, magereza 113 kati ya 130 yalikaguliwa sawa na 87%. Kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa

utendaji kazi wa Mahakama umesaidia Mahakama kudumisha uadilifu, ufanisi, kukuza utamaduni wa uwajibikaji, kuratibu michakato, kujenga imani kwa umma na kuhakikisha hukumu za haki na zisizo na upendeleo.

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama. Mahakama imeendelea na utekelezaji wa mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama wa miaka mitano (2021/2022–2025/2026) ambapo hadi kufikia Februari, 2026 miradi imefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama unahitimishwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na bado nchi haijaweza kujenga Mahakama katika maeneo mengine nchini hususani katika ngazi ya Kata; na kwa kuwa, kwa asilimia kubwa mpango huu ulitekelezwa kwa fedha za mkopo wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kutafuta fedha ili kuendeleza mpango huu na kuhakikisha kuwa huduma za utoaji haki zinapatikana katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto; pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mfuko wa Mahakama unaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(a) Ufinyu wa bajeti ya matumizi mengineyo ili kukidhi mahitaji ya huduma zilizoongezeka kutokana na Mahakama mpya katika baadhi ya mikoa;

(b) Uhaba na uchakavu wa majengo ya ofisi na makazi ya majaji hususan katika Mahakama za Mwanzo, Wilaya na Hakimu Mkazi;

(c) Upungufu wa vitendeakazi hususan magari; na

(d) Uhaba wa watumishi kwa baadhi ya Kada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi kwa ujumla zinachangiwa na kupanuka kwa shughuli za Mahakama na kuongezeka kwa vituo vya utoaji huduma. Aidha, Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuhakikisha inaiwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake. Kamati inatoa rai kwa Serikali kuwa, ihakikishe inatenga bajeti ya kutosha ili kugharamia utekelezaji wa mpango wa Mahakama na mipango ya taasisi zake, kwani hakutakuwa na tija kama ujenzi wa Mahakama unakamilika lakini hakuna rasilimaliwatu na vitendeakazi kwa ajili ya uendeshaji wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu;

(ii) Kuimarisha uwezo katika Ukaguzi na Usimamizi wa shughuli za Mahakama;

(iii) Kuandaa Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Majengo ya Mahakama kwa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031); na

(iv) Kutatua changamoto zozote zinazochelewesha utoaji haki kwa wakati na ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na malengo hayo Mahakama pia imepanga kufanya maboresho ya mfumo ya kisheria ambayo yanalenga kuleta ufanisi katika utoaji haki. Kamati ilijulishwa kuwa tayari Mahakama imeandaa maboresho ya sheria yenye malengo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kupunguza mashauri katika ngazi ya Mahakama ya Rufani. Kwa sasa Mahakama ya Rufani inakabiliwa na changamoto ya kuwa na mashauri mengi kuliko uwezo wake. Mahakama ya Rufani ina jumla ya majopo 12 na kila jopo lina wastani wa mashauri 787 kwa mwaka badala ya

mashauri 220 kwa mwaka yanayokubalika. Hii inafanya Mahakama ya Rufani kuelemewa na mzigo mkubwa wa mashauri na hivyo kuichukua muda mrefu kumaliza mashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuipunguzia Mahakama ya Rufani mzigo wa mashauri yanaoenda katika mahakama hiyo, Mahakama inapendekeza marekebisho ya sheria yatakayoanzisha ngazi mpya ya Mahakama itakayojulikana kama Mahakama ya Mkoa ambayo itakuwa Mahakama ya juu ya Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Mahakama hii kutasaidia kuchuja aina ya mashauri ambayo yatafanyiwa kazi kwenye Mahakama za juu, lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa mashauri yanayofika kwenye Mahakama ya Rufani ni yale mashauri ambayo yanahitaji kushughulikiwa kwenye ngazi hiyo. Hatua hii itapunguza mzigo mkubwa wa mashauri katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kurudisha mchakato wa kufanya maamuzi ya mashauri ya ardhi Mahakamani kutoka kwenye Mabaraza ya Ardhi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya na Kata yamekuwa na changamoto zifuatazo:-

(a) Ucheleweshaji wa utatuzi wa migogoro ya ardhi;

(b) Kutokuwa na wataalam wa Sheria;

(c) Kuwepo na ukiukwaji wa Sheria na kanuni katika kutoa haki katika Mabaraza; na

(d) Kukithiri kwa vitendo vya rushwa katika mabaraza ambapo asilimia kubwa ya malalamiko ya rushwa yanatokana na mashauri ya ardhi ya kwenye mabaraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kufuta Mabaraza ya Ardhi na kurejesha usuluhishi wa masuala ya ardhi

katika Mahakama katika mwaka mpya wa fedha ili utekelezaji wake uanze mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kufuta mabaraza ya ardhi na kurejesha usuluhishi wa masuala ya ardhi katika Mahakama katika mwaka mpya wa fedha ili utekelezaji wake uanze mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mfuko wa Mahakama umetengewa jumla ya shilingi bilioni 287.6 sawa na pungufu ya asilimia 1.18 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 ya shilingi bilioni 291.1. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 92.9 ni kwa ajili ya mishahara ya Mahakama, shilingi bilioni 2.4 ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na shilingi bilioni 169.6 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, fedha za matumizi ya maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni 22.7. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 18.6 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 4.1 ni fedha za nje. Mchanganuo wa bajeti umeainishwa kwenye jedwali Na.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa bajeti ya Mfuko kwa asilimia 1.18 kumesababishwa na kupungua kwa fedha za maendeleo kutoka nje zilizokuwa zinatokana na mkopo wa Benki ya Dunia ambapo ulifikia ukomo mwezi Disemba, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha fedha za matumizi mengineyo zimeongezeka kwa shilingi bilioni 26.3 kutoka shilingi bilioni 143 Mwaka wa Fedha 2025/2026 hadi Shilingi bilioni 169 sawa na ongezeko la 18.31%. Ongezeko hilo lina lengo la kukidhi mahitaji yaliyotokana na uanzishwaji wa Mahakama mpya katika baadhi ya mikoa pamoja na stahiki za msingi za Majaji na Mahakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maduhuli; katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Fungu 40 linakusudia kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi bilioni 15.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati; upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mahakama za mwanzo. Takribani 70.84% ya mashauri yote ya Mahakama yanatoka katika ngazi ya mahakama za mwanzo. Hata hivyo, kuna upungufu mkubwa wa mahakama hizi ambapo kuna mahakama za mwanzo 960 ikilinganishwa na idadi ya kata 3,956 zilizopo nchini. Hivyo, kuna uhaba wa mahakama za mwanzo takribani 2,996.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahakama mpya za mwanzo zilizopo hivi sasa kwa kiasi kikubwa zilijengwa kwa fedha za mkopo wa Benki ya Dunia ambapo mpango wake umekoma. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 22.7 ambazo hazikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya uendelezaji wa mradi huu muhimu. Aidha, Kamati inaisisitiza Serikali kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Wizara ya Fedha, Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kuhusu uendelezaji wa mradi huu kupitia ushirikiano baina ya taasisi hizi tatu sambamba na utengaji wa bajeti ya kutosha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama kupitia halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi kupewa kipaumbele. Migogoro ya ardhi imekuwa ni changamoto kubwa nchini inayosababisha mivutano ya kijamii, kisiasa na kiuchumi, hususan katika maeneo yenye shughuli za kilimo, ufugaji na uhifadhi na hivyo kuathiri ajenda za maendeleo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mashauri mengi ya migogoro ya ardhi; kwa mfano kwenye mashamba ya chai yaliyopo Mbeya na Tanga, ambayo kutokana na kuchelewa kutatuliwa kwake yameleta athari hasi kwa wakulima wa zao hilo na kwa zao hili kwa ujumla. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za makusudi kama ilivyofanya kwenye mashauri ya kiuchumi ili mashauri ya mashamba ya chai yaweze kuamuriwa ili kuendeleza mchango wa zao hili katika ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vituo jumuishi vya utoaji haki Kamati inaipongeza Mahakama kwa kuendeleza ujenzi wa vituo hivyo. Utaratibu wa utoaji haki katika paa moja bado ni mpya duniani ambapo Tanzania ni ya pili kwa kuwa na vituo hivi ikiongozwa na Nchi ya Guatemala. Hadi hivi sasa kuna vituo jumuishi sita vilivyokamilika na kuanza kutoa huduma na vingine tisa vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa utaratibu huu unaorahisisha upatikanaji wa huduma katika eneo moja, lakini pia umewezesha wananchi kupata haki kwa wakati, kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani, kuongeza kasi ya uondoshaji wa mashauri pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa mashauri kwa Mahakama na wananchi. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuendelea kuunga mkono ujenzi wa vituo hivi ambao mfumo wake umeleta mageuzi katika sekta ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge pamoja na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Spika kwa miongozo yenu katika kuendesha shughuli za Bunge. Aidha, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Juma Zuberi Homera, Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar, Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Mhandisi Mshamu Ali Munde, Naibu Waziri wa Fedha; na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula, Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao wakati Kamati inajadili bajeti ya Mfuko wa Mahakama - Fungu 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inamshukuru Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Dkt. Natu Elmaamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha pamoja na wataalam wote wa Ofisi ya Mahakama na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya bajeti ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali

kuhusu bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Majina ya Wajumbe hao ni kama yanavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndugu Baraka I. Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ninaliomba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria yenye jumla ya shilingi 287,632,943,714 ambapo kiasi cha shilingi 92,911,764,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Mahakama, shilingi 2,391,701,000 ni mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, shilingi 169,638,278,714 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 22,691,200,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA – FUNGU 40 KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za kudumu za Bunge za mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Mahakama ya Tanzania ni moja kati ya Mihimili mitatu ya Dola na majukumu yake makubwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ni kutafsiri Sheria na kutolea maamuzi mashauri mbalimbali yanayoletwa Mahakamani. Aidha, Ibara 107(A) (1) ya Katiba, imeipa Mahakama Mamlaka ya kuwa chombo pekee cha Usimamizi wa utoaji haki.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 moja ya jukumu la Kamati ya Bajeti ni kuchambua makadirio ya bajeti ya Mahakama Fungu 40. Hivyo, katika kutekeleza takwa hilo la kisheria tarehe 17 Machi, 2026 Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb), Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba (Mb), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kufanya majadiliano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Mfuko wa Mahakama kuanzia tarehe 01 Julai 2025 hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2026, pamoja na vipaumbele vinavyopendekezwa kwenye Mpango na Bajeti ya Mfuko kwa mwaka wa Fedha 2026/2027.

**2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Mfuko wa Mahakama uliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 291,056,230,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 82,028,785,000** ni mishahara ya Mahakama, **Shilingi 2,616,257,000** ni mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (Institute of Judiciary Administration - IJA) na **Shilingi 143,385,988,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Aidha, fedha za maendeleo zilizoidhinishwa ni **Shilingi 63,025,200,000** ambapo **Shilingi** 18,601,200,000 ni fedha za ndani na Shilingi **44,424,000,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi tarehe 28 Februari, 2026 Mfuko wa Mahakama ulikuwa umepokea jumla ya **Shilingi 220,757,090,527.83** sawa na **asilimia 75.85** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha zilizopokelewa **Shilingi 58,500,339,420.40** zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 106,988,304,264.04** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **Shilingi 55,268,446,843.39** zilipokelewa katika kipindi hicho. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 10,844,446,843.39** ni fedha za ndani na **Shilingi 44,424,000,000** ni fedha za nje. **Jedwali Na. 1** linaonyesha mwenendo wa utekelezaji Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Jedwali Na. 1: Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 40 kwa mwaka 2025/26 hadi kufikia Februari, 2026**

| Matumizi | Bajeti iliyoidhinishwa 2025/26 | Fedha iliyotolewa hadi Februari 2026 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara Mahakama + IJA | **84,645,042,000** | **58,500,339,420.40** | **69.1** |
| Matumizi mengineyo | **143,385,988,000** | **106,988,304,264.04** | **74.6** |
| Fedha za Maendeleo | **63,025,200,000** | **55,268,446,843.39** | **87.7** |
| • Maendeleo Ndani | 18,601,200,000 | 10,844,446,843.39 | **58.3** |
| • Maendeleo Nje | 44,424,000,000 | 44,424,000,000 | **100.0** |
| **JUMLA** | **291,056,230,000** | **220,757,090,428** | **75.8** |

***Chanzo*:** Randama ya Fungu 40

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa kipaumbele kwa Mfuko huu kwa kuupatia rasilimali fedha ili uweze kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba na Kisheria. Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kugharamia mahitaji maalum ya Mahakama ambayo yana

maslahi mapana kwa uchumi na nchi kwa ujumla ikiwa ni pamoja na usikilizwaji wa mashauri ya kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Novemba hadi Desemba, 2025, Mahakama ilifanikisha usikilizaji na kutolea uamuzi mashauri ya kiuchumi yaliyokuwepo yenye thamani ya takribani **Shilingi 13,100,000,000,000.** Uamuzi huu sio tu ulipunguza idadi ya mashauri lakini ulichochea mzunguko wa fedha kwenye uchumi kwa kuruhusu kiasi hicho cha fedha kuingia kwenye mzunguko ambacho kilikuwa kinashikiliwa na Mahakama.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kuipongeza Serikali inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa hatua hii ya makusudi ambayo itachagiza katika kuvutia na kuongeza uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje. Kwani uimara wa Mahakama ya nchi ni moja ya kigezo muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na kuvutia uwekezaji katika nchi. Bila mfumo wa haki ulio thabiti, wawekezaji hukosa imani ya kuwekeza katika nchi husika.

**Mheshimiwa Spika**, chanzo cha maduhuli cha Mfuko wa Mahakama ni faini na ada za Mahakama ***(Fines and Court Fees).*** Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Mfuko wa Mahakama ulipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 15,571,199,000**. Hadi mwezi Februari, 2026, jumla ya **Shilingi 5,226,491,848.37** zilikusanywa sawa na **asilimia 33.57** ya lengo. Ufanisi huu mdogo ni kiashiria kuwa kumekuwa na ongezeko la kutii Sheria nchini.

## 3.0. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 3.1. Mafanikio

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Mfuko wa Mahakama umefanikiwa kutekeleza majukumu yafuatayo;

#### a) Usikilizaji wa mashauri

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwezi Julai 2025 hadi Februari, 2026, Mahakama ilikuwa na jumla ya mashauri **183,220**.

Kati ya mashauri hayo mashauri **45,187** ni mashauri yaliyokuwepo mwanzoni mwa Julai, 2025 na mashauri **138,033** ni mashauri mapya yaliyofunguliwa katika kipindi husika. Kati ya mashauri yote **182,220**, mashauri **143,677** yameamuriwa katika kipindi tajwa na mashauri **39,543** yalikuwa yanaendelea kusikilizwa. Aidha, kati ya mashauri yote yaliyobaki Mahakamani, mashauri yenye umri mrefu (kati ya miezi 6 na miaka 2 kulingana na ngazi ya Mahakama) ni **3,317** sawa na **asilimia 4.**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mafanikio hayo Mahakama ya Tanzania imeendelea kuongoza katika ukanda wa Afrika kwa kuwa na kiwango cha chini cha **asilimia 4** cha mashauri ya muda mrefu. Hii imechagizwa na matumizi ya TEHAMA kutokana uwekezaji unaoendelea kufanywa na Serikali yetu Makini.

**b) Matumizi ya TEHAMA**

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama imeendelea kuimarisha na kutumia mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya mafanikio yaliyotokana na maboresho hayo ni pamoja Maamuzi **34,390** kuchapishwa katika Maktaba mtandao, Maamuzi **7,174** kuchapishwa katika mfumo wa TanzLII, Jumla ya majalada **3,571** yenye kurasa **191,478** ya kumbukumbu za mashauri zilizozalishwa kipindi cha ukoloni (19201960) yamebadilishwa kwenda kwenye mfumo wa kidigitali na kutoa taarifa za Mwenendo wa mashauri kupitia ujumbe mfupi wa meseji.

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya mifumo ya TEHAMA yamefanya Mahakama ya Tanzania kuwa miongoni mwa Mahakama zinazoongoza Afrika kwa kutumia mifumo ya TEHAMA katika kutekeleza majukumu yake.

Matumizi ya TEHAMA yameonyesha mafanikio makubwa sio tu katika kushughulikia mashauri bali katika kuokoa muda, gharama pamoja na kurahisisha utendaji kazi. Aidha, mifumo imeongeza uwazi katika mnyororo wa utoaji haki na kukabiliana na changamoto ya watumishi wasio waadilifu.

**c) Kuimarisha uwezo wa Ukaguzi na usimamizi wa shughuli katika ngazi zote za Mahakama na Magereza**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2025 – Februari, 2026 Ukaguzi wa shughuli za kimahakama ulifanyika katika Mahakama za chini kwa wastani wa **asilimia 99.9**. Aidha, magereza **113** kati ya **130** yalikaguliwa sawa na **asilimia 87**. Kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa utendaji kazi wa Mahakama umesaidia Mahakama kudumisha uadilifu, ufanisi, kukuza utamaduni wa uwajibikaji, kuratibu michakato, kujenga imani kwa umma na kuhakikisha hukumu za haki na zisizo na upendeleo.

**d) Utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama**

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama wa Miaka Mitano (2021/2022–2025/2026) ambapo hadi kufikia Februari, 2026 Miradi imefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Mpango wa Ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama unahitimishwa mwaka 2025/2026 na bado nchi haijaweza kujenga Mahakama katika maeneo mengine nchini hususani katika ngazi ya Kata. Na kwa kuwa, kwa asilimia kubwa Mpango huu ulitekelezwa kwa fedha za Mkopo wa Benki ya Dunia. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kutafuta fedha ili kuendeleza Mpango huu na kuhakikisha kuwa huduma za utoaji haki zinapatikana katika maeneo yote nchini.

**3.2. Changamoto**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Mfuko wa Mahakama unaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo: -

i. Ufinyu wa bajeti ya Matumizi Mengineyo ili kukidhi mahitaji ya huduma zilizoongezeka kutokana na Mahakama mpya katika baadhi ya mikoa;

ii. Uhaba na uchakavu wa majengo ya ofisi na makazi ya majaji hususan katika Mahakama za Mwanzo, Wilaya na Hakimu Mkazi;

iii. Upungufu wa vitendea kazi hususan magari; na

iv. Uhaba wa watumishi kwa baadhi ya Kada.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto hizi kwa ujumla zinachangiwa na kupanuka kwa shughuli za Mahakama na kuongezeka kwa vituo vya utoaji huduma. Aidha, Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuhakikisha inaiwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake. Aidha, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuwa ihakikishe inatenga Bajeti ya kutosha ili kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Mahakama na Mipango ya Taasisi zake. Kwani hakutakuwa na tija kama ujenzi wa Mahakama unakamilika lakini hakuna rasilimali watu na vitendea kazi kwa ajili ya uendeshaji wa vituo hivyo.

**4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (Backlog);

ii. Kuimarisha uwezo katika Ukaguzi na Usimamizi wa shughuli za Mahakama;

iii. Kuandaa Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Majengo ya Mahakama kwa miaka mitano (2026/2027 – 2030/2031); na

iv. Kutatua changamoto zozote zinazochelewesha utoaji Haki kwa wakati na ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na malengo hayo Mahakama pia imepanga kufanya maboresho ya mfumo ya kisheria ambayo yanalenga kuleta ufanisi katika utoaji haki. Kamati ilijulishwa kuwa tayari Mahakama imeandaa maboresho ya Sheria yenye malengo yafuatayo:-

**Kupunguza mashauri katika ngazi ya Mahakama ya Rufani**

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa Mahakama ya Rufani inakabiliwa na changamoto ya kuwa na mashauri mengi kuliko uwezo wake. Mahakama ya Rufani ina jumla ya majopo **12** na kila jopo lina wastani wa mashauri **787** kwa mwaka badala ya mashauri **220** kwa mwaka yanayokubalika. Hii inafanya Mahakama ya Rufani kuelemewa na mzigo mkubwa wa mashauri na hivyo kuichukua muda mrefu kumaliza mashauri.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuipunguzia Mahakama ya Rufani mzigo wa mashauri yanaoenda katika mahakama hiyo, Mahakama inapendekeza marekebisho ya Sheria yatakayoanzisha ngazi mpya ya Mahakama itakayojulikana kama Mahakama ya Mkoa ambayo itakuwa mahakama ya juu ya mahakama ya Wilaya.

**Mheshimiwa Spika**, kuanzishwa kwa Mahakama hii kutasaidia kuchuja aina ya mashauri ambayo yatafanyiwa kazi kwenye mahakama za juu lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa mashauri yanayofika kwenye Mahakama ya Rufani ni yale mashauri ambayo yanahitaji kushughulikiwa kwenye ngazi hiyo. Hatua hii itaenda kupunguza mzigo mkubwa wa mashauri katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani.

**Kurudisha mchakato wa kufanya maamuzi ya mashauri ya ardhi Mahakamani kutoka kwenye mabaraza ya ardhi**

Hii ni kutokana na ukweli kwamba Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya na Kata yamekuwa na changamoto zifuatazo:-

1) Ucheleweshaji wa utatuzi wa migogoro ya ardhi;

2) Kutokuwa na wataalam wa Sheria;

3) Kuwepo na ukiukwaji wa Sheria na kanuni katika kutoa haki katika Mabaraza; na

4) Kukithiri kwa vitendo vya rushwa katika mabaraza ambapo asilimia kubwa ya malalamiko ya rushwa yanatokana na mashauri ya ardhi ya kwenye mabaraza.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kufuta mabaraza ya ardhi na kurejesha usuluhishi wa masuala ya ardhi katika Mahakama katika mwaka mpya wa fedha ili utekelezaji wake uanze mapema iwezekanavyo.

**4.1. Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2026/2027**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Mfuko wa Mahakama umetengewa jumla ya **Shilingi 287,632,943,714** sawa na pungufu ya **asilimia 1.18** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/2026 ya **Shilingi 291,056,230,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 92,911,764,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Mahakama, **Shilingi 2,391,701,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) na **Shilingi 169,638,278,714** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha za matumizi ya maendeleo zilizotengwa ni **Shilingi 22,691,200,000,** kati ya fedha hizo **Shilingi 18,601,200,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 4,090,000,000** ni fedha za nje. Mchanganuo wa bajeti umeainishwa kwenye **jedwali Na.2.**

**Jedwali Na.2.** Ulinganisho wa Bajeti ya Fungu 40 kwa Mwaka 2025/26 na 2026/27

| Matumizi | 2025/26 | 2026/27 | Tofauti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya kawaida** | **228,031,030,000** | **264,941,743,714** | **36,910,713,714** | **16.19** |
| • **Mishahara** | 84,645,042,000 | 95,303,465,000 | 10,658,423,000 | 12.59 |
| •Mishahara ya Mahakama | 82,028,785,000 | 92,911,764,000 | 10,882,979,000 | 13.27 |
| • Mishahara ya IJA | 2,616,257,000 | 2,391,701,000 | -224,556,000 | (8.58) |
| • **Matumizi Mengineyo** | 143,385,988,000 | 169,638,278,714 | 26,252,290,714 | 18.31 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya Maendeleo** | **63,025,200,000** | **22,691,200,000** | **40,334,000,000** | **(64.00)** |
| • Ndani | 18,601,200,000 | 18,601,200,000 | 0 | - |
| • Nje | 44,424,000,000 | 4,090,000,000 | -40,334,000,000 | (90.79) |
| **JUMLA** | **291,056,230,000** | **287,632,943,714** | **-3,423,286,286** | **(1.18)** |

**Chanzo:** Randama Fungu 40

**Mheshimiwa Spika,** kupungua kwa bajeti ya Mfuko kwa **asilimia 1.18** kumesababishwa na kupungua kwa fedha za maendeleo kutoka nje zilizokuwa zinatokana na mkopo wa Benki ya Dunia ambao ulifikia ukomo mwezi Disemba 2025.

**Mheshimiwa Spika,** aidha Fedha za matumizi mengineyo zimeongezeka kwa **Shilingi 26,252,290,714** kutoka **Shilingi 143,385,988,000** mwaka 2025/2026 hadi **Shilingi 169,638,278,714** sawa na ongezeko la **asilimia 18.31.** Ongezeko hilo lina lengo la kukidhi mahitaji yaliyotokana na uanzishwaji wa Mahakama mpya katika baadhi ya mikoa pamoja na stahiki za msingi za majaji na mahakimu.

### 4.2. Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2026/2027 Fungu 40 linakusudia kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 15,571,000,000.**

## 5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 5.1. Upatikanaji wa Fedha kwa Ajili ya Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo

**Mheshimiwa Spika**, takribani **asilimia 70.84** ya mashauri yote ya Mahakama yanatoka katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo. Hata hivyo, kuna upungufu mkubwa wa Mahakama hizi ambapo kuna Mahakama za Mwanzo **960** ikilinganishwa na idadi ya Kata **3,956** zilizopo nchini**.** Hivyo, kuna uhaba wa Mahakama za Mwanzo takribani **2,996.**

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama mpya za Mwanzo zilizopo hivi sasa kwa kiasi kikubwa zilijengwa kwa fedha za mkopo wa

Benki ya Dunia ambapo Mpango wake umekoma. Katika mwaka 2026/2027 fedha za miradi ya maendeleo ni **Shilingi 22,691,200,000** ambazo hazikidhi mahitaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya uendelezaji wa mradi huu muhimu. Aidha, Kamati inaisisitiza Serikali kutekeleza maagizo ya **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa Wizara ya Fedha, Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kuhusu uendelezaji wa mradi huu kupitia ushirikiano baina ya taasisi hizi tatu sambamba na utengaji wa bajeti ya kutosha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama kupitia Halmashauri.

**5.2. Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi kupewa kipaumbele**

**Mheshimiwa Spika,** migogoro ya ardhi imekuwa ni changamoto kubwa nchini inayosababisha mivutano ya kijamii, kisiasa na kiuchumi hususan katika maeneo yenye shughuli za kilimo, ufugaji na uhifadhi na hivyo kuathiri ajenda za maendeleo nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kuna mashauri mengi ya migogoro ya ardhi mfano kwenye mashamba ya chai yaliyopo Mbeya na Tanga ambayo kutokana na kuchelewa kutatuliwa kwake yameleta athari hasi kwa wakulima wa zao hilo na kwa zao hili kwa ujumla. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za makusudi kama ilivyofanya kwenye mashauri ya kiuchumi ili mashauri ya mashamba ya chai yaweze kuamuriwa ili kuendeleza mchango wa zao hili katika ukuaji wa uchumi.

**5.3. Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Mahakama kwa kuendeleza ujenzi wa vituo jumuishi vya kutolea haki. Utaratibu wa utoaji haki katika paa moja bado ni mpya duniani ambapo Tanzania ni ya pili kwa kuwa na vituo hivi ikiongozwa na nchi ya Guatemala. Hadi hivi sasa kuna vituo jumuishi **6** vilivyokamilika na kuanza kutoa huduma na vingine **9** vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa utaratibu huu unaorahisisha upatikanaji wa huduma katika eneo moja lakini pia umewezesha wananchi kupata haki kwa wakati, kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani, kuongeza kasi ya uondoshaji wa mashauri pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa mashauri kwa Mahakama na wananchi.

Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuendelea kuunga mkono ujenzi wa vituo hivi ambao mfumo wake umeleta mageuzi katika sekta ya haki.

**6.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, (Mb) Spika wa Bunge pamoja na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, (Mb) Naibu Spika kwa miongozo yenu katika kuendesha shughuli za Bunge. Aidha, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba (Mb), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula (Mb), Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao wakati Kamati inajadili bajeti ya Mfuko wa Mahakama Fungu 40. Aidha, Kamati inamshukuru Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Dkt. Natu Elmaamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha pamoja na wataalamu wote wa Ofisi ya Mahakama na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb — Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Bal. Dkt. Pindi Azara Chana, Mb — Mjumbe

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Kakulu Buchard Kakulu, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Dkt. Catherine Canute Joachim, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Moses Charles Bujaga, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Asma Ali Mwinyi, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Haran Nyakisa Sanga, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Devotha Daniel Mburarugaba, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Thomas Mgonto Kitima, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Enock Zadock Koola, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Nancy Hassan Nyalusi, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndg. Baraka I. Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria yenye jumla ya **Shilingi 287,632,943,714** ambapo kiasi cha **Shilingi 92,911,764,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama, **Shilingi 2,391,701,000** ni Mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), **Shilingi 169,638,278,714** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 22,691,200,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
24 Aprili, 2026

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tunakushukuru kwa uwasilishaji wako. Waheshimiwa sasa tunaingia kwenye uchangiaji na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kupata fursa ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Ningependa nianze na Mhimili wa Mahakama. Takwimu zilizotolewa hapa zinaonesha bayana kutoka mwaka 2021 wakati Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani hadi mwaka 2025 takwimu za bajeti ya Mahakama zimekuwa zikiongezeka. Mwaka 2021 bajeti ya Mahakama ilikuwa ni bilioni 166, mwaka 2025 bajeti ya Mahakama ni shilingi bilioni 321, sawa na ongezeko la 95%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi si namba tu, ni namba ambazo zinaonyesha dhamira ya Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba Mhimili wa Mahakama unatenda haki kwa wananchi wake; na ili utende haki ni lazima wapewe vitendea kazi na moja kati ya vitendea kazi ni ongezeko la bajeti hiyo. Mheshimiwa Rais kwenye hili tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye ajira, katika kipindi cha miaka mitano Mahakama imeajiri wafanyakazi wapya 2081, ambapo Majaji wa Mahakama Kuu wameongezeka kutoka Majaji 84 hadi Majaji 104. Majaji wa Makahakama ya Rufani wameongezeka kutoka Majaji 25 hadi 37 na wengi wao wakiwa wanawake. Hapa lengo ni kupunguza msongamano uliokuwepo Mahakamani kwa muda mrefu; na matokeo yake sasa ukienda Magereza unaona kabisa msongamano umepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hapa kwenye hizi taarifa za leo, msongamano wa mashauri katika Mahakama zetu ni asilimia nne tu na kuifanya Mahakama ya Tanzania iongoze katika ufanisi kwenye hiki kigezo. Haya ni matokeo ya Mheshimiwa Rais kwa kufanya uteuzi wa Majaji na kuongeza ajira za Waheshimiwa Mahakimu ili tuweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miundombinu ya Mahakama jumla ya majengo 120 yamejengwa na kukarabatiwa

katika miaka mitano iliyopita. Kati ya majengo hayo majengo nane ni ya Mahakama Kuu, majengo 35 ni ya Mahakama za Wilaya, majengo 72 ni Mahakama ya Mwanzo. Hii inaonyesha kwa namna gani Serikali na Mheshimiwa Rais siyo tu wamejali ajira na kuongeza bajeti, pia amekwenda kuhakikisha majengo ambayo ndiyo vituo vya utoaji haki kuanzia Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya na Mahakama Kuu zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Kamati ya Bajeti tumesikia hapa; Tanzania ni nchi ya pili duniani kuwa na vituo vya pamoja vya utoaji haki na nchi ya kwanza Barani Afrika katika eneo hilo. Mimi kule Songea Mjini katika jimbo langu nimejengewa kituo cha pamoja cha utoaji haki ambacho tunatarajia baada ya kukamilika kitaleta ufanisi mkubwa sana. Hivyo, kwenye hili tunawapongeza Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ya kuhakikisha kwamba mabaraza ya ardhi na nyumba yanahamia Mhimili wa Mahakama. Mimi ninasema tumechelewa sana, hili lilipaswa lifanyike jana. Niliombe Bunge hili Tukufu tuichukue hii kama ajenda; na kwa kupitia hii bajeti ambayo inakwenda kupitishwa leo Mabaraza ya Ardhi na Nyumba yarudi katika Mhimili wa Mahakama. Kwa sababu kwa mujibu wa Katiba, Mahakama ndicho chombo kilichokasimiwa mamlaka ya utatuzi wa migogoro. Tuwaache ambao wana mamlaka ya Kikatiba waweze kufanya shughuli hiyo kwa mujibu wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu niongelee *Mama Samia Legal Aid Campaign*. Ni kampeni ambayo imefanyika kwa mafanikio makubwa, imezunguka mikoa yote 31 ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Katika Kampeni hii imejionyesha kwamba tatizo linaloongoza ni migogoro ya ardhi. Katika migogoro yote 7,600,000 ambayo imepatikana ndani ya mzunguko wa kwanza, migogoro 2,400,000, sawa na 32% inatokana na eneo la ardhi. Namba hizi zinatuonyesha kuna shida kwenye ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ile suluhu ambayo imependekezwa hapa, kwamba utatuzi wa migogoro ya ardhi urudi Mahakamani, ndiyo suluhu hasa ya kuipunguza hii 32%. Bila hivyo migogoro ya ardhi itaendelea, wananchi wataendelea

kupigana, wafugaji na wakulima wataendelea kuuana na sisi tupo tumekaa hapa tunaliangalia tu; hilo haliwezekani. Hili lazima tulisimamie vizuri kabisa

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kuongelea Dira 2050. Dira ya 2050 imesema kwamba, utawala bora, haki pamoja na mifumo imara ya kisheria ndiyo msingi wa kiuchumi. Tunapokwenda kuitafuta dola trilioni moja, ni lazima kwanza tuwekeze katika suala la utawala bora, ni lazima kwanza tuwekeze katika suala la haki, ni lazima kwanza tuwekeze katika mifumo imara ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ambayo Mheshimiwa Dkt. Juma Homera ameiwasilisha leo, inakwenda kutekeleza Dira ya 2050. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha bajeti nzuri, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri katika bajeti hii. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuleta bajeti hii ili Dira ya 2050 iweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, niliombe Bunge lako Tukufu lipitishe bajeti hii ambayo ninaiunga mkono ili tukatekeleze Dira ya 2050. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako na mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana wa leo atakuwa Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, ni mara yangu ya kwanza katika Bunge hili la Kumi na Tatu, nianze kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nikishukuru chama changu, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wote tunakubaliana, ninampongeza Mheshimiwa Rais, kwanza kwa umakini wake, lakini pili kwa uimara, tatu kwa ustahimilivu na nne kwa usimamizi thabiti wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani wote tunaendelea kushuhudia namna Mheshimiwa Rais anavyoendelea kutuongoza sisi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zangu za tatu, ninazipeleka kwa wanawake wa Mkoa wa Mtwara kwa kunipa tena nafasi ya kurudi katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nijikite katika hotuba iliyopo mezani ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kama nilivyotangulia kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais, ninarejea tena kumpongeza sana kwa sababu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri yameonekana mafanikio kadhaa tena ni mengi. Ninawapongeza sana Wizara kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, yapo mambo yamefanyika. Nikirejea katika mzungumzaji aliyepita katika ile kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia ambayo imejulikana kwa Kimakuwa kama Mama Samia *Legal Aid*. Tumeona yako mafanikio makubwa sana, lakini yale ni maono ya Mheshimiwa Rais. Ile kampeni imewawezesha wananchi ambao walikuwa na uhitaji mkubwa wa kuhakikisha kwamba haki yao inapatikana na hasa wanawake na makundi maalum na watu wa pembezoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonekana jumla ya watu waliofikiwa ni 4,157,065,000. Ukiangalia kwa makundi ya wanawake na wanaume unaona karibu kuna uwiano sawa. Lakini migogoro iliyoshughulikiwa ukiacha ardhi, kuna masuala ya mirathi, kuna masuala ya talaka na migongano ya ndoa, lakini kuna masuala ya ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ukiangalia kwa awamu ya kwanza imekuwa na mafanikio makubwa. Ni ombi langu, ninatambua awamu ya kwanza imeishia hii 2026, (2023 - 2026). Ni ombi langu na rai yangu kwa Serikali ya chama changu kwamba, awamu ya pili ni muhimu ianze sasa 2026 - 2030 kwa sababu, kuna uhitaji mkubwa wa wananchi walio pembezoni,

wanaohitaji kutatuliwa migogoro yao na kupata haki. Hii inathibitishwa na hata ziara za viongozi tunaona bado kuna wananchi wengi wanaowasilisha migogoro kama sehemu ya matatizo ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ninaomba nijielekeze ni Taasisi ya *RITA*. *RITA* iko chini kwenye Ofisi za Wakuu wa Wilaya na kwa ushahidi, ofisi hii haina *manpower* za kutosha, lakini haina pia hata vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi ofisi za ma-*DAS* ndizo zinazosimamia *RITA,* lakini kazi inayofanywa na *RITA* ni kubwa sana. Hapa kuna changamoto ambazo pengine ni kutokana na fedha, lakini fedha ambazo zinatakiwa ziende *RITA* zinatokana na *retention,* ambapo mara nyingi huwa haiendi. Hata kama kunakuwa kuna kazi imefanyika, lakini zile fedha hazirudi kwenye ofisi za *RITA* kwenye wilaya zetu. Inakwamisha kazi ya usajili wa vizazi na vifo na tunafahamu, sisi tumekuwa tukifanya sensa kila baada ya miaka 10. Je, hii miaka ya katikati hapa hatuhitaji kufahamu idadi ya vizazi vilivyopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati nchi inaendelea kupanga mipango ya maendeleo na Bunge tunapopitisha, ni muhimu kuzingatia pia idadi ya watu mwaka kwa mwaka na hii kazi inafanywa na *RITA*. Kukosekana kwa rasilimali katika *RITA* inakwamisha mamlaka nyingine za Serikali Ikiwemo *NIDA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu sasa hivi katika shughuli zote, cheti cha kuzaliwa ni muhimu sana. Tumekuwa tukishuhudia wakati vijana wetu wanapotaka kwenda chuo kumekuwa na foleni kubwa sana katika ofisi za *RITA,* lakini wakati wanapotaka kujiunga, kwa mfano na JKT, hata kazi zinazotolewa na vyombo lazima wawe na cheti cha kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni muhimu sana ili *NIDA* ifanye vizuri kwa kuwa cheti cha kuzaliwa ni kigezo kikubwa sana katika kupata namba ya *NIDA* ama namba ya utambulisho wa kitaifa, ni muhimu sana tukaimarisha *RITA* kwa vitendea kazi, rasilimali watu na fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu na ninaamini ni la mwisho; katika yale mafanikio ya Wizara ipo kazi kubwa pia wameifanya katika bajeti, tumeiona katika taarifa hii. Suala la urekebu wa sheria, Sheria 446 zote tulizonazo, zimefanyiwa urekebu. Kwanza suala la urekebu wa sheria ni gumu, lakini pia linahitaji muda na linahitaji fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa nini? Kwa sababu kazi hii ni ngumu. Ilifanyika kwa mara ya kwanza miaka 60 iliyopita, ikafanyika kwa mara ya pili mwaka 2002 na imefanyika kwa mara ya tatu mwaka 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee 2023 kwa nini? Mara ya kwanza ilitumia fedha za wahisani, mara ya pili ikatumia fedha za wahisani, *World Bank* lakini mara ya tatu tumetumia fedha za ndani, fedha za walipa kodi na wataalam wa ndani. Kwa hiyo, sisi lazima tutembee kifua mbele. Pamoja na yale mambo mengine yote katika sekta zote ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akiyasimamia na kuyatekeleza kikamilifu, lakini kwenye eneo hili la haki na usawa kwa Watanzania wote amekuwa akilifanya kwa kiwango cha juu cha kupigiwa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenye eneo la urekebu, kwa kuwa sasa juzuu zipo, ni muhimu sana tukapata *soft copy* ama nakala tete hasa kwa sisi Wabunge watunga sheria, lakini na kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili tuendelee kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Watakaoanza kuchangia jioni ni Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, Mheshimiwa Asha Hussein Saleh, Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja na Mheshimiwa Happiness Daniel Ngwando na orodha itaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Juma Zuberi Homera, Waziri wa Katiba na Sheria, ambao ni Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi na Wakuu

wa Vitengo kutoka Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 16 wa Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, hawa ni waliokuwa wagombea wa Udiwani kupitia CHAUMMA, Jimbo la Segerea. *(Makofi)*

Yupo pia diwani wa viti maalum kupitia CHAUMMA, Katibu na Mwenyekiti wa CHAUMMA, Jimbo la Segerea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninaomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.08 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

Mwenyekiti *(Mhe. Cecilia D. Paresso)* Alikalia Kiti

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya Bajeti ya Waziri wa Katiba na Sheria. Tunaanza na Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, ajiandae Mheshimiwa Asha Hussein Salehe, Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja ajiandae, Mheshimiwa Asha Hussein Saleh. Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja.

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia Wizara hii ya Katiba na Sheria. Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sisi sote hapa kwa uzima na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninapenda kuipongeza Wizara, kiukweli inafanya kazi nzuri sana. Tumesikiliza taarifa yake hata taarifa ya Kamati pia inafanya kazi nzuri sana. Mfano mzuri ninampongeza Waziri kwa kuanzisha siku maalum ya sema na Mheshimiwa Waziri; kwa hiyo, ile ni nafasi ya pekee ambayo wananchi wanaitumia kwa ajili ya kueleza kero zao zinazohusiana na sheria. Kwa hiyo, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka huduma ya uwakili kwa makundi maalum ikiwemo watu wenye ulemavu. Kwa kweli watu hawa, watu maalum, mfano wenye ulemavu unakuta hawana pesa ya kumlipa wakili au unakuta mwananchi wa kawaida hana uwezo wa kumlipa wakili, lakini Wizara imetoa hiyo huduma bure kwa haya makundi. Kwa hiyo, ninaipongeza sana Wizara sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pamoja na pongezi hizo kuna ambao wamesema kwamba Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, Fungu la 101 kwamba taarifa inaonyesha walitafsiri sheria mbalimbali kutoka lugha ya Kiingereza kuja ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sijasikia kwamba walitafsiri lugha ya watu wenye ulemavu, mfano, nukta nundu kwa wasioona kwa sababu wako wanasheria wengi sana wasioona, nadhani tunashuhudia kwamba wako mawakili pia wasioona. Sasa tusipotafsiri lugha hii kwenye nukta nundu kwa kujali haya makundi inaweza ikawa siyo ujumuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nina imani kwa kupitia hii ninadhani wanaweza wakaboresha zaidi katika hilo kama hizo nukta nundu hazipo. Pia katika hili nina imani niko sehemu sahihi kulizungumzia, Tanzania iliridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu iliridhia mwaka 2009 na ilipaswa ku-*submit* ripoti ile *initial report* kwa sababu na sisi

Tanzania ni wanachama. Kwa hiyo, ile *initial report* ilitakiwa ikabidhiwe baada ya miaka miwili na baada ya hapo inatakiwa ku-*submit progress report* kila baada ya miaka minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi naona *process* haifiki mwisho. Kwa lugha nyingine hata ukiangalia kwenye ile *link* hakuna ripoti ya Tanzania kuhusiana na masuala ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo pia yako mambo mengi mno ambayo nchi kama nchi imefanya kwa watu wenye ulemavu. Sifikirii kwamba hakuna kabisa, hapana! Maendeleo ni hatua, huwezi ukafananisha watu wenye ulemavu wa sasa hivi na wa miaka ile 2000 au miaka ya nyuma, kuna maendeleo hasa ukizingatia kwa Mheshimiwa Rais huyu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, amefanya mambo mengi sana; ukiangalia kwenye sekta ya elimu, ukiangalia kwenye afya, lakini bado kwenye uwekezaji kwenye dira tumejumuishwa mambo mengi sana matamu mazuri ya kuripoti kama nchi kwa masuala ya watu wenye ulemavu. Mpaka sasa tunaonekana hii Nchi ya Tanzania haifanyi chochote kuhusiana na mambo ya watu wenye ulemavu, lakini si kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana tuangalie namna ya kuripoti, kwa sababu tunavyozungumza sasa hivi hiyo *USRPD* ilitakiwa turipoti taarifa nne ukijumisha na ile *initial report* na tunakoelekea sasa hivi *USRPD* hiyo imeshaboreshwa tuko kwenye *ADP* ambayo na yenyewe tunatarajia Serikali iweze kuridhia kwa ajili ya kutekeleza mambo ya watu wenye ulemavu kwa muktadha wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ile *USRPD* ilikuwa kwa Kimataifa haiendani na mazingira ya Tanzania au ya Afrika. Kwa hiyo, wamekaa wameona hapana tutengeneze hii mkataba mwingine ambao ni itifaki *ADP* kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwa muktadha wa mazingira yetu kama Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Serikali pale inapokwama sijui inakwamia wapi kwa nini isiripoti mambo mazuri mazuri, matamu ya watu wenye ulemavu na sisi tunajivunia na

siyo tu sisi Serikali hata wadau wanazitumia hizi ripoti, wadau *NGOs, CBOs* na wadau wengi wanaojishughulisha na masuala ya watu wenye ulemavu, wanatamani nchi kama nchi itoe ripoti ambayo na wao itawasaidia katika mambo yao na *activity* zao za kuwaendeleza watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo pia kuna Tume ya Kurekebisha Sheria, Marekebisho ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na.9 ya 2010 iko haiendani na mazingira ya sasa hivi: mazingira ya sasa hivi mfano kama sasa hivi yako ujasiriamali, wako TEHAMA yaani mambo mengi ambayo yameendelea kwenye ile sheria na ile sheria tunahitaji iboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema kwamba wamerekebisha sheria mbalimbali; tulikuwa tunaomba pia kama haipo Sheria ya Watu Wenye Ulemavu na ni kweli haipo ninaomba pia iweze kurekebishwa. Tunaomba Wizara watusaidie tuweze kurekebisha ili mambo yetu na sisi yaende vizuri yaendane na kasi ambayo ipo ya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo pia tunaishukuru Tume, ukisoma Ibara ya 12, 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; inasema hakuna aliye juu ya sheria. Kwa hiyo, hata hili suala linaenda moja kwa moja kwa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wenye ulemavu siyo kwamba hatutendi makosa, wapo wanaotenda makosa na wanaadhibiwa kwa sababu hakuna aliye juu ya sheria, yapo magereza je, yale magereza ni rafiki kwa watu wenye ulemavu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wawaangalie, lakini pia kuna sheria ambazo zipo zinafanyika kule magereza; ukiangalia mimi ninatumia vifaa saidizi: vifaa saidizi ni chuma na ukiangalia sheria za kule zinaweza zikanizuia nisiingie na gongo au kifasaidizi changu. Matokeo yake mwisho wa siku inakuwa inatweza utu wa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeongea kwa mjumuisho katika hilo suala na nina imani Serikali yetu ni sikivu,

nina imani Wizara wanafanya kazi vizuri sana, nina imani kabisa kwa sababu kama alikuwa hamjui basi wanajua kwa ajili ya kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kupongeza sana Wizara kwa mambo makubwa ambayo wanaendelea kuyafanya kama Wizara sisi watu wenye ulemavu tunawapongeza sana, tuna imani na wao, tuna imani na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amewapa hii kazi wasaidie katika kazi hii ya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani mambo yetu ya watu wenye ulemavu hayatakwama badala yake yatasonga mbele hatua kwa hatua, maendeleo ni hatua. Tuna imani sasa hivi na tunakoelekea tulikotoka ni tofauti na kila kitu; sheria ndiyo msingi wa kila kitu. Kwa hiyo, tusipoangalia sheria tukaziweka vizuri na sisi watu wenye ulemavu tutakuwa hatujajumuishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani kabisa sheria zikikaa vizuri, sheria zikieleza vizuri watushirikishe pale ambapo wanaona hapa tunahitaji mawazo mengine, sisi tupo ambao ni wataalam, tumebobea na masuala haya ya watu wenye ulemavu kama Waheshimiwa Wabunge tutasongesha mbele mambo ya watu wenye ulemavu hasa katika sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante kwa mchango wako.

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ninamwita Mheshimiwa Happiness Daniel Ngwando na Mheshimiwa Bahati Kenneth Ndingo ajiandae.

**MHE. HAPPINESS D. NGWANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nami nimshukuru Mungu kwa afya aliyonijalia jioni ya leo. Nimshukuru sana pia Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutupambania wanawake katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitakuwa na mambo machache tu kuhusu sheria, nimesimama hapa kwa ajili ya wanawake wa Mkoa wa Ruvuma kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022, ni wanawake 953,000 ambao wako huko na wanatamani kuona nini juu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya leo nitakuwa kwenye mambo mawili au matatu. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kwa kazi nzuri anayoifanya hasa ile ya kusema na Waziri moja kwa moja, tunashukuru sana wakati akiwa anatatua kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana pia Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na kumpongeza kwa kazi anayofanya hasa ile kazi ya Mama Samia *Legal Aids* ambayo inatufikia hata kwenye mkoa wetu na watu wetu wanawake wanaendelea kupata haki zao, wanaendelea kusikilizwa kero mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina sehemu mbili au tatu. Niko kwenye suala la sheria ya mwanamke au binti upande wa ndoa. Sehemu ya kwanza ni ile ambayo inamtaka mtoto wa kike mwenye miaka 14, ndiyo yeye anatakiwa kuolewa kwa mujibu wa mzazi, lakini mtoto wa kiume wa miaka 18 yeye ndiye atakuwa akifikisha miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoona sasa hivi elimu msingi inaanzia awali mpaka kidato cha nne, mtoto huyu mwenye miaka 14 sheria hii ikiendelea kubaki ikikaa *silence* haieleweki vizuri, mtoto huyu hatapata haki ya kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mtoto mwenye miaka 14 bado katika uhalisia kwetu ni mtoto mdogo sana. Hapa nawaona wanangu wa darasa la saba sasa hivi wanapata mimba huko nyumbani leba akiingia mama unaanza kuchanganyikiwa nje. Si sahihi na tunaomba sana sheria hii isiwe na kigugumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa wenye miaka 14 tunaomba waingizwe kwenye miaka 18 kama watoto wa kiume kwa kuwa hata Katiba yetu inakataza ubaguzi kati ya mtoto wa kike na mtoto wa kiume. Sheria hii isiwe na kigugumizi tunaomba sana kama mwakilishi wa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Sheria za Ndoa yanasemwa mengi na wenye sheria zetu huko na wataalam walioziandika sheria hizi. Kiuhalisia sheria hizi zimepitwa na wakati ukilinganisha na mfumo wa mwanamke sasa hivi ulivyo. Mwanamke sasa hivi ndiyo mchumi kwenye nyumba zetu na familia zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru wametuelimisha sana na somo limeeleweka, wanawake sasa hivi nyumbani wanamiliki pesa, wanamiliki kila kitu ambacho mwanaume anaweza kumiliki. Sheria bado inamtaka mwanamke, huyu hata hasa pale kwenye mirathi unakuta anaambiwa mwanaume akifariki yeye anapata moja ya tatu anagawiwa kidogo, lakini haitoshi mama huyu huyu akitokea anafariki, katika baadhi ya sehemu, anatolewa kwenye nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapata meseji nyingi kama wawakilishi na hapa simwongelei mwanamke msomi, mwanamke mwenye *lace wig*. Mwanamke ninayemwongelea ni mwanamke wa kijijini, Mkoa wa Ruvuma kule ambaye haijui sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba uelewa kwenye hili; sheria inasemaje mwanamke huyu anapofiwa, kwa nini nyumba yake anayoishi na mume wake wa ujana iwe ndani ya mirathi? Kwa nini nimekaa na mume wangu ujana wote leo unaniambia ninatakiwa nitoke kwa sababu amefariki ile nyumba igawiwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi baba alienda sehemu kwa starehe zake akifika huko kule kuna watoto, sheria inasema mtoto si haramu baba ndiyo haramu, itabidi arudi huku kwa bibi mkubwa akachukue mali ambazo alichuma mama huyu na mume wake.  Mume aliyemvumilia miaka 40 mpaka 50, anarudi saa nane usiku, kichwa cha nyumba kinarudi kimeyumba, mama

amevumilia, ameishi vizuri, ametunza watoto, analima, anaenda kulima mikorosho yake, amechangia nyumbani vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo anaambiwa yeye moja ya tatu tu, lakini watoto wote wenye jina la baba watapata mali hiyo. Hata hivyo, mali ya kule inaelezwa ni zawadi hadi ithibitike. Kwa nini mali ya baba huyu haijathibitika kule lakini watoto wamethibitishwa? Ni kitu gani kimethibitisha kuwa wale ni watoto wake ili hali hawakuthibitisha kama zile mali pia ni za mume wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kama ni hivyo sheria iseme mali ya huku na kule zirudi sehemu moja tugawane pamoja. Siyo shida; ila tugawane zote na tusiwe na kigugumizi kusema eti imekuwaje kwa sababu ile ina majina yake hakuna aliyeona hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtueleweshe hatuelewi tunagombana, tunapigana wanawake tunakuwa *psychiatric* tunatembea tunaongea peke yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mama unamsalimia mama shikamoo anakwambia ona nimeachika talaka hii hapa, ameshapoteza akili. Mwanamke ni upendo kwenye jamii, leo Sheria ya Ndoa hii hii wanasema tumebadilisha na maneno yao, sheria ipo wazi, wanasema sheria iko wazi, wazi wapi? Mbona watu wetu hawaijui? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba uelewa iende huko kwenye vijiji. Wanasema sasa hivi kila mtu akiwa mwanaume na mwanamke wanachangiana wanaleta kitu pamoja; wewe unaonyesha ulichofanya na ulichochuma na mwenzako anaonyesha alichochuma, lakini unatakiwa uwe na ushahidi hata miamala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mahusiano kuna wakati wa kuangalia na kutunza miamala? Muda huo mpo lele; miamala hii unaitunzaje? Tumefikia sehemu tunavyojenga nyumba nyumbani, kwanza mila za kiafrika mwanamke huwa ham-*demote*

mwanaume, unacheza kikoba, unajinunulia mwenyewe marumaru unaweka kwenye nyumba.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante.

**MHE. HAPPINESS D. NGWANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, unapoweka unamwambia fundi weka vizuri mume wangu amenituma. Kwa hiyo, tunaomba sheria hii imepinda...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda.

**MHE. HAPPINESS D. NGWANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja na *wind up* moja tu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. HAPPINESS D. NGWANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nyumba ya mrithi isiwekwe kwenye mirathi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Bahati Kenneth Ndingo, wajiandae Mheshimiwa Nasoro Rashid Nasoro na Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nami niungane na wenzangu kuipongeza Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri Dkt. Juma Zuberi Homera, lakini na msaidizi wake Mheshimiwa Zainab Katimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kaka yetu Mheshimiwa Hamza Johari kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Nianze kwa kuipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kilikuwa kilio kikubwa cha Waheshimiwa Wabunge kwa Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa sasa Wizara hivi karibuni watakwenda kuzindua mpango wa kuanza kutumia

sheria zetu kwa lugha ya Kiswahili. Hiki kilikuwa ni kilio cha Wabunge wengi kuona tafsiri ya sheria hizi kwa lugha ambayo wananchi wengi wataelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna furahi kuona hatua kubwa ambayo imepigwa na itawasaidia wananchi wetu wengi kutafsiri vizuri sheria na itawasaidia katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, tunaishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu vilevile kuishukuru Serikali kwa *program* mbalimbali zilizopo chini ya Wizara hii ikiwepo hiyo ya Samia *Legal Aids* ambayo imewafikia wananchi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri hii kampeni iendelee na iwafikie na wananchi huko ndani vijijini kabisa ili waweze kupata msaada wa kisheria. Hata ile kampeni yako ya 'Ongea na Waziri' kwa kweli watu wanaifurahia sana. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri ikiwezekana aongeze muda kabisa ili wananchi wengi waweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri wa mambo machache kabisa kwenye Wizara hii. Tunatambua kama Taifa sasa hivi tunakwenda kwenye utekelezaji wa Dira ya 2050 na kiukweli katika Dira ile ili kuweza kutekelezeka tunaambiwa 70% ya mafanikio ya Dira yetu ile yatategemea sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, tumekuwa na sheria nyingi ambazo zinalalamikiwa na sekta binafsi. Nichukue nafasi hii kumwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini vilevile na Tume yetu ya Kurekebisha Sheria, tunatarajia Bunge hili tuone sheria nyingi zikija Bungeni kwa ajili ya marekebisho. Sheria za uwekezaji bado zinapigiwa kelele, milolongo ni mirefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo vilevile sheria za fidia. Leo hii mwananchi akipigiwa fidia, Serikali inapotaka kutwaa (kuchukua) maeneo kwa wananchi, mwananchi akishalipwa fidia hata robo ya mali alizorudisha Serikalini hawezi kwenda kununua. Hebu tupate sheria ambazo zinaendana na wakati wa bei halisi zilizopo,

lakini tuendane na wakati kama ilivyo dira yetu, tunasema tunakwenda kwenye uchumi jumuishi, hatuwezi kuwa na sheria ambazo bado zinawakandamiza wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, acha alama kaka yangu Hamza kwa kutuleta sheria nyingi ambazo zitabadilika kuendana na wakati. Tunahitaji kuona Bunge hili likileta sheria za kuwalinda wafugaji. Wapo wengine ambao kweli wanafanya makusudi kuingia huko hifadhini, wapo wale ambao ng'ombe wanaingia kwa bahati mbaya, leo wanaenda kutaifishwa ng'ombe wao. Kila ng'ombe mmoja shilingi 100,000, hii ni gharama kubwa sana. Tuwaombe wawasaidie wananchi hawa tusiendelee kuwakandamiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana pia kabisa na hoja ya Kamati ya Bajeti kwamba Mabaraza ya Ardhi yasiwe yanasikiliza kesi za ardhi. Kumekuwa kuna urasimu mkubwa, tunaomba mashauri yote ya ardhi yarudi kwenye Mahakama na haya mabaraza yasiendelee kwa sababu kuna malalamiko mengi ambayo yanawarudisha nyuma wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, niombe sana. ninasisitiza kwa Mwanasheria Mkuu wetu wa Serikali na Tume ya Kurekebisha sheria, niwaombe sana tunatarajia tupate mabadiliko mengi ya sheria ili kuendana na utekelezaji wa Dira ya 2050. Tunafahamu kwamba msingi ukiwekwa vizuri wa hii Dira na Dira hii wameibeba kwa sababu mambo mengi, vikwazo vingi vya kisheria vinatakiwa virekebishwe ili twende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunatarajia tupate sheria nyingi na kama kuna mambo ambayo ni ya kisera hayajakaa vizuri, basi nayo yarekebishwe ili tuweze kupata sheria bora ambazo zitatupelekea msingi imara wa kutekeleza Dira ya Maendeleo 2050. Tusipofanya hivyo tutabaki kuwa na mipango mizuri aliyoiandaa Profesa Kitila Mkumbo na wenzake itabakia kwenye karatasi, lakini utekelezaji wake hautowezekana. Niombe sheria nyingi zinazolalamikiwa ziletwe Bungeni tuzirekebishe tuweke msingi mzuri wa kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Nassoro Rashid Nassoro na Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule ajiandae. Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule; Mheshimiwa Yohana Stephen Msita na Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka wajiandae.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi hii ya kufika mahali hapa na pia ninaomba niweze kuipongeza sana Wizara hii ya Katiba na Sheria kwa kazi kubwa ambayo wanafanya. Ni chombo ambacho tunakitegema Watanzania wote cha kutunza haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Juma na pia nimpongeze Naibu Waziri mwanangu Zainab kwa kazi kubwa anazofanya. Ninampongeza Katibu Mkuu; ninawapongeza watendaji wote wa vitengo vyote vya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, tulifanikiwa kutembelea hata miradi ambayo wanaifanya, ni kazi nzuri sana ambayo imefanyika. Hivyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea sana, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli ameongoza nchi hii kwa kufuata Katiba na sheria, ndiyo maana tuna hii amani na utulivu. Si hivyo tu, ameiwezesha Wizara hii kufanya kazi yake kwa kuruhusu hela za kutosha kwenda kwenye Wizara hii. Kongole nyingi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ya kwamba chombo hiki sasa ni chombo ambacho sisi Watanzania wote tunakitegemea kwa ajili ya haki hasa tunapoongelea habari ya Mahakama.

Hivyo, tuna matarajio makubwa, Watanzania wana matarajio makubwa ndiyo maana Wabunge hapo wakisimama wanasema juu ya sheria mbalimbali ambazo zinabidi zibadilike ili ziweze kwenda sawa na wakati huu tulionao. Ninaamini kwamba Waziri Juma atakuwa anasikia jambo hili na atakwenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Wizara hii ya Katiba na Sheria imefanya jambo zuri sana hasa ile Kampeni ya *Mama Samia Legal Aid* ambayo imesaidia Watanzania wengi. Tumeona wamewafikia karibu Watanzania milioni 7.4, lakini wanaume wakiwa milioni 3.6 na wanawake wakiwa milioni 3.8. Ina maana Watanzania wengi wamenufaika na hii kampeni. Niombe tu kwamba iendelee, imekuwa faraja kubwa. Watu walikuwa na matatizo, lakini hawana fedha za kulipia mambo ya sheria. Sasa tuna huduma ya Miswada ya Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu na sisi UWT tuna Kamati ambayo pia ina wanasheria wabobezi ambao pia wanasaidia wanawake katika mambo haya ya msaada wa kisheria. Tume-*copy* na ku-*paste,* lakini inasaidia. Kwa hiyo, moja kwa moja tunaunga mkono jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo labda inabidi sasa tuweze kuona ambayo yanaweza yakakinzana kidogo na huu msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, mambo ya rushwa bado yapo ambayo yanaweza yakawa yanasumbua katika suala hili nayo tuyaangalie tuweze kudhibiti jinsi tunavyoweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu kuna gharama zingine ambazo mtu ambaye amepewa msaada wa kisheria, gharama kama za usafiri na *accommodation*. Yaani gharama nyingine ambazo zinaweza zikawa mzigo kwa mtu japokuwa amepewa msaada wa kisheria, lakini bado gharama zingine ambata zikawa kikwazo kwake. Wizara pia ipanue, inaweza kuwa hata na Mfuko tu maalum kwa ajili ya kuwasaidia hao watu ambao

wanawapatia msaada wa kisheria, lakini pia wapate na misaada mingine ya kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ucheleweshwaji wa kesi. Kesi zikiwa za muda mrefu sana, mtu anahangaika hata kama ana msaada, anahangaika hizo gharama, anasubiri kesi ni ya muda mrefu, inamaliza mwaka na inaanza mwaka mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema watu wanakata tamaa njiani kabla hawajapata hiyo haki yao, hata kama wana msaada wa kisheria. Hivyo, kesi ziwe zina muda mfupi, ziweze kumaliza kwa wakati ili huyu sasa aweze kufaidi huo msaada wa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mambo ya ubambikizwaji wa kesi. Kuna kesi zingine zinabambikizwa, watu wanalalamikia mambo kama haya. Hivyo basi, Wizara au Mahakama pia iweze kuona vitu kama hivyo. Yaani kweli unasikiliza, unasema kweli hivi huyu mtu anaweza akafanya hivi? Unatumia na vyanzo vingine, hata vyanzo vya kisaikolojia kwamba kitu hiki ninafikiri huyu mtu…; kwa hiyo, yapo mazingira ambayo yanaweza kuonesha kuwa huyu mtu amebambikizwa kesi ili pia tuweze kuwa sasa na huduma nzuri ya msaada wa kisheria, lakini haya mambo mengine manne ni muhimu pia kuyaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninaomba kuchangia ni mambo ya *RITA*. Kwa kweli *RITA* ni chombo muhimu ambacho kinatupa sisi vyeti vya kuzaliwa na vifo, lakini kuna shida kwenye *RITA*. *RITA* inabidi sasa hivi nayo ijirekebishe ili iweze kuwasaidia watu. Wanafunzi, mtu amefiwa na wazazi wote anaambiwa ukalete cheti cha kifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mrefu anapokwenda kutumia kutafuta cheti cha kifo cha wazazi wake, kwanza ana machungu yeye kuwa yatima, *RITA* iwe na kitu angalu kirafiki angalau cha kuweza kutoa huduma haraka kwa watu ambao wana maumivu. Pamoja na wajane, amefiwa na mume huku anaenda kutafuta mambo ya cheti, pia ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu *RITA* inabidi pia ibadilishe mambo. Zaidi ya kutumia zile kanuni walizonazo *RITA* iwaangalie...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, ajiandae Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na mimi kunipatia fursa hii ya kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia afya na uzima. Ninaomba kipekee sana niendelee kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Mheshimiwa Rais ana moyo wa uzalendo, amejitoa kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania. Nimpongeze pia Makamu wa Rais kwa kazi ambazo anaendelea kuzifanya, vilevile, Waziri wetu Mkuu kwa kazi kubwa ambazo wanaendelea kuzifanya nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana ninaomba nimpongeze Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Juma Homera pamoja na Naibu wake Zainab Katimba. Bila kumsahau Katibu Mkuu. Niseme tu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Hakika watu hawa wanafanya kazi nzuri sana. Watu wa Wizara ya Katiba na Sheria wanapambana kweli kweli. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu sasa nianze kwanza kwa kutambua kauli mbiu ya Wizara hii ambayo inasema: "Haki, usawa na utawala wa sheria kwa watu wote." Huu ndiyo msingi. Yako maandiko yanasema: "Kama misingi ikaharibika mwenye haki atafanya nini?" Tunapozungumzia Tanzania maana yake tunazungumzia Wizara hii ambayo ni Wizara mama ambao ndiyo msingi wa nchi. Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo inabeba mambo yote, ndiyo inayoifanya Tanzania inaonekana katika sura hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uniruhusu nianze kuzungumzia msaada wa kisheria. Ninapozungumza msaada wa kisheria hapa ninazungumzia Mama Samia *Legal Aid Campaign* ambayo kwa kweli imefanya kazi kubwa sana. Niendelee kuwapongeza kwa kuendelea kufanya jambo hili zuri kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninapitia takwimu za huu msaada wa kisheria wa Mama Samia *Legal Aid Campaign*. Takribani wananchi 3,000,000 hadi kufikia Juni 2025 wamefikiwa na msaada huu wa kisheria, hilo ni jambo kubwa sana. Kazi kubwa imefanyika katika kutatua migogoro ya ardhi, kutatua migogoro ya mirathi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo si la kupuuzwa. Watu 3,000,000 ni wengi sana, lakini niendelee kutoa ushauri wangu kwa Wizara kwamba jambo hili liwe endelevu. Limewasaidia Watanzania wenzetu ambao wamekutana na changamoto mbalimbali wakati mwingine wao kushindwa kuelewana. Chombo hiki kikifika kinafanya utatuzi mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada mingi ya kisheria imeendelea kuwepo ambayo kwa kweli takribani Watanzania milioni 7.4 wameendelea kusaidiwa katika kutatua changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu mambo machache ambayo katika kutembelea miradi ambayo inasimamiwa na Wizara hii tumeona kuna mambo fulani ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho kidogo au kuongeza kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema pale awali Wizara hii ndiyo msingi na Kamati katika kutembelea, tumetembelea miradi ikiwemo ya Jengo la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Singida. Jengo hili ni jengo zuri, lakini ujenzi umekuwa wa kusuasua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niiombe Serikali kama kweli tunataka kuelekea kwenye Dira ya 2050 kama ambavyo inasema katika ukurasa wa 30 kwamba Taifa la kidemokrasia linalozingatia utawala wa sheria, haki za binadamu na upatikanaji wa haki jamii lazima tuhakikishe tunaboresha miundombinu kwa kupeleka fedha ili miundombinu hii iweze kukamilika na wananchi wetu waweze kupatiwa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitembelea pia Kituo cha Jumuishi cha Taasisi za Kisheria Mwanza. Hapa tumekuta fedha nyingi zimetumika, lakini jengo halijakamilika, bado linasuasua sana. Sasa kusuasua huku maana yake tunawachelewesha Watanzania kupatiwa haki zao na kupata huduma kwa ukaribu. Niiombe sana Serikali iendelee kukimbiza na kupeleka fedha pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuligundua pale kuna changamoto kwa wajenzi wa Suma JKT. Hawa nao tumeona wanasuasua wameshapokea fedha karibu shilingi bilioni 2.9% lakini kwa kweli maendeleo ya kazi yalikuwa bado karibu 74%. Sasa hii ninaona ni jambo ambalo litatuchelewesha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambapo kwa kweli hapa ninadhani tunahitaji kuongeza kasi sana na Serikali ije na mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba tunafikia yale matarajio. Nimeona kwamba mashauri yalipokelewa karibu 10,398, lakini mpaka kufikia Februari, 2026 ni mashauri 604 tu ndiyo yaliyokamilika, ambayo ni sawasawa na 5.8%. Mashauri mengine bado yapo kwenye mchakato. Ninadhani Serikali ije na mpango mahususi wa kuhakikisha inaongeza kasi katika eneo hili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Muda wako umekwisha.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, Mheshimiwa Esther Edwin Malleko na Mheshimiwa Mariam Ussi Yahya wajiandae.

**MHE. KASSIMU A. MBARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani sana. Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia sote kuwemo humu tena na kuendelea kulitumikia Taifa katika hili Bunge Tukufu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii na nafasi hii ya kuweza kuchangia katika suala zima la msingi linalohusiana na masuala ya Wizara ya Katiba na Sheria katika siku hii ya leo. Pia, nitumie fursa hii kumpongeza kwa kiwango cha hali ya juu Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu wake, wasaidizi wao wote pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi na sote tunafahamu na tunaona namna wanavyoratibu mambo na namna yanavyokwenda hususani kuhusiana na kliniki mbalimbali za misaada ya kisheria hususani ile Samia *Legal Aid* ambayo inafanya kazi vizuri sana kwa kiwango cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijikite katika mchango wa msingi kabisa na umuhimu kwenye masuala ya kisheria. Jambo la msingi kubwa zaidi ni kwamba kuna madai mengi sana ambayo yanakuwepo Mahakamani na yanachelewa sana kupatiwa ufumbuzi kwa muda mrefu sana kiasi ambacho yanaathiri miradi mingi sana ya maendeleo katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, imefika mahali wakati mwingine kama imekuwa sehemu ya Mahakama ya watu

kufanya kitu kitaalam, tunakiita *technical delaying,* yaani kuchelewesha mambo kwa ajili ya faida binafsi au kwa ajili ya maslahi yao binafsi. Nitatoa mfano katika jambo ambalo limetokea katika Jimbo letu la Tanga Mjini. Hapa nitafanya *reference* kidogo ya *land case* namba tatu ya mwaka 2021 ndani ya Jimbo la Tanga Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale pana hospitali ambayo ni binafsi, ilianza kuwa *dispensary* ikaja mpaka ikafikia hatua ya kuwa hospitali. Inafanya kazi kubwa sana na kusaidia watu wa Tanga, lakini ukatokea mgogoro baina ya wamiliki pamoja na watu ambao ni wawekezaji katika lile eneo. Kesi ile imekwenda mpaka leo ni mwaka 2026 bado haijatoka Mahakamani na shauri lile halijakwisha, imekuwa ikiisha ikikatiwa rufaa, imebakia katika hali hiyo. Nini kilichotokea sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kwa mujibu wa Kanuni zetu kama kuna kesi iko Mahakamani inaendelea, haturuhusiwi kuijadili humu ndani.

**MHE. KASSIMU A. MBARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunifahamisha na kunielimisha kwa hilo. Kutokana na hilo naendelea, nukta nyingine ya msingi ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara ya Sheria na Katiba kwa kuonesha na kudadavua vizuri sana katika randama yao, hususan, kuonesha suala zima la elimu ya kisheria. Nimeona pale kwamba, kuna mchakato mzima wa kuingiza masuala ya elimu ya kisheria *VETA*, hali kadhalika mchakato mzima wa kuingiza kwenye mtaala elimu ya kisheria, hususan kwenye Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo Wizara inayachopeka kule ni ya msingi sana kwa sababu, migogoro yote tunayoiona kwenye jamii inatokana na Watanzania walio wengi sana katika masuala mbalimbali kutokufahamu vizuri sheria za nchi hii, ambalo ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili ninawapongeza sana, wamefanya jambo kubwa sana la kimageuzi na kimabadiliko na liende katika vyuo vyote nchini Tanzania. Kila kijana anayehitimu walau ngazi ya diploma aelewe sheria za msingi za nchi hii, aelewe Katiba ya Nchi yetu, aelewe sheria za mambo ya ardhi na umiliki wa ardhi. Itasaidia sana kutatua migogoro mingi hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo kuna suala la Katiba Mpya. Ninaipongeza sana Wizara ya Katiba na Sheria, jambo hili limekuwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambapo tumelinadi sana Wabunge wote Mwaka 2025 mpaka 2030 katika kipindi hiki. Nimeona tayari mchakato na utaratibu umeanza kupitia Wizara yetu ya Katiba na Sheria kwamba, jambo hili tayari limeshawekwa Mezani na mchakato umeanza kwa kuanza kushirikisha wadau na kuandaliwa taratibu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ninapongeza na ni jambo kubwa sana kwa sababu, mabadiliko ya Katiba ni jambo la kitaifa na linatuhusu sisi sote. Wakati umekwenda sana, muda umesogea, mazingira yamebadilika, jamii tuliyonayo ni changamani sana, tunahitaji zaidi kuliangalia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza walioliweka kwenye ilani, hali kadhalika ninaipongeza Wizara ya Sheria na Katiba, kwa mara nyingine tena, kuliona hili na kuanza kuchukua hatua mapema na kufanyia kazi utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninachangia kwa kusema, Samia *Legal Aid*, msaada ule wa kisheria ni jambo kubwa na adhimu sana, linawasaidia watu wengi sana ndani ya Taifa hili. Tumeona kliniki ile ikifanyika, sasa ninashauri msaada ule, wale mawakili 171 wa kujitegemea ambao Wizara ya Katiba na Sheria inawatumia kati ya mawakili wengi wa Serikali walionao, sasa uende magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kuna watuhumiwa wengi, wako mahabusu, wasikilizwe na wayasimamie mashauri yao mahakamani, wenye hatia wapate hatia, ambao hawana hatia

watoke waungane na ndugu zao. Hii itasaidia sana iwapo Samia *Legal Aid* itafika magerezani na kusikiliza wafungwa mbalimbali ambao hawana msaada wa kisheria kuweza kuwasaidia katika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya ninasema ninashukuru sana kwa siku ya leo nami kuweka mchango wangu kwenye randama hii ya Wizara, hoja hii ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Esther Edwin Malleko. Ajiandae Mheshimiwa Maryam Ussi Yahya.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. Ninaanza kwa kuipongeza Serikali chini ya Rais wetu makini kabisa, Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri na Naibu Waziri, ninampongeza pia, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda moja kwa moja kwenye kuchangia katika Mama Samia *Legal Aid Campaign*. Kipekee sana ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa maono makubwa ya kuanzisha na kutekeleza Mradi huu wa Msaada wa Kisheria unaojulikana kama Mama Samia *Legal Aid Campaign*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msaada huu wa kisheria umeleta mapinduzi makubwa sana katika upatikanaji wa haki nchini. Msaada huu umeweza kuleta haki karibu na wananchi, umeweza kupunguza migogoro iliyokuwa inatokana na masuala mbalimbali, ambayo yalikuwa hayawezi kupatiwa ufumbuzi, lakini pia, imeweza kuimarisha utawala wa sheria hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Kampeni ya Mama Samia *Legal Aid*, wameweza kuwafikia wananchi 7,462,387. Kipekee ninaipongeza sana Wizara, hawa ni watu wengi, wameweza kufikiwa kwa muda mchache kwa sababu, kazi hii imeanza Julai, 2025 mpaka leo Machi, 2026 wamewafikia watu hao, zaidi ya milioni saba. Tunaipongeza sana Wizara kwa kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mama Samia *Legal Aid Campaign* wameweza kupokea zaidi ya migogoro 5,209 ambapo migogoro 2,545 tayari imehitimishwa, kwamba, tayari imetatuliwa, imebaki migogoro 2,664 ambayo iko katika hatua mbalimbali kwenye vyombo vya maamuzi. Ninaipongeza sana Wizara kwa kazi hii kubwa iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika migogoro ambayo imetatuliwa na kampeni hii ya Mama Samia, 32% ni migogoro ya ardhi. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, asilimia kubwa ya migogoro ya ardhi inawatesa wananchi wetu kwa kiasi kikubwa sana, lakini ukiangalia migogoro hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na mfumo wa utatuzi wa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Wizara hii, ione ni namna gani inaweza kuhamisha Baraza la Ardhi lirudi Mahakamani, ili liweze kufanya kazi hii kwa umakini zaidi kwa sababu, tunaona mpaka sasa kazi haiwezi kufanyika kwa sababu ya ukwamishaji unaotokana na mabaraza haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuipongeza sana Wizara hii, kupitia kampeni ya Mama Samia *Legal Aid* wameweza kufikia madai ya matunzo ya watoto kwa 14% katika migogoro waliyoipokea. Sisi wote ni mashahidi, kupitia migogoro ya ndoa watoto walikuwa wanakosa haki zao, lakini kupitia kampeni hii watoto sasa wanapata haki zao za msingi, wazazi wanajua wajibu wao na sisi tunaenda kujenga Taifa imara linalojali watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi kubwa sana kwa kazi hii iliyofanyika. Wamefikia 13% ya migogoro ya ndoa, ambayo ni changamoto kubwa sana kwa masuala ya ndoa ambayo yanaenda kupeleka matatizo mengi yanayoaenda kuleta

migogoro ya kifamilia. Wamefikia pia, kwenye mirathi kwa asilimia nane, ukatili wa kijinsia asilimia nne, masuala ya jinai asilimia tatu, ajira asilimia tatu na masuala mengine asilimia nane. Tunawapongeza sana kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipopongeza maono mazuri waliyokuja nayo Wizara hii. Kupitia ile kampeni ya 'Sema na Waziri' inaweza kuwafikia wananchi wengi, wanaweza kupiga simu na kueleza matatizo yao na baadhi ya matatizo yanatatuliwa wakati huo huo. Hii inaendelea kuongeza ufanisi katika Wizara yetu, ninapongeza sana ubunifu huo na tuendelee kuona namna gani tunaweza kufanya kazi hii kwa muda mwingi zaidi, ili migogoro mingi zaidi iweze kutatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida kubwa sana kupitia Mama Samia *Legal Aid Campaign,* wananchi wengi wanapata ushauri wa kisheria bure. Tukumbuke kwamba, kuna wale wananchi ambao hawakuwa na uwezo wa kwenda kuweka mawakili, walikuwa wanapoteza haki zao, lakini wengine walikuwa wanashindwa kulipa gharama hizo na mwisho wa siku wanapoteza haki zao. Kupitia kampeni hii wameweza kupatiwa msaada wa kisheria, zaidi migogoro imetatuliwa, maridhiano yamepatikana, watu wanaelewana na haki inatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke pia, Mama Samia *Legal Aid Campaign* imepunguza kwa kiasi kikubwa sana idadi ya kesi Mahakamani.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Muda wako umekwisha.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Maryam Ussi Yahya. Wajiandae Mheshimiwa Dkt. Lazaro Killiani Komba na Mheshimiwa Selina Henry Kingalame.

**MHE. MARYAM USSI YAHYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninachukua nafasi hii kushukuru kwa kunipa nafasi

ya kuongea, lakini pia, kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia kuwepo hapa katika siku hii ya leo. Hakika yeye kwa rehema zake ndiyo tupo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwa kuipongeza Wizara, kwanza kwa mafanikio yao makubwa kwenye Mama Samia *Legal Aid,* lakini kabla ya hapo ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Makatibu na watendaji wao wote. Kwa kupitia wao Wizara hii safari hii imeweza kupatiwa bajeti kubwa zaidi kulinganisha na bajeti za miaka iliyopita kwa sababu, imeonesha umahiri katika utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia ninagusia pia, asilimia kubwa ya watu 7,000,000 iliyofikiwa kwenye Mama Samia *Legal Aid*. Hiyo ni zaidi ya 10% ya *statistics* ya wananchi wote katika nchi yetu. Inamaanisha kwamba, *Legal Aid* imeingia mikoa mbalimbali katika nchi yetu na kutuletea tija katika mustakabali mzima wa kuwapatia wananchi haki katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote katika hii Mama Samia *Legal Aid* ninagusia vilevile 14% ambayo ilisemwa kwenye kuhakikisha inaondoa migogoro hasa kwa watoto. Wote tunatambua ya kwamba, watoto ndiyo waathirika wakubwa katika migogoro hasa ya ardhi, ya mirathi na ya ndoa. Kwa hiyo, ninategemea na ninaishauri Wizara katika kuhakikisha inatekeleza majukumu yake, basi iipe kipaumbele sekta ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa ipo kwenye maendeleo ya jamii, lakini tunaona jinsi familia zinavyoanguka kwenye migogoro ya ndoa na ya mirathi, ndivyo tunavyopata watoto wa mitaani. Watoto wao hawawezi kwenda kuomba sheria katika vyombo vya sheria, wanawategemea wazazi au wasamaria wema. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali katika eneo la utatuzi wa migogoro, basi sehemu ya watoto ipewe kipaumbele mwaka wa fedha ujao, tuje tuone asilimia hii imepanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo la utatuzi wa migogoro, katika ripoti ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri imeeleza ya kwamba, katika kipindi cha Julai, 2025 mpaka Machi, 2026

watoa huduma wa msaada wa kisheria 47 na wasaidizi wa kisheria 243 walisajiliwa, kama ongezeko la asilimia 6.2. Tunaelewa fika kwamba, katika nchi yetu Chuo cha Wanasheria cha *Law School of Tanganyika* kinatoa wahitimu wengi kila mwaka. Chuo kile kina *cohort* mbili kila mwaka ambayo inatoa wanafunzi zaidi ya mia na katika mwaka wanatoka mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sasa Wizara pamoja na kwamba, ina-*train* watu kufanya kazi katika huu Mradi wa Mama Samia *Legal Aid*, lakini pia, iangalie kwa makini wanasheria wale ambao wana-*graduate* wanakaa zaidi ya miaka na miaka mitaani hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ifikirie sasa katika miradi inavyochukua wafanyakazi kuwa-*train*, kuliko kupoteza fedha ku-*train* watu wengine ni bora wakawachukua wanasheria ambao wamemaliza, wana elimu ya juu na pia, wamefanya *Law School*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba niongelee suala zima la utatuzi wa migogoro, hasa kwenye masuala ya *pre-bargain*. Pamoja na kwamba, tumeisifia Wizara na ni haki yake, inafanya kazi yake vizuri, lakini bado katika maeneo ya utatuzi wa migogoro, hasa kwenye maeneo ya *pre-bargain,* bado tunaona eneo hili ufanisi wake unasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mhalifu yeyote ambaye amekubalika na mahakama kutoa *pre-bargain*, kuilipa fidia Serikali ni kwamba, zile fidia ni mapato ya Serikali ambayo yanaenda kuendeleza uchumi wetu wa nchi. Kuna maeneo mbalimbali hawa walipa fidia wamekubali kulipa fidia, lakini bado inatokea ukiritimba wa wao kucheleweshwa kutoa hizi fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pia, ninaiomba Wizara katika utendaji wao, basi wafikirie kuhakikisha wanaofanyiwa *pre-bargain,* hasa wale wafanyabiashara wakubwa, ambao wanatakiwa walipe fedha nyingi katika Serikali, wanalipa fedha hizo kwa muda mwafaka na siyo kucheleweshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Dkt. Lazaro; ana dharura, hataweza kuchangia. Sasa namwita Mheshimiwa Selina Henry Kingalame, wajiandae Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu.

**MHE. SELINA H. KINGALAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi, ili niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Katiba na Sheria. Kwa kuwa, ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima, afya na kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia, ni Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi Taifa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kunipendekeza, kuteua jina langu na hatimaye leo niko humu kwenye Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana vilevile Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa *UWT*, Taifa kwa kunipa kura nyingi za kishindo. Ninawaahidi ile imani waliyonikopesha, basi nitawalipa kazi na utu. Mwisho, ila siyo kwa umuhimu, ninaishukuru sana familia yangu kwa upendo na kwa kuniombea muda wote, Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nijielekeze kwenye kuchangia katika bajeti hii ya Katiba na Sheria. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini pia, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kaka yangu, Mheshimiwa Juma Homera, hongera sana kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ille programu ambayo wameianzisha, Wizara ya Katiba na Sheria, inayosema 'Ongea na Waziri', ambayo wananchi wanaongea moja kwa moja na Waziri wa Katiba na Sheria, wanapeleka malalamiko yao, hongera sana kwa programu hiyo. Pili, nampongeza Naibu Waziri wa Katiba na

Sheria, dada yangu, Mheshimiwa Zainab Katimba, hongera sana kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelekeza mchango wangu kwenye jambo moja tu, jambo hilo ni *Law School of Tanzania*. *Law School of Tanzania* ilianza mwaka 2007, ni ukweli usiofichika *Law School of Tanzania* ipo moja tu Dar es Salaam, lakini lengo kuu la kuanzisha *Law School of Tanzania* ni kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu wa sheria, ili waweze kuwa mawakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika sasa hivi vyuo vinavyotoa *Degree* ya Sheria ni vingi, lakini hata wahitimu ambao wanamaliza *Degree* ya Sheria ni wengi. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 wahitimu waliomaliza *Degree* ya Sheria karibu 4,373 walimaliza, lakini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pia, wanafunzi waliomaliza *Degree* ya Sheria walikuwa 5,008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishauri Serikali yangu, pamoja na Wizara hii, waone namna ya kuweza kuongeza *branches* za *Law School of Tanzania,* ili kupanua wigo wa kuanzisha matawi kwenye mikoa tofauti tofauti. Wanaweza wakaanza hata kwa kanda; wakaanza hata Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa mdogo mdogo, ili kuwatendea haki hawa wasomi wa sheria, ambao nina imani Serikali yangu sikivu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania italiangalia hili suala kwa jicho la tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaomba niwapongeze sana Wizara ya Katiba na *management* yote na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri. Nilimtaja Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, ajiandae Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme mwanzoni kabisa kwamba nimeisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa umakini mkubwa sana, *page* kwa *page* na nimevutiwa nayo sana. Baadhi ya mambo mahsusi ambayo Mheshimiwa Waziri ameyasema kwenye hotuba hii, ninaomba niyataje matatu: Moja, anasema Sekta ya Sheria ni mlinzi wa amani, utulivu na usalama wa nchi; Pili, anasema Sekta ya Sheria ni mlinzi wa uwekezaji nchini; na Tatu, anasema sheria siyo kikwazo bali ni daraja la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo huu wa hii Wizara unaonesha jinsi ambavyo hii Wizara wamejipanga kuwa sehemu ya kutekeleza Dira 2050. Mheshimiwa Waziri, Dkt. Juma Zuberi Homera, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii na Naibu wenu hongereni sana kwa kazi nzuri ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, baada ya kuwapongeza hivyo, ninaomba pia niwasemee kwa kifupi waajiri wangu toka Jimbo la Lupembe, wananchi wa Jimbo la Lupembe wanaishukuru sana Serikali kwa kupeleka Mahakama ya Mwanzo Tarafa ya Lupembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wananchi wangu wa Kata ya Mtwango, Kata ya Kichiwa, Ninga, Igongolo, Ikuna, wanaomba Mahakama ya Mwanzo pale Mtwango. Ninamwomba sana Waziri na ninajua Katibu Mkuu ananisikia, wananchi wa Kata hizi tano muhimu hawana Mahakama ya Mwanzo wanafuata mahakama Njombe mjini na Makambako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mahakama ya Mwanzo pale Mtwango ili tuweze kuendeleza ujenzi wa Mji wa Mtwango ambapo tayari kuna kituo cha afya na vitu vingine, tupate huduma ya haki ya sheria pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninataka nichangie kuhusu eneo la mfumo wa Mahakama nchini. Kwanza kabisa, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Masaju, kwa jinsi ambavyo amekuwa *positive* sana kwenye *reforms* za kisheria nchini, kama Wabunge tumekuwa

tukimfuatilia namna ambavyo ana kiu ya kuona mabadiliko na mfumo wa sheria ukiwa rafiki kwa wananchi wa Tanzania. Tunamuunga mkono aendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa karibuni tumemsikia akisema kwamba ni muhimu mashauri mahakamani yakaisha kwa muda mfupi. Pia, amekuwa akisisitiza umuhimu wa Mahakama kuzingatia matumizi ya tamaduni na mila zetu kama Watanzania. Kama Waafrika, tunamuunga mkono na kwa hili aendelee kuchapa kazi. Pia, Mahakama nzima, majaji na Mahakimu wafuate aina hii ya mtazamo kwenye Mahakama yetu ili kutekeleza dira ya mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kwenye mfumo wa Mahakama asubuhi imesemwa hapa na ninaunga mkono sana, kwamba Mabaraza ya Ardhi Nchini ni muhimu yakarudi kwenye mfumo rasmi wa mahakama yetu na sababu zipo kadhaa. Sababu ya kwanza, haya mabaraza yameshindwa kuleta tija iliyokusudiwa. Kwa sababu takwimu zinaonyesha 32% ni migogoro ya ardhi, maana yake dhumuni la haya mabaraza halijafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya yako mbali sana na wananchi, kwa mfano, Mkoa wa Njombe, tunalo Baraza moja la Ardhi Mkoa mzima. Wananchi wa kule Madeke, umbali wa kilomita zaidi ya 120 wanafuata Baraza la Ardhi na Nyumba Wilayani Njombe. Barabara za matope, wananchi wa Ludewa na Wanging'ombe wanafuata Baraza Njombe Mjini.  Kwa hiyo, yako mbali na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu Mabaraza haya pia yamelalamikiwa mara kadhaa kwa ajili ya kesi mbalimbali za wananchi kutofanyiwa kazi vizuri. Kubwa kuliko yote, ipo kanuni ya haki ya asili au tuseme *natural justice,* kwamba hapa nchini Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yako chini ya Wizara ya Ardhi, lakini Wizara ya Ardhi ndiyo wanaopima ardhi, ndiyo wanaotoa hati. Sasa, haiwezekani ndani ya hii Wizara tena wakasimamia haya mabaraza. Kwa misingi ya *rule against bias*, jambo hili haliwezekani! Kwa hiyo ni muhimu haya mabaraza yakarudi kwenye mfumo wa Mahakama ili tutoe haki kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninataka pia nishauri. Kwa kuwa, tunazo Mahakama za Mwanzo nyingi nchini, ambazo kule chini wako Mahakimu wenye weledi wa *degree,* lakini pia tumeweka sheria Mawakili wanaruhusiwa kwenda Mahakama za Mwanzo, ninashauri Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tuanze kuruhusu Mahakama za Mwanzo kusikiliza mashauri ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hizi Mahakama za Mwanzo ndiyo zipo karibu na wananchi na Mabaraza ya Ardhi ya Kata tumeshayaondolea mamlaka ya kuamua kesi za ardhi. Kwa hiyo, ni muhimu Mahakama za Mwanzo sasa zikaingia kwenye mfumo wa kusikiliza mashauri ya ardhi nchini ili kusudi mfumo huu uweze kwenda kwenye Mahakama ya Wilaya, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, niseme kidogo hapa kuhusu *Law School of Tanzania*. *Law School of Tanzania* kama ambavyo imesemwa na wengi, iliundwa maalum kuzalisha wasomi wa sheria nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2025 Desemba, *Law School* au tuseme mawakili walioingia kwenye mfumo wetu wa uwakili walikuwa 774. Katika mawakili 774, mawakili 388 hawajapitia kusoma *Law School* darasani. Wamepata uwakili kwa njia ya kuomba nje ya kwenda kusoma *Law School*. Tafsiri yake ni nini? Kama utaratibu huu ukiendelea, tunaenda kuua *Law School*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hii ni *alert* kwamba watu baada ya kuona *Law School* ni ngumu, wameamua kutanua goli waweze kufunga magoli kwa urahisi zaidi. Ninaomba Serikali ilete sheria Bungeni, tubadili hii sheria ili watu wakasome *Law School* tupate mawakili wenye viwango, wenye ubora watakaoweza kufaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa, ninataka niseme kidogo sana hapa kuhusu uhuru wa Mahakama. Hapa ninaongelea mahsusi, uhuru wa Mahakama juu ya kuisaidia

Mahakama iwe na uwezo wa kuamua mashauri bila kuwa na sheria ambazo zinailazimisha mahakama kutoa adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninarejea Sheria ya Makosa ya Kujamiiana. Sheria ambayo imelazimisha Mahakama za Tanzania kutoa adhabu kwa washtakiwa wanaotiwa hatiani, kumfunga mtu kifungo cha *minimum* miaka 30 kwenda juu. Maana yake nini? Hata kama Jaji au hakimu ataona kesi ingefaa kumpunguzia mfungwa adhabu, amefungwa mikono kwenye sheria. Ninaomba Serikali ifike wakati tutunge sheria kuisaidia Mahakama iwe huru kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwa sababu hii bajeti ni nzuri, ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Waziri wa Sera, Bunge na Uratibu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Naibu Waziri wajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na wale wote walionitangulia kumpongeza sana Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha hotuba nzuri sana ya bajeti. Hotuba ambayo imeeleza mafanikio ambayo yamepatikana, lakini inayoeleza pia mipango katika mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na wengine wote ambao wamemshukuru sana Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mambo makubwa ambayo ameyafanya katika sekta hii ya Katiba na Sheria katika muhula wa kwanza wa uongozi wake na sasa katika huu muhula wa pili wa uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kilosa, ninapenda nimshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini pia na Mahakama ya Tanzania kwa kutujengea Mahakama

mpya ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo kule Kilosa katika eneo la Kondoa, Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukija Kilosa pia kuna eneo la Kondoa. Mahakama ni nzuri sana na tunashukuru kwa kuzingatia maombi yetu ya kwamba mahakama ile ziwe mahakama mbili ndani ya mahakama moja yaani Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo. Ninaamini kabisa tutapata pia msukumo wa kukamilisha Mahakama ya Mwanzo kule Magubike kwa ajili ya zile Kata Nane za juu za upande wa Tarafa ya Mabole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama ili nimshukuru sana Mheshimiwa Nyamizi Mhoja, ambaye ametoa hoja nzuri sana kuhusu masuala yote yanayohusu watu wenye ulemavu ambayo yanaangukia katika Wizara yangu. Mchango wake ni mzuri, maoni yake ni mazuri na tutayazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kabisa kama alivyosema, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka 2006, tarehe 30 Machi, 2007 na tukauridhia mkataba huo tarehe 10 Novemba, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda tu kumwarifu kwamba toka tulipojiunga katika mkataba huo, tumehudhuria mikutano yote ya mwaka inayohusu utekelezaji wa mkataba huu na mwaka huu Mkutano huo wa 19 utafanyika *New York* Marekani, Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, tarehe 9-11 Juni. Tanzania itawakilishwa na katika mkutano huo tutatoa pia taarifa ya utekelezaji wa mkataba huu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mengi ya kueleza ambayo yamefanyika chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo yameimarisha haki ya watu wenye ulemavu kwamba ni raia wa Tanzania wenye haki sawa na Watanzania wengine wote kwa mujibu wa Katiba, lakini pia kwa mujibu wa sheria ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia kabisa kwamba sasa tunakamilisha uandaaji wa taarifa ya utekelezaji

wa mkataba huo na tutashukuru sana baada ya shughuli hizi za Bunge kuweza kuonana ili na yeye atupe mchango wake ili uwe sehemu ya taarifa ambayo tutaiwasilisha Umoja wa Mataifa mwezi Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ajiandae Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia neema ya uhai na leo tuko mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo anaiongoza Wizara ya Katiba na Sheria. Pia, ninamshukuru Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji Wakuu wote wa taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri ambayo tunaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza tu kwa ujumla kwa kuwa Wajumbe wengi ambao wamechangia, walikuwa wanazungumzia kwa uzito wake umuhimu wa kurekebisha sheria ili ziweze kuendana na hali ya sasa, lakini ili ziweze kuendana na Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sisi sote tunakubali kwamba ili tuweze kutekeleza au kuyafikia malengo ya Dira yetu ya 2050, ni lazima tuhakikishe kwamba sheria zetu nazo tunazihuisha ili ziweze kuwa daraja la kutuwezesha kutufikisha katika malengo hayo tuliyojiwekea katika dira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii tumeianza kwa umakini mkubwa na kama wote tunavyofahamu, huu ndiyo mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa dira. Kwa hiyo, hakuna hata sheria

moja ambayo haitapitiwa. Ninarudia tena, hakuna hata sheria moja ambayo itaacha kupitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba sheria hiyo inakuwa na ubora ule ambao unatarajiwa ili tuweze kutimiza malengo ya dira. Kwa hiyo, sheria zote zitaguswa na kwa mwaka huu wa kwanza tumeshazibainisha chache ambazo tumeanza kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu tuliouweka na utaratibu uliopo sasa, ni kwamba sheria yoyote ile ambayo itakuwa inarekebishwa, ni lazima iwe zao la utafiti. Kwa sababu kwa kufanya hivyo ndiyo tutakuwa tunajijua kwamba tuko ndani ya mstari kuelekea Dira ya 2050 au tunakwenda nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sasa hivi utaratibu ni kwamba sheria zozote ambazo zitakuwa zinapendekezwa kurekebishwa, ni lazima kwanza zikapitie kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria ili waweze kuzichakata vizuri kupitia tafiti watakazokuwa wanazifanya na kwa kushirikisha wadau, ili tutakapotoka na sheria hiyo kuja kuileta Bungeni, basi ikaakisi yale malengo ya dira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda kuachana na ule utaratibu wa zamani ambapo tafiti zilikuwa hazifanyiki za kutosha na matokeo yake tukawa na sheria ambazo zinatuletea changamoto. Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo tunakwenda kulizingatia kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, zikiwemo na sheria zile za uwekezaji na zote ambazo zimesemwa, hata na zile za ndoa. Nimemsikia mchangiaji aliyezungumzia Sheria ya Ndoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hii Sheria ya Ndoa, sasa hivi tunaendelea na zoezi la kukamilisha maoni ya wananchi, ni lazima tuhakikishe kwamba tumepata maoni yote ya wananchi nchi nzima na tunakwenda vizuri ili tutakapokuja kufika mwisho tuhakikishe kwamba sheria hiyo imeakisi maoni ya wananchi vizuri na baadaye itakuja kuletwa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusubiri kazi hiyo inaendelea na inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo mengine ambayo yametolewa tumeyapokea, kwa mchangiaji aliyezungumza suala la *Law School*, kwa maana ya kwamba umuhimu wa kuwa na matawi sehemu mbalimbali za nchi yetu ili kurahisisha ufikiwaji wa wanafunzi katika shule yetu hii ya sheria uwe rahisi. Hayo ni maoni mazuri na tumeyapokea na yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapendekezo pia ya lile suala la *exemption*. Ninamtoa tu wasiwasi Mbunge kwamba, suala hili hukumu ya Mahakama ilishatoka na Serikali inaendelea na mchakato wa kufanya marekebisho ya sheria. Kwa hiyo, kwa kifupi tu ni kwamba hayo ndiyo mambo ambayo yalikuwa yanamhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la Mheshimiwa Agnes Hokororo ambaye yeye alizungumzia suala la Sheria Ndogo kwamba zimekuwa nyingi, kwa hiyo suala zima la kutafsiri katika lugha ya Kiswahili liongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea ushauri huu, lakini hata hivyo utaratibu wa kufanya ufasiri wa sheria unatanguliwa na kufanyika kwa lile zoezi la urekebu. Kwa hiyo, kwa sasa Serikali inaendelea na zoezi la urekebu ambapo mpango ni kufanya urekebu wa Sheria Ndogo 1,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia tena, mpango ni kufanya urekebu wa sheria 1,000 kwa mwaka, tukiamini kwamba kwa kasi hii tutaweza kuzifanyia urekebu sheria nyingi. Hata hivyo, ili kuongeza kasi ya kutafsiri sheria, Serikali sasa hivi tunajenga mfumo wa kielektroniki utakaorahisisha ufasiri wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge vile vile alizungumzia kwamba baada ya zoezi la ufasili wa sheria kuu kukamilika sheria hizo zitangazwe rasmi. Nimfahamishe tu kwamba baada ya zoezi hilo kukamilika sheria hizo zilitangazwa rasmi kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa

Serikali imejipanga vizuri katika kuhakikisha kwamba tunarekebisha sheria zote kwa kadri tafiti zitakavyotupa taarifa na kuhakikisha kwamba sheria hizo zinaendana na malengo yaliyowekwa katika Dira yetu ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa heshima na taadhima ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Naibu Waziri na ajiandae mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyopo mezani; hoja ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake mahiri, thabiti na wenye maono ya mbali ambao umeendelea kuleta mafanikio makubwa kwenye sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha ninaomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa uongozi wao imara na maelekezo yao thabiti ambayo yanatuongoza katika utekelezaji wa majukumu yetu Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Juma Homera kwa uongozi wake bora, malezi, miongozo na maelekezo mbalimbali ambayo ananipatia ambayo imekuwa ikiniwezesha kufanya majukumu yangu kwa amani, utulivu na ufanisi. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kutumia nafasi hii kumshukuru sana Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Mheshimiwa George Masaju na Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

Mheshimiwa Hamza Johari. Kwa hakika wamekuwa ni walimu wangu kwa siku zote na wamekuwa na mchango wa kipekee katika kunijenga kitaaluma pamoja na katika utekelezaji wa majukumu yangu; ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii vilevile kutambua mchango wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Ndugu Eliakim Maswi, pamoja na timu nzima ya *Management* ya Wizara ya Katiba na Sheria, bila kuwasahau wasaidizi wangu wa karibu, ambapo nina Katibu wangu Wakili Amani, Karani Shani Suleiman pamoja na dereva wangu Sabri. Kwa hakika ndugu Katibu Mkuu na timu yake yote hii ya Wizara ya Katiba na Sheria wamekuwa ni msaada mkubwa sana katika utekelezaji wa majukumu yangu; ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninatumia pia fursa ya kulishukuru Bunge hili Tukufu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitambue mchango wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, pamoja na Waheshimiwa wote ambao wamechangia hoja hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya Waheshimiwa Wabunge tumeisikiliza kwa makini, maoni yao tumeyapokea na maelekezo yao tutayazingatia katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi Mkuu wa Dira 2050 ni Utawala, Amani, Usalama na Utulivu. Huu ni msingi unaobeba mustakabali wa Tanzania ya kesho; ni msingi unaotofautisha Taifa linalokuwa kwa bahati na Taifa linalojengwa kwa makusudi. Ni muhimu kutambua kwamba katika historia ni kwa mara ya kwanza sekta ya sheria imewekwa katikati ya mjadala wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hatua ya kihistoria sana kwa kuwa tumetoka katika mtazamo wa kuitazama sekta ya sheria

kama sekta mtumiaji wa rasilimali na sasa tunaijenga sekta ya sheria kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi, mlinzi wa uwekezaji na nguzo ya kuaminika ya utulivu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna uchumi wa kisasa unaoweza kustawi bila uhakika wa sheria. Vilevile, hakuna mwekezaji anayeweza kuwekeza bila ulinzi wa haki; na hakuna maendeleo endelevu bila mifumo ya haki inayofanya kazi kwa ufanisi, usawa na uwazi.  ukiitazama Dira yetu hii 2050 ina nguzo tatu. Nguzo ya kwanza ni uchumi imara, jumuishi na shindani; nguzo ya pili ni uwezo wa watu na maendeleo ya jamii; na nguzo ya tatu uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo hizi za Dira 2050 haziwezi kuota, haziwezi kujengwa kama hatuna msingi imara ambao tumeutaja hapa, wa utawala, amani, usalama na utulivu; ambao kimsingi msingi mkuu huu pamoja na mambo mengine unahusisha mageuzi ya kina ya kimfumo, ili kujenga Taifa ambalo sheria siyo kikwazo bali ni daraja la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamechangia hapa, wamegusia maeneo kadha wa kadha. Hata hivyo, ninaomba kuzungumzia baadhi ya maeneo kwa sababu Mheshimiwa Waziri atakuja kuhitimisha atazungumza na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wabunge wengi wamezungumzia kuhusiana na kazi kubwa inayofanyika katika sekta hii ya sheria ambayo ni kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia *(Mama Samia Legal Aid campaign)*. Waheshimiwa Wabunge wafahamu kuwa mkakati huu na kampeni hii ilianzishwa kwa maono ya mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa ana nia na lengo la kuhakikisha kuwa anaimarisha upatikanaji wa haki kwa Watanzania wote na hususan wale wenye mahitaji maalum ambao hawawezi kumudu gharama za kuwa na mawakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waheshimiwa Wabunge walivyotambua hapa, awamu ya kwanza ya kampeni hii ambayo

ilianza mwezi Machi, 2023 na kwisha mwezi Februari, 2026. Ni awamu ambayo ilihusisha wataalam wa sheria, Mawakili kuzunguka katika mikoa yote 26 kwenda kuwatafuta wale wenye uhitaji na kutatua migogoro yao ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya Watanzania 7,462,000 walifikiwa katika huduma hii muhimu ya upatikanaji wa haki. Kampeni hii kwa kweli imezaa matunda makubwa sana kwa kuwa imepunguza migogoro na imeongeza upatikanaji wa haki kwa uharaka na kwa njia rafiki zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba, mpango sasa wa pili wa kampeni hii ya Mama Samia *Legal Aid campaign* tunatarajia kuizindua siku ya tarehe 30 Aprili, 2026 katika Mkoa wa Dodoma. Tunatarajia awamu hii lengo ni kwenda kufika katika maeneo yenye uhitaji mkubwa ya vijijini tofauti na kubakia kwenye miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu hii tutakuwa tunaweka kambi kwa siku 15, tofauti na awali ilikuwa ni siku 10. Hii yote ni dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata haki bila ubaguzi na ili wanapopata haki hiyo inaweza kuchangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Waheshimiwa Wabunge walizungumza kuhusiana na masuala ya mrundikano wa mashauri katika Mahakama na kuhusiana na kesi; kwamba, kuwe kuna uharaka wa kesi kusikilizwa. Kwenye eneo hili ninaomba kusema hivi; kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imefanya uwekezaji mkubwa sana katika mhimili huu wa Mahakama ili kuhakikisha na kuboresha upatikanaji wa haki kwa Watanzania wote. Ukisoma Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazungumza hapa, kwamba mamlaka ya mwisho ya kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa ni Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama inatambua kwamba utoaji haki hauishii tu kwenye kusikiliza mashauri; kwamba, upatikanaji wa haki na utoaji wa haki unahusisha pia katika

masuala mengine muhimu ikiwemo pia kuendeleza miundombinu ya majengo ya Mahakama ambayo Watanzania wanaweza wakafika kwa ajili ya kupata huduma za haki. Ndiyo maana Mahakama inatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi na ukarabati wa miundobinu ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huu mradi umeenda uwekezaji wa shilingi bilioni 524.9 tisa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Tanzania nzima majengo ya Mahakama yanakarabatiwa na kwenye maeneo ambayo hamna majengo, majengo ya kisasa yanajengwa kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa Watanzania. Hii ndiyo Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza wakati huu katika mikoa 25 kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara tayari kuna Mahakama Kuu, zipo na zinatoa huduma kwa wananchi. Katika kipindi hiki cha miaka mitano, Mahakama Kuu 15 zimejengwa katika muundo wa vituo jumuishi vya upatikanaji haki au vituo jumuishi vya Mahakama Kuu. Vituo hivi ni vya kipekee kabisa ambavyo vinakuwa na ngazi zote za Mahakama kwenye jengo moja; kwa maana ya jengo la Mahakama Kuu. Yaani kunakuwa na jengo la Mahakama Kuu, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya pamoja na Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Hii inaleta wepesi kwa Watanzania, kwa wananchi kupata haki yao. Kwa maana ule muda waliokuwa wanatumia, zile gharama walizokuwa wanatumia kutoka katika ngazi moja ya Mahakama kwenda kwenye ngazi nyingine ya Mahakama, wanakuwa wameepuka na maisha yao yanakuwa ni rahisi kwa kuwa changamoto zao na haki yao inaweza ikapatikana kwa gharama nafuu na kwa urahisi. Hii yote ni kazi kubwa na uwekezaji mkubwa ambao umefanyika katika Mhimili huu wa Mahakama katika kipindi cha Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upekee wa hivi vituo pia upo katika kuwa na wadau mbalimbali wa haki ambao nao wapo katika jengo moja. Wadau mbalimbali ninaowazungumzia hapa ni Jeshi la Polisi nao wanakuwa na chumba katika jengo hilo; watu wa ustawi wa jamii nao wanakuwa na chumba katika jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kunakuwa na watu wa huduma ya msaada wa kisheria, kunakuwa na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali, kuna hadi chumba cha kunyonyesha watoto ambacho akina mama wanaweza wakaenda wakanyonyesha watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unaona kwamba huu ni uwekezaji mkubwa sana unaofanya mapinduzi makubwa ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata haki na katika mazingira ambayo ni mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu siyo tu upatikanaji wa haki. Hata ukisoma Ibara hii ya 107A(2)(b) inasema kwamba pamoja na mambo mengine inaipa mamlaka Mahakama kwamba kutokuchelewesha haki bila sababu ya msingi. Wanasema hivi; *"Justice delayed is justice denied"*. Ukichelewesha haki ni sawasawa na umeinyima hiyo haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukiangalia muktadha wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inataka Watanzania wapate haki kwa wakati. Kwa hiyo hoja siyo tu upatikanaji wa haki, lakini hiyo haki iwe imepatikana kwa wakati. Kwa hiyo kuwa na mifumo na majengo bora ya namna hii unawezesha upatikanaji wa haki kwa wakati, kama ibara ya 107A(2)(b) inavyotaka iwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama kuna matokeo ambayo tunayaona; na ndiyo maana mlundikano wa mashauri umepungua. Kwa sasa tuna mlundikano wa mashauri katika Mahakama zetu kwa asilimia nne tu. Hii asilimia nne Mahakama tayari inaifanyia kazi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kunakuwa hamna mrundikano kabisa wa mashauri katika Mahakama, wananchi wapate haki yao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa Mahakama za Wilaya, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwa maana walipokuwa wanachangia wamegusia. Kwenye Mahakama za Wilaya, wilaya zimejengewa hizi Mahakama, wilaya 42. Kwa hiyo kwa wakati huu katika wilaya 139 tulizokuwa nazo, wilaya 136 tayari zina majengo ya Mahakama. Mahakama ambazo

zimebaki na ambazo zipo katika mpango unaofuata wa ujenzi ni pamoja na Wilaya ya Mkalama, Chamwino na Ikungi. Hizi ndizo wilaya tatu ambazo zimebakia hazina majengo ya Mahakama za Wilaya na zitakuja kujengewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mahakama za Mwanzo kwenye mpango huu zimejengwa Mahakama za mwanzo 72. Ninatambua kuwa Waheshimiwa Wabunge wana uhitaji bado wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu tuna kata 3,956 na Mahakama za Mwanzo tulizokuwa nazo kwa wakati huu ni 960, hivyo bado kuna uhitaji wa Mahakama za Mwanzo katika kata 2,996. Ninaomba kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba mkakati wa Mahakama ni kuhakikisha katika mpango wa tatu wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama, Mahakama hizi zitajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama hizi zitajengwa kwa ushirikiano kati ya Mahakama na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Kwa hiyo siku ya tarehe 5 Aprili, 2026 tukiwa kwenye uzinduzi wa Jengo la Makao Makuu ya Mahakama *(Judiciary Square),* Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo kwetu. Alisema kwamba Wizara ya TAMISEMI, Mahakama pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria tushirikiane kwa pamoja ili kuongeza kasi katika ujenzi wa Mahakama hizi za Mwanzo tukishirikiana na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba dhamira ile ya Serikali ya kuendelea kufanya uwekezaji katika Mahakama na katika eneo hili la miundobinu ya Mahakama ipo; na tayari kuna hadi Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na ninaomba niwatambue kwa majina yao. Ninaomba kumtambua Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mheshimiwa Zainab Telak; Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mheshimiwa Mwanamvua Mrindoko; Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mheshimiwa Charles Makongoro. Hawa wote tayari wameanza utekelezaji kwa kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo. Kwa hiyo Mahakama hizi zitajengwa ili kuendelea kuboresha upatikanaji wa haki kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji huo wa shilingi bilioni 524.9 haujaishia kwenye upande wa miundombinu, kwa maana ya majengo pekee; yamefanyika mapinduzi makubwa ya kidijitali, kwa maana ya kutengeneza mifumo ya kidijitali kwa ajili ya upatikanaji wa haki; pamoja na kutumia teknolojia ya TEHAMA kurahisisha na kusogeza huduma za upatikanaji wa haki kwa wananchi. Sasa hivi katika Mahakama tuna mfumo *ECMS* ambapo mwananchi anaweza akaingia kwenye mfumo na akafungua shauri, akafuatilia shauri lake na akapata hadi hukumu kupitia mfumo huo. Haya ni mapinduzi makubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna huduma ya Mahakama Mtandao ambapo Mtanzania anaweza akaingia kupitia mtandao huu, akahudhuria shauri lake. Haya ni mapinduzi makubwa sana. Tunaona kwenye upande huo huo wa mapinduzi kwenye mifumo ya kidijitali, Mahakama ina *call center*, kituo cha huduma kwa wateja, ambacho namba zake ni 0800750247.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtanzania anayehitaji mwongozo wa namna gani ya kupata haki zake katika mfumo wa Mahakama, anaweza akapiga namba hii na akapewa mwongozo sahihi wa taratibu za kufuata ili aweze kupata haki yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfumo pia wa namba ya *WhatsApp* ambayo kwa kutumia teknolojia ya *chatbot,* roboti hili lina-*chat* na Watanzania, linawaelekeza mambo tofauti tofauti na namna gani ya kupata haki zao na taratibu za kufuata Mahakamani ili kupata haki zao. Hii ni kazi kubwa sana ambayo imefanyika katika Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha ninawaomba Waheshimiwa Wabunge watupitishie hii Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ili twende tukaimarishe Sekta ya Sheria ili kuwezesha utekelezaji wa Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge watupitishie bajeti hii ili twende tukaimarishe upatikanaji wa haki kwa wote kupitia mifumo jumuishi yenye ufanisi na

inayofikika. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge watupitishie bajeti hii ili tukajenge mazingira bora ya uwekezaji kwa maana katika kipindi hiki cha ushindani wa kimataifa wa uwekezaji tunatakiwa kulinda maslahi ya Taifa kupitia sheria madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge watupitishie bajeti hii ili twende tukaimarishe utawala bora na uwajibikaji na kuhakikisha Taifa linaendelea kuwa na amani, usalama na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa mchango wako. Sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu pamoja na kuniwezesha kufanya kazi zangu vizuri katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania naishukuru sana na taasisi zote zilizoko chini ya hii Wizara ya Katiba na Sheria. Pia, ninawashukuru viongozi wangu wengine akiwemo Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Spika; na Viongozi wengine wote wa Bunge pamoja na wewe mwenyewe Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Naibu Waziri

wa Katiba na Sheria kwa namna anavyonisaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niishukuru Menejimenti ya Wizara, Mahakama ya Tanzania pamoja na kiongozi kinara kabisa Eliakim Maswi, Katibu Mkuu tukisaidiana vyema na Naibu Katibu Mkuu na Viongozi wote walioko chini ya Wizara hii ambao niliwataja hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Namtumbo kuendelea kuniombea wakiungana na wazazi wangu ambao niliwataja hapo awali pamoja na familia yangu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nishukuru Waheshimiwa takribani wa Bunge zaidi ya 19 wamechangia katika hoja yangu ambayo nimeitoa hapo asubuhi. Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Mariam Mungula, Mheshimiwa Asha Saleh, Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja, Mheshimiwa Happiness Daniel Ngwando, Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mheshimiwa Neema Peter Majule, Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, usiwataje kwa sababu ya muda…

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay,* sawa. Nitambue tu kwamba wako 19 ambao wamechangia kwenye hoja yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme machache ambayo hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Moja kuna suala ambalo lilitajwa hapa na Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Serikali ichukue hatua makusudi za haraka kuhakikisha Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha Taasisi ya Kisheria Ilemela, Mwanza ukamilike kwa wakati, ikibidi kumnyang'anya mkandarasi kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari mkakati umewekwa chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo imeunda timu ya

usimamizi wa mradi huu na tuna uhakika utakamilika kwa wakati. Hatua stahiki za haraka zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuvunja mkataba kwa mujibu wa sheria kama mkandarasi huyu ataendelea kusuasua kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilibuni mikakati kuhakikisha mashauri yanamalizika kwa wakati pasipo kuathiri ubora wa maamuzi. Ushauri umepokelewa Serikalini kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweka mikakati ifuatayo ili kumaliza mashauri kwa muda mrefu na kupunguza mashauri. Imeendelea kuweka mkakati wa kufanya majadiliano nje ya Mahakama kwa lengo la kupunguza mlundikano wa mashauri dhidi ya Serikali ambayo yameweza kuyamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, vilevile kwa kushirikiana na Mahakama kama mdau mkuu inaendelea na mkakati wa kumaliza masharti ya muda kwa muda mrefu kwa kusikiliza mashauri hayo kupitia vikao maalum *(Special Session [BRN])* ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa mkakati wa kupunguza na kumaliza mlundikano wa mashauri Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo ambalo lilizungumzwa pia na Kamati ya Kudumu ya Bunge, Serikali iharakishe utatuzi wa mgogoro wa ardhi ikiwemo mgogoro wa wakulima wa chai katika Mkoa wa Tanga. Serikali imepokea shauri hili na itahakikisha migogoro ya ardhi ikiwemo migogoro ya wakulima wa chai hususan katika Mikoa ya Tanga itatatuliwa kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ianzishe Mahakama ya Mkoa itakayokuwa na mamlaka ya rufaa kwa Mahakama za Wilaya ili kupunguza idadi ya kesi zinazowasilishwa Mahakamani. Ili kupunguza mzigo wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani, Serikali imepokea ushauri huu wa Wabunge wa kuanzisha Mahakama ya Mkoa itakayokuwa na Mamlaka ya Rufaa kwa Mahakama za Wilaya. Kwa kushirikiana na Mahakama tutafanya uchambuzi wa mapendekezo hayo na mara baada ya uchambuzi kukamilika, Serikali itatoa taarifa ya hatua zilizochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo alizungumzia kuhusiana na kwamba kumekuwepo na

changamoto za uwasilishwaji wa fedha za *retention* katika Ofisi za Wilaya na Halmashauri, vitendea kazi na watumishi ili kuwezesha utoaji wa huduma za *RITA* ikiwemo vyeti vya kuzaliwa na vifo, vilevile takwimu za vizazi na vifo na ni muhimu katika mipango ya nchi na vyema zitatuliwe hizo changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya uwasilishaji wa fedha za *retention* katika Ofisi za Wilaya na Halmashauri imetatuliwa ambapo asilimia tano ya mapato yanayokusanywa kwa kila Wilaya na Halmashauri huwasilishwa katika Ofisi hizo. Kuhusu vitendea kazi ni kweli changamoto hiyo ipo na kwa kutambua hilo katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, imetenga bajeti ya shilingi 850,000,000 kwa ajili ya kununua vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watumishi katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, *RITA* ilipokea watumishi 63 na kufanya jumla ya watumishi kufikia 405 ikilinganishwa na hapo awali kulikuwa na watumishi 342. Aidha, *RITA* imepata kibali cha kuajiri watumishi 73. Ni kweli utoaji wa takwimu za vizazi na vifo ni muhimu kwa kutambua *RITA* ndiyo chanzo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *RITA* tumeanzisha programu ya masaa 48 ya utoaji wa vyeti vya kuzaliwa na vyeti vya vifo. Kwa kushirikiana na Taasisi ya Ufilisi na Udhamini *(RITA)* tulifanya uzinduzi wa vyeti vya kuzaliwa kwa masaa 48 mwezi Desemba, 2025. Tangu uzinduzi uliofanyika Machi, 2026 Wakala umepokea jumla ya maombi 445,512. Kati ya maombi yaliyopokelewa 420,863 yalifanyiwa kazi na vyeti vilitolewa ndani ya masaa 48 hivyo tulifanikiwa kwa zaidi ya 94%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Serikali ikamilishe mchakato wa kuhamisha mashauri ya ardhi kwenda kwenye mfumo wa Mahakama na pia Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria naye alizungumzia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imeshaanza utaratibu wa kuhamisha mashauri yaliyokuwa yanashughulikiwa na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwenda katika mfumo wa Mahakama ya Tanzania. Hatua hii ilifikiwa baada ya

majadiliano na Wizara ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote kwa pamoja kupitia maelekezo ambayo aliyatoa Mheshimiwa Rais tarehe 13 Januari, 2026, katika Mkutano Maalum *Judicial Square;* mojawapo ya maelekezo aliyoyatoa aliyatoa kwamba, kuhamisha Mabaraza ya Ardhi kwenda kwenye Mahakama. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge jambo hili limefanyiwa kazi kwa kiwango cha hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kwa Waheshimiwa Wabunge, bajeti yetu mwaka huu inakwenda kumaliza kabisa changamoto ambazo zingeweza pia kwenda kuleta changamoto kubwa kwenye Dira ya 2050. Kwa hiyo, tunakwenda kurekebisha sheria kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria Nchini pamoja na Tume ya Kuandika Sheria Nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumzia masuala mbalimbali, ningependa nijibu pia machache. Mheshimiwa Happiness Ngwando ambaye ametupongeza, lakini pia tunashukuru sana kwa mchango wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya siku 120 pia tunakwenda kuzindua Mfumo wa *E-Legal Aid* ambao tutakuwa tuna uwezo wa kupeleka changamoto zetu kwenye mfumo na tukapatiwa majibu kwa haraka ili kuweza kuboresha zaidi mfumo wa msaada wa kisheria nchini. Ndani ya siku 120 tunakwenda kulifanya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kama vile Mheshimiwa Kenneth Ndingo ambaye ametupongeza, lakini amezungumzia masuala ya Mabaraza ya Ardhi na kusema kwamba masuala ya Dira ya 2050 tungetamani yasikwame kwa changamoto ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba sisi kama Wizara mojawapo ya kitu ambacho tunakwenda kukifanya ni ulinzi wa

watoa taarifa na mashahidi, kitengo ambacho hakikuwepo mwanzo. Sasa hivi kimewekwa kwenye bajeti hii na kitengo hiki kimeanzishwa baada ya Mheshimiwa Rais kutupa kibali cha kuanzisha kitengo hiki muhimu katika Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mageuzi ya sheria kwa ajili ya uwekezaji na uchumi nchini ambayo tunakwenda kufanya kazi kubwa ya mabadiliko ya sheria ili kuwavutia wawekezaji, lakini pia kuwafanya wawekezaji wawe na unafuu ili tuweze kujenga nchi yetu iende kwenye uchumi wa juu zaidi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda pia kusimamia utatuzi wa masuala ya ajira, uteuzi, nidhamu na maadili ya watumishi wa Mahakama na Taasisi zingine zote zilizoko chini ya hii Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, nikushukuru sana wewe binafsi kwa namna ambavyo ulivyotuongoza vyema hapa kwenye kikao chetu cha leo cha Bunge. Hakika unastahili pongezi za dhati sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, waweze kuiunga mkono bajeti hii ili tuweze tukafanye mabadiliko makubwa na mageuzi makubwa ya upatikanaji wa haki na maendeleo makubwa ya kasi kuelekea Dira ya 2050 pamoja na bajeti hii ya Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, Mheshimiwa tunakushukuru. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Unit*……….………….Sh. 17,973,531,143
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……......Sh. 1,048,460,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*…..........Sh. 1,696,496,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…….........................Sh. 676,536,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*….Sh. 784,648,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*….....Sh. 762,804,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*…………….…..……..Sh. 1,413,792,000
Kifungu 1008 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 648,204,133
Kifungu 2001 – *Human Right Division*…..……………....Sh. 2,088,244,000
Kifungu 2002 – *Legal Aid Service Unit*……….……..Sh. 11,453,745,924
Kifungu 2003 – Alternative Dispute Resolution Unit………...……………….……………...Sh. 3,000,000,000
Kifungu 2004 – *Public Legal Services Division*………Sh. 9,771,248,000
Kifungu 2005 – *Natural Wealth and Resource Observatory Unit*…..…………………..…Sh. 1,311,384,000
Kifungu 4001 – *Constitutional and Justice Monitoring Division*...........................Sh. 6,830,881,800
Kifungu 4003 – *Whistleblower and Witness Protection Division*….…………..…....Sh. 6,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama**

Kifungu 1001– *Administration and Human*

*Resources Management*…...……….Sh. 4,641,187,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………….....Sh. 269,550,000
Kifungu 1003 – *Procurement Management Unit*…......Sh. 189,110,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……..........................Sh. 200,510,000
Kifungu 1005 – *Recruitment, Appointment and Confirmation Unit*……………………..….Sh. 829,720,000
Kifungu 1006 – *Ethics and Discipline Section*…..........Sh. 578,895,000
Kifungu 1007 – *Planning, Monitoring and Evaluation*...........................................Sh. 395,677,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*………………….......Sh. 651,695,000
Kifungu 1009 – *Legal Service Unit*…………………….Sh. 137,700,000
Kifungu 1011 – *Government Communication Unit*….Sh. 253,500,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*………...Sh. 10,029,060,480
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……...Sh. 2,887,475,720
Kifungu 1003 – *Planning Budget & Innovation Unit*...................................................Sh. 3,148,056,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……........................Sh. 1,678,820,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*………………………………..….Sh.1,486,280,000
Kifungu 1006 – *Legal Registry Unit*……….………….. Sh. 550,000,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*…….……………………......................Sh.1,573,932,000
Kifungu 1008 – *Legal Research & Training Unit*.........Sh.2,464,720,000
Kifungu 1009 – *Information & Communication Technology Unit*…..……………………Sh.2,986,648,000
Kifungu 1010 – *Monitoring & Evaluation Unit*............Sh.1,397,160,000
Kifungu 2001 – *Coordination & Legal Service Division*…………………………………...Sh.8,159,428,610

Kifungu 2002 – *Contracts Negotiation, Management, & Dispute Resolution*.........................Sh.5,889,000,000
Kifungu 2003 – *Legislative Drafting*……………………………………Sh.0

Kifungu 3002 – *Treaties and Contracts Division*……..Sh.7,699,084,000
Kifungu 5001 – *Regional Attorney General's Office – Dar es Salaam*……..……….Sh.619,354,690
Kifungu 5002 – *Regional Attorney General's Office – Arusha*…….……….…………Sh.453,849,000
Kifungu 5003 – *Regional Attorney General's Office – Mbeya*……….....................Sh.453,797,000
Kifungu 5004 – *Regional Attorney General's Office – Kilimanjaro*…...………………...Sh.454,684,000
Kifungu 5005 – *Regional Attorney General's Office – Mtwara*…………………..…...Sh.446,935,000
Kifungu 5006 – *Regional Attorney General's Office – Mwanza*……………………...Sh.568,973,500
Kifungu 5007 – *Regional Attorney General's Office – Kagera*…….……..…………..Sh.445,867,000
Kifungu 5008 – *Regional Attorney General's Office – Tabora*………..………..……..Sh.447,997,000
Kifungu 5009 – *Regional Attorney General's Office – Tanga*……………………..….Sh.446,062,000
Kifungu 5010– *Regional Attorney General's Office – Kigoma*…………..……………Sh.164,950,000
Kifungu 5011– *Regional Attorney General's Office – Mara*…………………………...Sh.164,950,000
Kifungu 5012 – *Regional Attorney General's Office – Shinyanga*……………………Sh.164,950,000
Kifungu 5013 – *Regional Attorney General's Office – Ruvuma*……………………...Sh.164,950,000
Kifungu 5014 – *Regional Attorney General's Office – Iringa*………….………..…….Sh.164,950,000
Kifungu 5015 – *Regional Attorney General's Office – Songwe*……………………..…..Sh.164,950,000
Kifungu 5016 – *Regional Attorney General's Office – Singida*……..……………..…...Sh.164,950,000
Kifungu 5017 – *Regional Attorney General's Office – Morogoro*……………….……Sh.164,950,000
Kifungu 5018 – *Regional Attorney General's Office – Katavi*..……………….………Sh.164,950,000
Kifungu 5019 – *Regional Attorney General's Office – Pwani*…………………………Sh.164,950,000
Kifungu 5020 – *Regional Attorney General's*

*Office – Simiyu*……………………………Sh.164,950,000
Kifungu 5021 – *Regional Attorney General's Office – Geita*….…………………………Sh.164,950,000
Kifungu 5022 – *Regional Attorney General's Office – Lindi*………………………………Sh.164,950,000
Kifungu 5023 – *Regional Attorney General's Office – Njombe*…………………………Sh.164,950,000
Kifungu 5024 – *Regional Attorney General's Office – Dodoma*……………………..…Sh.164,950,000
Kifungu 5025 – *Regional Attorney General's Office – Manyara*…..…………………..…Sh.164,950,000
Kifungu 5026 – *Regional Attorney General's Office – Rukwa*…………………………..…Sh.164,950,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………...Sh.18,316,934,000

**MWENYEKITI:** Kwa mujibu wa Kanuni ya 126 sasa tunaingia kwenye *guillotine* kwa maana ya kupitisha vifungu kwa pamoja.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…….........Sh.18,316,934,000
Kifungu 1002 – *Finance & Accounts Unit*….................Sh.700,413,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*…..............................Sh.1,488,140,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…..............................Sh.466,612,000

Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*…......................................................Sh.644,536,000
Kifungu 1006 – *Information & Communication Technology Unit*..……………………..Sh.1,035,408,000
Kifungu 1007 – *Government Communication*

*Unit*……………………………………………Sh.956,827,000
Kifungu 1008 – *Library Service & Research Unit*……....Sh.523,606,000
Kifungu 1009 – *Legal Registry Unit*....……………..…..Sh.1,361,092,000
Kifungu 2001 – *Case Management & Quality Assurance*…………........……………Sh.1,953,352,000
Kifungu 2002 – *Arbitration Division*……….…………....Sh.6,046,242,000
Kifungu 2003 – *Litigation Division*...............................Sh.7,820,614,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management*…….......Sh.67,855,568,970
Kifungu 1002 – *Finance & Accounts Unit*…………….Sh.1,083,385,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*................................Sh.1,555,145,030
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*................................Sh.742,456,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*......................................................Sh. 663,891,000
Kifungu 1006 – *ICT & Information Unit*..........................Sh.789,762,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*…...................................................Sh.681,486,000
Kifungu 1008 – *Research & Library Services Unit*..........................................................Sh.408,737,000
Kifungu 1009 – *Legal Registry Unit*……….......................Sh.635,610,000
Kifungu 2002 – *Civilization & Prosecutions*…………......Sh.2,773,601,000
Kifungu 2004 – *Regional Office Arusha*.....................Sh.2,267,047,000
Kifungu 2005 – *Regional Office Dodoma*……………Sh.2,610,581,000
Kifungu 2006 – *Regional Office Dar es Salaam*.........Sh.3,173,636,000
Kifungu 2007 – *Regional Office Iringa*………………..Sh.1,584,158,000
Kifungu 2008 – *Regional Office Moshi*.......................Sh.2,434,307,000
Kifungu 2009 – *Regional Office Kagera*....................Sh.2,507,121,000
Kifungu 2010 – *Regional Office Mbeya*.....................Sh.2,287,443,000
Kifungu 2011 – *Regional Office Mtwara*....................Sh.1,808,983,000
Kifungu 2012 – *Regional Office Mwanza*..................Sh.3,214,532,000
Kifungu 2013 – *Regional Office Ruvuma*..................Sh.1,960,031,000
Kifungu 2014 – *Regional Office Sumbawanga*.........Sh.1,311,215,000
Kifungu 2015 – *Regional Office Tabora*....................Sh.2,430,085,000
Kifungu 2016 – *Regional Office Tanga*......................Sh.2,576,685,000

Kifungu 2017 – *Regional Office Shinyanga*...............Sh.1,735,132,000
Kifungu 2018 – *Regional Office Singida*.....................Sh.1,638,424,000
Kifungu 2019 – *Regional Office Lindi*…......................Sh.1,802,068,000
Kifungu 2020 – *Regional Office Mara*………………...Sh.1,424,973,000
*Kifungu* 2021 – *Regional Office Manyara*..................Sh.2,097,833,000
Kifungu 2022 – *Regional Office Kigoma*……………..Sh.2,214,459,000
Kifungu 2023 – *Regional Office Pwani*……………….Sh.2,742,149,000
Kifungu 2024 – *Regional Office Njombe*....................Sh.1,340,909,000
Kifungu 2025 – *Regional Office* Morogoro…….........Sh.2,438,930,000
Kifungu 2026 – *Regional Office* Geita…....................Sh.1,982,726,000
Kifungu 2027 – *Regional Office* Simiyu…....................Sh1,675,921,000
Kifungu 2028 – *Regional Office* Katavi.......................Sh.1,115,343,000
Kifungu 2029 – *Regional Office* Songwe……………Sh.1,059,946,000
Kifungu 2030 – *Regional Office* Ilala…........................Sh.1,130,693,000
Kifungu 2031 – *Regional Office* Kinondoni...............Sh.2,025,923,000
Kifungu 2032 – *Regional Office* Temeke……….…Sh.1,390,300,574
Kifungu 2033 – *Regional Office* Tarime.........................Sh.898,063,000
Kifungu 3001 – *Fraud, Money Laundering %*
*Corruption*……………..…..................Sh.2,932,049,426
Kifungu 3002 – *Assets Forfeiture Transnational*
*& Specialized Crime*………..………Sh.2,595,168,000
Kifungu 3003 – *Case Management, Coordination*
*of Criminal Cases*…..………………...Sh.5,060,736,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kifungu 1001 – *Administration & Human*
*Resources Management*…...........Sh.124,157,838,123
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*
*Unit*.....................................................……..Sh.962,861,000
Kifungu 1003 – *Planning & Monitoring Division*........Sh.29,872,762,889
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*.................................Sh.651,048,600
Kifungu 1005 – *Information, Communication*
*& Technology Unit*...............................Sh.4,612,613,492
Kifungu 1006 – *Information, Education &*
*Communication Unit*............................Sh.978,500,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*….......Sh.908,615,000

Kifungu 1008 – *Estates Management Unit*.................Sh.1,766,673,700
Kifungu 1009 – *Records Management unit*..................Sh.657,185,000
Kifungu 1010 – *Library Services Unit*…………....................Sh.503,559,900
Kifungu 1011 – *Legal Services Unit* ....……………..………Sh.165,942,400
Kifungu 1012 – *Transport Management Unit*.............Sh.2,326,018,900
Kifungu 1013 – *Monitoring & Evaluation Unit*...............Sh.774,138,845
Kifungu 2001 – *High Court Main Registry*...............…Sh.26,179,321,300
Kifungu 2002 – *Court of Appeal*.....…………………......Sh.13,195,766,672
Kifungu 2004 – *High Court Divisions*.…............................................Sh.0
Kifungu 2299 – *Commercial Court*……………………Sh.1,388,808,000
Kifungu 2300 – *Land Court*……………………………Sh.1,354,961,000
Kifungu 2301 – *Labour Court*……................................Sh.1,212,318,440
Kifungu 2302 – *Case Management Division*..………….Sh.960,331,508
Kifungu 2303 – *Complaints Management & Inspectorate*......................……………….....Sh.857,953,900
Kifungu 2310 – *Mediation Centre*…...........……………Sh.654,563,900
Kifungu 2326 – *Corruption & Economic Court*…….......Sh.871,205,200
Kifungu 2327 – *Judiciary Delivery Unit*.…………….…....Sh.471,940,000
Kifungu 2347 – *IJC Temeke*..........................................Sh.1,509,642,000
Kifungu 2352 – *Specialized Division*.…..........................Sh.355,000,000
Kifungu 3001 – *Arusha Zone*……................................Sh.1,888,166,564
Kifungu 3002 – *Coast Zone*……..................................Sh.1,129,040,524
Kifungu 3003 – *Dar es Salaam Zone*…........................Sh.4,758,953,574
Kifungu 3004 – *Dodoma Zone*...………….......................Sh.2,058,984,604
Kifungu 3005 – *Iringa Zone*……………............................Sh.1,264,197,673
Kifungu *3006* – *Simiyu Zone*………….…........................Sh.1,858,103,276
Kifungu *3007* – Kigoma Zone……………….......................Sh.1,539,715,622
Kifungu 3008 – *Moshi Zone*…….................................Sh.1,680,017,496
Kifungu 3009 – *Lindi Zone*……………….........................Sh.1,744,639,900
Kifungu 3010 – *Mara Zone*……………….........................Sh.1,711,462,460
Kifungu 3011 – *Mbeya Zone*………..…….......................Sh.1,805,702,170
Kifungu 3012 – *Morogoro Zone*…..…….........................Sh.1,962,997,220
Kifungu 3013 – *Mtwara Zone*…………………………...Sh.1,491,505,279
Kifungu 3014 – *Mwanza Zone*……...............................Sh.2,278,115,599
Kifungu 3015 – *Songea Zone*……………........................Sh.1,620,568,690
Kifungu 3016 – *Sumbawanga Zone*….........................Sh.1,366,334,567
Kifungu 3017 – Manyara Zone…….................................Sh.1,400,306,210
Kifungu 3018 – *Bukoba Zone*……………........................Sh.2,109,319,553
Kifungu 3019 – *Singida Zone*……….............................Sh.1,835,000,115
Kifungu 3020 – *Shinyanga Zone*……..…......................Sh.1,579,176,500

Kifungu 3021– *Tabora Zone*……..........….......................Sh.1,635,538,704
Kifungu 3022 – *Tanga Zone*…….….....………………..Sh.2,032,757,012
Kifungu 3023 – *Songwe Zone*…………………………..Sh.1,623,914,500
Kifungu 3024 – *Katavi Zone*……………......................Sh.1,809,908,789
Kifungu 3025 – *Njombe Zone*…………........................Sh.1,748,373,100
Kifungu 3026 – *Geita Zone*………………......................Sh.1,659,374,530

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management*….................Sh.6,331,993,997
Kifungu 1002 – *Finance & Accounts Unit*……………....Sh.541,967,900
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit*…..............................Sh.289,423,120
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit*…...........................Sh.1,116,415,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*.........Sh.391,791,174
Kifungu 1006 – *Management Information System Unit*............................................Sh.449,805,574
Kifungu 1007 – *Planning and Budget Unit*....................Sh.526,296,000
Kifungu 2001 – *Human Right & Good Governance Division*.………..........…Sh.1,539,559,000
Kifungu 2003 – *Public Education, Communication Research & Documentation*……….Sh.1,266,018,000
Kifungu 3001 – *Zanzibar Office* ……………………….Sh.1,174,524,589
Kifungu 3002 – *Mwanza Office*……………....................Sh.491,111,000
Kifungu 3003 – *Mtwara Office*…………………………...Sh.429,061,000
Kifungu 3004 – *Pemba Branch*…………………………..Sh.316,981,336
Kifungu 3005 – *Dar es Salaam Office*…………………Sh.1,406,629,310
Kifungu 3006 – *Tabora Office* ......................................Sh.367,950,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kifungu 1001 – *Administration & Human*

*Resources Management*……..……....Sh.2,984,720,985
Kifungu 1002 – *Finance & Accounts Unit*……………..…..Sh.790,016,958
Kifungu 1003 – *Planning & Coordination Unit*………....Sh.831,906,701
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……...........................Sh.449,388,589
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*…..….Sh.469,386,055
Kifungu 1006 – *Legal Education &*
*Awareness Unit*..................................Sh.1,471,910,709
Kifungu 1007 – *Law Review Division*…………………...Sh.2,053,403,750
Kifungu 1008 – *Law Research Division*.………………..Sh.1,995,068,750
Kifungu 1009 – *Legal Services Unit* ...............................Sh.314,868,943
Kifungu 1010 – *Information & Communication*
*Technology Unity*.................................Sh.370,233,896
Kifungu 1011 – *Monitoring & Evaluation Unit*...............Sh.142,521,365
Kifungu 1012 – *Government Communication Unit*......Sh.238,232,299

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 101 – Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources*
*Management*…………………………Sh.5,606,970,500
Kifungu 1002 – *Finance & Accounts Unit*……..……..Sh.909,706,000
Kifungu 1003 – *Planning & Budgeting Unit*...................Sh.968,562,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*……..Sh.722,808,000
Kifungu 1005 – *Information & Communication*
*Technology Unity*...............................Sh.1,713,378,500
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*……..........................Sh.673,856,000
Kifungu 1007 – *Monitoring & Evaluation Unit*...............Sh.351,844,000
Kifungu 1008 – *Quality Assurance Unity*.....................Sh.1,220,342,000
Kifungu 1009 – *Government Communication Unit*......Sh.631,334,000
Kifungu 2001 – *Legislative Drafting Division*……….....Sh.3,485,690,000
Kifungu 2002 – *Legal Translation Division*..................Sh.3,180,934,000
Kifungu 2003 – *Laws Revision, Research &*
*Training Division*..................................Sh.4,774,081,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE**

**MIRADI YA MAENDELEO**

**Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management*……….......Sh.4,000,000,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*…...............................................Sh.0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

Kifungu 1001 – *Administration & Hunan Resources Management*..................................Sh.15,866,110,000

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kifungu *1003 – Planning & Monitoring Division*…….Sh.22,691,200,000

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kifungu *1003 – Policy & Planning Division*……......Sh.94,862,320,000

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kifungu 1007 – *Planning, Monitoring & Evaluation*……………..…Sh.0

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mheshimiwa Waziri Mtoa Hoja. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Agosti, 2025, ninaomba kutoa taarifa kuwa, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Ninaomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji kuhusu kupitisha Hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nitangaze kwamba, Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria imepitishwa rasmi na Bunge hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nami nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa mnayoifanya na hatimaye leo mmeweza kuhitimisha zoezi la bajeti ya Wizara yenu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Ninawapongeza pia Katibu Mkuu pamoja na watumishi na watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria na upande wa Mahakama tunampongeza Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Gabriel, pamoja na viongozi na watendaji wote wa kwenye Mhimili wa Mahakama. Hongereni kwa kazi nyingi na kubwa mnazofanya na kutoa huduma kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Waziri, tunawatakia utekelezaji mwema wa bajeti hiyo mpya, na tunayo imani nanyi na tuna tumaini kwamba maono ya Mheshimiwa Rais ya kuleta tabasamu kwa Watanzania yatafikia na yatatimia na hasa kupitia maono yake ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia maarufu kama *Samia Legal Aid Campaign*. Kwa hiyo, tunawatakia utekelezaji mwema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya, sasa ninaahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu tarehe 27 Aprili, 2026, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.11 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 27 Aprili, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*